# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

### Kikao cha Thelathini – Tarehe 15 Mei, 2026

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae.

Waheshimiwa, karibuni kwenye ukumbi wetu wa muda, katika Mkutano wa Tatu, Kikao cha Thelathini.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MHE. COSMAS M. BULALA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya

Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Nimwite sasa Mheshimiwa Omary Marcus Msigwa, Mbunge wa Madaba, aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 347

**Hitaji la Walimu na Nyumba Shule za Msingi na Sekondari - Madaba**

**MHE. OMARY M. MSIGWA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Walimu na Nyumba za Walimu katika Shule za Msingi na Sekondari – Madaba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa niaba ya Waziri, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Omary Marcus Msigwa, Mbunge wa Jimbo la Madaba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mwaka wa fedha 2021/2022 – 2025/2026 Serikali imeajiri walimu 63,887 na kujenga nyumba za walimu 3,588 kote nchini ambapo Halmashauri ya

Madaba imepokea walimu wa ajira mpya 109 na ujenzi wa nyumba za walimu 17. Ujenzi wa nyumba hizi umekamilika na zinatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali wa kupunguza changamoto ya upungufu wa walimu ni kuendelea kuajiri walimu na kuwapangia katika halmashauri zote ikiwemo Halmashauri ya Madaba, sambamba na kuendelea na ujenzi wa nyumba za walimu kwa awamu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Omary Marcus Msigwa, swali la nyongeza.

**MHE. OMARY M. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Je, ni lini Serikali itajenga nyumba za walimu katika Shule ya Msingi Lipupuma na Magingo ambazo hazina nyumba za walimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Je, ni lini Serikali itapeleka walimu wa kike katika Shule za Msingi Ifinga, Ndelenyuma, Gadinda ambazo zina mwalimu mmoja mmoja wa kike?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Omary Msigwa, Mbunge wa Madaba amekuwa mfuatiliaji mzuri sana wa maslahi ya sekta ya elimu katika Jimbo la Madaba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali yetu ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kuweka kipaumbele cha hali ya juu katika kuiboresha sekta ya elimu, kuajiri walimu, kujenga nyumba za walimu na ndiyo maana katika kipindi cha miaka mitano iliyopita Halmashauri ya Madaba pia imepata walimu kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunafahamu hizo shule mbili alizozitaja zinahitaji nyumba za walimu katika Halmashauri ya Madaba. Tunazo jumla ya nyumba 156 kati ya nyumba 404 ambazo zinahitajika. Mpango wa Serikali katika kila mwaka wa bajeti ni kuendelea kutenga fedha kuhakikisha nyumba ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja katika shule hizo, pia zinapata nyumba za walimu pamoja na kupeleka walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuhusu walimu wa kike katika shule hizo; tunafahamu umuhimu wa walimu wa jinsi zote katika shule zetu, na tutaendelea kuwapeleka walimu wa jinsia zote katika shule zetu, lakini zipo shule na hususan za watoto wa kike ambazo mara nyingine tunahitaji kuwa na angalau walimu wa kike kwa ajili ya kuwasaidia kwenye masuala mahususi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa ajira zinazofuata tutaendelea kuweka kipaumbele kwenye shule hizo ili ikiwezekana tupate walimu wa kike kwa ajili ya kutimiza majukumu yao katika shule hizo.

**MWENYEKITI:** Nilikuona, Mheshimiwa Zuberi Mfaume.

**MHE. ZUBERI Y. MFAUME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali la nyongeza. Ni lini sasa Serikali itaanza kujenga nyumba za walimu katika maeneo ya milimani katika Jimbo la Morogoro Kusini ambako kuna shida kubwa sana ya makazi ya walimu?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna shule ambazo ziko katika maeneo magumu kijiografia na ambako mara nyingi hakuna nyumba za wakazi wa maeneo hayo ambazo zinatosheleza mahitaji ya walimu kupanga na kuishi ili kutoa huduma ya elimu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini kwamba, Serikali katika ujenzi wa nyumba za walimu hizi 3,588 ambazo zimeendelea kujengwa, kipaumbele kikubwa zaidi kimepelekwa kwenye maeneo yale ambayo ni magumu kufikika hususan vijijini na maeneo ambayo yana hali ngumu za kijiografia ili kuwawezesha walimu katika maeneo hayo kupata mahali pa kuishi na kutekeleza vizuri majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie tu kwamba katika shule hizo, tutoa kipaumbele kwa kadiri ya bajeti inavyopatikana ili kujenga nyumba za walimu maeneo hayo.

**MWENYEKITI:** Ninakuona, Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Katika Jimbo la Tarime Vijijini Shule ya Sekondari Inchugu ni miezi sita sasa hawana Mwalimu wa Kiingereza na kuna *O Level* na *A Level.* Ningeomba Mheshimiwa Naibu Waziri aniambie ni lini watafanya msawazo kwa jambo la kidharura ili watoto wale waendelee kufundishwa na kukumbuka kwamba Lugha ya Kiingereza ni lugha ya kufundishia katika masomo ya sekondari?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kumwelekeza Katibu Tawala Mkoa wa Mara kwa hali ya udharura kufanya msawazo wa ndani, ndani ya mkoa kuhakikisha tunapata Mwalimu wa Kiingereza kwa kipindi hiki cha mpito wakati Serikali Kuu ikifanya utaratibu wa kuhamishia walimu wa Kiingereza au wakati wa ajira nyingine ili kuhakikisha kwamba watoto wetu hawakosi masomo ya Kiingereza katika shule hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona, Mheshimiwa Halamga.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutujengea Shule ya Sekondari katika Kata ya Ishponga, kwani hatukuwahi kuwa na shule ya sekondari katika eneo hili. Je, ni lini sasa Wizara itatujengea nyumba ya walimu ili tuendelee kufurahia mema ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nipokee pongezi nyingi za Mheshimiwa Halamga kwa Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ni kweli na hakika kwamba Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana ya ujenzi wa shule za msingi, sekondari, kidato cha tano na sita, na kazi hii inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba safari ni hatua, tumejenga shule, na watoto wetu wameanza kusoma. Sasa hatua zinazofuata kwenye bajeti nyingine, nikuhakikishie kwamba tutaweka kipaumbele kuhakikisha kwamba tunajenga nyumba za walimu ili walimu wetu waishi katika mazingira bora na kutoa huduma ya elimu vizuri zaidi.

**MWENYEKITI:** Ninakuona, Mheshimiwa Alan Mvano.

**MHE. ALAN T. MVANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada nzuri za Serikali, zipo shule za sekondari ambazo zilijengwa, na yapo maeneo ambayo hakuna kabisa nyumba za kupanga katika Wilaya ya Kakonko. Hi ni katika shule za sekondari tatu, ninazitaja: Shule ya Sekondari ya Bukirilo, Shule ya Sekondari Ruhuru na Shule ya Sekondari ya Rutenga. Katika maeneo hayo, hakuna nyumba za kupanga kabisa. Ni lini Serikali itatusaidia kujenga nyumba za watumishi?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliweka mpango mahususi kabisa na ikaanda ramani au michoro ya nyumba za walimu, *three in one,* kuna nyumba za *two in one,* na nyumba zile zimekuwa zikijengwa kwa ushirikiano kati ya Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo ningependa kulisisitiza hapa ni kwamba Halmashauri ya Kakonko angalau kwa kuanza kupitia mapato yao ya ndani, waanze na hatua za awali za ujenzi wa nyumba za *two in one* au *three in one*. Pia Serikali Kuu imeendelea kuweka mpango wa kuhakikisha shule ambazo ziko katika mazingira magumu ambayo walimu hawawezi kupata nyumba za kupanga, tunatenga bajeti kwa awamu na kujenga nyumba katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mvano kwamba tutatoa kipaumbele kwa Halmashauri ya Kakonko, na pia halmashauri kupitia Baraza la Madiwani tupange kuanza kujenga nyumba hizi kwa awamu wakati Serikali Kuu ikiandaa taratibu za bajeti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nuru Issa Kashakari.

**MHE. NURU I. KASHAKARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Uvinza ni kati ya Wilaya ambazo zina jiografia ngumu na tuna shule za sekondari kama tano; Kata ya Kalya, Buhingu, Sunuka, na Sigunga. Kata ya Sunuka ndiyo ambayo haina walimu kabisa. Ukiangalia shule ya sekondari unakuta ina walimu watatu au wanne au watano. Je, ni lini Serikali itapeleka walimu katika maeneo haya?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Nuru, Mbunge wa Uvinza kwanza hakuna shule ambayo haina walimu kabisa kama ambavyo mwenyewe amerejea kwamba ina walimu wachache, lakini nimhakikishie tu

kwamba katika ajira ambazo zimeendelea kufanyika ikiwemo ajira zile za walimu 7,000 katika siku 100 za kwanza za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Wilaya ya Uvinza ilipata walimu. Tunajua hawatoshelezi, lakini tutaendelea kuleta walimu, na Uvinza ni moja ya Halmashauri zenye kipaumbele cha hali ya juu kupelekewa watumishi wa sekta ya elimu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tunaendelea. Nimwite sasa Mheshimiwa Fagason Aron Nkingwa, Mbunge wa Mbogwe, aulize swali lake.

Na. 348

**Ujenzi wa Barabara ya Ikunguigaze-Kiseke**

**MHE. FAGASON A. NKINGWA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Ikunguigaze hadi Kiseke kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Fagason Aron Nkingwa, Mbunge wa Jimbo la Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Ikunguigaze – Kiseke ipo ndani ya barabara ya Lulembela – Kiseke – Isevya yenye urefu wa kilometa 16.8 ambayo ipo katika utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania chini ya Programu ya Uboreshaji wa Barabara za Vijijini na Ufunguaji wa Fursa za kiuchumi na Kijamii *(RISE)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Ikunguigaze – Kiseke yenye urefu wa kilometa 16.8 ni sehemu ya uboreshaji wa barabara za vijijini zenye urefu wa kilometa 34 zilizosalia katika awamu ya pili ya uboreshaji wa barabara kwa kiwango cha lami. Barabara hiyo inatarajiwa kuanza kujengwa mara baada ya

kupata fedha za nyongeza kutoka benki ya Dunia ambapo kwa sasa maombi yamewasilishwa Tume ya Taifa ya Mipango kwa ajili ya kupata kibali ili kuwasilisha Benki ya Dunia, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nkingwa, swali la nyongeza.

**MHE. FAGASON A. NKINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini ninapenda niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa barabara hii ni muhimu sana kwenye Jimbo langu la Mbogwe, na kwa kuwa inaenda kufaidisha kata tatu ikiwemo Kata ya Lulembela, Ikunguigazi na Isebya, je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kujenga barabara hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa tunajua barabara zetu kwa 90% zimeharibika, lakini ninayo barabara ambayo iko Kata ya Masubwe inaenda mpaka Iponya, ni lini sasa Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kutengeneza barabara hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Nkingwa, Mbunge wa Jimbo la Mbogwe, amefuatilia mara kadhaa kuhusiana na barabara hii. Ninaomba nimhakikishie tu kwamba, kwanza Serikali ilishafika hatua nzuri sana ya kuanza ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usanifu umekamilika hatua zote za awali zimekamilika. Hatua ambayo Serikali sasa tunaendeleo nayo ni majadiliano na utaratibu wa kifedha na Benki ya Dunia kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Ujenzi utaanza mara tu baada Serikali yetu ya Tanzania na Benki ya Dunia kufikia hatua za kifedha na kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi itaanza mapema iwezekanavyo baada ya taratibu hizi kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tunafahamu kwamba ziko barabara nyingi ambazo zimeathiriwa na mvua mwaka huu ikiwemo Barabara ya Masumbwe – Iponya - Nyashimba ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja. Barabara hizi zote zilizoathirika Serikali imeshachukua taarifa zote na gharama zinazohitajika kwa ajili ya marekebisho. Mpaka wiki iliyopita ilikuwa takribani shilingi 300,000,000,000 zinahitajika kwa ajili ya marekebisho ya barabara hizi kote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali inaendelea na taratibu za kibajeti, na baada ya hali ya hewa kukaa sawa, basi tutaona namna ambavyo tutaanza kupeleka fedha kwa awamu kwa ajili ya marekebisho ya barabara hizi ikiwemo Barabara ya Masumbwe - Iponya na Nyashimba.

**MWENYEKITI:** Nilikuona, Mheshimiwa Edifonsi Kanoni.

**MHE. EDIFONSI J. KANONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Rukwa, Jimbo la Kalambo katika Kata ya Samazi kuna barabara ambayo inatoka ziwani kuja Makao Makuu ya Wilaya kilometa 22. Hii barabara haijakarabatiwa kwa zaidi ya miaka 13 na changamoto ni kubwa, wananchi wanafuata mahitaji, lakini basi kutoka pale Kijijini Samazi kuja wilayani inatumia saa mbili na nusu kwa kilometa 22...

**MWENYEKITI:** Swali lako.

**MHE. EDIFONSI J. KANONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini sasa Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kukarabati barabara hii ambayo ni muhimu sana kwa wananchi wa Samazi na katika Kata na Wilaya ya Kalambo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ya Kata ya Samazi katika Jimbo la Kalambo Mheshimiwa Kanoni ameifuatilia mara kadhaa, na bahati nzuri Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Rukwa pamoja na Meneja wa *TARURA* wa Wilaya ya Kalambo wameiwasilisha tayari katika orodha ya barabara ambazo zinahitaji bajeti ya dharura kwa ajili ya matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itahakikisha inapeleka fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya ukosefu wa barabara ya lami inaikumba Kata ya Azimio, Jimbo la Temeke. Je, Serikali lini itajenga barabara ya lami kutoka Mnyimati - Mashine ya Maji mpaka *BOA Bank*?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Jimbo la Temeke ni moja ya halmashauri tano za Mkoa wa Dar es Salaam ambazo zina huduma ya miradi ya barabara ya *DMDP II*, lakini pia na miradi ya barabara kupitia bajeti ya kawaida ya *TARURA* na dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba barabara ambayo ameitaja na barabara nyingine, Serikali itaendelea kuzifanyia tathmini na kuona uwezekano wa kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya kuzijenga kwa kiwango cha changarawe na kwa kiwango cha lami kwa kadiri ambavyo mipango ya kibajeti itakuwa inaendelea kuwa.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Agnesta Lambert, atafuatia Mheshimiwa Chaurembo. Ninaona Wabunge wa Dar es Salaam mmekazana kweli kwenye hili.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kuniona ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mara ya tatu leo ninaulizia suala la barabara inayotoka Segerea Kwa Bibi kuelekea Zahanati ya Segerea, barabara ambayo imekuwa ni mbovu kwa muda mrefu, na hivi sasa barabara ile imefungwa na Naibu Waziri alitoa maelekezo ya dharura iweze kufanyiwa ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo ya Naibu Waziri hayajafanyiwa kazi. Ningependa kufahamu, nini kauli ya Serikali kwa sababu wananchi wanashindwa kupata huduma kwa sababu ya uharibifu wa barabara? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze dada yangu Mheshimiwa Agnesta Lambert, pia nimpongeze sana Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Ilala ndugu yangu Mpogolo na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku mbili, tatu Mheshimiwa Mbunge aliuliza kuhusiana na changamoto ya Barabara ya Tabata Bima na niliona Mheshimiwa *DC* na Mkurugenzi na Timu ya *TARURA* wote wamehamia *site* na kazi inaendelea. Kwa hiyo, hii ni dalili kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita ni Serikali sikivu ambayo inanena na kutenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hata hiyo barabara ya Segerea kwenda zahanati ni kwa sababu tu ya hali ya hewa, na Serikali inajipanga, kwa sababu kimsingi siyo rahisi sana kufanya matengenezo kwenye barabara ambazo zimejaa maji au

ambazo bado mvua inaendelea kunyesha, kwa sababu tunakuwa tunapoteza zile fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunasubiri hali ya hewa ikae vizuri, na baada ya hapo, tutahakikisha kwa hali ya kidharura tunaenda kufanya matengenezo ya barabara hizo.

**MWENYEKITI:** Nimemwita Mheshimiwa Chaurembo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Mzambarauni – Mikoroshini – Sako Mwisho mpaka Kwa Mpalange ni kiungo muhimu cha kuondoa msongamano katika Barabara Kuu ya Kilwa na barabara hii ipo chini ya Mradi wa *DMDP*. Ni lini ujenzi wa barabara hii utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba barabara hiyo ya Mzamarauni – Mikoroshini – Kwa Mpalange ni muhimu sana na tayari imeingizwa kwenye Mpango wa *DMDP II*. Wiki moja iliyopita tumekaa na Wataalamu wetu wa *DMDP*, Dar es Salaam, na tumekubaliana kwamba, baada ya hali ya hewa kukaa sawa, iko miradi ambayo iko katika hatua za utangazaji wa zabuni na iko ambayo wakandarasi wamepatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Serikali kusimamia kuhakikisha kwamba barabara hizo zinajengwa. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Jafari Chaurembo kwamba, barabara hiyo ni kipaumbele cha Serikali.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Ninamwita sasa Mheshimiwa Silvery Luboja Salvatory, Mbunge wa Misungwi, aulize swali lake.

Na. 349

**Kuajiri Watumishi wa Afya, Misungwi**

**MHE. SILVERY L. SALVATORY** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuajiri Watumishi wa Afya Misungwi kwa kuwa, kuna upungufu wa asilimia 60?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Silvery Luboja Salvatory, Mbunge wa Jimbo la Misungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi ina mahitaji ya watumishi wa kada za afya 1,340 waliopo ni 645, sawa na 48%, na upungufu ni watumishi 695 sawa na 52%. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 hadi mwaka 2024/2025 jumla ya watumishi 179 wamepelekwa katika Halmashauri ya Misungwi. Aidha, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imeajiri watumishi 5,000 wa kada za afya na kuwapanga katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika siku 100 za kwanza za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi imepangiwa watumishi 56. Serikali itaendelea kutenga bajeti na kuajiri wataalam wa kada mbalimbali za afya na kuwapanga katika halmashauri zenye upungufu kote nchini, ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Silvery Salvatory.

**MHE. SILVERY L. SALVATORY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwanza,

ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Pamoja na juhudi ambazo Serikali imekuwa ikizifanya katika kuajiri watumishi wa umma, je, ni lini Serikali itahakikisha watumishi wanapatikana ndani ya kipindi kifupi ili kuendelea kupunguza vifo vya mama na mtoto, pamoja na wagonjwa wengine wa dharura?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Je, Serikali haioni kuna haja ya kuwahamisha watumishi angalau 150 kutoka sehemu nyingine na kuwapeleka Wilaya yetu ya Misungwi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele cha hali ya juu kwa kuhakikisha inaajiri watumishi wa sekta ya afya ili kuboresha huduma za afya na kupunguza vifo vya akinamama wajawazito na watoto wa umri wa chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imekuwa kinara katika Bara la Afrika kwa kupunguza kasi ya vifo vya akinamama wajawazito kutoka 556 kati ya vizazi hai 100,000 mpaka 103 kati ya vizazi hai 100,000. Haya ni matunda ya watumishi na vituo vya afya na vifaatiba kuendelea kuimarishwa katika maeneo yetu. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Luboja kwamba, tutahakikisha kila kibali cha ajira kinapojitokeza, tunapeleka watumishi katika Jimbo la Misungwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Tunafahamu, ni kwamba, Serikali imeendelea kuhakikisha inafanya msawazo wa ndani wa watumishi na ni kazi ya Makatibu Tawala wa Mikoa. Ikiwa kuna halmashauri ndani ya mkoa ina upungufu mkubwa, na kuna halmashauri ambayo ina angalau watumishi wengi, tunafanya msawazo wa ndani wa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninatumia nafasi hii kumkumbusha na kumsisitiza Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza kufanya msawazo wa ndani wakati Serikali inaendelea na taratibu nyingine za ajira na uhamisho kufuatia upungufu wa maeneo mbalimbali kote nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdalla Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Kituo cha Afya Nyundo kimekamilika zaidi ya miezi sita iliyopita, lakini hakijafunguliwa kwa sababu ya uhaba wa watumishi. Hata hivyo, ninaishukuru Serikali kwa sababu, hivi karibuni tumepata watumishi zaidi ya 60, wamepangwa Halmashauri ya Mji wa Nanyamba. Je, ni nini Kauli ya Serikali kuhusu ufunguzi wa kituo hiki kipya cha nyundo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kauli ya Serikali ni kwamba, vituo vyote vya afya vilivyokamilika ni wajibu wa halmashauri na Mkurugenzi wa Halmashauri husika kuhakikisha vinafunguliwa na vinaanza kutoa huduma. Viko vituo ambavyo vina upungufu wa vifaa vichache, kama mabenchi, viti na choo cha *OPD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakurugenzi wasisubiri fedha za Serikali Kuu, watumie mapato ya ndani kukamilisha matengenezo madogo madogo ili kuhakikisha kwamba vituo vinaanza kutoa huduma. Kwa hiyo, kwa muktadha huu, ninamwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Nanyamba ndani ya wiki mbili wahakikishe kwamba, kituo hicho cha afya kimefunguliwa na wananchi wanaanza kupewa huduma kwa sababu, Serikali imepeleka watumishi wa sekta ya afya zaidi ya 60, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge wa jimbo hilo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuna wachangiaji wengi sana leo, Maliasili na Utalii. Kwa hiyo, tutakwenda haraka kidogo kwenye maswali.

Mheshimiwa Naibu Waziri, ninakushukuru sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunakwenda Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana, ninamwita Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 350

**Ushirikiano wa *SIDO* na *VETA* kwa Vijana**

**MHE. BONNAH L. KAMOLI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kushirikiana na Taasisi kama *SIDO* na *VETA,* ili kuwajengea vijana uwezo wa kujiajiri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe majibu kwa Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mbunge wa Viti Maalum: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuratibu na kuimarisha programu mbalimbali za kuwawezesha vijana kiuchumi kupitia ushirikiano na Taasisi kama *VETA* na *SIDO*. Kupitia *VETA,* Serikali inaendesha programu za utambuzi na urasimishaji wa ujuzi, Programu ya *Integrated Training for Entrepreneurship Programme,* pamoja na Programu ya Wajibika *Scholarship* kwa kushirikiana na *NBC,* inatoa mafunzo ya stadi mbalimbali ikiwemo umeme, mabomba na ushonaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kupitia *SIDO,* Serikali imeendelea kutoa mafunzo ya ujasiriamali na kuwaandaa wakufunzi wa elimu hiyo, sambamba na kuwawezesha vijana kufikia fursa za mikopo yenye masharti nafuu inayotolewa na Serikali, pamoja na wadau wa maendeleo, ili waweze kujiajiri na kuajiri wengine kupitia shughuli za kiuchumi, ikiwemo biashara na viwanda vidogo vidogo. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bonnah Kamoli, swali la nyongeza.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Mheshimiwa Waziri, wanafunzi ambao wanapata ufaulu hafifu kidato cha sita, pamoja na kidato cha nne ni wengi. Je, kwa nini Serikali

isiwaruhusu hawa wanafunzi kwenda nyumbani mpaka watakapopata mafunzo stadi ambayo mnayasema?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kutokana na takwimu ambayo ameiongea Mheshimiwa Waziri, vijana walio wengi bado wako mtaani na hawana ujuzi wowote. Je, kwa nini Serikali isiongeze hawa vijana ikaendelea kuwafundisha, ili tukapata vijana ambao wana uelewa na ambao wana ufundi mitaani kwetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Bonnah Kamoli, ni kati ya Wabunge ambao katika jimbo lake ana programu nyingi sana za vijana, na ameendelea kuwahimiza vijana kupata ujuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa ujumla wake inathamini sana suala zima la ujuzi kwa vijana. Takwimu zinaonesha kwamba, tuna upungufu wa ujuzi kwa vijana kwa kiwango cha juu cha ujuzi. Matakwa yanataka katika sera tuwe na 12%, lakini sasa hivi tuna asilimia tatu nukta sita ya vijana wa ujuzi wa kiwango cha juu, na vijana wetu wengi wako katika ujuzi wa kiwango cha chini. Tunatakiwa tuwe na 54%, lakini tuna zaidi ya 72% ambao wana kiwango cha ujuzi wa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia programu mbalimbali ambazo zinafanywa, kama nilivyoeleza kwenye swali la msingi kupitia *SIDO, VETA* na pia, kupitia Wizara ya Elimu na uboreshaji wa mitaala tumeendelea kuhakikisha kwamba vijana wetu wanaendelea kusaidiwa kupata ujuzi wakiwa bado katika maeneo yao ya shule wanakoendelea na masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la pili la swali, ni kwamba, Serikali inaendesha programu maalum ya urasimishaji wa ujuzi kupitia Taasisi ya *VETA,* ambapo tunaangalia vijana ambao tayari wamejiajiri au wanafanya shughuli mbalimbali mtaani, ambao hawajaweza kutambuliwa rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu, mwezi uliopita, tayari zaidi ya vijana 14,400 nafasi zimetolewa kwa ajili ya kuhakikisha vijana hao wanaingizwa katika utaratibu maalumu, ambapo wanapewa mafunzo ya muda mfupi, na pia, wanaingizwa katika utaratibu rasmi, ili waweze kufaidika na fursa zinazotolewa na Serikali na sekta binafsi, ikiwemo mikopo ya kuwasaidia ambayo inajumuisha mafundi gereji, mafundi bomba na shughuli mbalimbali ambazo wanazifanya. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sylvia Sigula.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kumekuwa na taasisi binafsi ambazo zinatoa mafunzo kama hayo yanayotolewa na *VETA* na *SIDO*. Je, Serikali haioni haja sasa ya kuzitambua taasisi hizo na kufanya *assessment* ikijiridhisha kwamba, wahitimu wale wana-*qualify* waweze kupewa ithibati na Serikali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza tena Mheshimiwa Sigula Sylvia, ambaye pia amekuwa ni kinara kuhakikisha kwamba, masuala ya vijana yanapewa sauti. Serikali ina mpango huo na inaendelea kuufanya katika programu ambayo nimeizungumza kuhusu urasimishaji wa ujuzi, inayoshirikiana na sekta binafsi, ambao mara nyingi wanakuwa wanatoa mafunzo kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kwamba, wanakuwa na ujuzi unaotakiwa, kunakuwa na ukaguzi maalum ambao unasaidia kujua vile viwango ambavyo vimewekwa. Pia kama ambavyo dira yetu inaelekeza kwamba 70% ya mchango wa maendeleo tunaotarajia kufikia mwaka 2050 unatakiwa utokane na sekta binafsi, Serikali itaendelea kufanya kazi na sekta binafsi kwa ukaribu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbusha tu kwamba, katika ahadi 13 za Mheshimiwa Rais alizokuwa amezitoa, mojawapo alizungumzia juu ya mkakati maalum wa ushirikiano kati ya sekta binafsi, kwa maana ya viwanda, pamoja na Serikali katika kuhakikisha vijana wanapata ujuzi. Hadi sasa tuna kampuni na

viwanda zaidi ya 87 ambao wameingia mkataba na Serikali kuhakikisha kwamba, vijana wanapata ujuzi na wanarasimishwa. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakiri kwamba, *SIDO* na *VETA* zipo katika Mkoa wa Mtwara, lakini vijana wengi waliopo katika Mkoa wa Mtwara bado hawana ujuzi ambao wamejengewa katika taasisi hizo. Je, Serikali inafanya tathmini kwa kiasi gani kubaini changamoto ya vijana wengi waliopo katika Mkoa wa Mtwara kutopata ujuzi unaostahili kulingana na maeneo yao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Agnes Hokororo na ninampongeza kwa kuwasemea vijana wa Mkoa wa Mtwara. Miezi miwili iliyopita nilikuwa Mkoani Mtwara na nilipata nafasi ya kukaa na Meneja wa *SIDO* wa Mkoa wa Mtwara, wanayo programu maalum ya kuhakikisha kwamba, Vijana wa Mkoa wa Mtwara, kulingana na *database* ambayo tayari wameitengeneza, wanapatiwa mafunzo katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali kupitia Taasisi ya *SIDO,* imekuwa na utaratibu wa kujitathmini na kujua hasa ujuzi unaohitajika katika soko na kuwafikia wale ambao hawajaweza kufikiwa. Kwa hiyo, Mkoa wa Mtwara ni kati ya mikoa ambayo program hii inaendelea na itafanyika kwa ufanisi mkubwa.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Mndeme.

**MHE. CHRISTINA S. MNDEME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Serikali imekuwa na mpango mzuri wa kuwapatia vijana fursa mbalimbali ikiwemo mikopo na hususan vijana wa Mkoa wa Tabora, tunampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu

Hassan. Kwa kuwa, vijana wengi wamekuwa wakizifikia fursa hizi na ujuzi huu, lakini wengine bado hawajapata fursa ya kuzifikia, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha ubora wa bidhaa ambazo zinazalishwa na vijana hawa ambao wamepata ujuzi, pia wamepata mikopo na fursa mbalimbali kupitia *SIDO,* pamoja na *VETA* kwamba, bidhaa wanazozalisha zinakidhi soko la ushindani na ulimwengu wa sasa wa sayansi na teknolojia, na hususan vijana wa Mkoa wa Tabora?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mndeme. Serikali imekuwa inafanya juhudi kubwa sana kuhakikisha bidhaa za vijana zinapata ubora na ithibati katika maeneo mbalimbali, hasa kwa kuzingatia kwamba, kuna mikataba mbalimbali ya kikanda na Kimataifa, ambayo tumekuwa tukiingia kama nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudi hizo, Serikali imeandaa programu maalum ya kuhakikisha kwamba, kupitia *SIDO* kwa ushirikiano na *TBS,* inatembelea vijana katika maeneo mbalimbali na kuhakikisha inawapa ushauri unaotakiwa. Sasa Serikali imeandaa programu maalumu kwa kutoa na kuandaa wakufunzi 2,000 nchi nzima, ambao wanaganywa katika mikoa na kanda mbalimbali kuhakikisha wanawatembelea vijana hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku tano zilizopita Mkoa wa Iringa wamefanya ziara katika viwanda vinavyozalisha unga zaidi ya 20 kuhakikisha kwamba, wanapewa ushauri, lakini pia, kuwasaidia kuweza kukidhi vigezo, ili bidhaa zao ziwe na ubora. Tutaendelea kuhakikisha kwamba tunakuwa karibu na vijana, na kupitia taasisi ya *SIDO* pamoja na *TBS,* tutahakikisha kwamba vijana hao wanatoa ushauri unaotakiwa na kupata ithibati ya ubora wao. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Joel Nanauka kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Nishati. Ninamwita sasa Mheshimiwa Adonis Alfred Bitegeko, Mbunge wa Muleba Kaskazini, aulize swali lake.

Na. 351

**Kukatika kwa Umeme Mara kwa Mara Wilaya ya Muleba**

**MHE. ADONIS A. BITEGEKO** aliuliza: -

Je, upi mpango wa kutatua tatizo la kukatika kwa umeme Wilaya ya Muleba linalosababishwa na miti kugusa nyaya za umeme?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa niaba ya Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Adonis Alfred Bitegeko, Mbunge wa Muleba Kaskazini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Muleba, Serikali kupitia *TANESCO,* imeendelea kuimarisha ratiba ya ukaguzi wa njia za umeme pamoja na zoezi la kupunguza na kuondoa miti iliyo katika hatari ya kusababisha hitilafu na kukatika kwa umeme. Aidha, Serikali inaendelea kuboresha miundombinu ya usambazaji wa umeme kwa kutumia nyaya na vifaa vya kisasa, ikiwemo kuweka nguzo za zege kwa maeneo yote yasiyofikika kirahisi na yenye matindiga, ili kupunguza athari za changamoto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, pamoja na hatua hizo, Serikali inaendelea kutoa elimu kwa wananchi kwa kushirikiana na *TANESCO* kwa kutoa taarifa pale wanapoona miti au vihatarishi vingine vinavyoweza kuathiri huduma ya umeme katika maeneo yao. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bitegeko, swali la nyongeza.

**MHE. ADONIS A. BITEGEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Ninaomba kuuliza swali moja la nyongeza. Tatizo la kukatika umeme mara kwa mara kutokana na nyaya za umeme kuguswa na matawi ya miti limekuwa ni la miaka mingi sana katika Wilaya ya Muleba, limekuwa linaathiri sana shughuli za kiuchumi za wananchi pamoja na kusababisha kuungua kwa mali zao. Ninaomba kupata *commitment* ya Serikali. Je, ni lini itaweka nyaya za kisasa zenye *covered conductor,* ambazo ni imara zaidi kukabiliana na hili tatizo la kuguswa na miti?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa na ufuatiliaji mzuri kuhakikisha watu wa jimbo lake wanapata huduma bora ya nishati. Ninamhakikishia kwamba kwenye bajeti hii ambayo tumepitishiwa sisi Wizara ya Nishati, moja kati ya jambo kubwa tunalokwenda kulifanya ni *repair* ya miundobinu yote, hasa kwenye maeneo ya matindiga na ambayo yana changamoto za miundobinu ya kizamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaijua hiyo *concern* kwamba, kuna changamoto kubwa na wananchi wanapata hasara. Wizara ya Nishati tuna *commitment* kubwa ya kuhakikisha tunaelekea kule ambapo Mheshimiwa Rais anatamani watu wapate nishati bora ya uhakika na salama, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nimemwona Mheshimiwa Salum Khamis Salim.

**MHE. SALUM K. SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa. Kwa vile Tanzania ni mwanachama wa *Southern Africa Power Pool,* kwa nini Serikali isitumie fursa hiyo kuziunganisha *ZECO* na *TANESCO* katika miradi ya pamoja kuzalisha nishati mbadala, hasa ukizingatia na yeye ni *part,* badala ya kuishia kununua bidhaa ya mwisho? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Swali ni zuri. Mheshimiwa Naibu Waziri ninadhani wewe ni bingwa, unaweza ukalijibu, lakini Mheshimiwa

Mbunge angelileta kama swali la linalojitegemea, ingekuwa nzuri zaidi, angelifanyia utafiti.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** *Okay.*

**MWENYEKITI:** Ninadhani ulilete kama swali la msingi. Sawa, ninaona *gesture* yake, ni kwamba, ni bora lije kama swali linalojitegemea.

**MHE. SALUM K. SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia njema ya Serikali kupeleka umeme vijijini, Tarafa ya Kalema ni miongoni mwa vijiji vinavyopata shida ya kukatika umeme mara kwa mara kutokana na kuungua kwa nguzo na kuangukiwa nguzo za umeme na miti. Ni lini tatizo hili litatatuliwa ili wananchi waweze kupata umeme wa uhakika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Kakoso kwa ufuatiliaji wake wa karibu kuhakikisha wananchi wake wanapata nishati ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tunalifahamu tatizo au changamoto ya uchakavu wa miundombinu ambayo inapelekea umeme kukatika mara kwa mara. Kwa hiyo, tumetenga bajeti ambayo ilipitishwa katika bajeti ya Bunge hili Tukufu, kuhakikisha kwamba inaenda kwenye maeneo yote ambayo miundombinu ni chakavu au miundombinu inapelekea umeme kukatika mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ni nyingi, wakati mwingine ni *low voltage*, wakati mwingine miundombinu ni chakavu, wakati mwingine ni umeme mdogo kutokana na watumiaji kuwa wengi. Tunamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba

changamoto hii tutakwenda kuitatua mara tu baada ya kumaliza Bunge hili la bajeti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, bado tupo Wizara ya Nishati. Nimwite sasa Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, aulize swali lake.

Na. 352

**Kupeleka Umeme kwenye Maeneo ya Wachimbaji Wadogo**

**MHE. MASACHE N. KASAKA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme kwenye maeneo ya Wachimbaji Wadogo ili kusaidia shughuli zao?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* inaendelea na utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme katika maeneo ya wachimbaji wadogo wa madini, mashamba ya kilimo na viwanda katika Mikoa yote nchini ambapo mpango ulipo kwa sasa ni kufikisha umeme katika maeneo 308 ya wachimbaji wadogo ifikapo Juni, 2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Mei, 2026, jumla ya migodi 289 ya wachimbaji wadogo imepatiwa umeme ikiwemo migodi 18 katika Jimbo la Lupa Wilayani Chunya, pamoja na migodi ya Singa, Chokaa Moja, Mapogoro, Godima Beston, Matfra, Mwambe Mlimanjiwa, Mamboleo, Mbiwe na Mwaoga Mbili. Aidha, Serikali kupitia *REA* itaendelea kupeleka umeme katika migodi midogo iliyosalia ili kuwawezesha wachimbaji wadogo kuunganisha umeme katika migodi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kasaka, swali la nyongeza.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niishukuru Serikali kwa majibu yake, lakini kutokana na majibu ya Serikali tunaona hapa ndani ya Wilaya ya Chunya ni migodi 18 tu ya wachimbaji wadogo ndiyo ambayo imeweza kufikishiwa umeme. Japo ni kiasi kidogo sana kulinganisha na uchimbaji na uzalishaji wa madini ya dhahabu unaopatikana ndani ya Wilaya ya Chunya, kasi ya upelekaji umeme ni ndogo sana. Je, ni lini sasa Serikali itakuja na mpango mkakati kuhakikisha kwamba inapeleka umeme maeneo mengi ya wachimbaji wadogo wa Wilaya ya Chunya na Watanzania wote kwa ujumla ili kuongeza uzalishaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Wilaya ya Chunya inapokea umeme mdogo na umeme wenyewe siyo wa uhakika, unakatika mara kwa mara hali inayopelekea wachimbaji wetu kushindwa kutumia mitambo na mashine zao katika hali ya uzalishaji. Je, ni upi mpango wa Serikali wa muda mfupi wa kuhakikisha kwamba inaenda kupeleka umeme wa uhakika ambao haukatikikatiki kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo wakati tunasubiri ule mradi mkubwa ambao utaenda kujengwa ndani ya Wilaya ya Chunya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninampongeza Mheshimiwa Mbunge, amekuwa anafuatilia kwa karibu sana kuhakikisha wachimbaji wake wanapunguza gharama za uzalishaji wa dhahabu ili waweze kupata *profit margin* nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote kwa faida ya Bunge hili Tukufu, kwa mara ya kwanza tangu historia ya nchi hii iumbwe, Serikali katika bajeti hii imetenga zaidi ya shilingi bilioni 20 kwa ajili ya kupeleka umeme katika migodi midogo midogo. Hili ni jambo la kupongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge, kwa *commitment* kubwa hiyo, kwa

sababu tumeona sasa nishati ni kichocheo kikubwa cha uchumi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwa bajeti hii tuliyoitenga kwa mwaka huu, tunakwenda kuvunja historia kwa kupeleka umeme kwenye migodi mingi midogo midogo ili kuwasaidia wachimbaji waweze kuchimba kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali la pili, Mheshimiwa Mbunge alikuwepo Bunge lililopita, na amefuatilia sana kuhusu ujenzi wa *substation* katika Jimbo lake. Hiyo ilikuwa ni nia ya dhati ya Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba tunapata umeme mwingi wa uhakika kwa ajili ya kusukuma mitambo na mashine mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Lupa halitumii umeme kwa ajili ya matumizi ya nyumbani peke yake kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, wanao wachimbaji wadogo wadogo, wameanzisha viwanda ni lazima tuwaletee umeme mwingi na wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie kwamba fedha zimeshatengwa, mkandarasi ameshapatikana, tunakwenda kujenga *substation* pale kwa ajili ya kuhakikisha kwamba umeme haukatiki, na wanapata umeme mwingi kwa ajili ya uzalishaji. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Mkoa wa Shinyanga ni miongoni mwa mikoa ambayo ina wachimbaji wa madini wengi, hususan katika Halmashauri ya Msalala pamoja na Shinyanga, kuna machimbo kama Nyamishiga na Ndolwa ambapo wachimbaji wadogo hawajaunganishiwa umeme. Ni lini Serikali itawaunganishia umeme wachimbaji hao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Mnzava kwa kufuatilia kuhusiana na maslahi ya wachimbaji wadogo. Ni Mbunge

mwenzangu tunatoka wote Mkoa wa Shinyanga, kwa kweli ninamwona anavyowapigania wachimbaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoka kufanya ziara Wilaya ya Kahama na tumeshazungumza na Mameneja wote watatu wa Wilaya ya Kahama. *Commitment* yetu mpaka sasa hivi, tumeshajua bajeti ya migodi midogo ambayo haijapelekewa umeme, na Mungu akitujalia mara baada ya kumaliza Bunge hili, tutatenga fedha kwa hatua ili kuhakikisha wachimbaji wa Wilaya hiyo ya Kahama wanapata umeme, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, bado tupo Wizara ya Nishati. Nimwite Mheshimiwa Asha Salum Motto, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 353

**Idadi ya Vituo vya Gesi Nchini**

**MHE. ASHA S. MOTTO** aliuliza: -

Je, Serikali ina Vituo vingapi vya Gesi nchini na vipo katika Mikoa gani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Salum Motto, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC)* kwa kushirikiana na sekta binafsi wamefanikiwa kujenga na kuendesha vituo 18 vya gesi *(CNG)* ambapo vituo 15 vipo Mkoa wa Dar es Salaam. Kuna kituo kimoja kipo Mkoa wa Mtwara na kituo kimoja kipo Mkoa wa Pwani na kituo kimoja kipo katika Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo hivyo ninapenda nivitaje, ni *Tembo Energies Limited* iliyopo *Mandela Road* Dar es Salaam, *Taqa Dalbit Tanzania Limited* ipo *Kipawa – Airport*, Rafiki *CNG*

*Station and Conversion Centers Limited* ipo *Mandela Road; Tanzania Petroleum Development Corporation* ipo *Sam Nujoma Road* pale Ubungo, *Victoria Service Station* ipo *Nyerere Road*, *Puma Energy* ipo *Bagamoyo Road*, *Taqa Dalbit Tanzania Limited Sam Nujoma Road* – Ubungo, *Puma Energy Limited IPTL* Tegeta, *Puma Energy Limited Mbezi Beach - Bagamoyo Road*, *Anric Gas Technology Co. Limited* ipo *TAZARA*, *Nat-Energy Limited* ipo Kigamboni, *Dangote Cement Limited* ipo Mtwara, *Dangote Cement Limited* nyingine ipo Mkuranga, *Tan Health Limited* ipo *Africana – Mbezi Beach*, *Pan African Energy Limited* ipo Ubungo, *Tanzania State Goba; BQ -Goba* na *Ruvuma Coal CNG* ipo Goba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Motto.

**MHE. ASHA S. MOTTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri yenye kutia moyo na yenye kutoa ufahamu kwa wananchi wa Tanzania pamoja na Mkoa wa Mtwara. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mkoa wa Mtwara una kituo kimoja tu cha *CNG* kwa maana ya *Dangote cement,* na kituo hiki ni kwa ajili ya matumizi yake binafsi, je, ni lini Serikali itajenga vituo vya gesi vya *CNG* kwa ajili ya magari ya wananchi wa Mkoa wa Mtwara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Mkoa wa Mtwara una vituo vitano vya gesi kule Mnazi Bay. Kwa kuwa, Mkoa huu una kaya 491,811, hadi sasa ni kaya 428 tu ndizo zilizoweza kuunganishwa na gesi hii, je, ni lini Serikali itaunganisha gesi kwenye kaya hizi zilizosalia kwa kuwa uhitaji ni mkubwa sana na huu Mkoa ni wa kimkakati? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Asha kwa kufuatilia na ni kwa sababu anafahamu kwamba matumizi ya *CNG* au gesi asilia

kwenye magari yanapunguza zaidi ya 40% ya gharama ya matumizi ya mafuta ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali inayo dhamira ya dhati kuhakikisha kwamba nchi yetu inanufaika na rasilimali ilizonazo, na kwa sababu hiyo, pamoja na kwamba kulikuwa kuna kituo kimoja Mtwara, kwenye bajeti hii iliyopita tumeongeza kituo kingine. Hiyo ni kutambua mchango mkubwa wa wananchi wa Mtwara ambao wao gesi inatoka katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali la pili, ni kweli kabisa nyumba 425 ambazo zilishaunganishwa katika Mkoa wa Mtwara ni chache, lakini kwa sasa hivi Serikali ina mpango na tumeshafanya utafiti, kwenye bomba lile ambalo wananchi tayari wameshaunganishwa pamoja na wananchi wa Mtwara, yapo maeneo ambayo tunaweza kuongeza kasi ya usambazaji. Utafiti umeshafanyika, *TPDC* na *REA* wanaenda kushirikiana kuongeza kwa wakazi zaidi ya 1,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua kasi ni ndogo na Serikali peke yake haiwezi, na ndiyo maana Mheshimiwa Rais ametusisitiza kualika sekta binafsi na sasa hivi *TPDC* imeshaingia mkataba na sekta binafsi zaidi ya 80 ambazo zitakwenda kuongeza kasi ya usambazaji wa *CNG* na kujenga vituo nchi nzima. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahya Mhata.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa amekiri kwamba kituo kilichopo Mtwara ni cha mtu binafsi Dangote, hakipo kwa ajili ya wananchi au wananchi wanaoishi katika Mkoa wa Mtwara, sasa ninaomba nimwulize swali moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Jimbo langu la Nanyumbu lipo kilometa 350 kutoka Mtwara na amezungumza hapa kwamba kuna mpango wa kujenga kituo kimoja cha *CNG* katika Mkoa wa Mtwara, je, anaonaje kituo hicho akakileta

katika Jimbo langu ili iwe rahisi kuwahudumia wananchi wote wa kule kusini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa swali zuri sana la Mheshimiwa Mhata. Mimi ninafahamu mikoa ya kusini; Lindi, Mtwara yote wanatakiwa kunufaika na upatikanaji wa gesi katika maeneo yao. Nimtoe wasiwasi Mheshimiwa, tusiwanyang'anye wananchi wa Mtwara tusije tukagombana nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wizara, tutakaa pamoja na Wananyumbu kupitia mwakilishi wao kuhakikisha kwamba na wao wananufaika kwa kujenga kituo cha *CNG*. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni zamu ya Wizara ya Maji, Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 354

**Kupeleka Maji katika Vijiji vya Tunduru**

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka maji katika Vijiji vya Mkalekawana, Msingili, Mkonda na Nambalapi katika Jimbo la Tunduru?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua changamoto ya huduma ya maji katika vijiji vya Mkalekawana, Msingili, Mkonda pamoja na Nambalapi vilivyopo Wilaya ya Tunduru Mkoani Ruvuma. Kwa sasa vijiji hivyo vinapata huduma ya maji inayotolewa kupitia miradi ya maji mbalimbali iliyojengwa na Serikali kwa nyakati tofauti kuanzia mwaka 1980 hadi 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya maji kwa vijiji hivyo ni wastani wa lita 259,675 kwa siku wakati uzalishaji wake ukiwa haukidhi mahitaji kutokana na uchakavu wa miundombinu iliyopo. Serikali imepanga kuboresha huduma ya maji kwa kukarabati miundombinu ya maji nchini hususan ile ya zamani ikiwemo ya vijiji vya Msingili, Mkonda na Nambalapi kwa kutenga bajeti kila mwaka na kutekeleza kadri fedha zinavyopatikana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chikambo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mfumo wa ukumbi huu ni kwamba kama una swali la nyongeza kwa maana ya swali la msingi, simama ili uonekane, ukikaa ninajua huna swali.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ambayo yametolewa na Naibu Waziri, kwanza ninaomba nisahihishe hicho Kijiji siyo Msingili, ni Msinjili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimwambie Mheshimiwa Waziri mbele yako kwamba, hivi vijiji ambavyo amesema vinapata maji kupitia njia nyingine, havijawahi kupata mradi wowote wa Serikali. Kama majibu haya amepewa kule Wilayani, basi watakuwa wamemwongopea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ibaki kwenye kumbukumbu kwamba vijiji vile havijawahi kupata maji. Vijiji vya Mkalekawana, Nambalapi, Msinjili na Mkonda havijawahi kupata mradi wowote wa Serikali. Swali langu lingine, nilitamani kujua, ni lini hivyo vijiji vitapatiwa maji, tofauti na majibu ambayo Waziri amepewa ambayo siyo sahihi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kaulimbiu ya Mama Samia ni kumtua ndoo mama kichwani. Katika Wilaya yetu ya Tunduru hususan Jimbo la Tunduru Kaskazini tuna vijiji 91. Ninafahamu vipo vijiji ambavyo mpaka leo havina maji na wakina mama wanapata shida ya maji. Ninatamani kujua ni nini mkakati wa Serikali wa kuvitambua vijiji ambavyo havina maji ili viweze kuingia kwenye bajeti zijazo vipatiwe maji? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Sikudhani Chikambo kwa kutambua kwamba kuna maeneo ambayo Serikali bado haijayafikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kusema jambo moja kwamba Serikali inapotekeleza miradi ya maji, inahusisha Serikali yenyewe, wadau na ndiyo maana tumefanya maboresho ya Sera yetu ya Maji ya Mwaka 2002 Toleo la 2025, kutoa mawanda mapana ya *private sector,* pia kushiriki katika kuhakikisha kwamba miradi ya maji inaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, tunao wadau wengi ambao wanaendelea kushirikiana na Serikali. Tunao *WaterAid*, kuna *PDF,* na wadau wengine. Katika maeneo ambapo Serikali bado haijafikisha miradi ya maji, kuna hawa wadau wamekuwa wakishirikiana vizuri sana na Serikali. Lengo letu ni kwamba kila eneo watu wapate huduma ya maji, haijalishi mradi huo umejengwa na Serikali ama umejengwa na mdau wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa zaidi ni kwamba Serikali imeboresha sana, imeweka mazingira rafiki, mahusiano ya kidiplomasia na ndiyo maana wadau hawa wanaona ni sehemu sahihi kuja kuhakikisha kwamba inasaidiana na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vijiji hivi, kwa vile Mkoa wa Ruvuma tunafahamu kwamba tunavyo vijiji 484 ambapo 350 vyote mpaka sasa vina huduma ya majisafi na salama, lakini tunavyo vijiji 134 ambavyo hivi sasa ndiyo tunaviingiza kwenye

mpango wa vijiji 1,575 ambapo tunaenda kutekeleza awamu kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu wa fedha tumepanga Mkoa wa Ruvuma tunaenda kuondoka na vijiji 26, mwaka ujao wa fedha tunaondoka na vijiji 26. Kwa hiyo, maana yake vijiji 134 kwa kipindi cha miaka mitano, vikiwemo vijiji ambavyo vipo Tunduru Kaskazini vitakuwa vimekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, kuhusiana na vijiji ambavyo Mheshimiwa Mbunge anadhani kwamba huduma yake haijaridhisha, nimtoe hofu kwa sababu tutatuma wataalam wetu kwenda kufanya *need assessment to establish gap* tuone kuna tatizo gani sehemu gani ili sasa tuweze kutenga bajeti ya kuziba hilo *gap* ambalo linaonekana kwamba bado lipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, na kwa bajeti hii ambayo wametupitishia Waheshimiwa Wabunge, tuwatoe hofu, tunaenda kusimama nao. Lengo letu ni kusimama na falsafa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kumtua mama ndoo kichwani kwa vitendo zaidi ili Watanzania wapate huduma ya majisafi na salama. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwanza ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara hii ya maji. Je, ni lini sasa atatembelea katika Wilaya ya Kilolo aje aone vijiji 42 pamoja na ule mradi aliousaini wa Ng'ang'ange uweze kutoa maji wananchi wa Kilolo waweze kupata majisafi na salama?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali dogo la Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu wa Ng'ang'ange tuliusaini mwaka 2024 kama ninakumbuka vizuri, na mradi huu ni kweli kabisa kumekuwepo na uhitaji mkubwa wa fedha ili mkandarasi aanze kuutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu, kabla sijamwahidi kwenda Kilolo kujionea hii huduma ya maji katika eneo lake, ninaelekeza Katibu Mkuu kwa niaba ya Waziri wa Maji aweze kuharakisha, kwa sababu tulikuwa tumeupanga kwenye vipaumbele, apeleke fedha, na Mkandarasi aendelee na utekelezaji wa mradi huu ili uweze kukamilika. Mimi nikienda pale nikakague maendeleo ya mradi na siyo kuanza kutafuta namna gani mradi uanze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, ninamwelekeza Katibu Mkuu aweze kuharakisha, kwa sababu tulikuwa tumepanga kwenye vipaumbele, apeleke fedha mkandarasi aendelee na utekelezaji wa mradi huu ili uweze kukamilika, ili nikienda pale nikakague maendeleo ya mradi na siyo kuanza kutafuta namna gani mradi uanze. Lengo ni kwamba watu wake wa Kilolo wapate huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kama Serikali tuko tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo tumeelekezwa na Mheshimiwa Rais.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, nimwite Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa, Mbunge wa Kibaha Vijijini, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Rashid Shangazi.

Na. 355

**Kukamilisha Ujenzi wa Vituo vya Polisi – Kibaha Vijijini**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI K.n.y. MHE. HAMOUD A. JUMAA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumalizia ujenzi na kuweka samani vituo vya Polisi katika Kata za Gwata, Soga na Kikongo – kibaha Vijijini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa, Mbunge wa Kibaha Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vituo vya Polisi vya Kata za Gwata, Soga, na Kikongo vinajengwa kwa kutumia nguvu za wananchi pamoja na mchango wa fedha ya mfuko wa jimbo. Vituo vya Gwata na Soga ujenzi wake umefikia hatua ya umaliziaji na kituo cha Kikongo ujenzi umefikia hatua ya *lintel*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa wataalamu toka Halmashauri ya Wilaya ya kibaha wanafanya tathmini ili kubaini gharama halisi ya kumalizia ujenzi wa vituo hivyo vya Polisi. Pindi zoezi hilo litakapokamilika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi itatenga fedha kutoka kwenye bajeti ya Serikali ili kumalizia ujenzi pamoja na ununuzi wa samani za ofisi kwa lengo la kuunga mkono jitihada za wananchi. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangazi, kwa niaba.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali, lakini wananchi hawa wa Kibaha Vijijini kwa kushirikiana na Mbunge kupitia mfuko wa jimbo na pia jitihada binafsi za Mheshimiwa Mbunge, wamefanya juhudi kubwa kufikisha haya majengo katika hatua hiyo iliyo sasa. Je, Serikali haioni kwamba sasa ina jukumu la kufanya jitihada za haraka ili yale malengo ambayo wananchi wameyakusudia yaweze kutimia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, wananchi wa Tarafa ya Mlalo, Jimbo la Mlalo wamejenga kituo kwa nguvu zao na kimefikia hatua za usafi. Ipo ahadi ya Serikali ya kuwapatia

shilingi milioni thelathini na tano kwa barua ambayo imeandikwa na *IGP* tarehe 8 Mei, 2025. Sasa ninataka kufahamu, je, Serikali haioni kwamba kuendelea kuchelewesha ahadi hii ya wananchi wa Tarafa ya Mlalo ni kukwamisha jitihada za wananchi na pia kukwamisha Ilani ya Chama cha Mapinduzi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Hamoud kwa swali lake la msingi, na pia swali la nyongeza lililoulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Shangazi. Nimpongeze kwanza kwa kujali hali ya usalama ya wananchi wake na kuhakikisha kwamba anaanza jitihada za awali kupitia wananchi pamoja na Mfuko wa Jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa pongezi hizo hizo, nitumie pia fursa hii kumpongeza na Mheshimiwa Shangazi kwa namna ambavyo amejitahidi naye pamoja na wananchi, kuanza kazi ya ujenzi wa kituo kule Mlalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa ruhusa yako nimpongeze sana Mheshimiwa Azza ambaye anatoka Jimbo la Itwangi naye kwa kazi kama hii pamoja na Mheshimiwa Kassim wa Jimbo la Mwanakwerekwe. Waheshimiwa hao na Waheshimiwa Wabunge wengine wamekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kuwa wanaunga mkono jitihada mbalimbali za Serikali za kuhakikishia wananchi ulinzi na usalama kwa kujenga miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la nyongeza la msingi, Serikali imeona umuhimu wa kuhakikisha kwamba vituo hivyo vinakamilika, ndiyo maana mara baada ya kupata taarifa hiyo ya ujenzi, imepeleka wataalamu wa halmashauri kwenda kukagua na kufanya tathmini wa kujua gharama halisi ili kusudi kuweza kumaliza ujenzi wa vituo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Kituo cha Polisi Mlalo kule Lushoto, nirudie tena kumpongeza Mheshimiwa Shangazi, siyo tu kwa Lushoto au jimboni kwake Mlalo, kwa Mkoa

mzima wa Tanga amekuwa akifuatilia kwa karibu na kuhimiza ikiwemo barua ambayo alimpatia aliyekuwa Mheshimiwa Waziri, na Mheshimiwa Waziri alinithibitishia kuwa kweli alipokea barua hiyo na amemfikishia *IGP* barua hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Shangazi kwamba, kazi ya kukamilisha Kituo cha Polisi Mlalo itafanyika kwa haraka iwezekanavyo, na hizo fedha zitapatikana kupitia Jeshi la Polisi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea, ninaona hakuna maswali ya nyongeza hapa. Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara. Nimwite sasa Mheshimiwa Grace Elias Mkoma, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 356

**Kuanzisha Kongani za Viwanda kwa Wilaya za Mkoa wa Singida**

**MHE. GRACE E. MKOMA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha kongani za viwanda kwa Wilaya za Mkoa wa Singida.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Londo.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara ninaomba sasa nijibu swali Na. 356 kutoka kwa Mheshimiwa Grace Elias Mkoma Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa sasa inatekeleza mkakati wa kuanzisha kongani za viwanda katika wilaya zote nchini. Hivyo, sasa hivi Serikali inaendelea kuandaa mwongozo wa usimamizi wa kongani za viwanda Kitaifa ambao utaelezea sifa za eneo kuitwa kongani, ukubwa wake na sifa nyinginezo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Waheshimiwa tuwe na utulivu kidogo, ukumbi wetu ni mdogo, kwa hiyo, ninaomba tuwe na utulivu. Ninaomba uendelee.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hivi sasa ipo kwenye mpango wa kuandaa muongozo wa usimamizi wa kongani za Kitaifa ambao utaelezea sifa za eneo kuitwa kongani, ukubwa wake na sifa ambazo zinaambatana nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika kutekeleza mkakati wa kuandaa ama kuanzisha kongani za viwanda katika wilaya zote, Singida ni sehemu ya mkakati wa Wizara ya Viwanda na Biashara na Serikali kuhakikisha kwamba tunakwenda kuanzisha kongani za viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Disemba, 2025, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imefanikiwa kuanzisha kongani 36 katika mikoa 16 nchini. Kwa hivi sasa katika Mkoa wa Singida tunaweza kuona kwamba Iramba wameandaa eneo la ukubwa zaidi ya ekari 150 na Manyoni ekari zaidi ya 500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada za kupata fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu katika maeneo haya, zinaendelea ili kuwezesha uanzishwaji wa kongani hizo. Ninaomba kutoa rai kwa Wakurugenzi wote, kwa kuwa hili ni agizo na ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba wanaandaa maeneo ya kongani na wanaijulisha Serikali kwa ajili ya kutambua maeneo hayo, kuyapima na kuyapanga kwa ajili ya kuwekea miundombinu na kutangaza kama sehemu ya vivutio kwa wawekezaji wetu. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Elias Mkoma, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE E. MKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa majibu ya Serikali, lakini nina maswali yangu mawili ya nyongeza:-

(a) Je, ni lini Serikali itakuja na mwongozo wa Kitaifa wa kusimamia kongani za viwanda kwenye kila wilaya?

(b) Je, Serikali haioni haja ya kuja na mfuko maalum wa uwekezaji kwa sekta binafsi kupata kwa riba nafuu ili tuwekeze kwenye kongani za viwanda?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali kuhusu lini Serikali itakuja na mwongozo; kama nilivyotangulia kuzungumza katika jibu langu la msingi, ni kwamba hivi sasa tupo kwenye hatua za mwisho za kuandaa mwongozo wa Kitaifa ambao utawasilishwa kwa ajili ya wadau wote kujua sifa za maeneo kuitwa kongani. Mwongozo huo utatumika katika ngazi ya mkoa na halmashauri zetu zote Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuhusiana na mfuko wa uwekezaji kwa ajili ya kusaidia sekta binafsi, hivi tunavyozungumza tunatekeleza Dira ya Maendeleo ya 2020 - 2050 ambayo inajikita kwenye ongezeko la thamani. Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imetoa shilingi bilioni 200 kwa ajili ya kuwawezesha vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi kwa Wizara ya Viwanda na Biashara zinapitia *SIDO*. Lengo lake ni kuwezesha sekta binafsi kuanzisha viwanda vidogo vidogo. Pia tuna Benki ya Kilimo ambayo inatoa riba nafuu kabisa kwa ajili ya wadau wote ambao wanataka kwenda kuwekeza katika sekta ya kilimo katika viwanda vya kuongeza thamani ya mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina taasisi nyingine ambazo zinatoa mikopo, kwa mfano, Ofisi ya Waziri Mkuu kuna mifuko ya uwezeshaji wa biashara, ambayo lengo lake ni kuwezesha sekta binafsi kuanzisha viwanda kwa gharama nafuu kwa riba nafuu. Ninaomba kuwasilisha

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Saasisha Mafuwe.

**MHE. SAASISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni muda mrefu Serikali ilituahidi kuanzisha kongani ya viwanda eneo la *Kilimanjaro Machine Tools,* pamoja na mji wa kibiashara, njia panda ya Machame. Ningetamani kujua, je, Serikali imefikia wapi kwenye uanzishaji wa kongani hii pamoja na mji wa kisasa?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Saasisha Mafuwe kwa swali lake zuri, na amekuwa mpambanaji sana wa kuona kwamba maeneo ambayo yanazunguka Jimbo lake la Machame yanatumika kwa manufaa mapana ya wapiga kura wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ninatambua kwamba kuna eneo kubwa ambalo liko chini ya Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)* ambayo ni taasisi chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara ambayo tunaismamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi hii kumpa neno la faraja Mheshimiwa Mbunge kwamba jitihada zake zinaanza kuzaa matunda, kwa sababu tuna maelekezo ya Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba eneo lile la *Kilimanjaro Machine Tools* linaenda kutengenezwa *Industrial Smart City.* Hivi tunavyozungumza zabuni ya mshauri mwelekezi imeshatangazwa na tayari mkataba umeshasainiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya mshauri huyu mwelekezi ni kufanya *market survey,* kutengeneza *master plan*, mpango wa matumizi ya eneo, usanifu wa miundombinu na tathmini ya mazingira. Kazi hii tunatarajia itakamilika kabla ya Juni, 2027. Baada ya hapo, ninatumaini eneo hili litakuwa kitovu cha uchumi katika eneo lote; siyo tu Machame, siyo tu Hai, ni Mkoa mzima wa Kilimanjaro na kanda nzima ya kaskazini. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilikuona Mheshimiwa Josephine Kapoma.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiongelea Mkoa wa Morogoro huwezi kukwepa kuongelea viwanda, na Serikali ilishaahidi kuanzisha na kuendeleza kongani za viwanda vitano maeneo tisa ya kiuchumi pamoja na maeneo tisa huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali ikiwa inaendelea na mchakato wa kuangalia sehemu za kuanzisha kongani, wananchi wa Morogoro wanataka kujua, je, Serikali ina mkakati gani wa kuendeleza zile kongani ambazo tayari maeneo yapo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikubaliane na Mheshimiwa Josephine Kapoma, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Morogoro, kwamba Morogoro ni mkoa wa kimkakati wa viwanda. Mheshimiwa Mbunge anaweza kushuhudia kwamba mkakati wa Serikali kwanza ni kufufua viwanda ambavyo vimekufa, na baadhi ya viwanda vimefufuliwa na vinaendelea na kazi. Pili, kuvutia viwanda vipya, kazi ambayo inaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunaenda kuona viwanda vitatu vikubwa vipya; kiwanda cha tumbaku pale Mkwawa, kiwanda cha mabati na kiwanda cha sigara pale Morogoro. Kuhusiana na suala la kongani, tuna kongani moja pale Kihonda ambayo mwezi uliopita nilienda kuitembelea. Ninafahamu changamoto zao, uzalishaji unaendelea, uwezeshaji ndilo suala ambalo tunalizungumzia sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpe neno la faraja Mheshimiwa Mbunge, kwamba sehemu ya fedha za uwezeshaji kutoka kwa Mheshimiwa Rais, zaidi ya shilingi bilioni 200 kupitia *SIDO* zitaenda pale kwa ajili ya kuwaimarisha vijana katika shughuli za uzalishaji katika kongani ile ya viwanda pale Kihonda. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa bado tuko katika Wizara hiyo hiyo. Nimwite sasa Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 357

**Hitaji la Viwanda vya Kuchakata Zao la Chai**
**Bungu – Korogwe Vijijini**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatatua changamoto ya kukosekana kwa Viwanda vya kuchakata zao la chai Tarafa ya Bungu – Korogwe Vijijini?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali Na. 357 kutoka kwa Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Korogwe, hususan Tarafa ya Bungu, ni miongoni mwa maeneo yanayolima zao la chai hapa nchini. Msimu wa mwaka 2024/2025 wilaya hii ilizalisha kiasi cha tani 7,875. Kulingana na uzalishaji huu, Serikali iliona kuwa ni vyema kujenga kiwanda katika tarafa hii. Hadi kufikia sasa, bodi ya chai ipo kwenye hatua za mwisho za kukamilisha taratibu za ujenzi wa jengo la kiwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mtambo utakaokuwa na uwezo wa kuchakata majani tani 15 kwa siku, sawa na tani 5,475 kwa mwaka, umeagizwa na unatarajiwa kufungwa katika kiwanda hicho. Pindi ujenzi utakapokamilika, uzalishaji utaanza mara moja. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, pamoja na matumaini ya kiwanda hiki kipya, eneo lile tulikuwa na mwekezaji mwenye viwanda viwili; kiwanda cha *Mambangulu Tea Estate* na

kiwanda cha Dindira, na viwanda hivi vimefungwa kwa zaidi ya mwaka mmoja. Viongozi wote wakuu wa Serikali wametoa maelekezo, lakini hakuna dalili wala matumaini. Nchi inapata hasara ya kupoteza kodi pamoja na ajira za watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri aniambie tu kwamba sisi wananchi wa Korogwe na wananchi wa Tarafa ya Bungu sasa tukubali kwamba wako watu wenye nguvu kuliko Serikali kwenye nchi hii kwa sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Ahadi hii ya kiwanda hiki kipya alichokisema, imekuwepo tangu mwaka 2024. Wananchi wa Bungu na Korogwe wanataka kujua, je, ni lini hasa kazi hii itakamilika ili waweze kupata huduma ya kiwanda hiki?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba viwanda hivi vimesimamisha uzalishaji wake. Jitihada ya Serikali na maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwetu sisi ni kuhakikisha kwamba viwanda vyote ambavyo vimebinafsishwa na vimesimamisha shughuli za uzalishaji tunaenda kuvisimamia kufufua shughuli za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mkoa wa Tanga, kazi hiyo tumeanza kwenye kiwanda cha Mponde kule Lushoto, ambapo baadhi ya wakulima wa chai Korogwe wanauzia sasa hivi majani yao ya chai katika kiwanda cha Mponde, na hivi sasa kimeanza kufanya kazi. Wakulima wa Wilaya za Lushoto na Korogwe wameshalipwa zaidi ya shilingi bilioni 4.800 kupitia ufufuaji wa kiwanda hiki cha Mponde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasi ile ile ambayo tumeitumia na juhudi zile zile za kutafuta wawekezaji wa kufufua kiwanda cha Mponde, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *(PSSSF)* na Mfuko wa Fidia *WCF* ambao sasa hivi ndiyo wanasimamia kiwanda kile, tutatumia jitihada zile zile kuhamasisha sekta binafsi na taasisi za Serikali kuwekeza kwenye zao la chai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutasimama na mwekezaji kuhakikisha kwamba anafufua shughuli za uzalishaji pale, lakini akishindwa hatutasita kuchukua hatua kama tulizochukua kule Mponde kuhakikisha kwamba kiwanda hiki kinafufuka na kinaanza shughuli za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kwamba kama kuna mtu ambaye ana nguvu kwenye nchi hii; hakuna mtu mwenye nguvu zaidi ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ametuelekeza kusimamia ufufuaji wa viwanda hivi ambavyo vimebinafsishwa. Kazi hii tunaenda kuisimamia kwa kuwa hakuna mwenye nguvu zaidi ya Mheshimiwa Rais. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Kuna maswali machache ya nyongeza, nimekuona Mheshimiwa...

**MHE. FADHILI A. LIWAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Fadhili Liwaka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Liwaka, nilikuwa ninalitafuta jina.

**MHE. FADHILI A. LIWAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Wilaya ya Nachingwea ina viwanda viwili ambavyo vimekoma kufanya kazi yake; kiwanda cha kukamua ufuta na kiwanda cha kubangua korosho. Je, Serikali iko tayari kuja kufanya tathmini na kuona maeneo yaliyolala ili kuweza kufanya ufufuaji wa viwanda hivyo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fadhili Liwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunafanya tathmini katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya kuhakikisha kwamba tunaenda kuwa na viwanda vya kimkakati kila mkoa, na kongani katika wilaya. Moja ya mikoa ambayo tumefanya tathmini ni Mkoa wa Mtwara na Lindi, na moja ya mazao makubwa ambayo tunaona

ya kimkakati kule ni korosho, pia ufuta unakuja baada ya korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara imejizatiti kutafuta wawekezaji ambao wanaenda kuongeza tija katika mazao haya mawili ya korosho na ufuta na kuweka viwanda vya kuongeza thamani kwa kadiri ya Dira ya Maendeleo ya 2020 - 2050 inavyotuelekeza. Hivyo Mheshimiwa Mbunge, asiwe na wasiwasi baada ya Bunge hili, tutaongozana mimi na wewe kwenda kule, kukagua viwanda vilivyopo na kuangalia mahitaji. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kuniona. Jimbo la Tabora Mjini lina kiwanda kilichobinafsishwa miaka mingi iliyopita na mbinafsishaji ameshauza hadi majengo ambayo yalibinafsishwa katika Jimbo la Tabora Mjini. Kiwanda cha *TABOTEX* hakifanyi kazi na wala hakifanyi lolote zaidi ya kufuga popo. Nini kauli ya Serikali juu ya Kiwanda hiki ambacho kingeweza kusaidia ajira za Watanzania wengi wa Jimbo la Tabora Mjini na mkoa mzima wa Tabora?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Nyuzi cha Tabora ni moja ya viwanda vya kimkakati na hasa katika kipindi hiki ambacho tunazungumzia kuboresha sekta ya uvuvi, na pia kuongeza thamani ya zao la pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tabora ni mkoa wa kimkakati. Kama tulivyoshuhudia wiki iliyopita, Serikali imeingia makubaliano ya kupata fedha za kumalizia *SGR* ambayo itapita pale Tabora. Kwa hiyo, kiwanda hiki na viwanda vingine ambavyo tunaenda kuhamasisha ujenzi wake pale Tabora, siyo kwa Tabora tu, lakini kwa eneo lote la ukanda ule wa magharibi na hivyo tunaona kabisa thamani ya reli hii itaenda sambamba na ufufuaji wa viwanda hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuna maelekezo ya kufufua viwanda vyote, lakini kuanzisha viwanda vipya na Kiwanda cha Nyuzi Tabora ni sehemu ya viwanda hivyo ambavyo tumedhamiria kuhakikisha kwamba vinapata wawekezaji kwa ajili ya kuvifufua. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako. Mheshimiwa Singano kwa kifupi sana.

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikiri kwa kurejea kwa Kiwanda cha Mponde cha Chai - Bumbuli, ambacho kimesimama kwa takribani miaka nane. Changamoto ya sasa hivi ni uwezo mdogo wa kiwanda kile, lakini pia kimeelemewa zaidi baada ya ndugu zetu wa Korogwe kukitegemea. Ni lini Serikali itaona umuhimu wa kukipanua kwa haraka ili kuweza kuhimili mahitaji ya wakulima wa chai?

**MWENYEKITI:** Kwa kifupi sana Mheshimiwa Naibu Waziri, ulishalijibu hilo la chai.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuzidiwa kwa Kiwanda cha Mponde kunatokana na wakulima wa chai wa Korogwe kwenda kuuzia mazao yao kule Lushoto. Kiwanda kile kimekuwa muhimu kama soko kuu la chai kwa sasa hivi kwa Wilaya ya Korogwe, na jitihada za Serikali kufufua kiwanda cha chai pale Bungu - Korogwe inaenda sambamba na kupunguza mzigo ambao unaenda katika kiwanda cha Mponde. Hivyo, uimarishaji na ukamilishaji wa kiwanda hiki cha Bungu pale Korogwe kunaenda kutoa suluhu ya kudumu ya changamoto za mizigo kuzidiwa pale Mponde. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii. Nimwite sasa Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Kafiti Kafiti.

Na. 358

**Kisiwa cha Ukerewe kuwa Kivutio cha Utalii**

**MHE. KAFITI W. KAFITI K.n.y. MHE. DKT. REGINA C. MALIMA** aliuliza: -

Je, Serikali haioni umuhimu wa kufanya tathmini na kukiweka Kisiwa cha Ukerewe chenye visiwa 38 ndani yake kwenye vivutio vya kiutalii nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima, Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali inayolenga kutangaza, kukuza na kuendeleza mazao ya utalii yanayopatikana katika Kisiwa cha Ukerewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi za Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP)* - Tanzania na Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini Kampasi ya Mwanza, inaendelea na kazi ya utafiti na kuainisha vivutio vya utalii vilivyopo katika Kisiwa hicho kwa lengo la kuangalia namna ya kuunganisha shughuli za utalii wa Kisiwa cha Ukerewe na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kafiti Kafiti.

**MHE. KAFITI W. KAFITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Wizara. Sasa ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa kupitia Hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati anafungua Bunge alielekeza Wizara ya Maliasili na Utalii kuhakikisha inaongeza vyanzo na mapato yatokanayo na utalii, na kwa kuwa moja ya maeneo ya kimkakati ya Mkoa wa Mwanza ikiwemo Wilaya ya Ukerewe imekuwa na visiwa zaidi ya 38 vinavyoongoza kwa utalii, sasa ni

nini kauli ya Serikali kuhakikisha inakwenda kuimarisha visiwa hivyo na kuongeza mapato zaidi kwa Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Je, Serikali iko tayari sasa kutembelea Kisiwa hiki cha Ukerewe na kuona fursa hizo zitokanazo na utalii?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninaomba nimpongeze sana ndugu yangu Mheshimiwa Kafiti kwa namna anavyofuatilia kutaka kuboresha maendeleo ya utalii ndani ya visiwa hivyo vya Ukerewe kule Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika swali la msingi, ni kwamba wataalamu wako *site* kufanya utafiti ili kubaini na kuainisha vivutio mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Serikali iko tayari. Mimi mwenyewe niko tayari, na hata Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuambatana na Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher kwenda katika eneo hilo kuona maajabu hayo ya visiwa 38 kule Mwanza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako.

Waheshimiwa Wabunge, tumalizie swali la mwisho. Niendelee na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Nimwite sasa, Mheshimiwa Tinnar Andrew Chenge, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 359

**Wanafunzi Kuandika Lugha Zisizo za Staha Kwenye Mtihani**

**MHE. TINNAR A. CHENGE** aliuliza: -

Je, Serikali inachukua hatua gani kubaini chanzo cha tabia ya wanafunzi kuandika lugha zisizo na staha kwenye karatasi za mtihani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wanu Ameir.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, ninaomba kujibu swali Na. 359 la Mheshimiwa Tinnar Andrew Chenge, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2025 Serikali kupitia Baraza la Mitihani la Tanzania *(NECTA)* ilifanya utafiti na kubaini kuwa sababu za wanafunzi kuandika lugha zisizo na staha kwenye karatasi za mitihani zinasababishwa na mmomonyoko wa maadili, msongo wa mawazo, na kukata tamaa kitaaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Mitihani la Tanzania, mtahiniwa anayeandika matusi kwenye *script* hupewa adhabu ya kufutiwa matokeo ya mtihani husika. Hivyo, Baraza limekuwa likiziandikia shule ambazo zimebainika kuwa na watahiniwa wanaoandika matusi na lugha zisizo na staha katika mitihani, ili kuwaasa wanafunzi wao kutoandika lugha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali inaendelea kutoa elimu ya maadili kwa jamii, kuendesha mafunzo endelevu kwa walimu kuhusu mbinu bora za malezi, kuimarisha utoaji wa ushauri nasaha kwa wanafunzi, ili kupunguza msongo wa mawazo pamoja na kuchukua hatua stahiki za kinidhamu kwa wanafunzi wanaohusika na uandishi wa lugha zisizo na staha kwenye mitihani. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tinnar Andrew Chenge, swali la nyongeza.

**MHE. TINNAR A. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali

mawili madogo ya nyongeza. Nilikuwa nataka kufahamu, je, hivi vitendo vya wanafunzi hawa kuandika lugha zisizo na staha kwenye mitihani vinafanyika *randomly* au ni *specific* kwa kundi fulani kwa maana ya jinsia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa nchini kwetu kuna maeneo ambapo baadhi ya wazazi huwashawishi wanafunzi kufanya vibaya kwenye mitihani ili waweze kuwaozesha, je, Wizara imefanya utafiti wa kina kujua kwamba suala hili la kuandika maneno yasiyokuwa na staha na kuozesha watoto havina mahusiano? Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Tinnar Andrew Chenge kwa kuwa *concerned* na maadili ya wanafunzi ama vijana wetu, na nimpongeze kwa kazi nzuri anayoifanya kule jimboni ya kuhakikisha kwamba vijana na wanafunzi wanakuwa na maadili mema katika eneo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, Serikali kupitia Baraza la Mitihani la Tanzania kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi kwamba, limefanya utafiti kuhusu kadhia hii ya kuona kwamba baadhi ya wanafunzi wanaandika lugha za matusi katika mitihani. Utafiti huo ulibaini kuwa vitendo hivi havihusiani na jinsia moja tu, ni kwamba jinsia zote mbili huwa zinaandika lugha zisizo na staha katika mitihani yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Serikali inatambua kuna mdondoko wa wanafunzi wa kike katika baadhi ya maeneo, na kiwango cha mdondoko cha wanafunzi hawa huwa kinasababishwa na sababu tofauti tofauti ikiwemo hiyo ambayo amesema, kwamba, wazazi huwa wanawaachisha wanafunzi shule kwa makusudi. Pia, huwa wanawashauri kwamba waandike lugha zisizo na staha ili wapate kutoka nje ya mfumo wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeunda kikosi kazi maalum cha Kitaifa ambacho kinapita kila mkoa kuangalia nini hasa

tatizo la wanafunzi au vijana wetu kuandika lugha zisizo na staha katika mitihani? Taarifa hiyo itakapokamilika itawasilishwa na hatua stahiki zitachukuliwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ninakushukuru sana. Muda wetu umeisha, na suala la watu kuchora maumbo kwenye mtihani ni letu wote kuelimisha wapiga kura wetu.

Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, kipindi chetu cha maswali kimekwisha, na maswali yetu tumeyamaliza. Sasa niwaletee matangazo.

Kwanza kabisa ni wageni ambao tunao katika ukumbi wetu wa Bunge leo hii. Tunao wageni ambao wamekaa Jukwaa la Spika. Hawa ni wageni wa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, Waziri wa Maliasili na Utalii. Wageni hawa ni kama wafuatao:

Tunaye Dkt. Hassan Abbasi, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii; na Ndugu Nkoba E. Mabula, Naibu Katibu Mkuu, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye Jenerali (Mstaafu) George Marwa Waitara, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini Shirika la Hifadhi ya Taifa *(TANAPA);* Jenerali (Mstaafu) Venance Salvatory Mabeyo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro *(NCAA);* Meja Jenerali (Mstaafu) Hamis Semfuko, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania *(TAWA);* na mstaafu mwingine ni Luteni Chiku Gallawa, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania *(TFS)*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni Dkt. Ladslaus Batinoluho, Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Taifa cha Utalii – *NCT;* Ndugu Said Kamugisha, Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii Tanzania – *TTB;* Prof. Agness Sirima, Mwenyekiti wa Bodi Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi; na Prof. Jafari Kideghesho,

Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Uhifadhi wa Wanyamapori Tanzania. Karibuni sana. *(Makofi)*

Leo tuna bahati ya kuwa na Mawaziri wastaafu wa Wizara ambao wameendesha Wizara hii, hawa wako wawili. Nitaanza na wa kwanza ambaye ni Mheshimiwa Zakia Meghji aliwahi kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kipindi kirefu. Moja katika ya watu walio-*serve* kwa muda mrefu kwenye hii Wizara.

Pia, tunaye Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, naye aliwahi kuwa Waziri wa Wizara hii. Tunawakaribisha sana sana Mawaziri wetu wastaafu na wastaafu wote ambao mpo kwenye ukumbi huu kwa maana ya kwamba mnaendelea kulitumikia Taifa la Tanzania. *(Makofi)*

Wengine ni Dkt. Alexanda Lobora, Mkurugenzi wa Wanyamapori; Ndugu Mussa Juma Kuji, Kamishna wa Uhifadhi wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA);* Ndugu Abdulrazak Badru, Kamishna wa Uhifadhi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro *(NCAA);* na Ndugu Mlage Kabange, Kaimu Kamishna wa Uhifadhi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori *(TAWA)*. Karibuni sana *(Makofi)*

Wengine ni Dkt. Noel Lwoga, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Makumbusho ya Taifa Tanzania; Dkt. Florian Mtei, Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Utalii; na Alhaji Adam Kimbisa, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dodoma. Tunawakaribisha sana kwenye ukumbi wetu. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Kijaji ni familia yake. Hawa watu nitaanza kuwataja. Tunaye Dkt. Muhajir Kachwamba, Mume wa Mheshimiwa Waziri; karibu sana kwenye ukumbi wetu. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Aboubakar Muhajir, mtoto wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Zulfa Hemed, mtoto wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Samira Muhajir, mtoto wa Mheshimiwa Waziri; na Ndugu Shafii Minga, mtoto wa Mheshimiwa Waziri. Karibuni sana kwenye ukumbi huu. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Kijaji, hawa ni Makamanda wa Kanda za Jeshi la Uhifadhi kutoka Taasisi za *TANAPA, TAWA, TFS* na Ngorongoro. Nadhani wamekaa sehemu mbalimbali tunawakaribisha. *(Makofi)*

Tunao Wakurugenzi wa Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Wadau wa Sekta ya Utalii na Maliasili nchini; Wanafunzi wa Chuo cha Utalii Arusha; Wanafunzi wa Chuo cha Wanyamapori; Wamiliki wa kampuni za utalii nchini; Jumuiya ya Vijana kutoka Kondoa; na Watumishi kutoka Ofisi ya Mbunge Kondoa. Kwa umoja wenu karibu sana. Eneo letu siyo kubwa sana kuwaona wote, lakini tunatambua kwamba mpo nasi. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini, hawa ni Kikundi cha Kisanaa na wapiga kura wake kutoka Longido, Arusha. *(Makofi)*

Tunao wageni 27 wa Mheshimiwa Charles Mhando Njama, hawa ni wafanyakazi wake na Madiwani kutoka Korogwe Mkoani Tanga. *(Makofi)*

Tunaye Mzee Peter Mavunde, naye yupo katika ukumbi huu. Karibu sana mzee wetu. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Zainab Anslem, huyu ni kutoka *ZARA Tours – TATO* na Ndugu Rahma Ahmed, huyu ni *Board Member* wa *TATO*; karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo. Hawa ni wanafunzi 23 wa Shahada ya Pili ya Usimamizi wa Fedha kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* kutoka Jijini Dodoma.

Pia, tunao wanafunzi 34 na walimu wanne wa Taasisi ya *Mathematics Training Centre* kutoka Jijini Dodoma. Tunatambua uwepo wao na tunawakaribisha sana.

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo mengine mawili. Tangazo la kwanza; Waheshimiwa wote mnakumbushwa kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii imeandaa maonesho kuhusu shughuli za uhifadhi na utalii zinazotekelezwa na idara na taasisi zake. Maonesho haya yatafanyika kuanzia leo tarehe 15 hadi tarehe 18 Mei, 2026 katika viwanja vya maonesho karibu na Zahanati ya Bunge. Waheshimiwa wote mnakaribishwa kutembelea maonesho hayo ili muweze kuwa mabalozi wa uhifadhi endelevu na utangazaji wa utalii nchini.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine. Wote mnakumbushwa kuwa Maafisa Uhamiajia wanaendelea kutoa huduma ya hati za kusafiria katika viwanja vya Bunge. Zoezi hili litahitimishwa leo tarehe 15 Mei, 2026. Waheshimiwa Wabunge ambao hawajapata huduma ya hati za kusafiria wanaombwa kufika jengo la utawala *ground floor* ukumbi Na. 9 kuanzia saa 4.00 Asubuhi, ili kupata huduma hiyo. Hayo ndiyo matangazo kwa sasa.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaingia kwenye hoja iliyopo mbele ya Waziri wa Maliasili na Utalii. Sasa nimwite Mheshimiwa Waziri Dkt. Ashatu Kijaji, aweze kutoa hotuba yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ambayo imepitia na kuchambua Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema na Fadhila kwa kutujalia afya njema na hekima ya kutekeleza majukumu tuliyokasimiwa na Watanzania kwa ufanisi, uwajibikaji na kuzingatia maslahi mapana ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama kwa mara ya kwanza nikiwa Waziri wa Maliasili na Utalii mbele ya Bunge lako Tukufu la Kumi na Tatu, kuwasilisha Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wahenga wanasema, nguzo imara haisukumwi na upepo. Ninapenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuaminiwa na Watanzania na kuchaguliwa kuongoza nchi yetu kwa kipindi cha pili cha Awamu ya Sita kupitia Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Oktoba, 2025. Uongozi wake thabiti na wenye dira umeendelea kuimarisha uwazi na kuleta tija katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika kipindi cha Awamu ya Sita, nchi yetu imeshuhudia mwelekeo imara wa uendeshaji wa Serikali unaojengwa katika misingi ya utawala bora, maridhiano, utu na uwajibikaji uliowezesha kuimarika kwa usimamizi wa rasilimali za Taifa ikiwemo uhifadhi endelevu wa rasilimali za wanyamapori, misitu, nyuki na malikale pamoja na kuongeza thamani ya rasilimali hizi, hatua iliyochochea mchango wa sekta hii katika Pato la Taifa, ajira na mapato ya fedha za kigeni. Tunamwombea Mheshimiwa Rais afya njema, hekima na busara katika kutekeleza majukumu yake kwa maendeleo endelevu na jumuishi ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, ninapenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na kumteua Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, kuwa Naibu Waziri. Mimi pamoja na viongozi wenzangu katika Wizara hii, tunamwahidi Mheshimiwa Rais kuwa tutatekeleza dhamana tuliyopewa kwa ushirikiano, weledi, uadilifu, utu na uwajibikaji katika kuhakikisha Sekta ya Utalii pamoja na rasilimali za maliasili na malikale zinasimamiwa kwa uendelevu ili kuchangia ukuaji wa uchumi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kwa Awamu ya Pili; na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Iramba Magharibi kwa kuteuliwa kushika nafasi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninawapongeza viongozi hawa wote kwa kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi mkubwa katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kwa kutupatia maelekezo na miongozo ambayo imekuwa chachu katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kuimarisha uhifadhi endelevu wa rasilimali za maliasili pamoja na uendelezaji wa utalii kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa, ninaomba kumpongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Ilala kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuongoza Bunge letu Tukufu. Ni wazi kuwa uongozi wake umeendelea kuimarisha hadhi ya Bunge, nidhamu ya mijadala na ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yake ya kikatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninampongeza Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini kwa kumsaidia Mheshimiwa Spika kuendesha shughuli za Bunge kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ninawapongeza sana Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika; Mheshimiwa Najma Murtaza Giga na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, kwa kuchaguliwa na umahiri wao katika kusimamia mijadala ya Bunge na kuliwezesha Bunge lako Tukufu kuimarisha uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, ninaomba kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya uongozi wa Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mwenyekiti; Mheshimiwa Mary Francis Masanja, Makamu Mwenyekiti; na Wajumbe wote wa Kamati kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwa wasimamizi wakuu wa majukumu ya Bunge katika kusimamia na kuishauri Serikali kuhusu usimamizi endelevu wa ardhi, maliasili na maendeleo ya sekta ya utalii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninawashukuru kwa mchango wao mkubwa katika kuchambua na kutoa ushauri kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Wizara inathamini ushauri wao na itaendelea kuuzingatia ili kuimarisha utendaji wa sekta na kuongeza mchango wake katika ukuaji jumuishi wa uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, niwapongeze Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote za Kudumu za Bunge kwa kuendelea kuisimamia na kuishauri Serikali kwa weledi na ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano na ushauri wao wenye tija katika kuimarisha uhifadhi na usimamizi endelevu wa rasilimali za maliasili na malikale pamoja na maendeleo ya Sekta ya Utalii nchini. Niwahakikishie kuwa, Wizara itaendelea kuyafanyia kazi maoni na ushauri huo kwa vitendo ili kuongeza ufanisi wa

utekelezaji wa majukumu yake na kuhakikisha manufaa hayo yanawafikia Watanzania wote kwa usawa na kuleta tabasamu kwenye nyuso na mioyo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia fursa hii pia kuwapongeza na kuwashukuru Mawaziri wenzangu, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wa Wizara mbalimbali kwa ushirikiano wao wenye tija katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Kama wahenga wanavyosema, *Figa moja haliinjiki chungu,* ushirikiano huu umeendelea kuimarisha uratibu wa kazi za Serikali na kuongeza ufanisi katika kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa. Ninathamini sana mchango wao. Kwa pamoja tutaendelea kujenga Taifa lenye nguvu na ustawi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kunukuu hekima ya wahenga isemayo, *Mti mmoja haufanyi msitu*. Usemi huu umedhihirika wazi katika utendaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwamba umoja, ushirikiano na mshikamano ndiyo mafanikio yetu. Nitumie fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru viongozi pamoja na watendaji Wakuu wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, ninamshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri, kwa mchango wake katika kuratibu na kusimamia shughuli za Wizara kwa weledi. Aidha, ninampongeza Dkt. Hassan Abbas, Katibu Mkuu pamoja na Bwana Nkoba Mabula, Naibu Katibu Mkuu kwa uongozi thabiti, weledi na usimamizi madhubuti wa shughuli za Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa dhati kabisa ninawashukuru pia watendaji wote wa Wizara wakiwemo Wakurugenzi wa Idara, Wakuu wa Vitengo, Wenyeviti wa Bodi, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na wafanyakazi wote wa Wizara na taasisi kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi mkubwa katika kufanikisha malengo ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kuwa kupitia ushirikiano wao mkubwa, uzalendo na kujituma katika kusimamia na kutekeleza

majukumu ya sekta kwa ufanisi umewezesha Wizara kupata mafanikio makubwa tunayoyashuhudia hivi leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wahenga wasemavyo, Mwenda Tezi na Omo, Marejeo Ngamani. Kwa namna ya kipekee, ninawashukuru kwa dhati wananchi wa Jimbo la Kondoa kwa kuendelea kuniamini na kunichagua kuwa Mbunge wao kwa mara ya tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninawashukuru kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kuwatumikia, kuwawakilisha katika Bunge hili Tukufu na kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo katika Jimbo letu. Ninaomba nitumie fursa hii kuwaahidi kuwa nitaendelea kuwa mtumishi wao na muda wote nitadumu katika kuwatumikia kwa umahiri na moyo wa dhati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upendo mkuu, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mama yangu mpendwa, Hajat Aziza Selemani kwa malezi bora, maadili mema na msaada wake usioyumba ulionifikisha hapa nilipo leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninampongeza na kumshukuru kwa dhati mume wangu mpendwa Dkt. Muhajir Kachwamba, pamoja na watoto wangu Samirah na Aboubakar kwa upendo wao, subira na uelewa ambavyo vimekuwa nguzo muhimu katika kunipa nguvu na motisha ya kutekeleza majukumu yangu ya kila siku kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nawashukuru viongozi wangu wa dini, ndugu, jamaa na marafiki wote kwa kuniunga mkono na kuniombea ili niendelee kutekeleza wajibu wangu ipasavyo. Ninaomba kuwahakikishia nyote pamoja na Watanzania kwa ujumla kwamba Ashatu ni yule yule, nitaendelea kufanya kazi kwa bidii, uadilifu na uzalendo mkubwa katika kuwatumikia wananchi na Taifa letu kwa kuzingatia misingi ya haki, utu na uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, ninatoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania, wanafamilia, Bunge lako Tukufu, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) na Mbunge wa Jimbo la Isimani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kumkumbuka kwa mchango wake mkubwa katika kuendeleza kwa vitendo misingi ya ushirikishwaji, uwajibikaji na uratibu madhubuti wa utekelezaji wa sera na programu za maendeleo ili kuhakikisha hakuna Mtanzania anayebaki nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitoe pole kwako na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuondokewa na wapendwa wetu; Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho; na Mheshimiwa Halima Idd Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, ninaungana na Watanzania wote kuwapa pole familia, ndugu, jamaa na marafiki kwa kuondokewa na wapendwa wetu. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema Peponi, Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hali halisi ya matukio ya kiuhifadhi yanayohusisha migongano kati ya binadamu na wanyamapori katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, ninatoa pole za dhati kwa ndugu, jamaa, marafiki na wananchi waliopoteza wapendwa wao kwa kushambuliwa na wanyamapori wakali na waharibifu pamoja na wananchi ambao walijeruhiwa au mali zao kuharibiwa na wanyamapori hao katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio haya yanatukumbusha wajibu na umuhimu wa kuendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi wa maeneo ya hifadhi pamoja na kuongeza ushirikiano kati ya Serikali na wananchi wanaoishi jirani na maeneo hayo. Ninaomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali itaendelea kuchukua hatua madhubuti za kupunguza athari za

migongano hiyo ili kulinda maisha ya wananchi na mali zao sambamba na kuhakikisha uhifadhi endelevu wa rasilimali zetu za Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia kutambua mchango wa dhati wa Maafisa na Askari Shupavu wa Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu ambao wameendelea kutekeleza majukumu yao kwa ujasiri na weledi katika kulinda na kuhifadhi maliasili za Taifa letu zikiwemo wanyamapori, misitu, nyuki na malikale. Katika mwaka huu wa fedha 2025/2026, Maafisa na Askari watatu walipoteza maisha wakiwa kazini wakitimiza wajibu wao kwa Taifa na wengine 15 walipata majeraha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashujaa wetu waliofariki wakitekeleza majukumu yao ni Askari wa Uhifadhi Daraja la III, Ndugu Victor Jackson Laizer kutoka *TANAPA*, na Askari wa Uhifadhi Daraja la I, Ndugu Ally Sakasa Kajogoro na Askari wa Uhifadhi Daraja la II, Ndugu Enock Gration Rugaimukamu kutoka *TAWA*. Tunamwomba Mwenyezi Mungu awajalie afya njema waliojeruhiwa na azipumzishe roho za Marehemu wapendwa wetu mahali pema Peponi, Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, ninaomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tuanze kuangalia mafanikio ya Sekta ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 chini ya uongozi mahiri na shupavu wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhifadhi na Mwongoza Watalii Namba Moja nchini, Serikali imefanikiwa katika Sekta ya Maliasili na Utalii kama ifuatavyo: -

(i) Kuongezeka kwa idadi ya watalii:

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imefanikiwa kuongeza idadi ya watalii kufikia 5,935,561 mwaka 2025 ikiwa ni ongezeko la 10.7% ikilinganishwa na watalii 5,360,247 kwa mwaka 2024. Ongezeko hili linajumuisha watalii wa Kimataifa walioongezeka kwa asilimia saba nukta moja na watalii wa ndani walioongezeka kwa 13.1%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji huu pia umeonekana katika mizania ya dunia ambapo taarifa ya Shirika la Utalii Duniani imeonesha, kidunia Tanzania imeshika nafasi ya 11 mwaka 2025 kwa ongezeko la wageni wa Kimataifa ukilinganisha na mwaka 2019 kabla ya janga la UVIKO 19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Tanzania imekuwa ya sita kwa kanda ya Afrika, na Mashariki ya Kati kwa ongezeko la wageni wa Kimataifa ukilinganisha na mwaka 2019. Taarifa hizi zinaonesha uwekezaji uliofanyika na Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya Uongozi makini wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, unaendelea kuleta matunda mema kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ukuaji wa wageni wa Kimataifa katika mizania ya utalii, Tanzania mwaka 2025 imeshika nafasi ya tatu duniani kwa soko la utalii lililofanya vizuri ukilinganisha na mwaka 2024, ambapo watalii walitumia fedha kwa wingi.

(ii) Kuongezeka kwa mapato yatokanayo na utalii:

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Disemba, mwaka 2025, mapato yatokanayo na shughuli za utalii nchini yameongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 3.9, mwaka 2024 hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 4.4 kwa mwaka 2025, ikiwa ni ongezeko la 12.82%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii imeifanya sekta ya utalii nchini kuwa namba mbili kwa kuingiza fedha za kigeni. Mafanikio hayo yamechangiwa na juhudi mbalimbali zikiwemo kuongezeka kwa utangazaji utalii, uboreshaji wa miundombinu ya utalii na huduma na matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika kukusanya mapato.

(iii) Tanzania kuendelea kushinda mbalimbali na kutambulika Kimataifa:

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imefanikiwa kushinda tuzo mbalimbali za Kimataifa za utalii, zikiwemo Tuzo kubwa za *World Travel Awards*, tukio lililofanyika katika Jiji la Manama nchini Bahrain. Tuzo zilizotolewa ni Tanzania kutangazwa kuwa Nchi Bora ya Utalii wa Safari Duniani kwa mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Hifadhi ya Taifa Serengeti kushinda Tuzo ya Hifadhi Bora Duniani Mwaka 2025. Ushindi unaoifanya Hifadhi hii kuendelea kuwa moja ya Maajabu ya Dunia yenye mandhari, wanyamapori na tukio la kipekee la uhamaji wa nyumbu, na Zanzibar kutangazwa kuwa eneo bora la mikutano na matukio ya biashara kidunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, wadau wa sekta binafsi nao walishinda tuzo mbalimbali za Kimataifa ikiwemo Hoteli ya Jummeirah iliyopo kwenye Kisiwa cha Thanda, kushinda Tuzo ya *World's Leading Exclusive Private Island* na Serengeti *Balloon Safaris* kushinda Tuzo ya *World's Leading Hot Air Ballon Safari*. Mafanikio haya yameimarisha hadhi ya Tanzania Kimataifa, kuongeza ushindani wa sekta ya utalii katika utoaji wa huduma bora, pamoja na kuchangia ongezeko la watalii na uwekezaji nchini.

(iv) Kuimarika kwa Miundombinu ya Utalii:

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha ushindani wa sekta ya utalii na kuongeza mchango wake katika uchumi wa Taifa, Serikali imeendelea kuwekeza kwa kiwango kikubwa katika maendeleo ya miundombinu ya utalii nchini, kwa kukamilisha ujenzi wa viwanja vya ndege vitatu katika Hifadhi za Taifa za Nyerere, kiwanja cha ndege kimoja na Ruaha viwanja vya ndege viwili, pamoja na kukarabati viwanja vya ndege nane katika Hifadhi za Taifa Mikumi, Ruaha, Nyerere na Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, jumla ya kilometa 3,757.92 za barabara na kilometa 523.14 za njia za watembea kwa miguu

zimejengwa na kukarabatiwa katika maeneo yaliyohifadhiwa ili kurahisisha ufikaji kwenye vivutio vya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji huu umeleta matokeo chanya yanayoonekana kwa kuongeza urahisi wa kufikia vivutio vya utalii, kuboresha uzoefu wa wageni na kufungua fursa za ajira na biashara kwa wananchi wanaoishi jirani na maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, uwekezaji huu umechangia ongezeko la mapato ya Serikali na ukuaji wa sekta kwa ujumla. Mathalan, katika Ukanda wa Kusini, maboresho haya yamewezesha ongezeko la watalii kutoka 197,402 hadi kufikia 205,520 na mapato kuongezeka kutoka shilingi bilioni 24.6 hadi bilioni 27.7 katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026. Mafanikio haya yanaakisi dhamira ya Serikali yetu ya Awamu ya Sita ya kuendelea kuimarisha miundombinu ya utalii ili kuongeza ushindani wa Tanzania Kimataifa, kuchochea ukuaji wa uchumi na kuboresha ustawi wa wananchi wetu.

(v) Kukamilika kwa sensa ya wanyamapori nchini:

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekamilisha kwa mafanikio makubwa zoezi la sensa ya Kitaifa ya wanyamapori nchini. Sensa kama hii ni ya pili kufanyika na hufanyika kila baada ya miaka 10 kwa lengo la kubaini uwepo, idadi, mtawanyiko na mienendo ya wanyamapori, sambamba na kubaini viashiria hatarishi vinavyoweza kuathiri ustawi na mazingira yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, sensa hii imefanyika kwa kutumia fedha za ndani kwa mara ya kwanza tofauti na sensa ya awali, hatua inayodhihirisha uwezo na dhamira ya Serikali yetu ya Awamu ya Sita, chini ya shujaa wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kugharamia na kusimamia shughuli za kimkakati za uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya sensa hii yanaonesha mwenendo chanya wa ongezeko na ustawi wa wanyamapori katika mifumo ikolojia mbalimbali. Aidha, takwimu zilizopatikana ni nyenzo muhimu katika kupanga matumizi bora ya rasilimali

ikiwemo uwindaji endelevu, kubaini na kulinda jamii za wanyamapori zilizo hatarini kutoweka pamoja na kusaidia kupanga mikakati madhubuti ya kukabiliana na changamoto za shughuli za kibinadamu katika mifumo ikolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, takwimu hizi zitasaidia katika kuendeleza uwekezaji wa miundombinu ya utalii, kuongeza mapato ya Serikali pamoja na kufungua fursa za ajira na biashara kwa wananchi wanaozunguka maeneo ya hifadhi.

(vi) Kuongezeka kwa soko la asali ya Tanzania Kimataifa:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango cha asali kinachouzwa nje ya nchi kimeongezeka kutoka tani 951.6 mwaka 2024 hadi tani 1,596.8 mwaka 2025 sawa na ongezeko la 67.9%. Aidha, thamani ya mauzo ya asali imeongezeka kutoka shilingi bilioni 11.4 kwa mwaka 2024 hadi shilingi bilioni 19.2 mwaka 2025, sawa na ongezeko la 68.4%. Moja ya nguzo kuu iliyochangia mafanikio haya ni utekelezaji wa mpango madhubuti wa udhibiti wa mabaki ya kemikali katika asali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asali ya Taifa letu imeendelea kukidhi ubora kwa wastani kwa wastani 97% kwa viwango vya Umoja wa Ulaya kwa miaka mitatu mfululizo, hali iliyoongeza fursa za masoko ya nje ya nchi kama Marekani, nchi za Umoja wa Ulaya, Umoja wa Falme za Kiarabu na China. Vilevile, kwa mara ya kwanza mwaka 2025, asali ya Tanzania imefanikiwa kuuzwa katika Soko la Uingereza baada ya kukidhi vigezo vya soko hilo. *(Makofi)*

(vii) Kukamilisha ujenzi na kuzindua Makumbusho ya Jiopaki ya Ngorongoro – Lengai:

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekamilisha ujenzi na kuzindua Makumbusho ya kisasa ya Jiopaki ya Ngorongoro - Lengai iliyopo katika eneo la Kamni Wilaya ya Karatu, Arusha ambapo ni makumbusho ya pili ya aina hiyo barani Afrika baada M'Guon iliyopo Morocco. Hatua hii imeongeza zao jipya la utalii wa jiolojia ambalo pia litakuza utafiti wa kisayansi na elimu ya miamba, kuwezesha jamii na wanafunzi kujifunza historia ya

sayansi na mazingira, kuongeza ajira na kipato kwa wananchi wa maeneo jirani na kuimarisha nafasi ya Tanzania Kimataifa kama kinara wa uhifadhi, utalii na elimu ya miamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii pia ni miongoni mwa mikakati ya Wizara katika kuliongezea thamani eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, ambalo mwaka 2018 lilipewa hadhi ya jiopaki inayotambuliwa na *UNESCO*, na kuwa jiopaki pekee yenye hadhi hiyo katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa na mikakati ya kukuza utalii kupitia matukio ya Kimataifa yatakayofanyika hapa nchini. Ibara ya 23 ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 inaelezea umuhimu wa sekta ya utalii katika kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Aidha, katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii, Chama cha Mapinduzi kimeielekeza Serikali yake, kuongeza wigo wa mazao ya utalii na kuendelea kuitangaza hazina ya utalii tuliyonayo, kwa mbinu za kisasa ili kuongeza idadi ya watalii kufikia milioni nane, mwaka 2030. Pia, kuongeza mchango wa sekta ya utalii katika pato la Taifa kutoka 17% mwaka, 2025 hadi 20% mwaka 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuzingatia maelekezo hayo, Wizara imeendelea kutumia utalii wa mikutano na matukio kama nyenzo muhimu ya kukuza uchumi. Aidha, Wizara inatambua uwepo wa matukio manne ya Kimataifa yanayotarajiwa kufanyika hapa nchini kwa mwaka 2026/2027, na imejipanga kutumia matukio hayo kukuza na kuendeleza utalii nchini kabla, wakati na baada ya matukio hayo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukio la kwanza ni Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani *(Inter-Parliamentary Union Assembly)*. Mkutano huu unakutanisha Mabunge ya Nchi Wanachama wa Umoja wa Mabunge Duniani na utafanyika tarehe 5 - 9 Oktoba, 2026 Jijini Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkutano huu unatarajiwa kuwa na washiriki zaidi ya 1,500, wakiwemo Maspika 183 kutoka nchi mbalimbali duniani, ambapo Tanzania ni mwanachama na

Mwenyekiti wa Umoja huo. Katika kuhakikisha Tanzania inafaidika kikamilifu na mkutano huu, Wizara imeandaa na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kutangaza mazao ya utalii na ukarimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua za maandalizi, Wizara iliandaa onesho la kutangaza utalii wetu wakati wa Mkutano wa 152 wa *IPU* uliofanyika tarehe 15 hadi 19 Aprili, 2026, Jijini Istanbul nchini Uturuki. Aidha, katika mkutano huo, Wizara ilifanikiwa kutangaza vivutio na fursa za utalii wa Tanzania kwa washiriki waliohudhuria na kuwashawishi kutembelea maeneo ya utalii kabla, wakati na baada ya Mkutano wa *IPU* wa 153.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa utalii, itaandaa vifurushi vya safari na kuvitangaza kwenye tovuti ya *IPU*. Vifurushi hivyo vitakuwa na *link* ambayo wageni wataweza kufanya *booking* ya kutembelea maeneo yetu moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua nafasi za Waheshimiwa Maspika, na misafara yao, Wizara itatumia Ofisi za Ubalozi wa Tanzania kwenye nchi mbalimbali kufikisha taarifa ya vivutio vya utalii vilivyopo nchini pamoja na vifurushi vya utalii ili wapange safari zao mapema. Pamoja na hilo, Wizara itaweka mabanda ya taarifa za utalii katika eneo la mkutano, ili kuhamasisha washiriki kutembelea vivutio vyetu kipindi na baada ya mkutano kwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukio la pili ni Tukio la *World Travel Awards* Mwaka 2026. Tukio hili la Kimataifa huandaliwa kila mwaka kwa lengo la kutoa tuzo za ubora katika sekta ya utalii duniani. Aidha, linatarajiwa kufanyika nchini, mwezi Disemba, 2026 na kuhudhuriwa na washiriki zaidi ya 1,000 kutoka Mabara ya Afrika, Ulaya, Asia, Amerika ya Kaskazini na Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa utalii itaandaa vifurushi maalumu vya mazao ya utalii na huduma kwa washiriki katika tovuti ya Bodi ya Utalii Tanzania na *World Travel Awards* pindi itakapofunguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Wizara itatumia fursa za kidigitali, machapisho na taarifa za mitandaoni kuwafikishia wadau mbalimbali taarifa muhimu za vivutio vya utalii Tanzania wakati wa tukio hilo. Pia, Wizara itaendelea kuhamasisha wageni kutembelea vivutio vya utalii na maeneo mbalimbali kupitia vifurushi vilivyoandaliwa na kuwekwa katika jukwaa la utalii la *TTB booking platform* ili kuendelea kutoa wigo mpana kwa wageni kufanya uchaguzi wa kutembelea vivutio hata baada ya tukio hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukio la tatu la Kimataifa ni Shindano la 74 la Ulimbwende wa Dunia 2027 *(Miss World 2027)*. Shindano hili la Kimataifa linahusisha masuala ya urembo likiwa ni miongoni mwa mashindano makubwa duniani yanayojulikana kama *Big Four Beauty Pageants*. Tukio hili linatarajiwa kufanyika nchini mwezi Mei, 2027 na linatarajiwa kuhudhuriwa na watu takribani 20,000 wakiwemo washindani 120 kutoka nchi mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kabla ya tukio hili, Wizara itawatangazia wadau na kuwahamasisha kuandaa na kuuza vifurushi vya safari, kupitia jukwaa la utalii la *TTB booking platforms* na kutangaza tukio hili kupitia tovuti ya *TTB*, mitandao ya kijamii, televisheni, redio na vyombo mbalimbali vya habari vya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Wizara itaandaa ziara ya mafunzo kwa kuwapa fursa walimbwende hao na waandishi wa habari kutembelea maeneo ya vivutio vyetu *(FAM Trip)* kabla ya shindano, kwa lengo la kukuza uelewa wa vivutio vyetu, na kurusha maudhui hayo kwenye mitandao yao ya kijamii, pamoja na kuvitangaza katika vyombo vya habari mbalimbali ulimwenguni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine, Wizara itaweka mabanda ya kutangaza utalii na kutoa taarifa kwa watalii ndani ya maeneo yatakapofanyika mashindano na kuendelea kutumia maudhui ya mashindano hayo, ikiwemo yatakayomhusu mshindi wa mashindano *(Miss World)*, kujitangaza zaidi duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shindano, Wizara kwa kushirikiana na wadau, itaratibu safari za kutembelea vivutio kwa washiriki watakaokuwa wamejisajili kupitia Jukwaa la Utalii la *TTB*. Vilevile, washindani wa juu watano wa shindano hilo, watapewa ubalozi wa hiari wa kutangaza utalii wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukio la nne la Kimataifa tunalolitarajia ndani ya mwaka huu wa fedha, ni mashindano ya mpira wa miguu kwa nchi za Afrika *(Africa Cup of Nations - AFCON 2027)*. Mashindano ya *AFCON* 2027 yanayoandaliwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika *(CAF)*, yanatarajiwa kufanyika kwa pamoja katika nchi za Afrika Mashariki ikiwemo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashindano hayo yatahusisha timu 24 kutoka Mataifa mbalimbali ya Afrika na yanatarajiwa kuvutia zaidi ya watazamaji milioni 1.8 viwanjani, pamoja na watazamaji wa televisheni bilioni 1.9 duniani kote, kupitia vituo zaidi ya 185 vya utangazaji. Aidha, mashindano hayo yanakadiriwa kuzalisha faida za kiuchumi zinazoweza kufikia zaidi ya Dola za Marekani bilioni mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na fursa hiyo, Wizara imeandaa mkakati maalumu wa kuitangaza Tanzania kama kivutio cha kipekee cha utalii, kabla, wakati na baada ya mashindano hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya mashindano, Wizara itaanza kampeni za Kimataifa za utangazaji, kupitia mashindano ya Kombe la Dunia la *FIFA* 2026, yatakayofanyika nchini Marekani, *Canada* na *Mexico* kwa kushirikisha wadau mbalimbali, wakiwemo watangazaji maarufu wa michezo, watu wenye ushawishi mkubwa pamoja na matumizi ya majukwaa ya kidijitali na mabango katika maeneo ya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara inaendelea kuboresha miundombinu muhimu ya utalii na usafiri, ikiwemo viwanja vya ndege, barabara, malazi na mageti ya kuingilia hifadhini, ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora kwa wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua nyingine, Wizara itaunganisha Hifadhi ya Taifa ya Mikumi na reli yetu ya kisasa ya *SGR,* kupitia lango la Kilosa ili kurahisisha safari za watalii watakaoshiriki *AFCON* 2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha ubora wa huduma, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo watoa huduma za utalii, ambapo tayari waongoza watalii 2,228 wamepatiwa mafunzo katika Awamu ya Kwanza. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi itaandaa vifurushi maalumu vya safari vitakavyojumuisha vivutio vya utalii, usafiri, malazi na huduma nyingine muhimu kwa washiriki na mashabiki wa *AFCON* 2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wakati wa mashindano Wizara itatumia viwanja vya michezo, maeneo ya ufuatiliaji wa mechi mbashara, yaani *fun zones,* pamoja na vyombo mbalimbali vya habari kutangaza vivutio vya utalii vya Tanzania kwa lengo la kuwahamasisha wageni kutembelea maeneo mbalimbali ya utalii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu kuendelea kuaminiwa kuwa mwenyeji wa matukio haya makubwa ya Kimataifa ni matokeo ya maono, uongozi thabiti na diplomasia ya uchumi inayofanywa kwa ustadi mkubwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia juhudi zake za kufungua nchi yetu, kuimarisha mazingira ya uwekezaji kuitangaza Tanzania Kimataifa na kuboresha miundombinu ya kimkikati, nchi yetu imeendelea kujijengea heshima na kuaminiwa katika Jukwaa la Kimataifa, kama kitovu cha utalii, biashara na uwekezaji duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio haya ya Kimataifa yataendelea kuwa kichocheo muhimu cha ukuaji wa sekta ya Maliasili na Utalii, pamoja na uchumi wa Taifa letu kwa ujumla. Hivyo kupitia Bunge lako Tukufu, ninatoa rai kwa Watanzania wote hudumisha asili yetu ya ukarimu kwa wageni, ili kuendelea kujenga taswira chanya ya Taifa letu na kuimarisha nafasi ya Tanzania kama kivutio cha utalii pekee duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa kuwasilisha Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maliasili na Utalii imepewa dhamana ya kusimamia Kisheria maeneo yenye ukubwa wa kilomita za mraba takribani 307,800 sawa na 32.5 ya eneo lote la nchi. Maeneo haya yanajumuisha Hifadhi za Taifa 21, eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, mapori ya akiba 29, mapori Tengefu 23, maeneo matatu ya ardhioevu chini ya Mkataba wa *Ramsar*, Hifadhi za misitu ya asili 465 ikijumuisha Hifadhi za Misitu ya Mazingira Asilia 26, Mashamba ya Miti ya Serikali 26, Hifadhi za Nyuki 14, maeneo ya Malikale 158 na Makumbusho za Taifa saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha Wizara inaratibu shughuli za uhifadhi katika maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori 40, ambapo kati ya hizo 26 zimeidhinishwa na 14 zipo kwenye hatua mbalimbali za kuidhinishwa. Mashamba sita ya ufugaji wa wanyamapori, bustani 41 za wanyamapori, maeneo 36 ya uzalishaji wa wanyamapori, pamoja na ranchi sita zinazomilikiwa na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara iliidhinishiwa kukusanya jumla ya shilingi trilioni 1.18 ambapo hadi kufikia Aprili, 2026 Wizara imekusanya jumla ya shilingi bilioni 989.33 sawa na 83.45% ya lengo la makusanyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 336.51 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 254.23 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 82.28 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Aprili, 2026 Wizara ilipokea jumla ya shilingi bilioni 252.56 sawa na 75%. Fedha hizi zinajumuisha fedha za matumizi ya kawaida shilingi bilioni 205.7 na fedha za miradi ya maendeleo shilingi bilioni 46.86. Kati ya Fedha za Matumizi ya Kawaida zilizopokelewa shilingi bilioni 98.63

ni Fedha za Matumizi Mengineyo na shilingi bilioni 107.07 ni za mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Afua Maalum za Kukabiliana na Migongano Baina ya Binadamu na Wanyamapori Wakali na Waharibifu. Lazima tukiri kwamba, licha ya mafanikio yaliyopatikana katika uhifadhi, bado kuna changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiasi kikubwa migongano hii imechangiwa na matumizi yasiyo rafiki ya ardhi, yasiyozingatia mipango ya matumizi bora ya ardhi, kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu katika maeneo yanayopakana na hifadhi, shoroba, maeneo ya mtawanyiko na wanyamapori, pamoja na athari za mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha ukame na kulazimisha baadhi ya wanyamapori kutoka nje ya hifadhi kutafuta maji na malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto hii Wizara imekamilisha ujenzi wa vituo vipya tisa vya Askari katika halmashauri za wilaya nne, na taratibu za ujenzi wa vituo vingine 21 zinaendelea katika wilaya 18. Kukamilika kwa ujenzi huu kutafanya jumla ya vituo vya Askari vilivyojengwa kufikia 49. Halikadhalika, Wizara imeweka vituo 40 vya muda vya Askari, kwa ajili ya kudhibiti matukio ya wanyamapori kwa haraka katika wilaya mbalimbali hapa nchini. Hatua hii imewezesha Askari kuitikia kwa haraka na kukabiliana na matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu wanapovamia maeneo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua nyingine, Wizara imechimba mabwawa 12 katika mapori ya akiba sita na Hifadhi ya Taifa ya Mikumi. Aidha, taratibu za uchimbaji wa mabwawa mengine saba zinaendelea katika Hifadhi za Taifa na mapori ya akiba. Juhudi hizi zimeimarisha upatikanaji wa maji kwa wanyamapori ndani ya hifadhi, hasa katika kipindi cha kiangazi ambacho wanyamapori wamekuwa wakitoka nje ya hifadhi kutafuta maji na kusababisha madhara kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imejenga vizimba nane vya kudhibiti mamba na viboko katika wilaya tano na hivyo, kufanya

idadi ya vizimba vilivyojengwa nchi nzima kufika 35. Aidha, taratibu zinaendelea kwa ajili ya ujenzi wa vizimba vingine 36 katika wilaya 20 nchini. Hatua hii imechangia kuimarika kwa usalama wa wananchi wanaotumia vizimba hivyo ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha matumizi ya teknolojia kwenye kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu, Wizara kwa kushirikiana na wadau imefunga visukuma mawimbi kwa wanyamapori 76 kati ya 50 vilivyopangwa kufungwa sawa na 152% kwa makundi mbalimbali wakiwemo tembo viongozi 51 katika halmashauri za wilaya 15 na hivyo, kufanya tembo viongozi waliofungwa visukuma mawimbi nchini kufikia 205.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wizara kwa kushirikiana na wadau, Wizara imenunua ndege nyuki 59 kwa ajili ya udhibiti wa wanyamapori hao. Matumizi ya teknolojia hizi yameongeza ufanisi katika ufuatiliaji wa mienendo ya wanyamapori kwa wakati na kuchukua hatua za haraka kabla ya kusababisha madhara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua nyingine, Wizara inaendelea na taratibu za ujenzi wa uzio wa umeme wenye urefu wa kilometa 53, ambapo kilometa 15 ni katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na kilometa 38 katika Hifadhi ya Taifa Serengeti. Uzio huo utaimarisha ulinzi wa mali na maisha ya wananchi kwa kudhibiti wanyamapori kutoka hifadhini kwenda kwenye maeneo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha ulinzi wa rasilimali za wanyamapori na udhibiti wa Wanyamapori wakali na waharibifu, Wizara imeajiri Askari wa wanyamapori 551 na kutoa mafunzo kwa Askari Wanyamapori wa Vijiji 95 kutoka halmashauri za wilaya 19 na hivyo, kufanya idadi ya Askari Wanyamapori wa Vijiji kufikia 1,298. Hatua hii imewezesha Askari hao kuitikia kwa haraka na kudhibiti matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha usalama wa maisha na mali za wananchi, jumla ya wanyamapori wakali na

waharibifu 175 walivunwa katika maeneo mbalimbali nchini, wakiwemo mamba 33, viboko 43, tembo 22, nyati 19, fisi 50, simba watano na chui watatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine, Wizara imehamisha tembo 390 kutoka Ranchi ya Taifa Kitengule na nyani 294 kutoka Geita kwenda Hifadhi ya Taifa Burigi, Chato, simba sita na chui watatu kutoka katika maeneo ya wananchi na kuwarudisha hifadhini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza ufanisi na tija katika kupokea taarifa na malipo ya kifuta jasho na machozi, Wizara imeanza kutumia mfumo wa kielektroniki kulipa waathirika wa madhara yatokanayo na wanyamapori wakali na waharibifu. Mfumo huo umerahisisha malipo kufanyika kwa wakati, kati ya siku saba hadi 14, ikilinganishwa na utaratibu wa awali ambapo zoezi hilo lilichukua miezi sita hadi 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Aprili, 2026 Wizara imelipa kiasi cha shilingi bilioni 8.15 ikiwa ni kifuta jasho na machozi kwa wananchi 22,696 waliopatwa na madhara ya wanyamapori katika halmashauri za wilaya 81.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea kutumia mbinu mbalimbali ili kuhakikisha uharibifu unaosababishwa na wanyamapori wakali na waharibifu unadhibitiwa kwa kiwango kikubwa. Ninatoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu na wananchi kwa ujumla kuendelea kuiunga mkono Serikali katika jitihada za kukabiliana na matukio ya wanyamapori hao kwa kutoa taarifa kwa wakati, kuchukua tahadhari dhidi ya wanyamapori hao na kuzingatia maelekezo yanayotolewa na wataalamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyoahidi mwaka 2025, Serikali imeongeza juhudi za kukabiliana na changamoto hii kwa kutekeleza mipango madhubuti, kama inavyoonekana kwa kina kuanzia ukurasa wa 36 - 44 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Ufugaji Nyuki kwa Tanzania Iliyo Bora Inayofahamika Kama Achia

Shoka Tundika Mzinga. Katika kuendelea kuwawezesha wananchi kunufaika na rasilimali za misitu kupitia ajira na uchumi wa kijani, Wizara inaendelea kutekeleza mpango maalum wa kuendeleza sekta ya ufugaji nyuki ujulikao kama Achia Shoka, Tundika Mzinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mpango huu, vikundi 236 vyenye wafugaji nyuki 4,934 vimepatiwa mafunzo ya ufugaji nyuki kibiashara na mizinga ya kisasa 9,215 kusambazwa nchini. Vilevile Wizara imeanza ujenzi wa kiwanda cha kuongeza thamani mazao ya nyuki Wilayani Kaliua, ambapo kwa sasa ujenzi umefikia 40%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hizi zinaendelea kufungua fursa za ajira, kuongeza kipato cha wananchi na kuchochea matumizi endelevu ya rasilimali za misitu na nyuki. Maelezo kuhusu utekelezaji wa mpango huu yamefafanuliwa kwa kina katika ukurasa wa 85 hadi 86 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa kuleta mbele yako Mpango na Bajeti wa Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara imejipanga kutekeleza vipaumbele tisa, kama ifuatavyo: -

(1) Kuimarisha utangazaji utalii ndani na nje ya nchi kwa kutumia mikakati mahususi ikiwemo masoko ya mashariki ya mbali na mashariki ya kati;

(2) Kuendeleza na kuboresha mazao ya utalii ya kimkakati ikiwemo utalii wa meli, mikutano na matukio (kama nilivyoeleza awali) pamoja na kutambua na kusajili mazao mapya;

(3) Kuimarisha miundombinu wezeshi katika maeneo ya utalii na hifadhi ikiwemo barabara, viwanja vya ndege, mawasiliano na huduma za kijamii;

(4) Kuimarisha ulinzi, uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori, misitu, nyuki na malikale;

(5) Kuimarisha uzalishaji, uongezaji thamani na masoko ya mazao ya misitu na nyuki;

(6) Kuimarisha matumizi ya teknolojia za kisasa katika usimamizi wa rasilimali, ulinzi, ufuatiliaji, ukusanyaji wa mapato pamoja na utangazaji wa utalii;

(7) Kufanya mapitio ya sera, sheria, kanuni na miongozo ili kuendana na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kiteknolojia;

(8) Kuimarisha utafiti ubunifu na maendeleo ya rasilimali watu; na

(9) Kuboresha mazingira ya kazi mifumo ya usimamizi wa utendaji na uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukusanyaji wa Maduhuli. Katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Wizara inakadiria kukusanya jumla ya shilingi trilioni 1.48 kutoka kwenye idara na taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Wizara iweze kutekeleza malengo na vipaumbele iliyojiwekea, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 334,345,870,000 kwa matumizi ya Fungu – 69 kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Kati ya fedha hizo, shilingi 272,044,425,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 62,301,445,000 ni za Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha Mishahara shilingi 144,691,490,000 na Matumizi Mengineyo shilingi 127,352,935,000. Fedha za Miradi ya Maendeleo zinajumuisha shilingi 23,134,770,000 ambazo ni fedha za ndani na shilingi 39,166,675,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa namna ya kipekee kuyashukuru na kuyatambua mashirika na taasisi za Kimataifa, pamoja na wadau wa ndani ambao wameendelea kushirikiana na Serikali katika kuimarisha sekta ya maliasili na utalii, kama walivyotajwa kwa urefu wake katika kitabu cha hotuba yangu. Ushirikiano wao umeendelea kuwa nguzo muhimu katika

kuhifadhi, kulinda na kuendeleza maliasili, malikale na utalii kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa rai kwa Watanzania wenzangu kuendelea kushiriki kikamilifu katika kuendeleza utalii, uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili na malikale ambazo ni urithi wa Taifa letu na mhimili muhimu wa ukuaji wa uchumi. Uhifadhi wa rasilimali hizi siyo jukumu la Serikali pekee, bali ni wajibu wa kila Mtanzania kuhakikisha tunalinda na kuendeleza hazina hii muhimu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka kuwa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, wakati akizindua Bunge la Kumi na Tatu, alieleza dhamira yake ya kuacha tabasamu la utu kwenye nyuso za Watanzania mwisho wa utumishi wa Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi, kama sekta, tuna wajibu wa kutafsiri maono hayo na kuimarisha ustawi wa wananchi wetu, hususan kuongeza ajira, kipato, fursa za kibiashara na kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi yanayotokana na uhifadhi endelevu wa maliasili na maendeleo ya sekta ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ni wajibu wetu sote kufanya kazi kwa bidii, ili kufikia malengo ya Taifa ya kuongeza idadi ya watalii kufikia milioni nane mwaka 2030 na kuongeza mchango wa sekta yetu ya utalii katika pato la Taifa, kufikia 20%, kama tulivyoelekezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijahitimisha hotuba yangu, ninapenda kutumia fursa hii kuwakaribisha Waheshimiwa Wabunge wote kutembelea maonesho yaliyoandaliwa na Wizara katika Viwanja vya Bunge. Maonesho haya yanatoa fursa ya kujionea mafanikio, huduma, bidhaa na ubunifu mbalimbali unaotekelezwa katika sekta ya maliasili na utalii. Aidha, katika maonesho haya, ipo pia huduma ya tiba ya kudungwa na nyuki, ambayo imekuwa ikivutia watu wengi kutokana na manufaa yake mbalimbali kiafya, ikiwemo kuimarisha kinga ya miili yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa ninaomba kutoa shukrani zangu za dhati kwako, kwa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote walionifuatilia na kunisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kama inavyoonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. ASHATU KIJAJI (MB) WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2026/2027 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, ambayo imepitia na kuchambua Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema na Fadhila kwa kutujalia afya njema na hekima ya kutekeleza majukumu tuliyokasimiwa na Watanzania kwa ufanisi, uwajibikaji na kuzingatia maslahi mapana ya Taifa letu. Aidha, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama kwa mara ya kwanza nikiwa Waziri wa Maliasili na Utalii mbele ya Bunge la 13 kuwasilisha Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

## 1.1 SHUKURANI NA PONGEZI

3. **Mheshimiwa Spika,** wahenga wanasema: **"Nguzo Imara Haisukumwi na Upepo"** ninapenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuaminiwa na Watanzania na kuchaguliwa kuongoza nchi yetu kwa kipindi cha pili cha Awamu ya Sita kupitia Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Oktoba 2025. Uongozi wake thabiti na wenye dira umeendelea kuimarisha uwazi na kuleta tija katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Aidha, katika kipindi cha Awamu ya Sita, nchi yetu imeshuhudia mwelekeo imara wa uendeshaji wa Serikali unaojengwa katika misingi ya utawala bora, maridhiano, utu na uwajibikaji uliowezesha kuimarika kwa usimamizi wa rasilimali za Taifa ikiwemo uhifadhi endelevu wa rasilimali za wanyamapori, misitu, nyuki na malikale pamoja na kuongeza thamani ya rasilimali hizi. Hatua iliyochochea mchango wa sekta hii katika Pato la Taifa, ajira na mapato ya fedha za kigeni. Tunamwombea afya njema, hekima na busara katika kutekeleza majukumu yake kwa maendeleo endelevu na jumuishi ya Watanzania.

4. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee, ninapenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na kumteua Mheshimiwa Hamad Hassan Chande (Mb.), kuwa Naibu Waziri. Mimi pamoja na viongozi wenzangu katika Wizara hii, tunamuahidi Mheshimiwa Rais kuwa tutatekeleza dhamana tuliyopewa kwa ushirikiano, weledi, uadilifu, utu na uwajibikaji katika kuhakikisha sekta ya Utalii pamoja na rasilimali za maliasili na malikale zinasimamiwa kwa uendelevu ili kuchangia ukuaji wa uchumi nchini.

5. **Mheshimiwa Spika,** ninampongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninapenda kumpongeza kwa kazi kubwa anayoifanya katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kuwaletea wananchi maendeleo. Vilevile, ninamshukuru kwa dhati kwa maelekezo na miongozo yake ambayo imekua chachu katika kukabiliana na

mabadiliko ya tabianchi, kuimarisha uhifadhi endelevu wa rasilimali za maliasili pamoja na uendelezaji wa utalii kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

**6. Mheshimiwa Spika,** ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuaminiwa tena na wananchi na kuchaguliwa kuendelea kushika wadhifa huo kupitia Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025. Nimpongeze pia kwa uongozi wake ambao umeendelea kuweka msingi thabiti wa kukuza shughuli za kiuchumi na kuimarisha ustawi wa wananchi wa Zanzibar. Aidha, nimpongeze kwa ushirikiano thabiti katika kuendeleza na kuimarisha sekta ya utalii nchini.

**7. Mheshimiwa Spika,** vilevile ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Iramba Magharibi kwa kuaminiwa na kuteuliwa kushika wadhifa huo. Ninamshukuru pia kwa uongozi wake na miongozo yake inayoendelea kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Kupitia miongozo hiyo, Wizara imefanikiwa kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maliasili na malikale, kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za utalii pamoja na kuchochea ukuaji wa mapato yatokanayo na sekta hizo kama mhimili muhimu wa uchumi wa Taifa letu.

**8. Mheshimiwa Spika,** kwa dhati kabisa, ninaomba nikupongeze wewe binafsi, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Ilala kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuongoza Bunge letu Tukufu. Ni wazi kuwa uongozi wako umeendelea kuimarisha hadhi ya Bunge, nidhamu ya mijadala na ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yake ya kikatiba. Aidha, Wizara imeendelea kunufaika kwa kiasi kikubwa na uongozi wako kupitia usimamizi madhubuti wa mijadala ya kibunge, ushauri na maelekezo yanayosaidia kuboresha sera, sheria na utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Maliasili na Utalii.

**9. Mheshimiwa Spika,** nimpongeze pia Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini kwa kuchaguliwa na kwa mchango wake muhimu katika kukusaidia kuendesha shughuli za Bunge kwa ufanisi. Vilevile, niwapongeze Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb.); Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika (Mb.); na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso (Mb.) kwa kuchaguliwa na umahiri wao katika kusimamia mijadala ya Bunge na kuliwezesha Bunge lako Tukufu kuimarisha uwajibikaji.

**10. Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee, ninaomba kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya uongozi wa Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava (Mb.), Mwenyekiti; Mheshimiwa Mary Francis Masanja (Mb.), Makamu Mwenyekiti; na Wajumbe wote wa Kamati kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwa wasimamizi wakuu wa majukumu ya Bunge katika kusimamia na kuishauri Serikali kuhusu usimamizi endelevu wa ardhi, maliasili na maendeleo ya sekta ya utalii nchini. Aidha, nawashukuru kwa mchango wao mkubwa katika kuchambua na kutoa ushauri kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Wizara inathamini ushauri huo na itaendelea kuuzingatia ili kuimarisha utendaji wa sekta na kuongeza mchango wake katika ukuaji jumuishi wa uchumi wa Taifa. Vilevile, niwapongeze Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote za Kudumu za Bunge kwa kuendelea kuisimamia na kuishauri Serikali kwa weledi na ufanisi.

**11. Mheshimiwa Spika,** ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano na ushauri wao wenye tija katika kuimarisha uhifadhi na usimamizi endelevu wa rasilimali za maliasili na malikale pamoja na maendeleo ya Sekta ya Utalii nchini. Niwahakikishie kuwa Wizara itaendelea kuyafanyia kazi maoni na ushauri huo kwa vitendo ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yake na kuhakikisha manufaa hayo yanawafikia Watanzania wote kwa usawa na kuleta tija.

**12. Mheshimiwa Spika,** ninatumia fursa hii pia kuwapongeza na kuwashukuru Mawaziri wenzangu, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wa Wizara

mbalimbali kwa ushirikiano wao wenye tija katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Kama wahenga wanavyosema, **“Figa moja haliinjiki chungu,”** ushirikiano huu umeendelea kuimarisha uratibu wa kazi za Serikali na kuongeza ufanisi katika kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa. Ninathamini sana mchango wao, kwa pamoja tutaendelea kujenga Taifa lenye nguvu na ustawi zaidi.

**13. Mheshimiwa Spika,** ninaomba kunukuu hekima ya wahenga isemayo, “**Mti mmoja haufanyi msitu,”** usemi huu umedhihirika wazi katika utendaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwamba umoja, ushirikiano na mshikamano ndiyo mafanikio yetu. Nitumie fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru viongozi pamoja na watendaji Wakuu wa Wizara kwa ushirikiano wao mkubwa, uzalendo na kujituma katika kusimamia na kutekeleza majukumu ya sekta kwa ufanisi. Kipekee, namshukuru Mheshimiwa Hamad Hassan Chande (Mb.), Naibu Waziri, kwa mchango wake katika kuratibu na kusimamia shughuli za Wizara kwa weledi. Aidha, nampongeza Dkt. Hassan Abbasi, Katibu Mkuu pamoja na Bwana Nkoba Mabula, Naibu Katibu Mkuu (Utalii) kwa uongozi thabiti, weledi na usimamizi madhubuti wa shughuli za Wizara.

**14. Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee ninawashukuru pia watendaji wote wa Wizara wakiwemo Wakurugenzi wa Idara, Wakuu wa Vitengo, Wenyeviti wa Bodi, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ambazo ni Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania – TANAPA, Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro – NCAA, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania – TAWA, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania - TFS, Shirika la Makumbusho ya Taifa la Tanzania - NMT, Bodi ya Utalii Tanzania - TTB, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania - TAWIRI, Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania - TAFORI, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka - CAWM, Chuo cha Taifa cha Utalii - NCT, Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi - PWTI, Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii Likuyu Sekamaganga - CBCTC, Chuo cha Misitu Olmotonyi - FTI, Kituo cha Mafunzo ya Misitu na Viwanda vya Misitu – FWITC, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora - BTI, Chuo cha Viwanda vya Misitu - FITI na Mfuko wa Misitu Tanzania – TaFF pamoja na

Watumishi wote kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Ninawapongeza kwa moyo wa kujituma, uwajibikaji na uzalendo wao katika kulinda, kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za Taifa. Ninawatakia afya njema, ari na nguvu ya kuendelea kulitumikia Taifa kwa bidii ili kuhakikisha malengo na vipaumbele vya Serikali vinafikiwa kwa ufanisi na kwa manufaa mapana ya Watanzania wote.

**15. Mheshimiwa Spika,** kama wahenga wasemavyo "**Mwenda Tezi na Omo Marejeo Ngamani",** kwa namna ya kipekee, ninawashukuru kwa dhati wananchi wa Jimbo la Kondoa kwa kuendelea kuniamini na kunichagua kuwa Mbunge wao. Aidha, ninawashukuru kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kuwatumikia, kuwawakilisha katika Bunge hili Tukufu na kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo katika Jimbo letu. Ninaomba nitumie fursa hii kuwaahidi kuwa nitaendelea kuwa mtumishi wao na muda wote nitadumu katika kuwatumikia kwa umahiri na moyo wa dhati.

**16. Mheshimiwa Spika,** kwa upendo mkuu, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mama yangu mpendwa, Hajat Aziza Selemani kwa malezi bora, maadili mema na msaada wake usioyumba ulionifikisha hapa nilipo leo. Aidha, ninampongeza na kumshukuru kwa dhati mume wangu mpendwa Dkt. Muhajir Kachwamba pamoja na watoto wangu Samirah na Aboubakar kwa upendo wao, subira na uelewa ambavyo vimekuwa nguzo muhimu katika kunipa nguvu na motisha ya kutekeleza majukumu yangu ya kila siku kwa ufanisi. Vilevile, nawashukuru viongozi wangu wa dini, ndugu, jamaa na marafiki wote kwa kuniunga mkono na kuniombea ili niendelee kutekeleza wajibu wangu ipasavyo. Ninaomba kuwahakikishia nyote pamoja na Watanzania kwa ujumla kwamba nitaendelea kufanya kazi kwa bidii, uadilifu na uzalendo mkubwa katika kuwatumikia wananchi na Taifa letu kwa kuzingatia misingi ya haki, utu na uwajibikaji.

## 1.2 SALAMU ZA POLE

**17. Mheshimiwa Spika,** kwa masikitiko makubwa ninatoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, wanafamilia, Bunge lako Tukufu, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) na Mbunge wa Jimbo la Isimani. Tutaendelea kumkumbuka kwa mchango wake mkubwa katika kuendeleza kwa vitendo misingi ya ushirikishwaji, uwajibikaji na uratibu madhubuti wa utekelezaji wa sera na programu za maendeleo ili kuhakikisha hakuna Mtanzania anayebaki nyuma.

**18. Mheshimiwa Spika,** pia nitoe pole kwako na Waheshimiwa Wabunge kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho; na Mheshimiwa Halima Idd Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (Wafanyakazi). Kwa namna ya pekee, naungana na Watanzania wote kuwapa pole familia, ndugu, jamaa na marafiki kwa kuondokewa na wapendwa wetu.

**Tunamuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.**

**19. Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia hali halisi ya matukio ya kiuhifadhi yanayohusisha migongano kati ya binadamu na wanyamapori katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, ninatoa pole za dhati kwa ndugu, jamaa, marafiki na wananchi waliopoteza wapendwa wao kwa kushambuliwa na wanyamapori wakali na waharibifu pamoja na wananchi ambao walijeruhiwa au mali zao kuharibiwa na wanyamapori hao katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Matukio haya yanatukumbusha wajibu na umuhimu wa kuendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi wa maeneo ya hifadhi pamoja na kuongeza ushirikiano kati ya Serikali na wananchi wanaoishi jirani na maeneo hayo. Naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali itaendelea kuchukua hatua madhubuti za kupunguza athari za migongano hiyo ili kulinda maisha ya wananchi na mali zao sambamba na kuhakikisha uhifadhi endelevu wa rasilimali zetu za Taifa.

**20. Mheshimiwa Spika,** ninaomba pia kutambua mchango

wa dhati wa Maafisa na Askari Shupavu wa Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu ambao wameendelea kutekeleza majukumu yao kwa ujasiri na weledi katika kulinda na kuhifadhi maliasili za Taifa letu zikiwemo wanyamapori, misitu, nyuki na malikale. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, maafisa na askari watatu (3) walipoteza maisha wakiwa kazini wakitimiza wajibu wao kwa Taifa na wengine 15 walipata majeraha. Mashujaa wetu waliofariki wakitekeleza majukumu yao ni: Askari wa Uhifadhi Daraja la III, Victor Jackson Laizer kutoka TANAPA; na Askari wa Uhifadhi Daraja la I, Ally Sakasa Kajogoro na Askari wa Uhifadhi Daraja la II, Enock Gration Rugaimukamu kutoka TAWA. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awajalie afya njema waliojeruhiwa na azipumzishe roho za marehemu wapendwa wetu mahali pema peponi, Amina.

**21. Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, ninaomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

## 2.0 MGAWANYO WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

**22. Mheshimiwa Spika**, maelekezo ya mgawanyo wa majukumu yaliyotolewa na Hati Idhini ya Rais (Presidential Instrument) ya tarehe 19 Desemba, 2025 kupitia Tangazo la Serikali Namba 685 yanaainisha majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kama ifuatavyo: -

i. Kuandaa Sera za Misitu, Ufugaji nyuki, Wanyamapori, Malikale, Makumbusho na Utalii na kusimamia utekelezaji wake;
ii. Kusimamia misitu na upandaji miti;
iii. Kusimamia maendeleo ya Ufugaji nyuki;
iv. Kusimamia Hifadhi za Taifa, uendelezaji wa Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu na ulinzi wake;
v. Kuhamasisha uanzishwaji wa mashamba ya wanyamapori, ranchi na bustani za wanyamapori zinazomilikiwa na watu binafsi;
vi. Kuratibu, kukuza na kuendeleza vivutio vya utalii;
vii. Kubainisha, kuendeleza na kukuza mazao mapya ya utalii;


viii. Kusimamia Urithi wa Taifa, Malikale na Makumbusho;
ix. Kusimamia shughuli za Jeshi la Uhifadhi;
x. Kuimarisha utendaji na kuendeleza rasilimali watu wizarani; na
xi. Kusimamia Taasisi na miradi chini ya Wizara.

## 3.0 MAFANIKIO YA SEKTA YA MALIASILI NA UTALII KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**23. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 chini ya uongozi mahiri na shupavu wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhifadhi na Muongoza Watalii Namba Moja nchini, Serikali imefanikiwa katika Sekta ya Maliasili na Utalii kama ifuatavyo:-

**(i) *Kuongezeka kwa Idadi ya Watalii***

Tanzania imefanikiwa kuongeza idadi ya watalii kufikia 5,935,561 mwaka 2025 ikiwa ni ongezeko la asilimia 10.7 ikilinganishwa na watalii 5,360,247 mwaka 2024. Ongezeko hili linajumuisha watalii wa kimataifa walioongezeka kwa asilimia 7.1 kutoka 2,141,895 mwaka 2024 hadi 2,294,495 mwaka 2025 na watalii wa ndani walioongezeka kwa asilimia 13.1 kutoka 3,218,352 mwaka 2024 hadi 3,641,066 mwaka 2025. Ukuaji huu pia umeonekana katika mizania ya dunia ambapo taarifa ya Shirika la Utalii Duniani (UN Tourism) imeonesha, kidunia Tanzania imeshika nafasi ya 11 mwaka 2025 kwa ongezeko la wageni wa kimataifa (51%) ukilinganisha na mwaka 2019 kabla ya janga la UVIKO 19. Vilevile, Tanzania imekuwa ya 6 kwa kanda ya Afrika, na Mashariki ya Kati kwa ongezeko la wageni wa kimataifa ukilinganisha na mwaka 2019. Taarifa hizi zinaonesha uwekezaji uliofanywa na serikali ya awamu ya sita (6) unaendelea kuleta matunda mema. Pamoja na ongezeko la wageni wa kimataifa, Tanzania katika mizania ya utalii mwaka 2025 imeshika nafasi ya tatu duniani kwa soko la utalii lililofanya vizuri ukilinganisha na 2024 ambapo watalii walitumia fedha kwa wingi (best performing market by spending).




*Ukuaji wa Utalii wa Tanzania kama inavyooneshwa na Shirika la Utalii Duniani (UN Tourism), Januari 2026*

**(ii) *Kuongezeka kwa Mapato Yatokanayo na Utalii***

Hadi kufikia Desemba 2025, mapato ya jumla yatokanayo na shughuli za utalii nchini yameongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 3.9 mwaka 2024 hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 4.4 mwaka 2025 ikiwa ni ongezeko la asilimia 12.82. Hatua hii imeifanya sekta ya utalii nchini kuwa namba mbili (2) kwa kuingiza fedha za kigeni nchini ikitanguliwa na Sekta ya Madini. Mafanikio hayo yamechangiwa na juhudi mbalimbali zikiwemo kuongezeka kwa utangazaji utalii, uboreshaji wa miundombinu ya utalii na huduma na matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato.

**(iii) *Tanzania Kuendelea Kushinda Tuzo Mbalimbali na Kutambulika Kimataifa***

Tanzania imefanikiwa kushinda tuzo mbalimbali za kimataifa za

utalii zikiwemo Tuzo kubwa za World Travel Awards, tukio lililofanyika katika Jiji la Manama nchini Bahrain. Tuzo zilizotolewa ni Tanzania kutangazwa kuwa Nchi Bora ya Utalii wa Safari Duniani 2025 (World's Leading Safari Destination 2025) ikiwa ni kwa mara ya tatu (3) mfululizo kuanzia mwaka 2023; Hifadhi ya Taifa Serengeti kushinda Tuzo ya Hifadhi Bora Duniani (World's Leading National Park 2025), ushindi unaoifanya Hifadhi hii kuendelea kuwa moja ya Maajabu ya Dunia yenye mandhari, wanyamapori na tukio la kipekee la Uhamaji wa Nyumbu (The Great Wildebeest Migration); na Zanzibar kutangazwa kuwa Eneo Bora la Mikutano na Matukio ya Biashara. Aidha, wadau wa sekta binafsi nao walishinda tuzo mbalimbali za kimataifa ikiwemo Hoteli ya Jummeirah iliyopo kwenye Kisiwa cha Thanda kushinda Tuzo ya World's Leading Exclusive Private Island na Serengeti Balloon Safaris kushinda Tuzo ya World's Leading Hot Air Ballon Safari. Katika hatua nyingine, Wizara imekuja na ubunifu wa kutoa Tuzo za Uhifadhi na Utalii za The Serengeti Awards zilizofanyika Januari, 2026 ambazo zilichangia kuongeza wigo wa utangazaji wa vivutio vya utalii na huduma. Mafanikio haya yameimarisha hadhi ya Tanzania kimataifa, kuongeza ushindani wa Sekta ya Utalii katika utoaji wa huduma bora pamoja na kuchangia ongezeko la watalii na uwekezaji nchini.



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akiwa na Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb.), na Naibu Waziri Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb.), mara baada ya kukabidhiwa Tuzo za World Travel Awards 2025 katika Ikulu Ndogo Tunguu, Zanzibar.*

### (iv) *Kuimarika kwa Miundombinu ya Utalii*

Katika kuimarisha ushindani wa Sekta ya Utalii na kuongeza

mchango wake katika uchumi wa Taifa, Serikali imeendelea kuwekeza kwa kiwango kikubwa katika maendeleo ya miundombinu ya utalii nchini. Katika kipindi cha utekelezaji, Serikali imekamilisha ujenzi wa viwanja vya ndege vitatu (3) katika Hifadhi za Taifa za Nyerere (1) na Ruaha (2). Aidha, ujenzi wa Kiwanja cha Mikumi utakamilika kufikia Oktoba, 2026. Vilevile, Wizara imekarabati viwanja vya ndege nane (8) katika Hifadhi za Taifa za Mikumi (1), Ruaha (2), Nyerere (2) na Serengeti (3).



*Kiwanja cha ndege katika Hifadhi za Taifa Ruaha*

Aidha, jumla ya kilomita 3,757.92 za barabara na kilomita 523.14 za njia za watembea kwa miguu zimejengwa na kukarabatiwa katika maeneo yaliyohifadhiwa ili kurahisisha ufikaji kwenye vivutio vya utalii. Vilevile, miundombinu ya huduma za utalii imeimarishwa kupitia ujenzi wa maeneo sita (6) ya mapumziko kwa wageni na malango tisa (9) ya kuingilia wageni katika Hifadhi za Taifa za Nyerere, Mikumi na Ruaha pamoja na vituo vya utalii katika misitu ya Meru, Vikindu, Mwambesi, Pindiro, Mlima Rungwe na Ziwa Duluti. Sambamba na hilo, kambi moja (1) ya watalii imejengwa katika Hifadhi ya Misitu ya Mazingira Asilia ya Kilombero.



*Miundombinu ya Utalii katika Hifadhi ya Taifa Nyerere*

Uwekezaji huu umeleta matokeo chanya yanayoonekana kwa kuongeza urahisi wa kufikia vivutio vya utalii, kuboresha uzoefu wa wageni na kufungua fursa za ajira na biashara kwa wananchi wanaoishi jirani na maeneo ya hifadhi. Aidha, umechangia ongezeko la mapato ya Serikali na ukuaji wa sekta kwa ujumla. Mathalan, katika Ukanda wa Kusini, maboresho haya yamewezesha ongezeko la watalii kutoka 197,402 hadi kufikia 205,520 na mapato kuongezeka kutoka Shilingi bilioni 24.6 hadi bilioni 27.7 katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili, 2026. Mafanikio haya yanaakisi dhamira ya Serikali ya kuendelea kuimarisha miundombinu ya utalii ili kuongeza ushindani wa Tanzania kimataifa, kuchochea ukuaji wa uchumi na kuboresha ustawi wa wananchi.

**(v) *Kukamilika kwa Sensa ya Wanyamapori Nchini***

Wizara imekamilisha kwa mafanikio makubwa zoezi la sensa ya kitaifa ya wanyamapori nchini. Sensa kama hii ni ya pili kufanyika na hufanyika kila baada ya miaka 10, ikiwa ni sehemu ya Mpango wa Kitaifa wenye lengo la kubaini uwepo, idadi, mtawanyiko na mienendo ya wanyamapori, sambamba na kubaini viashiria hatarishi vinavyoweza kuathiri ustawi na mazingira yao kwa kulinganisha na matokeo ya awali. Aidha, sensa hii imefanyika kwa kutumia fedha za ndani kwa mara ya kwanza tofauti na sensa ya awali, hatua inayodhihirisha uwezo na dhamira ya Serikali katika kugharamia na kusimamia shughuli za kimkakati za uhifadhi.

Matokeo ya sensa yanaonesha mwenendo chanya wa ongezeko na ustawi wa wanyamapori katika mifumo ikolojia mbalimbali, hali inayothibitisha mafanikio ya juhudi za Serikali katika kuimarisha uhifadhi endelevu wa rasilimali hizi. Aidha, takwimu zilizopatikana ni nyenzo muhimu katika kupanga matumizi bora ya rasilimali ikiwemo uwindaji endelevu, kubaini na kulinda jamii za wanyamapori zilizo hatarini kutoweka pamoja na kusaidia kupanga mikakati madhubuti ya kukabiliana na changamoto za shughuli za kibinadamu katika mifumo ikolojia. Vilevile, Takwimu hizi zitasaidia katika kuelekeza uwekezaji wa

miundombinu ya utalii, kuongeza mapato ya Serikali pamoja na kufungua fursa za ajira na biashara kwa wananchi wanaozunguka maeneo ya hifadhi.

**(vi) *Kuongezeka kwa Soko la Asali ya Tanzania Kimataifa***

Kiwango cha asali kinachouzwa nje ya nchi kimeongezeka kutoka tani 951.6 mwaka 2024 hadi tani 1,596.8 mwaka 2025 sawa na ongezeko la asilimia 67.85. Aidha, thamani ya mauzo ya asali imeongezeka kutoka Shilingi bilioni 11.4 kwa mwaka 2024 hadi Shilingi bilioni 19.2 mwaka 2025 sawa na ongezeko la asilimia 68.4. Mafanikio haya yanatokana na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali katika kuimarisha Sekta ya Ufugaji Nyuki na upatikanaji wa masoko ya kimataifa, wafugaji nyuki na wadau wa maendeleo katika kuongeza kiwango cha uzalishaji wa asali inayokidhi viwango vya kimataifa. Moja ya nguzo kuu iliyochangia mafanikio haya ni utekelezaji wa mpango madhubuti wa udhibiti wa mabaki ya kemikali katika asali. Asali ya Tanzania imeendelea kukidhi ubora kwa wastani wa asilimia 97 kwa viwango vya Umoja wa Ulaya kwa miaka mitatu mfululizo, jambo lililoongeza fursa za masoko ya nje ya nchi kama vile Marekani, nchi za Umoja wa Ulaya, Umoja wa Falme za Kiarabu na China. Aidha, kwa mara ya kwanza asali ya Tanzania imefanikiwa kuuzwa katika soko la Uingereza baada ya kukidhi vigezo vya soko hilo.

**(vii) *Kuimarika kwa Hadhi ya Tanzania Kimataifa katika Uhifadhi na Usimamizi wa Urithi wa Dunia***

Tanzania imeendelea kuthibitisha umahiri wake Duniani katika uhifadhi na usimamizi wa maeneo ya urithi wa Dunia ambapo imechaguliwa kuwa mjumbe wa Kamati ya Urithi wa Dunia katika kipindi cha miaka minne (4) kuanzia mwaka 2025 hadi 2029. Kwa nafasi hiyo, Tanzania imeingia katika chombo cha juu cha UNESCO chenye jukumu la kufanya maamuzi kuhusu uhifadhi na usimamizi wa maeneo ya urithi wa Dunia kinachojumuisha nchi 21 kati ya 195. Kupitia ujumbe huo, Tanzania ina fursa ya kushiriki katika maamuzi ya kuongeza au kuondoa maeneo katika orodha ya urithi wa Dunia.

**(viii)** ***Kukamilisha Ujenzi na Kuzindua Makumbusho ya Jiopaki ya Ngorongoro - Lengai***

Wizara imekamilisha ujenzi wa miundombinu ya utalii na kuzindua Makumbusho ya kisasa ya Jiopaki ya Ngorongoro-Lengai iliyopo katika eneo la Kamyn Wilaya ya Karatu, Arusha ambayo ni makumbusho ya pili ya aina hiyo barani Afrika baada M'Guon iliyopo Morocco. Hatua hii imeongeza zao jipya la utalii wa jiolojia ambalo pia litakuza utafiti wa kisayansi na elimu ya miamba, kuwezesha jamii na wanafunzi kujifunza historia ya sayansi na mazingira, kuongeza ajira na kipato kwa wananchi wa maeneo jirani na kuimarisha nafasi ya Tanzania kimataifa kama kinara wa uhifadhi, utalii na elimu ya miamba. Hatua hii pia ni miongoni mwa mikakati ya Wizara katika kuliongezea thamani Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro ambalo mwaka 2018 lilipewa hadhi ya jiopaki inayotambuliwa na UNESCO na kuwa jiopaki pekee yenye hadhi hiyo katika Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara.



*Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb.), akiwa ameambatana na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge*

*ya Ardhi, Maliasili na Utalii wakati wa ziara ya kutembelea Makumbusho ya Jiopaki ya Ngorongoro – Lengai*

### (ix) *Mageuzi ya Kidijitali katika Sekta ya Uhifadhi na Utalii*

Wizara imefanya maboresho ya mfumo wa **MNRT Portal**, ambao umekuwa ukitumiwa na Wizara pamoja na taasisi katika kusimamia utoaji wa huduma mbalimbali ikiwemo leseni za shughuli za utalii, huduma za malazi, uwindaji wa kitalii, minada ya vitalu na vibali vya kuingia katika vivutio vya utalii. Maboresho hayo yamelenga kuboresha uzoefu wa watumiaji, kuhuisha teknolojia ili mfumo uweze kuendana na mahitaji ya sasa pamoja na kufungamanisha na mifumo mingine inayotoa huduma za utalii na kurahisisha utoaji wa huduma kufanyika kwa ufanisi na tija.

Wizara imeanzisha mfumo wa **Problem Animals Information System (PAIS)** mahsusi kwa ajili ya kusimamia taarifa za matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu pamoja na kuratibu na kuwezesha ulipaji wa vifuta jasho/machozi kwa wananchi wanaoathirika na matukio hayo. Mfumo huo umerahisisha ukusanyaji, uwasilishwaji wa taarifa sahihi na kuepuka udanganyifu, uchakataji, utunzaji wa taarifa za matukio ya uharibifu wa wanyamapori wakali na waharibifu. Vilevile, mfumo umerahisisha malipo ya kifuta jasho na machozi kwa wananchi waliopata madhara ya wanyamapori wakali na waharibifu ambapo kwa sasa taratibu za malipo zinachukua siku saba (7) hadi 14 tofauti na taratibu za awali ambapo malipo yakichukua miezi sita (6) hadi 12. Sambamba na hilo, mfumo umeongeza uwazi na uwajibikaji kwa kuwa mfumo unawezesha kufuatilia kila muamala.

Kufuatia agizo la kufungamanisha mifumo ya Serikali lililotolewa na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, Wizara imeanzisha jukwaa la kidijitali (FARU GATEWAY) la kubadilishana taarifa kati ya mifumo ya Wizara na Taasisi zake. Jukwaa hili limefungamanishwa na Mfumo wa Serikali wa Kuwasiliana na Kubadilishana Taarifa (GovESB) hivyo kufanya taarifa za Sekta ya Maliasili na Utalii kubadilishana taarifa na Taasisi zilizopo katika sekta nyingine za Serikali, hatua hii

imeongeza ufanisi, tija na ushirikiano katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

Wizara imeendelea kufanya mageuzi ya kidijitali katika Sekta ya Utalii kwa kuanzisha mfumo wa kisasa unaojulikana kama Tanzania Travel Companion, ambao ni sehemu ya utekelezaji wa kituo cha Uendeshaji wa Masoko ya Utalii Kidijitali (DDMCC). Mfumo huo umelenga kuboresha uzoefu wa mtalii (travel experience) kuanzia hatua ya upangaji wa safari, wakati wa safari na baada ya safari. Aidha, kupitia mfumo huo watalii wataweza kupanga safari zao kabla ya kuwasili nchini kwa kupata taarifa sahihi, kufanya booking ya huduma mbalimbali zikiwemo malazi, migahawa, usafiri na vivutio vya utalii, pamoja na taarifa kuhusu maeneo ya vivutio yasiyo maarufu (hidden gems) yaliyopo katika miji yetu. Vilevile, mfumo umefungamanishwa na Mifumo ya Taasisi za Wizara ili kurahisisha malipo ya huduma mbalimbali ikiwemo ada za viingilio, malazi katika hoteli/loji, kambi za kitalii na magari katika vivutio kwa lengo la kuongeza ufanisi na kupunguza gharama katika ukusanyaji wa mapato.

Mfumo huu pia umejumuisha ramani ya kidijitali ya vivutio na huduma muhimu kwa watalii pamoja na chatbot ya akili unde (AI Chatbot) itakayotoa mwongozo wa papo kwa papo kwa watalii kwa lugha za kimataifa zaidi ya 56. Aidha, Mfumo huu unatarajiwa kuwa na mchango mkubwa katika maandalizi na wakati wa michuano ya AFCON 2027 kwa kuwezesha upatikanaji wa taarifa sahihi na huduma za utalii kwa urahisi kwa wageni watakaotembelea nchi yetu. Kupitia DDMCC na Travel Companion, taarifa na mwenendo wa soko la utalii zitachakatwa kwa wakati ili kuwezesha maamuzi ya kimkakati katika kukuza na kulinda chapa ya utalii wa Tanzania pamoja na kuongeza muda wa wageni kukaa nchini na hivyo kuongeza mapato ya utalii yatakayochangia kwa kiasi kikubwa katika pato la Taifa.

## 4.0 FURSA NA MIKAKATI YA KUKUZA UTALII KUPITIA MATUKIO YA KIMATAIFA YATAKAYOFANYIKA NCHINI

**24.** **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Utalii ni sekta ya kimkakati na ya kimageuzi katika kuchochea maendeleo ya kiuchumi na

kijamii nchini ambapo Ibara ya 23 ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 inaelezea umuhimu wa Sekta ya Utalii katika kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Aidha, katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii, Chama cha Mapinduzi kimeielekeza Serikali kuongeza wigo wa mazao ya utalii na kuendelea kuitangaza hazina ya utalii kwa mbinu za kisasa ili kuongeza idadi ya watalii. Lengo ni kuongeza mchango wa Sekta ya Utalii katika Pato la Taifa kutoka asilimia 17 mwaka 2025 hadi asilimia 20 mwaka 2030.

**25.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuzingatia maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2025–2030) kuhusu kuimarisha Sekta ya Utalii, Wizara imeendelea kutumia utalii wa mikutano na matukio (MICE) kama nyenzo muhimu ya kukuza uchumi kwa kuongeza idadi ya watalii, ajira na Pato la Taifa.

**26.** **Mheshimiwa Spika,** ili kufikia malengo hayo, Wizara inaendelea kutumia fursa na mikakati mbalimbali ya kukuza utalii kupitia matukio ya kimataifa yatakayofanyika nchini ikiwemo: -

i. **Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (Inter-Parliamentary Union - IPU Assembly)**

Mkutano huu unakutanisha Mabunge ya Nchi wanachama wa umoja wa mabunge Duniani na utafanyika tarehe 5 hadi 9 Oktoba, 2026 Jijini Arusha. Mkutano huu unatarajiwa kuwa na washiriki zaidi ya 1,500 wakiwemo Maspika 183 kutoka nchi mbalimbali duniani ambapo Tanzania ni mwanachama na mwenyekiti wa umoja huo. Katika kuhakikisha Tanzania inafaidika kikamilifu na mkutano huu Wizara imeandaa na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kutangaza mazao ya utalii na ukarimu. Katika hatua za maandalizi, Wizara iliandaa onesho la kutangaza utalii wakati wa Mkutano wa 152 wa IPU uliofanyika tarehe 15 hadi 19 Aprili, 2026 Jijini Istanbul, Uturuki. Aidha, katika mkutano huo Wizara ilifanikiwa kutangaza vivutio na fursa za utalii wa Tanzania kwa washiriki waliohudhuria na kuwashawishi kutembelea maeneo ya utalii kabla, wakati na baada ya mkutano wa IPU wa 153. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa utalii itaandaa vifurushi vya safari na kuvitangaza

kwenye tovuti ya IPU. Vifurushi hivyo vitakuwa na link ambayo wageni wataweza kufanya booking ya kutembelea maeneo yetu moja kwa moja. Pamoja na hilo, Wizara itaweka mabanda ya taarifa za utalii katika eneo la mkutano ili kuhamasisha washiriki kutembelea vivutio vyetu kipindi na baada ya mkutano kuisha. Pia, tovuti ya IPU itatumika kuweka taarifa za utalii na matukio mbalimbali ya wageni hao walipokua Tanzania ili kuendelea kuvutia wageni wengi zaidi kutembelea Tanzania.

**ii. Tukio la World Travel Awards (WTA) 2026**

Tukio hili la kimataifa huandaliwa kila mwaka kwa lengo la kutoa tuzo za ubora katika Sekta ya Utalii duniani. Aidha, linatarajiwa kufanyika nchini mwezi Desemba, 2026 na kuhudhuriwa na washiriki zaidi ya 1,000 kutoka Mabara ya Afrika, Ulaya, Asia, Amerika ya Kaskazini na Kusini. Wizara kwa kushirikiana na wadau wa utalii itaandaa vifurushi maalum vya mazao ya utalii na huduma kwa washiriki katika tovuti ya Bodi ya Utalii Tanzania na WTA pindi itakapofunguliwa. Sambamba na hilo, Wizara itatumia fursa za kidijitali, machapisho na taarifa za mitandaoni kuwafikishia wadau mbalimbali taarifa muhimu za vivutio vya utalii Tanzania wakati wa tukio hilo. Pia, Wizara itaendelea kuhamasisha wageni kutembelea vivutio vya utalii na maeneo mbalimbali kupitia vifurushi vilivyoandaliwa na kuwekwa katika jukwaa la utalii la TTB "booking platform" ili kuendelea kutoa wigo mpana kwa wageni kufanya uchaguzi wa kutembelea vivutio hata baada ya tukio hilo.

***iii. Shindano la 74 la Ulimbwende wa Dunia 2027 -*** **Miss World 2027**

Shindano hili la Kimataifa linahusisha masuala ya urembo likiwa ni miongoni mwa mashindano makubwa duniani yanayojulikana kama Big Four Beauty Pageants. Tukio hili linatarajiwa kufanyika nchini mwezi Mei, 2027 na linatarajiwa kuhudhuriwa na watu takriban 20,000 wakiwemo washindani 120 kutoka nchi mbalimbali Duniani. Aidha, kabla ya tukio hili, Wizara itawatangazia wadau na kuwahamasisha kuandaa na kuuza vifurushi vya safari kupitia jukwaa la utalii la TTB "booking platforms" na kutangaza tukio hili kupitia tovuti ya TTB, mitandao

ya kijamii, televisheni, redio na vyombo mbalimbali vya habari vya ndani na nje ya nchi.

Sambamba na hilo, Wizara itaandaa ziara ya mafunzo kwa kuwapa fursa Walimbwende na waandishi wa habari kutembelea maeneo ya vivutio (FAM Trip) kabla ya shindano kwa lengo la kukuza uelewa wa vivutio vyetu na kurusha maudhui hayo kwenye mitandao yao ya kijamii pamoja na kuvitangaza katika vyombo vya habari mbalimbali ulimwenguni. Kwa upande mwingine, Wizara itaweka mabanda ya kutangaza utalii na kutoa taarifa kwa watalii ndani ya maeneo yatakapofanyika mashindano na kuendelea kutumia maudhui ya mashindano hayo ikiwemo yatakayomhusu Mshindi wa Mashindano (Miss World) ili kujitangaza zaidi duniani. Baada ya shindano, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaratibu safari za kutembelea vivutio kwa washiriki watakaokuwa wamejisajili kupitia jukwaa la utalii la TTB. Pia, washindi wa juu watano wa shindano hilo, watapewa ubalozi wa hiari wa kutangaza utalii wa Tanzania.

#### *iv. Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa Nchi za Afrika (Africa Cup of Nations - AFCON) 2027*

Mashindano haya yanaandaliwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) kila baada ya miaka miwili (2) na kuhusisha timu za Mataifa kutoka Bara la Afrika. Kwa mwaka 2027, mashindano hayo yanatarajiwa kuandaliwa kwa pamoja na nchi tatu za Afrika Mashariki ikiwemo Tanzania. Katika mashindano hayo, timu 24 zilizofuzu zitashindana na kutarajiwa kuwa na watazamaji wa viwanjani milioni 1.8 na wafuatiliaji katika televisheni bilioni 1.9 kupitia vituo vya utangazaji zaidi ya 185. Aidha, mashindano hayo yanakadiriwa kuwa na faida za kiuchumi zinazoweza kufikia zaidi ya Dola za Marekani bilioni 2.

Kwa kuwa Tanzania ni moja ya waandaaji wa mashindano hayo, Wizara imeandaa mkakati wa kuitangaza Tanzania kama kivutio cha kipekee cha utalii. Mkakati huo unahusisha shughuli za kabla, wakati na baada ya mashindano ambapo kabla ya mashindano hayo, shughuli zinazotarajiwa kutekelezwa ni pamoja na kuanza kutangaza utalii wa Tanzania wakati wa Mashindano ya Dunia ya Mpira wa Miguu yaani FIFA World Cup yatakayofanyika nchini

Marekani kati ya mwezi Juni na Julai mwaka 2026. Kupitia mashindano hayo Tanzania itashirikisha wadau muhimu wakiwemo watangazaji mashuhuri wa michezo duniani na kujitangaza kupitia mabango ya kidijitali "billboards" yatakayowekwa katika maeneo ya kimkakati nchini Marekani.

Katika kuongeza hamasa ya kufuatiliwa na watu wengi zaidi kwenye mitandao ya kijamii duniani, Wizara itatumia watu maarufu na wenye ushawishi mkubwa kama vile wanamichezo ili kuendelea kujitangaza kwa kuwaleta kutembelea maeneo yenye vivutio vya utalii. Kupitia watu hao maudhui mbalimbali yenye kulenga kuitangaza Tanzania yatarekodiwa na kurushwa kwenye tovuti mbalimbali sambamba na mitandao ya kijamii ya watu hao kama vile Instagram, LinkedIn, Tiktok, Facebook na mtandao wa X. Vilevile, Wizara inaendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali ikiwemo viwanja vya ndege, barabara, malazi na mageti ikiwemo barabara ya Seronera kuelekea Naabi, Ikoma na Lobo na njia za utalii katika Hifadhi ya Taifa Serengeti ili kuhakikisha zinafikika na kupitika kipindi chote hususan kabla, wakati na baada ya mashindano ya AFCON. Pia, kuendelea na ujenzi wa malazi na kuimarisha huduma za wageni katika maeneo ya Sahare, Makuyuni, Wamimbiki na Pande ili kurahisisha na kutoa huduma zenye viwango vya kimataifa wakati na baada ya mashindano ya AFCON.

Halikadhalika, Wizara itaunganisha Hifadhi ya Taifa Mikumi na reli ya SGR kupitia ujenzi wa lango la kuingia wageni katika eneo la Kilosa. Hatua hiyo itarahisisha wageni watakaokuja jijini Dar es Salaam kushiriki AFCON waweze kusafiri na reli kwenda kutalii Mikumi. Vilevile, Wizara imekamilisha ujenzi wa uwanja wa gofu wenye hadhi ya Kimataifa katika Ikolojia ya Serengeti ili kuvutia watalii wa michezo hususan watakaotembelea Tanzania kipindi cha mashindano ya AFCON 2027.

Ili kuhakikisha utoaji wa huduma bora, Wizara ilizindua programu ya maandalizi ya kuwanoa watoa huduma za utalii na kuwajengea uwezo wadau waliopo katika mnyororo wa thamani wa utalii ambapo katika awamu ya kwanza, waongoza watalii 2,228 wamepatiwa mafunzo ya kuboresha huduma na programu

hiyo inaendelea kwa maeneo mengine ya kimkakati yatakayopokea wageni kwa kuzingatia fursa za ugeni huo. Wizara itashirikiana na wadau wa sekta binafsi kuandaa vifurushi vya safari kwa washiriki wa AFCON 2027 vikifungamanisha mazao ya utalii na huduma muhimu ikiwemo usafiri, malazi na chakula. Vilevile, Wizara imeendelea na zoezi la kupanga huduma za malazi katika daraja za ubora hususan katika maeneo ya kimkakati ili kutoa uzoefu mzuri kwa wageni.

Kama moja ya mikakati ya utangazaji utalii wakati wa mashindano, Wizara itaweka matangazo yenye maudhui mbalimbali kuhusu utalii wa Tanzania katika viwanja vitakavyotumika ili kuwahamasisha mashabiki kutembelea vivutio vya utalii hapa nchini. Wizara itaendelea kuboresha miundombinu, kutangaza vifurushi maalum vya safari na kuhamasisha mashabiki kupitia maeneo maalum ya ufuatiliaji mashindano mubashara (fan zones). Aidha, Wizara itaandaa na kurusha maudhui ya utalii katika vyombo mbalimbali vya habari vitakavyoonesha na kutangaza mashindano hayo katika kipindi chote cha AFCON 2027.

Sambamba na hilo, Wizara itaendelea kutangaza utalii wa Tanzania hata baada ya AFCON 2027, kwa kuandaa kampeni maalum za kuhamasisha washiriki na mashabiki wa mashindano haya kutembelea vivutio vya Utalii baada ya mashindano kukamilika. Kampeni hii itahusisha utoaji wa safari za motisha kwa baadhi ya washiriki wa mashindano pamoja na kuwashawishi washiriki maarufu kutangaza vivutio vya Tanzania. Vilevile, Wizara itatumia tukio hilo kuchochea ukuaji wa utalii na uchumi kwa kuendeleza na kutumia miundombinu mbalimbali iliyoboreshwa ikiwemo viwanja vya ndege, barabara na huduma za malazi ili kuvutia matukio mengine ya kimataifa pamoja na kuvutia uwekezaji.

**27. Mheshimiwa Spika,** mafanikio ya Tanzania kuendelea kuaminiwa kuwa mwenyeji wa matukio haya makubwa ya kimataifa ni matokeo ya maono, uongozi thabiti na diplomasia ya uchumi inayoendelezwa kwa ustadi mkubwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kupitia juhudi zake za kufungua nchi, kuimarisha

mazingira ya uwekezaji, kuitangaza Tanzania kimataifa na kuboresha miundombinu ya kimkakati, nchi yetu imeendelea kujijengea heshima na kuaminiwa katika jukwaa la kimataifa kama kitovu cha utalii, biashara na uwekezaji duniani. Matukio haya ni uthibitisho wa namna ambavyo diplomasia ya uchumi imeendelea kufungua fursa mpya za ajira, mapato na ukuaji wa uchumi kwa wananchi wetu.

**28. Mheshimiwa Spika,** matukio haya ya kimataifa yataendelea kuwa kichocheo muhimu cha ukuaji wa Sekta ya Maliasili na Utalii pamoja na uchumi wa taifa kwa ujumla. Hivyo, kupitia Bunge lako Tukufu, ninatoa rai kwa Watanzania wote kudumisha asili yetu ya ukarimu kwa wageni ili kuendelea kujenga taswira chanya ya Taifa letu na kuimarisha nafasi ya Tanzania kama kivutio cha pekee Duniani.

## 5.0 UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**29. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maliasili na Utalii imepewa dhamana ya kusimamia kisheria maeneo yenye ukubwa wa kilometa za mraba takriban 307,800 sawa na asilimia 32.5 ya eneo lote la Nchi. Maeneo haya yanajumuisha Hifadhi za Taifa 21, Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Mapori ya Akiba 29, Mapori Tengefu 23, maeneo 3 ya Ardhioevu chini ya Mkataba wa Ramsar, Hifadhi za Misitu ya Asili 465 ikijumuisha Hifadhi za Misitu ya Mazingira Asilia 26, Mashamba ya Miti ya Serikali 26, Hifadhi za Nyuki 14, Maeneo ya Malikale 158 na Makumbusho za Taifa 7. Aidha, Wizara inaratibu shughuli za uhifadhi katika maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori (WMAs) 40 ambapo kati ya hizo 24 zimeidhinishwa na 16 zipo kwenye hatua mbalimbali za kuidhinishwa, mashamba sita (6) ya ufugaji wa wanyamapori, bustani 41 za wanyamapori, maeneo 36 ya uzalishaji wa wanyamapori pamoja na ranchi sita (6) zinazomilikiwa na sekta binafsi.

**30. Mheshimiwa Spika,** maeneo ya hifadhi za wanyamapori, misitu, nyuki, fukwe na malikale yana mchango mkubwa katika uhifadhi wa mazingira, ustawi wa wananchi, urithi wa utamaduni na ukuaji wa uchumi kitaifa na kimataifa. Sekta ya Maliasili na

Utalii inachangia asilimia 21.5 katika Pato ghafi la Taifa ambapo asilimia 17.2 ni utalii na asilimia 4.3 ni misitu na nyuki. Aidha, Sekta hii inachangia asilimia 30.9 ya mapato ya fedha za kigeni ambapo asilimia 25 yanatokana na utalii; na asilimia 5.9 misitu na nyuki; na kuajiri watu takriban milioni 3.6 wenye ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kwa mwaka. Kwa upande mwingine, maeneo ya hifadhi pia ni vyanzo vikuu vya maji, nishati, makazi ya wanyamapori na viumbe hai wengine. Vilevile, sehemu kubwa ya Watanzania katika maeneo ya vijijini hutegemea rasilimali hizo kwa ajili ya kujikimu.

**31.** **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara umezingatia miongozo mbalimbali ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 - 2025/2026), Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020, Sera na Sheria mbalimbali, Mpango Mkakati wa Wizara (2021/2022 - 2025/2026), Mwongozo wa Mpango na Bajeti wa Mwaka 2024/2025, Mikataba ya Kikanda na Kimataifa na maelekezo mbalimbali ya viongozi wakuu wa kitaifa.

**32.** **Mheshimiwa Spika,** ninaomba sasa kuwasilisha utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

### 5.1 *Ukusanyaji wa Maduhuli*

**33.** **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara iliidhinishiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 1,185,584,115,330.55.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 860,106,097,959.74** zinakusanywa na Wizara kupitia Taasisi za TANAPA na NCAA na kuwasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA); **Shilingi 115,536,198,276.65** zilipangwa kukusanywa na Idara za Wizara, Mfuko wa Mambo ya Kale na Taasisi ya TAWA na kuwasilishwa Mfuko Mkuu wa Serikali; na **Shilingi 209,941,819,094.16** zilipangwa kukusanywa na Taasisi zinazokusanya na kutumia kupitia mfumo wa MNRT Portal ambazo ni: Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania - TAWIRI, Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania - TAFORI, Wakala wa

Huduma za Misitu Tanzania - TFS, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka - CAWM, Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi - PWTI, Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii Likuyu Sekamaganga - CBCTC, Chuo cha Misitu Olmotonyi - FTI, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora - BTI, Chuo cha Viwanda vya Misitu - FITI, Bodi ya Utalii Tanzania - TTB, Chuo cha Taifa cha Utalii - NCT na Shirika la Makumbusho ya Taifa la Tanzania - NMT.

**34. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara imekusanya jumla ya **Shilingi 989,329,108,105.60** sawa na **asilimia 83.45** ya lengo la makusanyo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 725,277,756,030.43** zimekusanywa na Wizara kutokana na vyanzo vya Taasisi za TANAPA na NCAA. Aidha, **Shilingi 85,229,074,781.41** zimekusanywa na Idara za Wizara, Mfuko wa Mambo ya Kale na Taasisi ya TAWA na **Shilingi 178,822,277,293.76** zimekusanywa na Taasisi zinazokusanya na kutumia.

### 5.2 *Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo*

**35. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 336,518,895,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 254,232,349,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 82,286,546,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**36. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 252,563,506,536.21** sawa na asilimia **75**. Fedha hizi zinajumuisha Fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 205,703,467,197.19** na Fedha za Miradi ya Maendeleo **Shilingi 46,860,039,339.02.** Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida zilizopokelewa, **Shilingi 98,628,956,143.53** ni fedha za Matumizi Mengineyo na **Shilingi 107,074,511,053.66** ni Mishahara.

### 5.3 *Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara*

#### *5.3.1 Sekta ya Wanyamapori*

**37. Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Wanyamapori ina jukumu la

kuhifadhi, kusimamia, kutoa mafunzo pamoja na kufanya tafiti kuhusu rasilimali za wanyamapori ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa. Majukumu haya yanatekelezwa na Wizara kupitia Idara ya Wanyamapori na Taasisi za uhifadhi ambazo ni Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania (TWPF), Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Afrika - Mweka (CAWM), Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori - Pasiansi (PWTI) pamoja na Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii - Likuyu Sekamaganga (CBCTC).

**38. Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa majukumu ya sekta unaongozwa na Sera ya Taifa ya Wanyamapori ya Mwaka 2007; Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283; Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura ya 282; Sheria ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Sura ya 284; Sheria ya Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori - Mweka, Sura ya 209; na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania, Sura ya 260.

**39. Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Wanyamapori inasimamia jumla ya Hifadhi za Taifa 21, Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Mapori ya Akiba 29, Mapori Tengefu 23, Maeneo matatu (3) ya Ardhioevu na Bustani tano (5) za Wanyamapori zinazomilikiwa na Serikali. Aidha, Sekta hii inaratibu shughuli za uhifadhi katika maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori (WMAs) 40 ambapo kati ya hizo 24 zimeidhinishwa na 16 zipo kwenye hatua mbalimbali za kuidhinishwa, mashamba sita (6) ya ufugaji wa wanyamapori, bustani 41 za wanyamapori, maeneo 36 ya uzalishaji wa wanyamapori pamoja na ranchi sita (6) zinazomilikiwa na sekta binafsi.

#### 5.3.1.1 *Utekelezaji wa Afua Maalum za Kukabiliana na Migongano Baina ya Binadamu na Wanyamapori Wakali na Waharibifu*

**40. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kukabiliana na changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu kupitia utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa

Kusimamia Utatuzi wa Migongano baina ya Binadamu na Wanyamapori (2020/2021-2024/2025). Kwa kiasi kikubwa, migongano hii imechangiwa na matumizi yasiyo rafiki ya ardhi na yasiyozingatia mipango ya matumizi bora ya ardhi, kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu katika maeneo yanayopakana na hifadhi, shoroba na maeneo ya mtawanyiko wa wanyamapori pamoja na athari za mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha ukame na kulazimisha baadhi ya wanyamapori kutoka nje ya hifadhi kutafuta maji na malisho.

**41.** **Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto hii, Wizara imekamilisha ujenzi wa vituo vipya tisa (9) vya askari katika Halmashauri za Wilaya za Babati (1), Monduli (1), Tunduru (1) na Rufiji (1) na hifadhi za Taifa za Ibanda-Kyerwa (3) na Mto Ugalla (2); na taratibu za ujenzi wa vituo vingine 21 unaendelea katika wilaya za Kilwa (1), Mbarali (1), Bariadi (1), Serengeti (1), Karatu (2), Bunda, Kiteto (1), Ikungi (1), Nkasi (1), Kilosa (1), Mkinga (1), Lushoto (1), Kondoa (1), Iramba (1), Malinyi (1), Simanjiro (1), Namtumbo (1) na Nachingwea (1) na Hifadhi ya Taifa Rumanyika-Karagwe (2). Kukamilika kwa ujenzi huu kutafanya jumla ya vituo vya askari vilivyojengwa kufikia 51. Aidha, Wizara imeweka vituo 40 vya muda vya askari kwa ajili ya kudhibiti matukio ya wanyamapori kwa haraka katika Wilaya mbalimbali hapa nchini. Hatua hii imewezesha askari kuitikia kwa haraka na kukabiliana na matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu wanapovamia maeneo ya wananchi.

**42.** **Mheshimiwa Spika**, katika hatua nyingine, Wizara imechimba mabwawa 12 katika Mapori ya Akiba Rungwa (1), Muhesi (2), Kizigo (2), Msanjesi (1), Selous-Liwale (2) na Lukwika-Lumesule (1); na Hifadhi ya Taifa Mikumi (3). Aidha, taratibu za uchimbaji wa mabwawa mengine saba (7) zinaendelea katika Hifadhi ya Taifa Mikumi (1), Mapori ya Akiba Maswa (2), Wami-mbiki (2), Katavi (1) na Selous-Kingupira (1). Juhudi hizo zimeimarisha upatikanaji wa maji kwa wanyamapori ndani ya hifadhi hasa katika kipindi cha kiangazi ambacho wanyamapori hususan tembo wamekuwa wakitoka nje ya hifadhi kutafuta maji na kusababisha madhara kwa wananchi.



*Kushoto ni bwawa la maji katika Pori la Akiba Muhesi na kulia ni bwawa la maji katika Hifadhi ya Wanyamapori Makuyuni*

**43. Mheshimiwa Spika**, sambamba na hilo, Wizara imejenga vizimba nane (8) vya kudhibiti mamba na viboko katika Wilaya za Nyasa (2), Nkasi (1), Kalambo (2), Namtumbo (1) na Songwe (2) na kufanya idadi ya vizimba vilivyojengwa nchi nzima kufikia 39. Aidha, taratibu zinaendelea kwa ajili ya ujenzi wa vizimba 36 katika Wilaya za Geita (2), Buchosa (2), Ukerewe (2), Kibiti (2), Rufiji (2), Morogoro (2), Kibaha (2), Mkuranga (1), Mvomero (1), Kilosa (2), Iringa (2), Nkasi (2), Busega (2), Nanyumbu (2), Uvinza (2), Sengerema (3), Mkinga (1), Nanyamba (1), Songwe (1) na Tarime (2). Aidha, hatua hii imechangia kuimarika kwa usalama wa wananchi wanaotumia vizimba hivyo ipasavyo.



*Vizimba vya Kuzuia mamba na viboko vilivyojengwa katika Wilaya ya Nyasa.*

**44. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia taasisi zake imeendelea

kuimarisha matumizi ya teknolojia katika kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu kwa kufuatilia mienendo yao na kuwadhibiti. Katika kutekeleza hilo, Wizara kwa kushirikiana na wadau, imefunga visukuma mawimbi kwa wanyamapori 76 kati ya 50 vilivyopangwa kufungwa sawa na asilimia 152 kwa makundi mbalimbali wakiwemo tembo viongozi 51 katika Halmashauri za wilaya za Karagwe, Misenyi, Itigi, Manyoni, Ikungi, Singida, Same, Korogwe, Handeni, Kondoa, Chamwino, Iringa, Morogoro, Mvomero na Chalinze na kufanya tembo viongozi waliofungwa visukuma mawimbi nchini kufikia 205; simba 20 katika Hifadhi za Taifa Nyerere (3), Ruaha (8), Serengeti (7) na Pori la Akiba Maswa (2); mbwamwitu (4) katika Pori la Akiba Selous; na chui mmoja (1) katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Matumizi ya teknolojia hiyo yameongeza ufanisi katika ufuatiliaji wa mienendo ya wanyamapori kwa wakati na kuchukua hatua za haraka kabla ya kusababisha madhara. Vilevile, matumizi ya ndege nyuki 59 zilizonunuliwa na Wizara kwa kushirikiana na wadau yameboresha uwezo wa kudhibiti tembo wanaovamia maeneo ya wananchi, hasa katika maeneo yenye ugumu wa kufikika. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, zaidi ya tembo 191 walidhibitiwa na kurejeshwa ndani ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro kabla ya kusababisha madhara.



*Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb.), akipokea maelezo na kufunga kisukuma mawimbi katika Pori la Akiba Mkungunero.*

**45.** **Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Wizara inaendelea na taratibu za ujenzi wa uzio wa umeme wenye urefu wa kilomita 53 ambapo kilomita 15 ni kutoka Shamba la Acacia Hills Limited (Mang'ola juu) hadi Kijiji cha Makhoromba, Kitongoji cha Endawishi kinachopakana na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro; na kilomita 38 kutoka eneo la Tabora B hadi Mto Mara katika Hifadhi ya Taifa Serengeti. Uzio huo utaimarisha ulinzi wa mali na maisha ya wananchi kwa kudhibiti wanyamapori kutoka hifadhini kwenda kwenye maeneo ya wananchi. Sambamba na hilo, Wizara inaendelea kufanya tathmini nchi nzima ya maeneo mengine yenye migongano mikubwa yanayoweza kujengwa uzio wa umeme ili kuimarisha udhibiti wa matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu.

**46.** **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara imenunua pikipiki 46 kwa ajili ya Maafisa Wanyamapori wa Halmashauri za Wilaya za Liwale, Tunduru, Nachingwea, Namtumbo, Serengeti, Malinyi, Rufiji, Karatu, Itilima, Korogwe, Mvomero, Same, Monduli, Iringa, Bunda, Babati, Mbarali, Mwanga, Kilosa, Lushoto, Bariadi, Morogoro, Meatu, Chalinze, Longido, Kalambo, Itigi, Handeni, Ikungi, Busega, Ruangwa, Manyoni, Arumeru, Kilwa, Nsimbo, Mkinga, Kiteto, Kondoa, Kondoa Mji, Lindi, Nkasi, Buchosa na Siha. Hatua hii itawezesha kuimarisha ufuatiliaji wa haraka wa matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu. Sambamba na hilo, Wizara inakamilisha manunuzi ya vilipuzi 10,000; ndege nyuki 52; na inaendelea na manunuzi ya helikopta mbili (2) kupitia taasisi za TANAPA na NCAA kwa ajili ya kuimarisha shughuli mbalimbali za uhifadhi.

**47.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ulinzi wa rasilimali za wanyamapori na udhibiti wa wanyamapori wakali na waharibifu, Wizara imeajiri askari wa wanyamapori 551 ambao wamepangiwa majukumu katika hifadhi mbalimbali. Hatua hii imewezesha Askari hao kuitikia kwa haraka na kudhibiti matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo mbalimbali. Sambamba na hilo, Wizara imetoa mafunzo kwa Askari Wanyamapori wa Vijiji (VGS) 95 kutoka Halmashauri za Wilaya 19 za Buchosa, Chalinze, Itigi, Kalambo, Karagwe, Chemba, Kilolo, Kiteto, Kondoa, Kondoa Mji, Longido, Meru,

Morogoro Manispaa, Nanyumbu, Ngara, Ngorongoro, Nsimbo, Siha na Uvinza hivyo kufanya idadi ya VGS kufikia 1,298.

Vilevile, Wizara imeendelea kuwashirikisha VGS 752 na vikundi vya ulinzi shirikishi 230 katika kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo mbalimbali nchini.

**48.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ushiriki wa wananchi kwenye uhifadhi, Wizara imetoa elimu ya uhifadhi na mbinu za kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu kwa wananchi 885,189 kupitia mikutano 3,481 iliyofanyika katika Vijiji vinavyopakana na Hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Vilevile, mafunzo ya mbinu rafiki za kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu yalitolewa kwa wananchi wakufunzi 81 katika Wilaya za Tanganyika (41) na Nsimbo (40). Hatua hiyo imewezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika utatuzi wa changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu.



*Kushoto ni wananchi wakipewa elimu katika kitongoji cha Misrai kijiji cha Mtryiyangwi Kata ya Hindomairo Wilaya ya Kondoa na kulia ni wananchi wa Kijiji cha Chinyahuku Kata ya Rudi Wilaya ya Mpwapwa.*

**49.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kudhibiti matukio 3,585 ya wanyamapori wakali na waharibifu kwa kufanya doria 5,771 za mwitikio wa haraka. Vilevile, katika kuimarisha usalama wa maisha na mali za wananchi jumla ya wanyamapori wakali na waharibifu 175 walivunwa katika maeneo mbalimbali nchini wakiwemo mamba 33, viboko 43, tembo 22, nyati 19, fisi 50, simba watano (5) na chui watatu (3).

**50.** **Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, Wizara imehamisha tembo 390 kutoka Ranchi ya Taifa Kitengule na

nyani 294 kutoka Geita kwenda Hifadhi ya Taifa ya Burigi Chato; simba sita (6) ambapo simba wawili (2) walihamishwa kutoka Kondoa kwenda Pori la Akiba Swagaswaga; wawili (2) kutoka Kijiji cha Pakinyigot - Wilaya ya Serengeti kwenda Hifadhi ya Taifa Serengeti; mmoja (1) kutoka Kijiji cha Iyoli, Wilaya ya Kondoa na Simba mmoja (1) kutoka Wilaya ya Serengeti kwenda Bustani ya Wanyamapori Dar es Salaam. Vilevile, chui watatu (3) wamehamishwa kutoka maeneo ya wananchi ambapo wawili (2) walikamatwa kutoka Kijiji cha Robanda na kupelekwa katika Bustani ya Wanyamapori ya Dar es Saalam (1) na Pori la Akiba Pande (1), na mmoja (1) alikamatwa kutoka Wilaya ya Itilima na kupelekwa katika Pori la Akiba Maswa.

**51. Mheshimiwa Spika,** ili kuongeza ufanisi na tija katika kupokea taarifa na malipo ya kifuta jasho na machozi, Wizara imeanza kutumia mfumo wa kielektroniki kulipa waathirika wa madhara yatokanayo na wanyamapori wakali na waharibifu. Mfumo huo umerahisisha malipo kufanyika kwa wakati kati ya siku saba (7) hadi 14 ikilinganishwa na utaratibu wa awali ambao zoezi hilo lilichukua miezi sita (6) hadi 12. Hadi kufikia Aprili 2026, Wizara imelipa kiasi cha Shilingi 8,149,314,750.00 ikiwa ni kifuta jasho na machozi kwa wananchi 22,696 waliopatwa na madhara ya wanyamapori katika Halmashauri za Wilaya 81 ikilinganishwa na kipindi kama hiki katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 ambapo jumla ya Shilingi 4,604,909,750 zililipwa kwa wananchi 16,939. Katika kuimarisha utekelezaji wa matumizi ya Mfumo huo, Wizara imetoa mafunzo kwa Maafisa Wanyamapori na ugani ambapo hadi sasa jumla ya maafisa 842 kutoka Halmashauri za Wilaya 109 nchini wamepatiwa mafunzo.

**52. Mheshimiwa Spika,** Wizara itaendelea kuimarisha na kutumia mbinu mbalimbali za kudhibiti madhara yanayosababishwa na wanyamapori wakali na waharibifu ili kupunguza athari hizo kwa jamii. Nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu na wananchi kwa ujumla kuendelea kuiunga mkono Serikali katika jitihada za kukabiliana na matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu kwa kutoa taarifa kwa wakati, kuchukua tahadhari dhidi ya wanyamapori hao na kuzingatia maelekezo yanayotolewa na wataalam.

### 5.3.1.2 *Idara ya Wanyamapori*

**53. Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara imefanya mapitio ya Kanuni za Utalii wa Picha za Mwaka 2016; Kanuni za Uwindaji wa Kitalii za Mwaka 2024; Kanuni za Ufugaji wa Wanyamapori za Mwaka 2020 kwa lengo la kuboresha mazingira ya kibiashara na kuongeza tija katika uhifadhi; Kanuni za Usimamizi wa Maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori (WMAs) za Mwaka 2018, na Mwongozo wa Utengaji na Usimamizi wa Maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori ili kuongeza ufanisi katika usimamizi na utendaji wa Jumuiya hizo.

**54. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara imefanya mapitio ya Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti Migongano kati ya Binadamu na Wanyamapori wa Mwaka 2020/2021-2024/2025 na kuandaa Mkakati mpya wa miaka 10 (2026/2027-2036/2037) ambao umeandaliwa na utatekelezwa kwa pamoja na Wizara nyingine za Kisekta. Mkakati huo unalenga kupunguza madhara ya wanyamapori wakali na waharibifu ikiwemo uharibifu wa mazao, majeraha na vifo vya binadamu na mifugo kwa kulinda makazi yao na kuhakikisha wanyamapori wanatumia muda mwingi ndani ya maeneo yaliyohifadhiwa. Aidha, kwa kushirikiana na Wizara nyingine za Kisekta ikiwemo Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Kilimo, Mifugo na Uvuvi, mkakati huu utaboresha upangaji wa matumizi ya ardhi, ufugaji, uvuvi na kilimo. Sambamba na hilo, Wizara imeandaa Mwongozo wa Kusimamia Nyara za Serikali ili kuongeza ufanisi katika utunzaji na matumizi ya nyara.

**55. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na ujangili nchini, Wizara imeendelea kuratibu doria maalum kupitia Kikosi Kazi Taifa Dhidi ya Ujangili na kanda za kiikolojia dhidi ya ujangili. Doria hizi hufanyika kwenye mifumo ikolojia yote nchini na maeneo ya mipakani. Katika Mwaka wa Fedha wa 2025/2026, doria hizo zimewezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 416 wa ujangili na biashara haramu ya nyara ambapo wamefikishwa Mahakamani na hatua mbalimbali za kisheria zinaendelea kuchukuliwa dhidi yao.

**56.** **Mheshimiwa Spika**, katika kuendelea kuwashirikisha na kuwezesha wananchi kunufaika na rasilimali za wanyamapori, Wizara imeratibu uundaji na usajili wa Asasi za kijamii zinazojihusisha na wanyamapori; uandaaji wa Katiba na Mipango ya Kanda ya Usimamizi wa Rasilimali kwa Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori Ikungi, Ndonda na Kilolo na kuidhinisha mipango ya jumla ya usimamizi wa WMAs tatu (3) za Enduimet, Uyumbu na Mungata. Sambamba na hilo, Wizara imewajengea uwezo viongozi 170 wa WMAs nane (8) zisizo na wawekezaji za Kimbanda na Kisungule zilizopo katika Wilaya ya Namtumbo; Chingoli katika Wilaya ya Tunduru; ISAWIMA katika Wilaya ya Kaliua; Iluma katika wilaya za Kilombero na Ulanga; Chamwino katika Wilaya ya Chamwino; UMEMARUWA katika wilaya za Wanging'ombe na Mbarali; na Mpimbwe katika Wilaya ya Mlele kuhusu usimamizi na uendelezaji wa jumuiya hizo kwa manufaa ya uhifadhi na maendeleo ya wananchi.

**57.** **Mheshimiwa Spika,** pamoja na hayo, Wizara imewezesha ununuzi wa pikipiki 15 kwa ajili ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA) saba (7) ambazo hazina wawekezaji. Jumuiya hizo ni Ndonda (2), Ifinga (2), ISAWIMA (2), Mpimbwe (2), UMEMARUWA (2), Iluma (2) na JUKUMU (3). Hatua hiyo itawezesha kuimarisha shughuli za uhifadhi na ulinzi wa wanyamapori katika maeneo hayo. Vilevile, Wizara imefanya tathmini ya eneo linalopendekezwa kuwa WMA kwa ajili ya matumizi ya kijadi, hususan kabila la Hadzabe katika Kijiji cha Munguli kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, Mkoa wa Singida. Kwa sasa, Jumuiya hiyo imekamilisha hatua nne (4) za uanzishwaji ambazo ni uhamasishaji wa jamii, vijiji kuridhia na kutenga maeneo, kuunda na kusajili Asasi ya Kijamii (CBO) na kuhuisha mipango ya matumizi ya ardhi. Aidha, hatua zinazofuata ni kuandaa Mpango wa Kanda wa Matumizi na Usimamizi wa Jumuiya; Kuwasilisha maombi ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali na kuidhinishwa kwa Asasi ya Kijamii kuwa Jumuiya iliyoidhinishwa; na Kutoa haki ya kutumia rasilimali za wanyamapori katika eneo husika.

**58.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuendelea kutekeleza Mikataba ya Kikanda na Kimataifa ambayo nchi yetu imeridhia, Wizara imeshiriki kikamilifu katika mikutano mbalimbali ya

uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori. Miongoni mwa mikutano hiyo ni Mkutano wa 20 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Kimataifa wa Biashara ya Wanyamapori na Mimea Iliyohatarini Kutoweka (CITES) uliofanyika Samarkand, Uzbekistan mwezi Novemba 2025; na Mkutano wa 79 na 80 wa Kamati Kuu ya CITES iliyofanyika nchini Uzbekistan. Kupitia mikutano hiyo, Tanzania imechaguliwa kuwa Mjumbe wa Kamati za Wanyamapori, Mimea na Kamati ya Fedha na Mipango kwa kipindi cha pili. Fursa hiyo itawezesha Tanzania kushiriki kikamilifu katika maamuzi muhimu ya kimataifa, kulinda na kutetea maslahi ya Taifa, kupata uzoefu na taarifa za kisasa katika uhifadhi pamoja na kuimarisha ushirikiano na nchi nyingine.

**59.** **Mheshimiwa Spika**, sambamba na hilo, Wizara imeshiriki katika Mkutano wa tisa (9) wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Kimataifa wa Uhifadhi wa Ndegemaji Wahamao uliofanyika Bonn Ujerumani mwezi Novemba, 2025 na Mkutano wa 23 wa Jukwaa la Uhifadhi wa Wanyamapori Barani Afrika uliofanyika Zambia mwezi Septemba, 2025. Kupitia ushiriki huo, Tanzania imeendelea kutekeleza wajibu wake wa kuhifadhi maeneo ya ardhi oevu, mazalia na njia zinazotumiwa na ndegemaji wahamao kusafiri kwenda mabara mengine kupitia Tanzania. Kutokana na jitihada mbalimbali katika usimamizi wa wanyamapori, Tanzania imechaguliwa kuwa mwenyeji wa Mkutano wa 24 wa Jukwaa la Uhifadhi wa Wanyamapori Barani Afrika utakaofanyika mwezi Novemba, 2026 jijini Arusha. Mkutano huo unaratajiwa kuhudhuriwa na washiriki zaidi ya 200 kutoka nchi zinazofanya uwindaji wa kitalii ndani na nje ya Afrika. Kupitia mkutano huo, Tanzania itapata fursa ya kubadilishana uzoefu na mbinu bora za uhifadhi na usimamizi wa rasilimali za wanyamapori na kutangaza utalii katika medani za kimataifa na hivyo kuvutia wawekezaji na watalii zaidi.

**60.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ushirikiano na wadau wa uhifadhi na utalii, Wizara imefanya vikao sita (6) vya mashauriano na wadau wa Sekta ya Wanyamapori wakiwemo wadau wa utalii wa picha, uwindaji wa kitalii, uwindaji wa wenyeji, wafugaji wa wanyamapori pamoja na wamiliki wa mabucha ya kuuza nyamapori kisheria. Kupitia vikao hivyo, jumla

ya changamoto 23 ziliwasilishwa kati ya hizo 13 zimetatuliwa na 10 zinaendelea kufanyiwa kazi ikiwa ni pamoja na zile zinazohusisha mabadiliko ya Sheria na Kanuni.

#### 5.3.1.3 *Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania – TWPF*

**61. Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania una jukumu la kuwezesha shughuli za uhifadhi wanyamapori nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo, Mfuko umewezesha utekelezaji wa kazi za utatuzi wa changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu kwa kuwezesha mafunzo ya kukabiliana na matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu kwa VGS 95 wa Halmashauri za Wilaya 19 na kufanya kuwa na jumla ya VGS 1,298 waliopatiwa mafunzo; Mafunzo ya mbinu rafiki za kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu kwa wakufunzi 81 wa Halmashauri mbili (2) na ununuzi wa pikipiki 40 kwa ajili ya Maafisa Wanyamapori wa Wilaya na pikipiki 15 kwa ajili ya WMAs ambazo zimegawiwa kwa Jumuiya saba (7) zisizo na wawekezaji. Katika hatua nyingine, Mfuko umewezesha ujenzi wa vizimba 45, mabwawa matano (5), vituo 14 vya askari na ujenzi wa uzio wa umeme wenye urefu wa kilomita 15; ununuzi wa mabomu baridi 10,000; ndege nyuki 40; visukuma mawimbi 25; na kuwajengea uwezo viongozi 170 wa WMA nane (8) zisizo na wawekezaji.

**62. Mheshimiwa Spika,** Mfuko kwa kushirikiana na wadau wa uhifadhi umewezesha kujenga Mfumo wa kielekroniki ujulikanao kama Problem Animal Information System - PAIS ambao umerahisisha ukusanyaji, uwasilishwaji wa taarifa sahihi na kuepuka udanganyifu; uchakataji, utunzaji wa taarifa za matukio ya uharibifu wa wanyamapori wakali na waharibifu. Vilevile, Mfumo umerahisisha malipo ya kifuta jasho na machozi kwa wananchi waliopata madhara ya wanyamapori wakali na waharibifu ambapo taratibu kwa sasa taratibu za malipo zinachukua siku saba (7) hadi 14 tofauti na taratibu za awali ambapo malipo yakichukua miezi sita (6) hadi 12. Sambamba na hilo, Mfumo umeongeza uwazi na uwajibikaji kwa kuwa mfumo unawezesha kufuatilia kila muamala. Katika kuimarisha utekelezaji wa matumizi ya Mfumo huo, Mfuko umewezesha mafunzo kwa Maafisa Wanyamapori na ugani

ambapo hadi sasa jumla ya maafisa 842 kutoka Halmashauri za Wilaya 109 nchini. Hadi kufikia Aprili, 2026 kupitia mfumo huo, Mfuko umewezesha malipo ya madai ya kifuta jasho na machozi kiasi cha Shilingi 8,149,314,750.00 kwa wananchi 22,696 waliopatwa na madhara yaliyosababishwa na wanyamapori.

**63. Mheshimiwa Spika**, katika hatua nyingine, Mfuko umewezesha Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI); Ujenzi wa Mradi wa Bweni la wanafunzi katika Chuo cha Taaluma ya Wanyamapori, Pasiansi; Ujenzi wa Maktaba ya Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka; ujenzi wa nyumba mbili (2) za watumishi katika Chuo cha Mafunzo ya Uhifadhi kwa Jamii - Likuyu Sekamaganga. Hatua hizo zimelenga kuimarisha uwezo wa taasisi hizo kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na tija. Kwa upande mwingine, Mfuko umewezesha doria za kudhibiti ujangili na biashara haramu za nyara zinazoendeshwa na Kikosi Kazi Taifa Dhidi Ujangili (NTAP) na Kanda za Kiikolojia Dhidi Ujangili (TCGs) katika mifumo ikolojia yote nchini; kutekeleza majukumu ya kisera na kisheria kwa masuala yanayohusu uratibu wa sekta ya wanyamapori; utekelezaji wa mikataba ya Kikanda na Kimataifa kuhusu uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori; tathmini za kiikolojia katika Mapori ya Akiba na Tengefu pamoja na utatuzi wa migogoro baina ya vijiji na maeneo ya hifadhi.

#### 5.3.1.4 *Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania – TANAPA*

**64. Mheshimiwa Spika,** Shirika limeendelea kutekeleza jukumu la kulinda na kuhifadhi wanyamapori, mimea, na mifumo ya ikolojia katika Hifadhi za Taifa 21 kwa kufanya jumla ya doria 42,941 zilizowezesha kukamata majangili 5,294 katika matukio ya ujangili 4,929, mifugo 59,881 iliyoingia ndani ya hifadhi kinyume cha sheria, silaha 78 pamoja na kutegua mitego ya nyaya 9,847 iliyotegwa ndani ya maeneo ya hifadhi. Watuhumiwa wamefikishwa Mahakamani na kuchukuliwa hatua za kisheria. Aidha, Shirika limeendelea kuimarisha usalama wa wanyamapori kwa kutumia teknolojia ya visukuma mawimbi kwa kuweka alama za masikio kwa faru 17; na vifaa vya ufuatiliaji kwa faru watatu (3) katika Hifadhi ya Taifa Serengeti pamoja na kufanya

doria kwa kutumia ndege na ndege nyuki zilizowezesha kudhibiti matukio ya ujangili.

**65. Mheshimiwa Spika,** Shirika limeendelea kuboresha makazi na malisho ya wanyamapori na kuimarisha mifumo ikolojia kwa kudhibiti mimea vamizi. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kuondoa mimea vamizi katika eneo lenye ukubwa wa hekta 4,253.22 katika Hifadhi za Taifa Arusha (hekta 30), Ibanda-Kyerwa (hekta 69.5), Katavi (hekta 24.25), Kilimanjaro (hekta 12), Kitulo (hekta 4.2), Milima ya Mahale (hekta 219), Ziwa Manyara (hekta 363.2), Mikumi (hekta 202.3), Mkomazi (hekta 43), Nyerere (hekta 2,811.88), Ruaha (hekta 47), Rumanyika-Karagwe (hekta 16.34), Kisiwa cha Rubondo (hekta 160.7), Saadani (hekta 154.5), Kisiwa cha Saanane (hekta 7.06), Serengeti (hekta 13.23), Gombe (hekta 0.56), Tarangire (hekta 23.7), Milima ya Udzungwa (hekta 28.8) na Mto Ugalla (hekta 22). Vilevile, Shirika limefyeka eneo lenye ukubwa wa Hekta 363.2 za vichaka vilivyojumuisha mimea vamizi katika Hifadhi ya Taifa Ziwa Manyara kwa ajili ya kuboresha eneo la malisho ya wanyamapori na Wanyama kuonekana kwa urahisi.

**66. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha mahusiano kati ya Hifadhi za Taifa na wananchi waishio katika vijiji vinavyopakana na Hifadhi za Taifa, Shirika limeendelea kuchangia katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kijamii. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Shirika limewezesha ujenzi wa Ofisi ya Kijiji cha Migudeni katika Wilaya ya Kilombero; ujenzi wa nyumba ya walimu moja (2 in 1) katika Shule ya Sekondari Mdori katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati na kugawa mizinga ya nyuki 200 kwa vikundi vya wafugaji nyuki wa Wilaya ya Karatu. Vilevile, Shirika liliwezesha safari ya mafunzo kwa wananchi 11 kutoka Wilaya ya Nsimbo ambao walikwenda kupata elimu na mbinu za kutekeleza mradi wa ufugaji wa samaki kwa kutumia mabwawa katika Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji Mwamapuli kilichopo Wilaya ya Igunga Mkoa wa Tabora. Shirika litawezesha ujenzi wa bwawa la kufugia samaki kwa wananchi hao. Aidha, Shirika linaendelea na taratibu za manunuzi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya ujenzi wa maabara katika zahanati mbili (2) katika Wilaya ya Karagwe (1) na Kigoma (1); Jengo la wagonjwa wa nje (OPD); Kituo cha afya Mwakijembe, Wilaya ya Mkinga; na ujenzi wa jengo la

“infusion unit” katika Hospitali ya Mpanda. Sambamba na hilo, elimu ya uhifadhi imetolewa kwa wananchi 188,938 wa vijiji 466 vinavyopakana na maeneo ya hifadhi. Hatua hii imeboresha mahusiano na jamii ikiwa ni pamoja na kudhibiti matukio mbalimbali ya ujangili.

**67.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha miundombinu ya uhifadhi na utalii, Shirika limefanya matengenezo ya mara kwa mara ya barabara zenye urefu wa kilomita 2,506.6, katika Hifadhi za Taifa Tarangire (259.3km), Serengeti (1,568km), Ziwa Manyara (36.3km), Kilimanjaro (64km), Mikumi (200km), Nyerere (68km), Mkomazi (84km), Katavi (63km), Ruaha (128 km), Arusha (17km), Saadani (4km) na Udzungwa (15km). Aidha, Shirika limekarabati njia za kutembea kwa miguu zenye urefu wa kilomita 218.24 katika Hifadhi za Taifa Milima ya Mahale (km 50); Milima ya Udzungwa (km 168); na Kisiwa cha Saanane (km 0.24). Vilevile, Shirika limekarabati viwanja vya ndege nane (8) katika hifadhi za Taifa Mikumi (1), Ruaha (2), Nyerere (2) na Serengeti (3). Sambamba na hilo, Shirika limejenga mnara na kufunga mifumo ya mawasiliano ya redio na kujenga minara katika Hifadhi za Taifa Burigi – Chato mmoja (1) na Nyerere mitano (5) kwa lengo la kuimarisha mawasiliano hifadhini.

**68.** **Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha na kuongeza miundombinu ya malazi hifadhini, Shirika linaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa cottage tatu (3) katika Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro eneo la Horombo. Kukamilika kwa ujenzi wa cottages hizi zenye vitanda 90 kutasidia kuongeza idadi ya watalii wanaopanda Mlima Kilimanjaro. Ujenzi wa cottages mbili (2) Hifadhi ya Taifa Arusha umefikia asilimia 70. Vilevile, Shirika limefanya ukarabati wa Miriakamba cottages pamoja na ujenzi wa Rest House katika Hifadhi ya Taifa Arusha ambapo kwa sasa umefikia asilimia 80. Ukarabati wa Rest House nyingine katika hifadhi hiyo uko katika hatua ya awali za utekelezaji wa mradi huo. Sambamba na hilo, Shirika linaendelea na ujenzi wa jiko moja (1) katika Hifadhi ya Taifa Tarangire ambapo ujenzi umefikia asilimia 26 na kazi inaendelea.

**69.** **Mheshimiwa Spika,** Shirika limeendelea kuibua na kuendeleza mazao mapya ya utalii ikiwemo: utalii wa matibabu

kwenye chemchem za maji moto katika Hifadhi za Taifa Ruaha na Ziwa Manyara; mbio za Marathon katika maeneo ya ndani na pembezoni mwa Hifadhi za Taifa Serengeti, Arusha, Mkomazi, Ruaha, Katavi, Mahale, Gombe, Burigi-Chato, Kisiwa cha Rubondo, Ziwa Manyara, Kitulo na Kilimanjaro; utalii wa Mikutano katika Hifadhi za Taifa Mikumi na Ziwa Manyara; utalii wa kuangalia na kuwapatia majina faru katika Hifadhi za Taifa Mkomazi na Serengeti; utalii wa kutembea juu ya daraja la kamba katika Hifadhi za Taifa Ziwa Manyara na Milima ya Udzungwa ambao ujenzi wa daraja unaendelea na umefikia asilimia 75; utalii wa anga (astro-tourism) katika Hifadhi za Taifa Ziwa Manyara na Tarangire – utalii huu ni wa kipekee na tulivu unaolenga kutazama nyota, sayari na anga la usiku katika maeneo yenye giza na anga safi bila mwanga mwingi; utalii wa kupiga kasia na kupanda farasi katika Hifadhi ya Taifa Arusha; pamoja na utalii wa michezo na burudani (mchezo wa tennis na gofu - Hifadhi ya Taifa Serengeti na mpira wa miguu, pete na kikapu - Hifadhi ya Taifa Mikumi). Shirika linaendelea na ukamilishaji wa uwanja wa mpira wa Gofu katika mfumo ikolojia Serengeti ambao umefikia asilimia 99 Hivyo, nitumie fursa hii kukukaribisha wewe binafsi, Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kutumia uwanja huo kukuza utalii wa michezo.



*Waziri wa Maliasili na Utalii, Dkt. Ashatu Kijaji (Mb.), akiwa na Katibu Mkuu wa Maliasili na Utalii, Dkt. Hassan Abbasi, akikagua mradi wa ujenzi wa Uwanja wa Kimataifa wa Gofu katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.*

**70. Mheshimiwa Spika,** Shirika limeendelea kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi kwa kurusha matangazo ya moja kwa moja, kushiriki matukio ya utalii, kutumia majukwaa ya mitandao ya kijamii na kutumia watu maarufu duniani ili kuvutia watalii kutembelea Hifadhi za Taifa wakiwemo Braydon Bent shabiki wa mpira wa miguu kutoka nchini Uingereza na mpenzi wa shughuli za uhifadhi, Mwanariadha mtanzania Gabriel Geay, Mtangazaji Millard Ayo, MC. Garab, Mwanamitindo wa kimataifa Flaviana Matata, Mlimbwende Rosey Manfere, balozi wa utalii Nakaaya Sumari (Safari channel) pamoja na muandaa maudhui ya mapishi Georgies Kitchen waliotembelea hifadhi za Taifa Serengeti, Arusha, Mikumi, Ruaha na Kitulo. Aidha, kuanzishwa kwa mifumo ya kidijitali ya upatikanaji wa taarifa na huduma za utalii ikiwemo mfumo wa TANAPA Go unaopatikana kwenye simu janja pamoja na matumizi ya majukwaa ya mawasiliano kama Podcast, kumeongeza ufanisi wa utoaji wa taarifa, kurahisisha malipo ya huduma na kuvutia wageni wengi zaidi kutembelea Hifadhi za Taifa.

**71. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Shirika lilishiriki matukio ya Kimataifa ikiwemo IFTM – Top Resa (Paris), My Tanzania Road Show – Southern Europe, Magical Kenya Travel Expo, WTM London, Qatar Travel Mart, FITUR – Spain, Outbound Travel Mart (OTM India) pamoja na ITB Berlin. Aidha, Shirika lilishiriki matukio ya kitaifa yakiwemo maonesho ya Sabasaba, Nane Nane, Tanzania Samia Connect, ZITF, 6th e-Government Annual Meeting, Kili Marathon, Minority Interest Forum Exhibition, pamoja na Siku ya Wanyamapori Duniani. Matukio haya ya kitaifa na kimataifa yameendelea kutumika kama majukwaa yakutangaza vivutio tulivyonavyo pamoja na fursa za uwekezaji zinazopatikana katika hifadhi zetu. Vilevile, Shirika limeendelea kutumia mitandao ya kijamii na vyombo mbalimbali vya habari vikiwemo Televisheni ya Taifa (TBC), ITV, Pori TV, Global TV, Azam, Millard Ayo, Mwananchi, Lemutuz TV, tanzaniaparks ili kuhamasisha wananchi kutembelea hifadhi za Taifa.

**72. Mheshimiwa Spika,** Shirika limeendelea kuhamasisha utalii wa ndani kupitia kampeni na matukio mbalimbali yakiwemo Siku ya Utalii Duniani Septemba, 2025 katika Hifadhi ya Taifa Katavi; A Vote Now Campaign kwa ajili ya kupigia kura Hifadhi ya

Serengeti kama hifadhi bora duniani, Kitulo hifadhi yenye eneo bora la kufanyia fungate duniani na Mlima Kilimanjaro kama kivutio bora duniani kwa mwaka 2025 ilifanyika Oktoba 2025; Shangwe la Sikukuu na TANAPA mwezi Desemba hadi Januari wakati wa sikukuu za kufunga mwaka; New Year Eve Safari Celebration wakati wa kufunga na kufungua mwaka 2026 katika Hifadhi ya Taifa Mikumi; Upendo Porini wakati wa kipindi cha sikukuu ya wapendanao mwezi Februari 2026; Siku ya Wanawake duniani Machi 2026 hifadhi ya Saanane na Saadani; Vote Now Campaign kwa Hifadhi za Taifa 10 (Kilimanjaro, Serengeti, Kitulo, Nyerere, Tarangire, Ruaha, Katavi, Arusha, Milima ya Mahale na Milima ya Udzungwa) zinazowania tuzo katika makundi 8 kwa ‘World Travel Awards’ kwa Bara la Afrika 2026 iliyoanza tarehe 30 Machi 2026 hadi tarehe 17 Julai 2026. Nitumie fursa hii kuwaalika kuendelea kupigia kura hifadhi zetu ziweze kupata tuzo na kuendelea kutambulika zaidi kitaifa na kimataifa.




*Hifadhi za Taifa zinanazowania tuzo za World Travel Awards, 2026.*

**73.** **Mheshimiwa Spika,** Shirika limeendelea kutangaza fursa za uwekezaji katika hifadhi za Taifa ambapo jumla ya maeneo ya uwekezaji 98 yalitangazwa katika Hifadhi za Taifa Mikumi (6), Nyerere (52), Ruaha (31) na Saadani (9). Aidha, hadi sasa maeneo 26 katika Hifadhi za Taifa Mikumi (4), Nyerere (10), Ruaha

(10) na Saadani (2) yamepata wawekezaji. Vilevile, Shirika linaendelea kutangaza maeneo ambayo bado hayajapata wawekezaji ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu muhimu ya kuyafikia maeneo hayo.

**74. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha utendaji kazi kwa watumishi, Shirika limejenga nyumba za watumishi 15 katika Hifadhi za Taifa Ibanda-Kyerwa (5), Serengeti (5) na Tarangire (5). Vilevile, limekarabati nyumba za watumishi 118 zilizopo ndani ya hifadhi za Taifa ili kuwezesha watumishi kuongeza morali ya ufanyaji kazi. Ukarabati huu umefanyika katika hifadhi za Taifa Ibanda-Kyerwa (1), Milima ya Mahale (36), Mkomazi (1), Nyerere (62), Ruaha (5), Rumanyika-Karagwe (1), Serengeti (1), Tarangire (2), Milima ya Udzungwa (7) na Kitulo (2)



*Moja ya nyumba za watumishi 2 in 1 zilizojengwa katika hifadhi ya Taifa Tarangire.*

#### 5.3.1.5 *Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania - TAWA*

**75. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ina jukumu la kusimamia rasilimali za wanyamapori nje ya maeneo ya Hifadhi za Taifa na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro ili kudhibiti ujangili, uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa na biashara haramu ya nyara sambamba na kusimamia na kuendeleza utalii kwa manufaa ya jamii zinazozunguka maeneo ya hifadhi na Taifa kwa ujumla.

**76.** **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mamlaka imefanya doria 16,039 ndani na nje ya Mapori ya Akiba na Tengefu. Doria hizo zimefanikisha kukamata vielelezo mbalimbali ikiwemo mifugo 33,147 na kutegua mitego 1,338 ya nyaya za kutegea wanyamapori. Aidha, watuhumiwa 2,117 walikamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria. Hatua hii imeimarisha hali ya usalama kwenye maeneo ya hifadhi na kuendelea kuimarisha usalama wa wanyamapori dhidi ya ujangili.

**77.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha miundombinu ya shughuli za utalii, Mamlaka imekamilisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 72.04 katika Mapori ya Akiba Mpanga-Kipengere (26km), Wami-Mbiki (35km) na Pande (11.04km) pamoja na kufanya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 1,021 katika Mapori ya Akiba Muhesi (960km) na Kizigo (61km). Vilevile, ujenzi wa kiwanja kidogo cha ndege na eneo la kupumzikia wageni (lounge) unaendelea katika Pori la Akiba Mpanga-Kipengere pamoja na vituo vitatu (3) vya askari katika Mapori ya Akiba Moyowosi (1), Kizigo (1) na Kilombero (1) upo katika hatua za mwisho za ukamilishaji. Pia, Mamlaka inaendelea na ujenzi wa eneo la kupumzikia wageni, kujenga eneo la kutazama wanyamapori (animal observation hide-out) na kambi moja (1) ya utalii katika Hifadhi ya Wanyamapori Makuyuni. Kazi nyingine zinazoendelea ni ujenzi wa bwawa la kuogelea na miundombinu ya michezo mbalimbali ikiwemo uwanja mdogo wa mpira wa miguu, uwanja wa tenisi, mpira wa wavu, mpira wa kikapu katika Pori la Akiba Pande; na kukarabati eneo la chakula na vinywaji kwa wageni (lounge) katika Pori la Akiba Wami-Mbiki.



*Eneo la kupumzikia wageni (lounge) katika Pori la Akiba Mpanga-Kipengere.*

**78. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Mamlaka imekamilisha mapitio ya Mpango wa Jumla wa Usimamizi wa Pori la Akiba Selous na Mpango Jumuishi wa Usimamizi kwa ajili ya Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara. Aidha, Mamlaka imeboresha nyanda za malisho kwa kuondoa mimea vamizi katika eneo la hekta 10,481.31 katika Mapori ya Akiba Kijereshi (hekta 500), Maswa (hekta 9,810), Mpanga-Kipengere (hekta 3.81), Kilombero (hekta 118), Uwanda (hekta 15), Mkungunero (hekta 14.5), Mto wa Mbu-Longido GCA (hekta 16.5) na Lunda-Nkwambi (hekta 3.5).

**79. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka imeendelea kutangaza uwindaji wa kitalii, utalii wa picha na fursa za uwekezaji katika maeneo inayoyasimamia kupitia maonesho saba (7) ya kitaifa ambayo ni: Maonesho ya Biashara ya 49 ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba), Maonesho ya Wakulima (Nanenane), Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Zanzibar, Nyangumi migration festival, Wiki ya Utalii, Maadhimisho ya Siku ya Wanyamapori Duniani, Maadhimisho ya Siku ya Misitu Duniani na onesho moja (1) la kimataifa la Abu Dhabi International Hunting & Equestrian Exhibition (ADIHEX, 2025). Sambamba na hilo, Mamlaka iliandaa na kushiriki kampeni 10 za kuhamasisha utalii wa ndani ambazo ni: World Tourism Day, Nyerere Day, Tabora Nyamachoma festival (Tabora zoo), Shangwe la mabingwa wa Yanga na TAWA Sea Cruiser, Kaliua Wildlife Festival, Korosho

Marathon (Mtwara), Funga mwaka kijanja na TAWA, University Bash, Siku ya Wanawake Duniani na Shangwe la Valentine na Mishkaki pori. Aidha, katika kuimarisha utalii wa kitamaduni, Mamlaka imejenga sanamu ya Ibn Batutta katika Hifadhi ya Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara. Batutta anatajwa kuwa msafiri na msomi maarufu aliyesaidia kukuza lugha ya Kiswahili kwenye ukanda wa Pwani ya Afrika Mashariki ambaye alitembelea Mji wa Kilwa ilipo Hifadhi ya Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara mnamo karne ya 14.



*Sanamu ya Ibn Batutta, msomi na msafiri maarufu duniani iliyotengenezwa katika Hifadhi ya Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara.*

**80. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ilishiriki kikao cha 20 cha Mkutano wa nchi wanachama wa CITES kinachotoa fursa ya kujadili masuala ya uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori na misitu. Aidha, Mamlaka imesaini mikataba tisa (9) ya uwekezaji katika Mapori ya Akiba Mpanga Kipengere (1), Kijereshi (1), Wami-Mbiki (1) na Selous (3); Mapori Tengefu Lolkisale (1), Rungwa (1) na Burko Open Area (1).

**81. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka imeendelea kuhakikisha wananchi wananufaika na uhifadhi kwa kurejesha stahili zitokanazo na shughuli za utalii ambapo jumla ya Shilingi 13,011,464,743.64 zimetolewa kwa WMAs 15, Halmashauri za

Wilaya 40 na Vijiji 144. Aidha, TAWA imechangia jumla ya Shilingi 1,127,058,772 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa jamii ikiwemo ujenzi wa zahanati, madarasa manne (4) na ofisi mbili (2) katika Wilaya ya Meatu; ununuzi wa madawati 3,314 katika Wilaya za Bunda (1,534), Serengeti (1,480), Bariadi (150), na Itilima (150); na ununuzi wa vitanda vya Hospitali vikiwemo 28 vya kujifungulia wakinamama katika Wilaya za Serengeti (16) na Bunda (12), na Kompyuta 23 katika Wilaya za Bunda (16) na Serengeti (7). Vilevile, Mamlaka imeendelea kuratibu shughuli za uvuvi na ufugaji nyuki katika Mapori ya Akiba ya Ugalla, Uwanda, Moyowosi, Rukwa na Kilombero ambapo jumla ya wavuvi 30,811 na wafugaji nyuki 515 walipewa vibali kutoka katika Halmashauri za Wilaya 14 za Sumbawanga, Momba, Ulanga, Ifakara, Mlimba, Malinyi, Mlele, Sikonge, Urambo, Tabora, Kibondo, Kasulu, Kakonko na Nsimbo.



*Kushoto ni Zahanati ya Matale katika kijiji cha Matale Wilaya ya Meatu na kulia ni Madarasa na Ofisi katika Shule ya Msingi Mbugayabanya katika Kijiji cha Mbugayabanya Wilaya ya Meatu.*



*Kushoto ni madawati yaliyogawiwa kwenye Shule za Msingi katika Wilaya za Bunda, Serengeti, Bariadi, na Itilima na kulia ni kompyuta, vitanda na madawati vilivyogawiwa kwenye Shule za Msingi katika Wilaya za Bunda na Serengeti.*

**82. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi, Mamlaka imekamilisha ujenzi wa ofisi moja (1) katika Pori la Akiba Kilombero; na malango madogo sita (6) ya kukusanya mapato katika Mapori Tengefu Mto wa Mbu na Ziwa Natron. Sambamba na hilo, Mamlaka imenunua pikipiki 33 za doria na magari sita (6) kwa ajili ya shughuli za utawala na doria. Aidha, Mamlaka imeendelea kujenga ofisi kwa ajili ya shughuli za kiutawala ambapo ujenzi wa ofisi ya Hifadhi ya Magofu ya kale Kunduchi umekamilika. Pia, ujenzi wa ofisi mbili (2) upo katika hatua za ukamilishaji ambapo ofisi moja (3 in 1) ni kwa ajili ya Mapori ya Akiba matatu (3) yaliyopo Kanda ya Magharibi na ofisi nyingine ni kwa ajili ya Pori la Akiba Wami-Mbiki.



*Jengo la Ofisi katika Pori la Akiba Kilombero.*

**83. Mheshimiwa Spika**, katika kuongeza nguvu kazi na ufanisi katika kutekeleza majukumu, Mamlaka imeajiri askari 551 wa ajira ya kudumu ambapo kati yao, askari 256 wamekamilisha mafunzo ya ukakamavu na kupangiwa vituo vya kazi na 295 wanaendelea na mafunzo ya ukakamavu na utayari.

### 5.3.1.6 *Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro – NCAA*

**84. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro ina jukumu la kuendeleza uhifadhi wa maliasili na malikale; kuendeleza utalii na kutoa huduma kwa jamii. Aidha, Mamlaka inasimamia na kuendeleza maeneo ya urithi wa kiutamaduni ya mapango ya Amboni, Kimondo cha Mbozi,

mabaki ya Engaruka Monduli-Arusha, maeneo ya historia ya zama za mawe Eyasi (Mumba Rock-Shelter) yaliyopo Wilayani Karatu pamoja na Pori la Akiba Pololeti.

**85. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imeendelea kuimarisha ulinzi wa maliasili na malikale kwa kufanya doria za kawaida 6,068 na doria shirikishi 15 kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama. Doria hizo zimewezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 575, mifugo 26,878, meno ya tembo mazima nane (8), vipande vya meno ya tembo 82, risasi tisa (9) pamoja na kutegua mitego 215 ya nyaya za kutega wanyamapori. Aidha, Mamlaka imefunga visukuma mawimbi kwa faru 10, simba wanne (4), chui mmoja (1) na imeweka alama za utambuzi kwa faru tisa (9) kwa ajili ya kufuatilia mienendo yao. Vilevile, Mamlaka imekamilisha ukarabati wa Kituo cha Askari cha Nayobi na inaendelea na ujenzi wa kituo kimoja (1) cha askari katika Eneo la Mbulumbulu-Lositete Wilayani Karatu na ukarabati wa vituo viwili (2) vya askari vya Endamagha (1) na Lemala (1).

**86. Mheshimiwa Spika,** Katika hatua nyingine, Mamlaka imesafisha mpaka wa kilomita 158.9 na kuweka vigingi 19 kwa ajili ya kupunguza migogoro ya mipaka kati ya Eneo la Hifadhi na vijiji vinavyopakana na hifadhi pamoja na kudhibiti matukio ya mioto holela. Utekelezaji wa shughuli hizi umeimarisha uhifadhi wa maliasili ndani ya Hifadhi, umepunguza migongano baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu pamoja na kudhibiti majanga ya moto na migogoro ya mipaka kati ya hifadhi na maeneo yanayoizunguka.

**87. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha mahusiano na jamii inayoishi ndani ya hifadhi na pembezoni mwa hifadhi, Mamlaka imetoa elimu ya uhifadhi na mbinu mbadala za kukabiliana na matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu kwa jamii kwa kufanya mikutano 66 kwa wananchi 12,020. Vilevile, Mamlaka imetoa elimu kwa jamii kupitia vipindi 12 vya redio na mafunzo ya ufugaji nyuki kwa vikundi 11 kwa lengo la kuwawezesha wananchi kujikwamua kiuchumi. Vilevile, Mamlaka imetoa ufadhili wa ada kwa wanafunzi 1,183 katika ngazi ya shule za msingi Mahitaji maalumu (2), Sekondari (1027) vyuo vya kati (141) na vyuo vikuu (16). Hadi mwezi Aprili, 2026 jumla ya Shilingi

778,677,520 zimetumika kuwezesha wanafunzi hao. Aidha, katika kuboresha ufadhili katika ngazi ya elimu ya vyuo vikuu Mamlaka imeingia makubaliano na Bodi ya Mikopo kwa ajili ya kuona namna bora ya utoaji wa ufadhili. Utekelezaji wa majukumu haya umeimarisha mahusiano na ustawi wa jamii inayoishi ndani ya hifadhi.

**88. Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Mamlaka imegawa unga wa mahindi kilo 1,782 na sukari kilo 230 kwa ajili ya huduma ya uji kwa shule 28 za msingi zilizopo ndani ya Hifadhi. Katika hatua nyingine, Mamlaka inaendelea na ujenzi wa vyoo katika shule tano (5) za Meshili, Bulati, Misigyo, Endulen na Makao Mapya. Pia, Mamlaka imeendelea kutoa huduma za afya bure katika Zahanati ya Ngorongoro kwa wananchi 8,935 waishio ndani ya Hifadhi. Jitihada hizi zinalenga kuongeza ustawi wa wakazi wanaoishi ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro pamoja na kudumisha mahusiano baina ya Mamlaka na jamii inayoishi ndani ya Hifadhi.

**89. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha nyanda za malisho ya wanyamapori ndani ya Eneo la Hifadhi, Mamlaka imefyeka na kung'oa mimea vamizi katika eneo lenye ukubwa wa hekta 1,063.3 na kuchoma moto eneo lenye ukubwa wa hekta 9,030 kwa utaratibu wa moto mpango. Vilevile, Mamlaka imegawa jumla ya miche ya miti 55,183 kwa jamii inayozunguka Hifadhi na wadau mbalimbali wa mazingira kwa ajili ya kutunza mazingira nchini. Jitihada hizi zimeboresha maeneo ya malisho ya wanyamapori pamoja na mazingira kwa ujumla.

**90. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha miundombinu ya utalii, Mamlaka imeanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa barabara ya Loduare hadi Golini yenye urefu wa kilomita 29.5 kwa kiwango cha tabaka gumu. Aidha, Mamlaka imekarabati mtandao wa barabara wenye urefu wa kilomita 356 ndani ya hifadhi. Mamlaka pia imefanya maboresho ya kawaida katika kiwanja cha ndege cha Ndutu na matengenezo maalum ya kiwanja cha ndege cha Ngorongoro yanaendelea. Vilevile, Mamlaka imekarabati njia za utalii za kutembea kwa miguu zenye urefu wa kilomita 18 katika maeneo ya Endoro (1km), Lolmalasin (14km), njia ya kushuka Empakaai (1.5km) na njia ya

kupanda Empakaai (1.5km). Kwa upande mwingine, Mamlaka imekamilisha ujenzi wa miradi miwili (2) ya maji katika maeneo ya Olduvai na Ndutu ambapo miradi hii imejumuisha ujenzi wa matenki ya kuhifadhia maji yenye ujazo wa lita 135,000 kwa Olduvai na lita 35,000 kwa Ndutu. Sambamba na hilo, Mamlaka imechimba visima viwili (2) vya maji katika maeneo ya Kakesio na Endulen kwa ajili ya jamii na matumizi ya ofisi.

**91. Mheshimiwa Spika,** katika kuongeza mazao mapya ya utalii, Mamlaka kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China imekamilisha ujenzi na kuzindua Makumbusho ya Jiolojia ya Ngorongoro - Lengai katika eneo la Kamyn iliyopo Wilayani Karatu, ambayo ni makumbusho ya pili ya jiopaki Barani Afrika. Kukamilika kwa makumbusho haya kumeongeza idadi ya vivutio vya utalii na kuongeza idadi ya watalii.



*Jengo la Makumbusho ya kisasa ya Jiopaki ya Ngorongoro Lengai lililopo nje kidogo ya Lango la kuingilia katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro wilayani Karatu, Mkoani Arusha.*

**92. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha matumizi ya TEHAMA, Mamlaka imebuni na kutekeleza Mfumo wa Kidijitali wa Makazi Online Portal – MoPo. Mfumo huo umerahisisha usimamizi wa maeneo ya kambi za msimu za kitalii kuanzia usajili wa wawekezaji hadi usimamizi wa mikataba, ukiwa na vipengele vya e-Auction, malipo mtandaoni, usimamizi wa mikataba kwa njia ya kidijitali na ufuatiliaji wa mapato na utendaji. Vilevile, Mamlaka inaendelea na ujenzi wa malango janja (smart gates) katika

malango ya Loduare, Seneto, Lemala na Golini ndani ya Hifadhi ambapo ujenzi umefikia asilimia 70.

**93. Mheshimiwa Spika,** katika kutangaza vivutio vya utalii vinavyopatikana ndani ya Hifadhi, Mamlaka imeshiriki jumla ya maonesho 10 nje ya nchi ambayo ni: Akwaaba-Nigeria, Southern roadshow by KILIFAIR, APIMONDIA Congress-Denmark, Magical Kenya, Roadshow in Europe-By Mount, WTA Bahrain, OTM Mumbai India, Qatar travel Matt, FITUR Madrid Spain na My Tanzania Road show 2026-Hamburg-Germany & Norway. Aidha, imeshiriki maonesho nane (8) ya ndani ya nchi yakiwemo: Sabasaba (Dar es Salaam) na Nanenane (Mbeya na Arusha); Maonesho ya Biashara Afrika Mashariki-Mwanza; Siku ya Wanyamapori Duniani-Arusha, SHIMMUTA-Morogoro, Kongamano la 15 la Kimataifa la Kisayansi la TAWIRI-Arusha, Rombo Marathon-Rombo. Vilevile, Mamlaka imefanya kampeni tano (5) kwa ajili ya kuhamasisha utalii wa ndani ambazo ni Merry and Wild Awaits, camping bulati and hiking lolmalasin, uzinduzi wa chapa ya Ngorongoro, Amboni Caves: Educational Tour na Valentine Day Promotional campaigns. Kwa upande mwingine, Mamlaka inatangaza vivutio vyake mubashara kupitia Ngorongoro live streaming pamoja na kuongeza kamera tatu (3) mpya. Mfumo huu umeunganishwa na mitandao ya kijamii ya NCAA ili kuwafikia wadau wa utalii duniani. Hatua hizi zimewezesha kuongeza idadi ya wwatalii wakigeni katika maeneo ya hifadhi.

**94. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha watumishi wanatekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi, Mamlaka imeendelea kuwajengea uwezo kwa kuwawezesha kuhudhuria mafunzo mbalimbali ya kitaaluma. Askari 207 wamepatiwa mafunzo ya ulinzi wa rasilimali za wanyamapori na misitu; na askari nane (8) walipatiwa mafunzo ya urushaji wa ndege nyuki. Vilevile, askari 57 wamepatiwa mafunzo mahsusi kwa ajili ya uangalizi wa faru na watumishi 20 wanaendelea na mafunzo ya kijeshi katika kituo cha Mafunzo Mlele. Katika hatua nyingine, Mamlaka imekamilisha ujenzi na kuanza kutumia ofisi ya Makao Makuu katika eneo la Kamyn, Wilayani Karatu. Sambamba na hilo, Mamlaka imefunga nishati ya umeme wa jua katika Kituo cha Askari cha Garlus na Makumbusho ya Olduvai. Aidha, Mamlaka iliwezesha watumishi 125 kushiriki mashindano ya

SHIMMUTA kwa ajili ya kuimarisha afya, kuongeza motisha ya kazi pamoja na kukuza mahusiano mema miongoni mwa watumishi.

#### *5.3.1.7 Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania - TAWIRI*

**95. Mheshimiwa Spika,** Taasisi ina jukumu la kufanya, kuratibu na kusimamia tafiti za wanyamapori nchini, kwa lengo la kuishauri Serikali na wadau namna bora ya kusimamia na kuendesha shughuli za uhifadhi na utalii endelevu.

**96. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Taasisi imeendelea kufanya tafiti za kimkakati na ufuatiliaji wa wanyamapori kwa lengo la kuhakikisha uhifadhi na utalii endelevu. Maeneo ya kipaumbele katika tafiti zilizofanyika ni pamoja na; sensa ya wanyamapori nchini, utatuzi wa migongano baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu; matumizi ya teknolojia katika uhifadhi; uchunguzi na ufutialiaji wa afya ya mifumo ikolojia; na kusambaza matokeo ya tafiti.

**97. Mheshimiwa Spika**, Taasisi imetekeleza jumla ya miradi 24 ya utafiti, iliyojikita katika kutatua changamoto za uhifadhi ikiwemo; migongano baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu nne (4), matumizi ya teknolojia katika uhifadhi nne (4), afya ya mifumo ikolojia mbili (2), mahusiano ya viumbe na ikolojia zao saba (7), uhifadhi wa bioanuai tatu (3), urejeshwaji wa baadhi ya jamii za wanyamapori zilizotoweka katika mifumo ikolojia moja (1) na tafiti za nyuki tatu (3). Aidha, Taasisi imeratibu na kusimamia miradi ya tafiti za wanyamapori 184 zenye jumla ya watafiti 430, ambapo watafiti 271 sawa na asilimia 63.02 ni watanzania. Idadi hii ya watafiti wa ndani inaonesha mwamko mkubwa wa watanzania katika jitihada za kuendeleza na kusimamia uhifadhi wa wanyamapori na maendeleo ya utalii nchini.

**98. Mheshimiwa Spika**, Taasisi imekamilisha zoezi la Sensa ya Wanyamapori nchini. Sensa kama hii ni ya pili kufanyika na hufanyika kila baada ya miaka 10, ikiwa ni sehemu ya Mpango wa Kitaifa wenye lengo la kubaini uwepo, idadi, mtawanyiko na mienendo ya wanyamapori, sambamba na kubaini viashiria

hatarishi vinavyoweza kuathiri ustawi na mazingira yao kwa kulinganisha na matokeo ya awali. Aidha, sensa hii imefanyika kwa kutumia fedha za ndani kwa mara ya kwanza tofauti na sensa ya awali. Hii inaonesha wazi juhudi madhubuti za Serikali katika kuimarisha uhifadhi wa rasilimali zetu za asili. Matokeo ya sensa hii yanaonesha mwenendo chanya wa uwepo na idadi ya wanyamapori na umuhimu wake katika kusimamia sera, uhifadhi, uendelezaji utalii na pato la Taifa kwa ujumla. Aidha, tofauti na sensa ya awali zoezi hili lilitumia teknolojia ya kamera zenye uwezo mkubwa (High resolutions Obliques Cameras Counts-OCC) na teknolojia ya akili mnemba yenye uwezo wa kuchakata, kutambua na kuidadi wanyamapori na hivyo kuwezesha matokeo kutoka kwa muda mfupi ukilinganisha na ile ya awali.



*Zoezi la kuhesabu wanyamapori kwa kutumia teknolojia ya kamera zilizo na uwezo mkubwa pamoja na akili mnemba.*

**99. Mheshimiwa Spika,** katika kutatua changamoto ya migongano baina ya binadamu na wanyamapori, Taasisi kwa kutumia matokeo ya tafiti zake ilishirikiana na Shirika la Mzinga (JWTZ), kuboresha kilipuzi kilichobuniwa hapo awali (bomu baridi) na kubuni kifaa cha kurushia (launchers) mabomu baridi, ambapo kwa maboresho hayo na kwa kutumia kirushio hicho, bomu baridi sasa lina uwezo wa kufika umbali wa mita 150 hadi

170 ikilinganishwa na hapo awali likirushwa kwa mkono ambapo lilikuwa linafika umbali wa mita 15 hadi 30 pekee. Hatua hiyo imeongeza ufanisi katika kuondoa tembo kutoka maeneo ya wananchi na kuongeza usalama kwa watumiaji wa mabomu baridi.

**100. Mheshimiwa Spika,** Katika hatua nyingine, elimu ya kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu ilitolewa kwa wakufunzi (ToTs) 672 (wanawake 187) katika Wilaya za Mkinga, Korogwe, Same, Mwanga, Babati, Karatu, Meatu, Bunda, Serengeti, Itigi, Manyoni, Iringa Vijijini, Wanging'ombe na Mbarali. Mafunzo hayo yalijikita kwenye mbinu zilizoboreshwa na zenye ufanisi mkubwa zikiwemo matumizi ya mipira (noise ball) inayotoa milio mbalimbali inayoweza kuwafukuza tembo, matumizi sahihi ya vilipuzi na virushio vyake na uzio unaotoa milio na mwanga tofauti kulinda maghala ya mazao; vyanzo vya maji; na mazizi ya mifugo. Wakufunzi hao wataendelea kuelimisha jamii kwenye maeneo yao jambo ambalo litapunguza kadhia inayotokana na migongano baina ya binadamu na wanyamapori. Pia Taasisi ilitoa mafunzo ya njia bora za ufugaji nyuki na uboreshaji wa thamani wa mazao yatokanayo na nyuki kwa wadau 499 (wanawake 182) wa Jijini Arusha na maeneo ya jirani ya Wilaya za Ngorongoro na Kiteto. Lengo kuu ni kuongeza jitihada za Serikali katika kuimarisha mnyororo wa thamani na kuinua vipato vya wananchi.



*Maaskari wa Vijiji (VGS) wakipatiwa mafunzo ya matumizi sahihi ya kirushio cha mabomu baridi.*

**101. Mheshimiwa Spika,** Katika hatua nyingine, Taasisi imefunga visukuma mawimbi (GPS Satellite collars) 51 kwa tembo viongozi katika maeneo ya Wilaya za Manyoni (2), Itigi (2), Ikungi (1), Singida (1), Igunga (2), Same (1), Korogwe (2), Bunda (2), Karagwe (3), Meatu (2), Chemba, Chamwino (2), Uyui (2), Iringa (3), Mvomero (2), Bagamoyo/Chalinze (3), Itilima (2), Kondoa (2), Morogoro, Tunduru (2), Kilombero (2), Mbarali (3) na hifadhi za Nyerere (3), Ruaha (2). Visukuma mawimbi hivi vinawezesha kufanya ufuatiliaji wa makundi hayo na kuyarejesha mapema kabla hayajatoka nje ya maeneo yaliyohifadhiwa na kusababisha madhara kwa jamii.



*Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb.), akipokea maelezo ya zoezi la kukamata tembo toka Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI) kabla ya kumvisha kisukuma mawimbi katika Pori la Akiba Mkungunero.*

**102. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ulinzi, ufuatiliaji na uhifadhi wa wanyamapori walio hatarini kutoweka, jumla ya faru weusi 34 waliwekewa visukuma mawimbi na alama za utambuzi katika Mfumo ikolojia Serengeti. Visukuma mawimbi hivyo vinawezesha kufuatilia mienendo ya faru hao ili kuhakikisha usalama wao muda wote na kuwatambua kila mmoja. Aidha, mbwa mwitu dume mmoja (1) alihamishwa kutoka Hifadhi ya Taifa Nyerere na kupelekwa Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi kwa lengo la kuimarisha vinasaba (Genetic diversity) vya makundi yaliyopo katika hifadhi hiyo.

**103. Mheshimiwa Spika,** Taasisi imeendelea kufuatilia afya za wanyamapori na mifumo ikolojia yote nchini. Zoezi hili ni endelevu na hufanyika ili kubaini mapema uwepo wa magonjwa na kuyadhibiti kabla ya mlipuko na kuhakikisha uhifadhi endelevu, utalii na ustawi wa jamii zinazozunguka maeneo ya hifadhi. Aidha, katika kipindi hiki hakukuwa na ugonjwa ulioripotiwa na hivyo mifumo ikolojia yetu imeendelea kuwa salama.



*Daktari wa Wanyamapori, akichukua sampuli za damu kutoka kwa simba ikiwa ni sehemu ya ufuatiliaji wa afya za wanyamapori na mifumo ikolojia.*

**104. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha matokeo ya tafiti yanawafikia wadau mbalimbali, Taasisi iliandaa Kongamano la 15 la Kimataifa la Kisayansi lililofanyika tarehe 03-05 Desemba, 2025 Jijini Arusha. Mada kuu ya Kongamano ilikuwa "Ubunifu katika Uhifadhi wa Wanyamapori na Utalii Endelevu: Kuelekea Dunia yenye Mabadiliko" ("Innovations in Wildlife Conservation and Sustainable Tourism: Navigating the Future in a Changing World"). Kongamano hilo lilihudhuriwa na washiriki zaidi ya 600 kutoka nchi 24 duniani ambapo jumla ya mada 264 ziliwasilishwa na kujadiliwa. Kongamano hilo limetoa fursa ya kutumia matokeo ya tafiti za kisayansi ili kuboresha mbinu za uhifadhi na kuendeleza utalii kwenye maeneo mbalimbali na kukuza uchumi wa Taifa.

**105. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha mazingira ya

utendaji kazi kwa watumishi wake, Taasisi inaendelea na ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makao Makuu ambapo kwa sasa utekelezaji wake umefikia asilimia 18. Aidha, Taasisi imewapatia mafunzo ya muda mrefu watumishi 18 na muda mfupi watumishi 32 ili kuwajengea uwezo katika kutekeleza majukumu yao na kuongeza ufanisi.

### 5.3.1.8 *Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori MWEKA – CAWM*

**106. Mheshimiwa Spika,** Chuo kina jukumu la kutoa mafunzo kuanzia Cheti cha Msingi, Cheti cha Ufundi, Stashahada, Shahada ya kwanza na Shahada ya Uzamili. Aidha, Chuo kina jukumu la kufanya tafiti na kutoa huduma za ushauri wa kitaalam na ugani katika nyanja za usimamizi wa wanyamapori na utalii.

**107. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Chuo kimedahili jumla ya wanafunzi 1,348 sawa na asilimia 134.8 ya lengo la wanafunzi 1,000 ambapo wanafunzi 563 ni wa kike na 785 ni wa kiume. Aidha, Chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 172 kuhusu uongozaji wa watalii wapanda milima, uongozaji wa wageni, na ukamataji na uhamishaji wa nyoka. Vilevile, Chuo kimeanza kutoa mafunzo kwa programu mpya za Usimamizi wa Mazingira na Udhibiti wa Taka pamoja na Usimamizi wa Maliasili kwa ngazi ya Cheti cha Msingi hadi Shahada ya Uzamili. Sambamba na hilo, Chuo kimedahili wanafunzi 101 ngazi ya Shahada ya kwanza katika kozi za Usimamizi wa Mazingira na Udhibiti wa Taka pamoja na Usimamizi wa Maliasili. Juhudi za kutangaza kozi mpya zilizosajiliwa kwa wadau ndani na nje ya nchi zinaendelea kupitia tovuti ya Chuo, mitandao ya kijamii na maonesho mbalimbali yakiwemo: Karibu - Kili Fair – Arusha, Sabasaba – Dar es Salaam, Wiki ya Elimu ya Juu – Zanzibar, Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia – Tanga, Majimaji - Ruvuma, Siku ya Misitu Duniani - Lindi, na Siku ya Wanyamapori Duniani - Arusha pamoja na kutembelea shule za sekondari katika mikoa mbalimbali.

**108. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha utoaji wa mafunzo na kutatua changamoto zinazokabili Sekta za Wanyamapori na

Utalii, Chuo kimeendelea kufanya tafiti mbalimbali katika nyanja za bioanuwai, uhifadhi wa mazingira, uhifadhi wa wanyamapori, magonjwa ya wanyamapori, usimamizi wa utalii na migongano baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo mbalimbali nchini. Tafiti hizo zimechangia upatikanaji wa taarifa muhimu za kufundishia, mbinu za utatuzi wa migongano baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu katika jamii inayozunguka maeneo yaliyohifadhiwa, kupambana na ujangili pamoja na kuendeleza shughuli za uhifadhi na utalii nchini. Baadhi ya tafiti zilizofanyika ni pamoja na Ufuatiliaji wa wanyamapori; maisha na ikolojia ya paka wa dhahabu (African golden cat) aliyegundulika nchini mwaka 2019 katika msitu wa Minziro Mkoani Kagera anayepatikana katika nchi za bonde la ufa la Albertine; tathmini ya maeneo mbadala ya kuhifadhi kobe chapati (pancake tortoise) kaskazini mwa Tanzania; na utafiti juu ya changamoto za ufanisi wa usimamizi shirikishi wa maeneo ya Jumuiya za Wanyamapori Nchini. Aidha, kupitia tafiti hizo wataalam wameweza kutoa machapisho 15 katika majarida ya kisayansi ya kimataifa pamoja na kuhudhuria na kutoa mada katika makongamano ya kisayansi ndani na nje ya nchi.



*Picha ya paka wa dhahabu (African Golden Cat) katika msitu wa Minziro wilaya ya Misenyi mkoani Kagera.*

**109. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi pamoja na mazingira ya kujifunzia kwa wanafunzi, Chuo kinaendelea na ujenzi wa darasa moja (1), jiko, vyoo na bafu katika eneo la mafunzo kwa vitendo lililopo katika Kijiji cha Arash, Tarafa ya Loliondo Wilayani Ngorongoro

ambapo ujenzi umefikia asilimia 70. Aidha, Chuo kimekarabati nyumba tano (5) za watumishi, vyumba vitano (5) vya madarasa, hosteli nne (4) za wanafunzi na ofisi nane (8) za watumishi. Vilevile, Chuo kimefunga meza 20 na makabati 18 kwenye ofisi za watumishi na kuendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma ya mtandao wa intaneti kwa wanafunzi na watumishi. Sambamba




na hilo, taratibu za ununuzi wa magari matatu (3) aina ya KAMAZ kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo zinaendelea.

*Gari aina ya Kamaz inayotumika katika shughuli za mafunzo kwa vitendo katika Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka.*

#### 5.3.1.9 *Taasisi ya Taaluma ya Usimamizi wa Wanyamapori Pasiansi - PWTI*

**110.** **Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi ina jukumu la kutoa mafunzo ya Askari Wahifadhi wa Wanyamapori na Waongoza Wataliii katika ngazi ya Astashahada ya Awali, Astashahada na Stashahada. Vilevile, taasisi hutoa mafunzo ya muda mfupi kwa Askari Wanyampori wa Vijiji (VGS), Askari wa Misitu ya vijiji (VFG) na Vikosi vya Ulinzi wa Fukwe.

**111.** **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Aprili 2026, Taasisi imedahili jumla ya wanafunzi 681, kati yao wa kike ni 195 na wa kiume ni 486. Aidha, Taasisi imeanzisha kozi mpya ya stashahada ya Uaskari wa Wanyamapori na Himasheria ambapo jumla ya wanafunzi 11 wamedahiliwa ili kuongeza wigo wa mafunzo. Vilevile, Taasisi imetoa mafunzo ya muda mfupi kwa wanafunzi 88 waliofundishwa mbinu mbalimbali za kupambana na

wanyamapori wakali na waharibifu kutoka Halmashauri za Wilaya ya Tanganyika, Iringa vijijini, Kibondo na Longido.

**112.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha mazingira ya kujifunzia, Taasisi inaendelea na ujenzi wa bweni lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 400 ambapo hadi kufikia Aprili, 2026 umefikia asilimia 23.5 na unatarajia kukamilika Desemba, 2026. Aidha, Taasisi imeanza taratibu za ujenzi wa vyumba vinne (4) vya madarasa na imeendelea kukarabati mabweni mawili (2) na kukamilisha uwekaji wa umeme katika kituo cha mafunzo kwa vitendo Matongo Wilayani Bariadi. Vilevile, ujenzi wa hanga la darasa katika eneo la mafunzo Fort Ikoma linaloweza kuchukua wanafunzi 300 umekamilika. Sambamba na hilo, Taasisi imenunua mahema (20), projekta (5), kompyuta 20 na kuendelea kusimamia kampuni ya Ulinzi ya Pasiansi Wildlife Security Company Limited-PASCO ambayo hadi sasa imeajiri askari 302.

**113.** **Mheshimiwa Spika,** ili kuwajengea watumishi uwezo wa kufanya kazi kwa weledi na kuongeza tija, Taasisi imewezesha watumishi sita (6) kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi sita (6) kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi.

### 5.3.1.10 *Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii, Likuyu Sekamaganga - CBCTC*

**114.** **Mheshimiwa Spika**, Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii – Likuyu Sekamaganga kina jukumu la kuijengea jamii uwezo kwa njia ya mafunzo ili iweze kushiriki kikamilifu katika uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za maliasili. Kituo kinatoa mafunzo ya muda mfupi ya kozi za Uaskari Wanyamapori wa Vijiji (VGS), Askari wa Misitu wa Vijiji (VFG), Vikosi vya Ulinzi wa Fukwe pamoja na Viongozi na Wajumbe wa Kamati za Maliasili za Vijiji. Aidha, kituo kinatoa mafunzo ya muda mrefu ya kozi ya Utalii na Uongozaji Watalii kwa ngazi ya Astashahada ya Awali, Astashahada na Stashahada.

**115.** **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Aprili 2026, Kituo kimetoa mafunzo kwa wanafunzi 266 wakiwemo wanaume 213 na wanawake 53, ambapo kati yao wanafunzi 73 walipatiwa mafunzo ya muda mrefu ya kozi ya Utalii na Uongozaji Watalii, wanafunzi 135 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi ya Askari

Wanyamapori wa Vijiji (VGS) na wanafunzi 58 ambao ni viongozi na wajumbe wa kamati za maliasili za vijiji walipatiwa mafunzo ya usimamizi shirikishi wa maliasili. Aidha, Kituo kimeendelea kuwajengea uwezo watumishi kwa kuwawezesha watumishi sita (6) kupata mafunzo ya muda mfupi na watumishi wanne (4) wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu.

**116. Mheshimiwa Spika**, sambamba na hilo Kituo kimeendelea na ujenzi wa nyumba moja (2 in 1) ya watumishi ambapo kwa sasa ujenzi umefikia asilimia 89; ujenzi wa bweni moja (1) la wasichana lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 64 limekamilika; na darasa moja (1) lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 50 limekamilika. Aidha, katika kuboresha huduma za afya kwa wanafunzi, Kituo kimeanza ujenzi wa zahanati ambao kwa sasa ujenzi upo kwenye hatua ya msingi. Vilevile, Kituo kimefanikiwa kununua vifaa vya kielektroniki (firewall and routers) ili kuboresha mfumo wa intaneti wa kiserikali (e-Government) pamoja na kuweka mfumo wa maktaba mtandao. Halikadhalika, Kituo kimenunua mahema nane (8) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 10 kila moja kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo. Pia, Kituo kimekamilisha taratibu za ununuzi wa viona mbali 30 na GPS 50 na taratibu za manunuzi kwa ajili ya ujenzi wa bweni moja la wavulana na nyumba mbili (2) za watumishi zinaendelea.



*Jengo la bweni la wasichana katika Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii - Likuyu Sekamaganga.*

### 5.3.2 *Sekta ya Misitu na Nyuki*

**117. Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Misitu na Nyuki ina jukumu la kusimamia uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu

na nyuki. Sekta hii inaongozwa na Sera ya Taifa ya Misitu (1998) na Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki (1998). Utekelezaji wa shughuli za sekta unasimamiwa na Sheria ya Misitu, Sura ya 323; Sheria ya Ufugaji Nyuki, Sura ya 224; Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania, Sura ya 270 (TAFORI); pamoja na kanuni na miongozo mbalimbali. Aidha, jukumu hili hutekelezwa kupitia Idara ya Misitu na Nyuki, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI), Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF), Chuo cha Misitu Olmotonyi (FTI), Chuo cha Viwanda vya Misitu (FITI) Moshi, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki (BTI) Tabora na Kituo cha Mafunzo ya Misitu na Viwanda vya Misitu (FWITC).

#### 5.3.2.1 *Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Ufugaji Nyuki kwa Tanzania Iliyo Bora (Achia Shoka, Tundika Mzinga)*

**118. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kuwa Watanzania wanaendelea kunufaika na rasilimali zilizopo nchini kwa kukuza na kuchochea ajira kwa makundi mbalimbali katika jamii, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Tanzania alielekeza kuwepo na mpango maalum wa ufugaji nyuki utakaochochea ajira hasa kwa vijana. Katika kutekeleza maelekezo hayo, Wizara imeandaa na kuanza kutekeleza Mpango maalum wa Kuendeleza Sekta ya Ufugaji Nyuki kwa Tanzania Iliyo Bora ujulikanao kama "Achia Shoka, Tundika Mzinga". Mpango huo unatarajiwa kuleta mageuzi makubwa kwenye Sekta ya Ufugaji Nyuki kwa kuongeza kiwango cha uzalishaji wa asali kutoka tani 33,861 hadi tani 75,000 kwa mwaka, mauzo ya asali nje ya nchi kutoka asilimia 5 hadi asilimia 30 pamoja na kuongeza ajira mpya 43,055 hasa kwa vijana.

**119. Mheshimiwa Spika**, Mpango huu unatekelezwa kwa kipindi cha miaka kumi (2025 - 2035) na unashirikisha wadau mbalimbali ikiwemo Serikali, Sekta Binafsi, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Wadau wa Maendeleo. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara imewezesha mafunzo ya ufugaji nyuki kibiashara kwa vikundi 236 vyenye jumla ya wafugaji nyuki 4,934 nchi nzima. Aidha, mafunzo ya kutengeneza mizinga ya nyuki ya kisasa yametolewa kwa Mafundi Seremala 50 katika Halmashauri

za Itigi (6), Singida (5), Manyoni (5), Kaliua (4), Sikonge (4), Korogwe (22) na Urambo (4). Vilevile, mizinga ya nyuki ya kisasa 9,215 (sawa na asilimia 83.8 ya lengo) imetolewa kwa wafugaji nyuki. Vilevile, ujenzi wa kiwanda kimoja (1) cha kuongeza thamani mazao ya nyuki katika Wilaya ya Kaliua umeanza ambapo kwa sasa ujenzi umefikia asilimia 40.

**120. Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya utafiti kuhusu changamoto za uzalishaji mdogo wa mazao ya nyuki, kuhama kwa makundi ya nyuki na maeneo yanayofaa kwa ufugaji nyuki. Utafiti huu umefanyika katika maeneo 21 yanayowakilisha kanda saba (7) za uoto wa ikolojia ya kilimo nchini. Matokeo ya awali yanaonyesha kuwa mizinga ya kisasa inafanya vizuri kwa asilimia 73.1. Aidha, Wizara imeboresha kanzidata ya Misitu na Ufugaji Nyuki kwa kuongeza taarifa za wafugaji nyuki wapya 912 na vikundi 65, hatua iliyofanya idadi ya wafugaji nyuki waliosajiliwa kuongezeka kutoka 9,323 hadi 10,235.

#### ***5.3.2.2 Kampeni ya Upandaji miti kwa Tanzania ya Kijani***

**121. Mheshimiwa Spika**, katika kuongeza kasi ya uhifadhi na upandaji miti kwa lengo la kuifanya nchi kuwa ya kijani na kukidhi mahitaji makubwa ya malighafi ya Misitu nchini kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ilipanga kuzalisha na kupanda miche ya miti milioni 35.2. Aidha, hadi kufikia Aprili 2026, Wizara imezalisha miche ya miti milioni 32.8 ya aina mbalimbali ambayo imeendelea kupandwa katika mashamba 26 ya Serikali na kugawanywa kwa wadau mbalimbali kwa ajili ya kupanda katika maeneo yao. Hatua hii imechochea na kuhamasisha wananchi kushiriki katika zoezi la upandaji miti na uhifadhi nchini.

**122. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Wizara imeshiriki katika Kampeni maalum ya kupanda miti ijulikanayo kama 27 YA KIJANI. Kampeni hii imeasisiwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa ni jitihada zake binafsi katika kutunza mazingira na kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi. Mheshimiwa Rais aliongoza Watanzania kushiriki kupanda miti ambapo takribani miche ya miti 2,529,810 ilipandwa kote nchini kwa siku hiyo.

Tangu kuanzishwa kwa kampeni hiyo mwaka 2023, jumla ya miche ya miti 113,199,359 ilikuzwa na kupandwa katika maeneo mbalimbali hapa nchini.



*Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akipanda mche wa mti katika siku ya kumbukizi ya kuzaliwa kwake tarehe 27 Januari, 2026.*

**123. Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Wizara imeratibu Maadhimisho ya Siku ya Misitu Duniani na Kampeni ya Upandaji Miti yaliyofanyika Kitaifa Mkoani Lindi. Maadhimisho haya yaliongozwa na Kaulimbiu isemayo Misitu ni Uchumi Endelevu, Tuihifadhi kwa Maendeleo ya Taifa" na yalifunguliwa rasmi na Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tukio hilo lilihudhuriwa na wananchi wapatao 10,000 kutoka mikoa mbalimbali ambapo miche ya miti 11,458,029 ilipandwa katika kipindi cha maadhimisho. Hivyo, naomba kutumia nafasi hii kutoa rai kwa Watanzania wote kutambua na kuunga mkono jitihada za viongozi wetu kwa kupanda na kutunza miti katika maeneo yetu.




*Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akimwagilia mti alioupanda katika Siku ya Uzinduzi wa Kampeni ya Upandaji Miti Kitaifa katika eneo la Hospitali ya Mkoa wa Lindi, tarehe 19 Machi, 2026.*

#### 5.3.2.3 *Idara ya Misitu na Nyuki*

**124.** **Mheshimiwa Spika**, katika kuendelea kuimarisha usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu na nyuki nchini, Wizara imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Elimu Ugani wa Misitu (2025 – 2031); Mkakati wa Ufugaji Nyuki Endelevu kwa Uhifadhi wa Misitu na Kuimarisha Maisha ya Wananchi katika Ukanda wa Misitu ya Ikolojia ya Miombo (2025-2035); Mkakati wa Uzalishaji wa Mbegu Bora za Miti na Urejeshaji wa Miti katika Ukanda wa Miombo (2025-2035); na Mpango kazi wa Utekelezaji wa Mkakati wa Mazao Yasiyo Timbao (2026-2035). Aidha, Wizara imefanya mapitio ya Kanuni za Jumla za Ufugaji Nyuki, Mwongozo wa Uvunaji Endelevu wa Biashara ya Mazao ya Misitu yanayovunwa katika Misitu ya Asili; Mwongozo wa Tathmini Shirikishi ya Rasilimali za Misitu na Mwongozo wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii.

**125.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuharakisha maendeleo ya viwanda, kuchochea ajira na mchango wa Sekta ya Misitu katika uchumi wa Taifa, Wizara iliandaa Mpango wa Kitaifa wa Kuendeleza Mazao ya Mbao yaliyohandisiwa (2021-2031). Mpango huo, umeweka malengo mbalimbali ikiwemo kuongeza viwanda vya mazao ya mbao yaliyohandisiwa kutoka 22 hadi 252 ifikapo 2031. Katika kuhakikisha lengo hili linafikiwa, Wizara imefanya tathmini na kubaini uwepo wa viwanda 82 vya kuongeza thamani ya mazao ya mbao ikiwa ni asilimia 32.5 ya lengo lililowekwa. Viwanda hivi vinazalisha bidhaa za mbao ikiwemo Medium Density Fiber board (MDF), plywood na marine-

board. Vilevile, matokeo yanaonesha kuwa takribani vijana 5,000 wameajiriwa katika viwanda hivyo. Hatua hii imechangia katika kuchochea ukuaji wa uchumi wa nchi kupitia ajira hasa kwa vijana na wanawake; na mapato na kodi zinazokusanywa na Serikali.

**126. Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza Sekta ya Ufugaji Nyuki, Wizara imewezesha vijiji kutenga na kutangaza hifadhi tano (5) za nyuki zenye jumla ya hekta 1,751.69 katika mikoa ya Kigoma na Katavi. Hifadhi hizo ni Hifadhi ya Nyuki ya Kijiji cha Bizilankweto A (hekta 488.34), Bizilankweto B (hekta 350.48), Mlima Nzagwa (hekta 41.92), Mikobe Chini (hekta 204.09) zilizopo Mkoani Kigoma na Hifadhi ya Nyuki ya Nkulati yenye hekta 666.86 iliyopo katika Mkoa wa Katavi.

**127. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha ushirikishwaji wa wadau katika kusimamia na kuendeleza rasilimali za misitu na nyuki kwa kufanya vikao vitano (5) vilivyohusisha wadau wa Sekta za Misitu na Ufugaji Nyuki kwa ajili ya kujadili fursa, changamoto na kuweka mikakati ya pamoja ya kutatua changamoto zinazoikabili sekta. Vilevile, Wizara imeratibu kikao kimoja (1) cha Kamati Endeshi ya Mazao ya Misitu yaliyohandisiwa (EWP), kikao kimoja (1) cha Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Misitu (NAFAC) na Vikao (2) vya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya Kilimomisitu (NAAC). Kupitia vikao hivyo, masuala mbalimbali yanayohusu Sekta ya Misitu na Nyuki yalijadiliwa na kupatiwa ufumbuzi.

**128. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa, Wizara imeshiriki katika mikutano ya Kikanda ambapo ilishiriki kwenye mafunzo ya usimamizi shirikishi wa misitu ya asili na namna ya kukabiliana na moto katika maeneo ya misitu ambayo yaliandaliwa na Jumuiya ya nchi za Kusini mwa Afrika - SADC. Wizara imeshiriki katika Mkutano wa 25 wa Kamisheni ya Afrika ya Misitu na Wanyamapori na Wiki ya Tisa (9) ya maonesho ya Misitu na Wanyamapori Afrika (AFWW9) uliofanyika nchini Gambia. Mkutano huo ulijadili na kuweka mikakati ya pamoja ya usimamizi na uendelezaji wa misitu, kuimarisha mifumo ya chakula na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kuendeleza uhifadhi na usimamizi endelevu wa misitu. Pia,

Wizara imeshiriki Kongamano la Zámba Heritage lililoandaliwa na Shirika la Kimataifa lisilo la Kiserikali la Uthibitishaji wa Misitu (Forest Stewardship Council – FSC) lililofanyika Nairobi-Kenya ambalo liliweka mikakati ya pamoja ya kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za misitu.

**129.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeshiriki Kongomano kuhusu mjadala wa matumizi ya nishati safi ya kupikia lililofanyika Jijini Arusha. Kongamano hilo ni mojawapo ya harakati za kukuza matumizi ya nishati safi nchini pamoja na kuunga mkono jitihada za Mheshimiwa Rais katika kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia. Kupitia kongamano hilo, mikakati mbalimbali imewekwa itakayowezesha Serikali kushirikiana na Sekta binafsi katika kuwezesha wananchi kupata nishati safi ya kupikia kwa uhakika. Vilevile, Wizara imeshiriki Mkutano wa 11 wa Baraza la Mawaziri wa Sekta za Maliasili na Usimamizi wa Mazingira wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika Jijini Arusha, ambapo masuala mbalimbali yanayohusu ushirikiano kwenye maliasili na mazingira yalijadiliwa na kuwekewa mikakati ya pamoja.

### 5.3.2.4 *Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania - TFS*

**130.** **Mheshimiwa Spika**, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) ulianzishwa kwa lengo la kusimamia, kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za misitu na nyuki zilizo chini ya Serikali Kuu. Wakala unatekeleza majukumu mbalimbali yakiwemo kusimamia hifadhi za misitu ya asili, hifadhi za mikoko, hifadhi za nyuki za Serikali Kuu, mashamba ya miti, mashamba ya nyuki na manzuki; na kusimamia rasilimali za misitu na nyuki katika ardhi ya jumla.

**131.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za misitu na nyuki, Wakala umeandaa mipango ya usimamizi wa misitu 15 yenye ukubwa wa hekta 1,436,896; kufanya doria za kimkakati 363 na doria za kawaida 12,854 katika maeneo ya hifadhi za misitu na nyuki. Kupitia doria hizo, jumla ya watuhumiwa 1,925 walikamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria. Vilevile, doria hizo zimewezesha kukamatwa na kutaifishwa kwa mazao ya misitu yaliyovunwa bila kufuata utaratibu yakiwemo magunia ya mkaa 39,900; mbao 31,046 zenye mita za ujazo 1,321; kuni zenye mita za ujazo 205.6 na

magogo 1,556 yenye mita za ujazo 351. Sambamba na hilo, mifugo 29,538; pikipiki 1,707; na magari 328 yalikamatwa na hatua mbalimbali za kisheria zinaendelea kuchukuliwa.

**132. Mheshimiwa Spika**, Wakala umeendelea kuimarisha mipaka ya misitu 119 kwa kuhakiki mipaka yenye urefu wa kilomita 620; kusafisha mipaka yenye urefu wa kilomita 1,140; kuweka vigingi 676 na mabango 165; pamoja na kuchimba mitaro 115 inayoonesha uelekeo wa mipaka ya hifadhi za misitu na nyuki. Katika hatua nyingine, Wakala umesafisha njia za kuzuia moto zenye urefu wa kilomita 2,723; kusimamia minara 17 ya kuangalizia matukio ya moto na vituo saba (7) vya kufuatilia na kudhibiti matukio ya moto katika maeneo ya hifadhi. Aidha, Wakala umetoa mafunzo ya mbinu za kukabiliana na kudhibiti moto kwa vikosi 45 vyenye jumla ya watu 705. Vilevile, mafunzo yametolewa kwa wananchi 20,297 kutoka vijiji 245 vinavyopakana na hifadhi za misitu na mashamba ya miti yaliyopo katika maeneo mbalimbali nchini. Pia, Wakala umeimarisha matumizi ya mitambo ya kuzimia moto na mfumo wa satelite wa kubaini matukio ya moto mapema ili kuukabili kabla ya kuenea na kusababisha madhara. Kupitia juhudi hizo, matukio ya moto yamepungua kwa wastani wa asilimia 11 kwa mwaka na ukubwa wa maeneo yanayoathirika kwa moto kila mwaka yameendelea kupungua.

**133. Mheshimiwa Spika**, Wakala pia umewezesha zoezi la kuandaa na kutoa hati za Hakimiliki za Kimila 1,459 kwa wananchi wanaopakana na Msitu wa Hifadhi Nyahua Mbuga katika vijiji vya Mtakuja (223), Makibo (339), Zugimlole (241), Ukumbisiganga (323) na Tumaini (333) vilivyopo katika Wilaya ya Sikonge, Mlele, Kaliua na Urambo. Lengo la kusaidia zoezi hilo ni jitihada za Wakala kuepusha migogoro ya ardhi baina ya hifadhi na vijiji jirani. Vilevile, Wakala umewezesha kurasimisha misitu 17 ya vijiji yenye ukubwa wa hekta 4,077.27 na kuandaa mipango ya usimamizi na Sheria ndogo ya misitu hiyo katika vijiji vya Kimange (5), Kwaruhombo (3), Kwamduma (8) na Kwamsanja (1) vilivyopo Wilaya ya Chalinze, Mkoa wa Pwani. Hatua hii itawezesha kuimarisha ulinzi, usimamizi endelevu wa misitu, kupunguza uvamizi pamoja na kuongeza thamani ya ardhi kwa vijiji vinavyopakana na misitu hii.




*Wananchi wakipokea Hati za Hakimiliki za Kimila katika Wilaya za Sikonge, Mlele, Kaliua na Urambo ikiwa ni jitihada za Wakala kuepusha migogoro ya ardhi baina ya hifadhi za misitu na vijiji.*

**134. Mheshimiwa Spika,** katika kuongeza kasi ya uhifadhi na upandaji miti ili kuifanya Tanzania kuwa ya kijani na kukidhi mahitaji makubwa ya malighafi ya mazao ya misitu nchini, Wakala umeanzisha mashamba mawili (2) ya miti ya Geita na Rwamgasa yenye ukubwa wa hekta 28,000 katika Wilaya ya Geita. Mashamba haya yameanzishwa kama juhudi za kurejesha uoto wa asili katika maeneo ya misitu yaliyoharibiwa. Aidha, vyanzo vipya sita (6) vya mbegu za miti vyenye ukubwa wa hekta 66 vimeanzishwa. Pia, kituo kipya cha mbegu za miti katika Wilaya ya Kaliua kimejengwa pamoja na kukarabati Kituo cha Mbegu za Miti Shinyanga. Vilevile, Wakala umezalisha miche ya miti milioni 32.8 ya spishi mbalimbali ambayo imeendelea kupandwa katika mashamba 26 ya Serikali na kugawanywa kwa wadau mbalimbali kwa ajili ya kupanda katika maeneo yao. Hatua hii imechochea na kuhamasisha wananchi kushiriki katika zoezi la upandaji miti na uhifadhi nchini.



*Kitalu cha miche ya miti aina ya msindano (Pines) katika Shamba la Miti Sao Hill, Iringa.*

**135.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza mashamba ya miti, Wakala umepanda miti katika eneo lenye ukubwa wa hekta 9,558; kurudishia miti iliyokufa kwenye eneo la hekta 1,925; kupalilia eneo lenye hekta 25,633.33; kupogolea hekta 9,239; na kupunguzia miti kwenye hekta 8,512 katika mashamba yanayosimamiwa na Wakala. Aidha, Wakala umepanda miche ya mikoko 45,000 kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 42.2 katika mwambao wa Bahari ya Hindi katika wilaya za Temeke, Tanga na Lindi. Vilevile, Wakala kwa kushirikiana na wadau wakiwemo Earthlungs, WWF na WIOMN umepanda jumla ya miche ya mikoko 37,253,952 katika Mikoa ya Tanga na Pwani.

**136.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza utalii ikolojia na malikale, Wakala umeimarisha miundombinu ya utalii katika misitu ya hifadhi kwa kujenga malango sita (Meru, Vikindu, Mwambesi, Pindiro, Mlima Rungwe na Ziwa Duluti); board walk mbili (Sahare – Tanga na Msitu wa Mazingira Asilia Amani); mabanda sita (6) ya kupumzikia watalii katika Misitu ya Mazingira Asilia Rau (5) na Matogoro (1); jiko moja (1) na vyoo viwili katika Misitu ya Mazingira Asilia Nilo na Chome. Aidha, Wakala umekarabati kilomita 287.14 za njia za watembea kwa miguu katika hifadhi za misitu 24; kilomita 41.32 za barabara za msituni katika hifadhi za Kilombero, Kalambo na Mlima Rungwe; kilomita 8.6 za barabara za kufika katika hifadhi za Pindiro na

Matogoro; na kilomita 48 za barabara za mashindano ya magari katika hifadhi za Pugu Kazimzumbwi, Vikindu, Amani, Nilo na Rau. Vilevile, Wakala umekarabati kambi nane (8) za watalii katika hifadhi za misitu za Magamba (2), Kilombero (2), Amani (3) na Rau (1). Sambamba na hilo, Wakala umekarabati mnara mmoja (1) wa kutazama vivutio katika Hifadhi ya Msitu Magamba.



*Mradi wa Ujenzi wa Daraja la Watembea kwa Miguu (Board Walk) katika Hifadhi ya Misitu ya Mikoko Sahare, Tanga.*

***137.*** **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utangazaji wa vivutio vya utalii ikolojia na malikale, Wakala umezalisha na kurusha vipindi 19 vya redio na 38 vya televisheni pamoja na kusambaza machapisho 8,859. Aidha, Wakala uliandaa na kushiriki matamasha 15 ya ndani kwa ajili ya kutangaza utalii ambayo ni: - *Mt. Hanang Nyama Choma Festival, Tukacharu Rau Forest, The Epic Nyama Choma, Meru Adventure Race, Rubare Trail Run, Mkwawa Rally, Rombo Marathon, Ndafu Festival, Magamba Walkthon, Kalambo Waterfalls Utalii Festival, Twendezetu Lake Ngosi, Itulu Hill Staff Tour, West Kill Tour Challenge, Tukutane Mt. Rungwe Season II na Uni Pugu Easter Experience.*



*Mashindano ya Magari katika Shamba la Miti Morogoro, Eneo la Makunganya na Shamba la Miti Sao Hill, Iringa.*

**138. Mheshimiwa Spika**, juhudi hizi zimewezesha kuongezeka kwa idadi ya watalii wanaotembelea vituo vya utalii ikolojia kufikia watalii 329,753 hadi mwezi Aprili, 2026 sawa na ongezeko la asilimia 20 ikilinganishwa na watalii 275,723 katika kipindi kama hicho Mwaka wa Fedha 2024/2025. Aidha, kutokana na shughuli za utalii, Wakala umekusanya kiasi cha Shilingi 3,093,145,720 ikiwa ni ongezeko la asilimia 43 ikilinganishwa na Shilingi 2,169,711,149 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**139. Mheshimiwa Spika,** Wakala umeimarisha shughuli za ufugaji nyuki kwa kusimamia manzuki 222 na mashamba matatu (3) ya Nyuki ya Kipembawe (Chunya), Mwambao (Wilaya za Handeni na Kilindi) na Kati (Wilaya za Manyoni na Chemba) ambapo tani 18.5 za asali na tani 0.8 za nta zimezalishwa. Aidha, Wakala umetoa mafunzo ya ufugaji nyuki kibiashara, uchakataji na ufungashaji bora wa mazao ya nyuki kwa vikundi 98 vya ufugaji nyuki vyenye jumla ya wafugaji nyuki 882 katika Wilaya 13. Vilevile, Wakala umejenga kiwanda kimoja (1) cha kuchakata mazao ya nyuki katika Wilaya ya Kaliua pamoja na kuzalisha mizinga 500 ya nyuki.

**140. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Wakala umekusanya sampuli 132 za asali kutoka Wilaya 31 na kupelekwa kwenye maabara ya kimataifa nchini Ujerumani kwa lengo la

kupima ubora wa asali inayozalishwa nchini ikiwa ni kukidhi hitaji la usalama wa watumiaji wa ndani na nje pamoja na kukidhi mahitaji maalum ya masoko ya nje hususan Ulaya na Marekani. Matokeo ya ubora wa sampuli yanaonyesha kuwa asali ya Tanzania ni bora na inakidhi vigezo vya kuuzwa katika masoko ya ndani, Kikanda na Kimataifa. Hatua hii imefanikisha wafanyabiashara wa kitanzania kupata kibali cha kuuza asali katika nchi hizo ambapo jumla ya tani 1,076.8 za asali zenye thamani ya Shilingi 12,921,756,000 zimeuzwa katika masoko ya nchi hizo.

**141.** **Mheshimiwa Spika** katika kuhamasisha jamii kushiriki katika uhifadhi wa rasilimali za misitu na nyuki, Wakala umetoa elimu ya uhifadhi kwa wananchi 1,502 katika vijiji 74 vinavyopakana na hifadhi za misitu nchini. Aidha, Wakala umeshiriki katika miradi ya maendeleo kwa wananchi wanaopakana na hifadhi za misitu ambapo miradi mbalimbali imewezeshwa ikiwemo ujenzi wa nyumba ya watumishi katika Shule ya Msingi Bondo wilayani Kilindi; kutoa vifaa vya ujenzi wa madarasa kwa shule 24 za msingi na sekondari; na vifaa vya ujenzi wa zahanati moja wilayani Manyoni. Pia, jumla ya madawati 201 yametolewa katika shule za msingi Wilaya ya Urambo na Kilolo. Vilevile, mizinga ya nyuki 670 imetolewa kwa vikundi vya ufugaji nyuki 15 na wanakijiji 16 katika Wilaya za Singida, Sumbawanga, Kaliua, Mlele, Urambo na Sikonge. Sambamba na hilo, wananchi wamepatiwa jumla miche milioni 11.5 kwa ajili ya kupanda katika maeneo yao kama sehemu ya kuendeleza miradi ya upandaji miti. Miradi hii yenye thamani ya bilioni 3.9 imechangia wananchi kushiriki katika shughuli za kiuhifadhi na hivyo kuongeza ulinzi wa rasilimali za misitu na nyuki nchini.

**142.** **Mheshimiwa Spika**, ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi, Wakala umeimarisha na kuendeleza mikakati ya kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi kwa kujenga majengo 15 ikiwemo ofisi nane (8) na vituo saba (7) vya ulinzi; na kukarabati majengo 45 zikiwemo ofisi nne (4), nyumba 40 za watumishi na stoo moja (1). Aidha, Wakala umenunua vitendea kazi ikiwemo magari 33, pikipiki 36 na ndege nyuki 5. Vilevile, Wakala umewezesha mafunzo ya utayari kwa watumishi wapya 369.

Mafunzo haya yatawezesha watumishi kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi.



*Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb.), akizindua vitendea kazi mbalimbali kwa shughuli za uhifadhi wa misitu.*

### 5.3.2.5 *Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania - TAFORI*

**143. Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) ina jukumu la kufanya na kuratibu tafiti za misitu na ufugaji nyuki na kutoa ushauri wa kitaalam katika nyanja za misitu na ufugaji nyuki. Katika kutekeleza majukumu yake, TAFORI imefanya jumla ya tafiti 20 zikiwemo tafiti 7 za kimkakati. Tafiti za kimkakati zilizofanyika ni pamoja na utafiti kuhusu mbinu za kuzuia na kudhibiti mimea vamizi; utafiti wa nyuki wasiodunga na aina ya mizinga inayofaa kwa kufugia katika maeneo mbalimbali nchini; utafiti kuhusu gharama na faida ya uzalishaji wa utomvu unaofanywa na wakulima wadogo wa miti; na utafiti wa kuchunguza athari za mizunguko miwili ya uvunaji wa jamii za miti aina ya misindano (Pinus patula) kwenye uzalishaji na ubora wa

mbao katika mashamba ya misindano yaliyopo katika Shamba la Miti la Sao Hill.

**144.** **Mheshimiwa Spika**, TAFORI imeendelea kufanya utafiti wa kudhibiti mimea vamizi kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Center for Agriculture and Bioscience International (CABI) kupitia mradi uitwao Native Plants for Environment and People (NATIVE PEP). Kupitia mradi huo, majaribio 10 ya kurudisha uoto wa asili kwa kutumia majani ya asili yameanzishwa katika vijiji vitano (5) ambavyo ni Tingatinga (Longido) pamoja na Mawasiliano, Ndinika, Magadini na Leikirumuni (Siha). Matokeo ya awali yanaonesha kuwa urejeshaji wa uoto wa asili unapunguza kasi ya kuenea kwa mimea vamizi na hivyo kuimarisha uhifadhi wa mifumo ikolojia. Sambamba na hilo, Taasisi imetoa elimu ya mbinu za kuzuia mimea vamizi kwa wananchi 125 katika vijiji vitano (5), walimu na wanafunzi wa shule mbili (2) za msingi za Mawasiliano (Siha) na Tingatinga (Longido) pamoja na shule mbili (2) za sekondari ambazo ni Tingatinga (Longido) na Shule ya Wasichana Kilimanjaro (Siha).

**145.** **Mheshimiwa Spika,** TAFORI imeendelea na utafiti wa nyuki wasiodunga na aina ya mizinga inayofaa kwa ufugaji wa nyuki katika Wilaya tisa (9) za Rufiji, Mkinga, Siha, Kondoa, Manyoni, Mpanda, Biharamulo, Mbeya na Magharibi A (Unguja) zinazowakilisha kanda nne (4) za tabianchi. Matokeo ya utafiti huo yameonesha jamii tano (5) za nyuki wasiodunga ambazo ni Axestotrigona togoensis, Axestotrigona ferruginea, Hypotrigona araujoi, Hyptorigona sp na Liotrigona sp ndizo zinazofaa kufugwa kwa ajili ya uzalishaji na wafugaji wanaweza kuwapata katika ukanda husika. Utafiti pia umebaini kuwa unene wa kiota cha asili cha nyuki hawa ni kati ya sentimita 2.5 hadi sentimita 6 huku ujazo wa viota hivyo asili ukiwa kati ya lita 4.5 hadi lita 12, hali inayochangia ustawi wa kundi na kuongeza ufanisi wa uzalishaji wa asali. Aidha, aina mbili za mizinga imetengenezwa kwa ajili ya kuendeleza utafiti wa ukuaji wa makundi katika vibanda vya majaribio ya kufuga nyuki wasiodunga.

**146.** **Mheshimiwa Spika,** TAFORI imefanya utafiti kuhusu gharama na faida ya uzalishaji wa utomvu unaofanywa na

wakulima wadogo wa miti. Tafiti hizi zimefanyika katika Mikoa ya Kagera, Mwanza na Iringa kwa lengo la kubaini ufanisi wa kiuchumi na kuboresha tija katika shughuli hiyo. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa ugemaji wa utomvu ni fursa kubwa ya kiuchumi na kimazingira kwa wakulima wadogo wa miti nchini Tanzania. Aidha, matokeo ya utafiti yanaonesha mkulima wa miti anaweza kupata kiasi cha Shilingi 1,500,000 hadi Shilingi 1,900,000 kwa mwaka kutokana na ugemaji wa utomvu. Kwa upande wa mashamba ya Serikali yanayosimamiwa na TFS, utafiti umebaini kuwa mapato yanayopatikana kutokana na uvunaji wa utomvu ni Shilingi millioni 40 hadi 80 kwa hekta moja, jambo linaloonesha uwepo wa fursa kubwa ya kiuchumi katika shughuli hiyo. Hata hivyo, ushiriki wa wakulima wadogo wa miti bado ni mdogo hali inayochangiwa na wakulima kuvuna miti katika umri mdogo kwa ajili ya mbao. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, juhudi za kutoa elimu juu ya fursa za kiuchumi zinazotokana na zao la utomvu zinaendelea.

**147. Mheshimiwa Spika,** TAFORI imefanya utafiti wa kuchunguza athari za mizunguko miwili (2) ya ukuaji (rotation age) wa miti aina ya misindano (Pinus patula) kwenye uzalishaji na ubora wa mbao katika mashamba ya misindano yaliyopo katika Shamba la Miti la Sao Hill. Matokeo yanaonesha kutokuwepo na mabadiliko makubwa ya virutubisho kwenye udongo katika mzunguko wa kwanza na wa pili wa ukuaji wa miti. Aidha, baadhi ya virutubisho vimeonesha kuongezeka na vingine kupungua. Hata hivyo, kuongezeka na kupungua kwa virutubisho hivyo hakujaathiri ukuaji wa miti na ubora wa mbao.

**148. Mheshimiwa Spika,** TAFORI imeendelea kufanya utafiti kuhusu changamoto za uzalishaji mdogo wa mazao ya nyuki, kuhama kwa makundi ya nyuki na maeneo yanayofaa kwa ufugaji nyuki. Utafiti huu umefanyika katika maeneo 21 yanayowakilisha kanda saba (7) za uoto wa ikolojia ya kilimo nchini. Matokeo ya awali yanaonesha kuwa mizinga ya kisasa inafanya vizuri kwa asilimia 73.1. Aidha, utafiti umebaini kuwa uzalishaji wa asali kwa mzinga unatofautiana kutoka eneo moja la uoto hadi jingine. Mathalan, mzinga wa kisasa unaobeba michi 17 umeweza kuzalisha kilo 21.6 katika Wilaya ya Chamwino na kilo 6 Wilaya ya Lindi. Matokeo haya yanaonyesha kuwa

uzalishaji kwa mzinga unategemea kwa kiasi kikubwa aina ya mzinga na kiwango cha mbochi ya mimea ya mahali husika.

**149. Mheshimiwa Spika,** TAFORI imeendelea kushirikiana na Taasisi ya Tiba Asilia ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kwa kufanya utafiti wa matumizi na hali ya uhifadhi wa mimea dawa iliyopo mashambani katika Milima ya Tao la Mashariki, kwa upande wa Tanzania. Utafiti huo umefanyika katika Halmashauri za Wilaya ya Lushoto na Muheza Mkoani Tanga. Utafiti umebaini mimea dawa 102 kwenye maeneo ya mashamba ya watu binafsi ambayo yanahitaji kuhifadhiwa kwa ajili ya vizazi vijavyo. Vilevile, utafiti umebaini kuwa asilimia 48 ya wananchi wanatumia mimea dawa kutatua changamoto za kiafya hasa upumuaji na mmeng'enyo wa chakula. Matokeo haya yanaonesha umuhimu wa kuhifadhi mimea dawa na kuimarisha matumizi endelevu kwa ajili ya afya ya jamii na uhifadhi wa rasilimali za asili.

**150. Mheshimiwa Spika,** TAFORI kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Copenhagen cha Denmark na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kupitia ufadhili wa Shirika la Maendeleo la DANIDA, imeendelea kutekeleza mradi wa utafiti unaoangalia athari za mabadiliko ya hali ya hewa kwa huduma ya uchavushaji wa mazao ya kilimo na shughuli za uchumi wa jamii katika milima ya Uluguru na Udzungwa. Utafiti huo umeweza kuwatambua na kuwashirikisha wananchi 150 katika maeneo yenye viwango tofauti vya mwinuko katika Milima ya Uluguru na Udzungwa. Aidha, kupitia utafiti huo mizinga ya nyuki 380 imetengenezwa na kutundikwa katika maeneo ya mashamba ya wananchi Wilaya ya Morogoro na Kilombero. Utafiti huu ni muhimu kwa ajili ya utunzaji wa baionuai kwa lengo la kutoa huduma za kiikolojia kwenye sekta nyingine za kiuchumi.

**151. Mheshimiwa Spika**, TAFORI imeendelea kuimarisha mazingira ya kazi kwa kutoa stahiki kwa watumishi wake ambapo watumishi 27 walipandishwa vyeo, watumishi 21 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 130 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi. Aidha, katika kuongeza nguvu kazi katika utafiti, watumishi 25 wameajiriwa katika kada ya utafiti na saba (7) kada saidizi. Vilevile, TAFORI imeendelea kuboresha mazingira ya

utendaji kazi kwa kununua samani za ofisi pamoja na vifaa vya kufanyia utafiti kwa ajili ya Kituo cha Utafiti kilichopo Kibaha Mkoa wa Pwani.

#### 5.3.2.6 *Mfuko wa Misitu Tanzania - TaFF*

**152. Mheshimiwa Spika**, Mfuko una jukumu la kuwezesha na kugharamia shughuli na miradi ya kuboresha uhifadhi, usimamizi na uendelezaji rasilimali za misitu na nyuki. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mfuko umetekeleza jukumu la uwezeshaji kwa kutoa ruzuku yenye jumla ya Shilingi 3,486,644,003.00 kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa miradi 160 inayoendelea (sawa na asilimia 85 ya lengo) na miradi mipya 72 (sawa na asilimia 60 ya lengo). Miradi hiyo inahusiana na uanzishwaji wa vitalu vya miche ya miti, upandaji miti, uboreshaji uhifadhi wa misitu kupitia ufugaji nyuki pamoja na utengenezaji na uhamasishaji wa matumizi ya nishati mbadala. Miradi hiyo inatekelezwa katika wilaya 189 kwenye mikoa 26 nchini.

**153. Mheshimiwa Spika**, Mfuko umeendelea kujenga uwezo wa vyuo vya mafunzo ya misitu, viwanda vya misitu na ufugaji nyuki ili kuboresha mazingira ya utoaji elimu kwa kuendelea kuwezesha ujenzi wa bweni la wasichana lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 200 katika Chuo cha Viwanda vya Misitu (FITI) na kuwezesha kuanza kwa ujenzi wa bweni la wanafunzi lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 208 katika Kituo cha Mafunzo ya Misitu na Viwanda vya Misitu (FWITC) kilichopo Mafinga, Iringa. Vilevile, Mfuko umewezesha fedha kwa ajili ya mafunzo ya ufugaji bora wa nyuki kwa vikundi vya wafugaji nyuki 109 vyenye jumla ya wanachama 1,309 ambavyo vimewezeshwa mizinga ya nyuki ya kisasa 3,640 ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya nyuki ikiwemo asali na kupunguza utegemezi na uharibifu wa misitu.



*Mizinga ya nyuki ya kisasa iliyowezeshwa na Mfuko wa Msitu Tanzania katika Eneo la Msufini, Kongowe, Kibaha.*

**154. Mheshimiwa Spika**, Mfuko umeendelea kuwezesha ujenzi wa jengo la Ofisi ya Kituo cha Utafiti wa Misitu Mkoani Tabora na kuwezesha ukarabati wa jengo la Makao Makuu ya TAFORI. Aidha, Mfuko umewezesha uanzishwaji wa shamba la mfano la majaribio ya utafiti wa misitu lenye jumla ya hekta 112, ununuzi wa gari moja (1) na vitendea kazi vingine ili kuboresha shughuli za utafiti wa misitu na nyuki. Vilevile, Mfuko umeiwezesha TAFORI kukamilisha utekelezaji wa tafiti tano (5) za kimkakati zenye lengo la kutatua changamoto zinazoathiri uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za misitu na nyuki. Sambamba na hilo, Mfuko umeendelea kugharamia masomo ya Shahada ya Uzamili na Uzamivu kwa wanafunzi watatu (3) kwa fani za misitu zenye watalaam wachache hapa nchini ambazo miongoni mwake ni uboreshaji wa vizazi vya miti (tree breeding) na utambuzi wa magonjwa ya miti na misitu (forest pathology). Fani hizo zinahitajika nchini kwa ajili ya kuboresha na kuongeza uzalishaji wa mazao ya misitu hususan mazao ya misitu kutoka mashamba ya miti ya kupandwa.

**155. Mheshimiwa Spika**, Mfuko umeendelea kuhamasisha vijana kujiunga na masomo ya fani za misitu na ufugaji nyuki kwa kutoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi 25 waliofanya vizuri zaidi katika masomo yao kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada ya Misitu, Viwanda vya Misitu na Ufugaji Nyuki. Aidha, Mfuko umetoa tuzo kwa wanafunzi nane (8) waliofanya vizuri katika masomo ya Shahada ya kwanza ya Misitu kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA). Vilevile, Mfuko umeendelea kuwezesha vikao vya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri

ya Misitu (NAFAC) na Kamati ya Kusimamia Utekelezaji wa Mpango Kazi wa Mazao ya Misitu yaliyohandisiwa (EWP Action Plan); na ushiriki wa Tanzania katika mikutano miwili (2) ya Kikanda na mikutano miwili (2) ya Kimataifa. Mfuko umeendelea kuimarisha mazingira ya utendaji kazi kwa kuanza ujenzi wa jengo la Ofisi za Mfuko katika eneo la Nzuguni 'C' Jijini Dodoma. Hatua iliyofikiwa ya ujenzi ni kukamilika kwa usanifu wa jengo, tathmini ya athari za mazingira na kijamii (ESEA), tathmini ya hali ya udongo na jiolojia na kuandaliwa kwa gharama za ujenzi (BOQ).

#### *5.3.2.7 Chuo Cha Misitu, Olmotonyi – FTI*

**156. Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Misitu, Olmotonyi kilianzishwa kwa lengo la kutoa mafunzo ya ufundi sanifu ya uhifadhi wa misitu, mafunzo ya muda mfupi na ushauri wa kitaalam wa uhifadhi misitu na mazingira. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Chuo kimedahili na kutoa mafunzo ya Astashahada na Stashahada ya Uhifadhi wa Misitu, Misitu ya Mjini na Jioinfomatiki kwa wanafunzi 931 sawa na asilimia100.1 ya lengo la kudahili wanafunzi 930 ambapo wanafunzi 397 ni wa kike na wanafunzi 534 ni wa kiume. Aidha, Chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi ya upimaji misitu kidijitali, udhibiti wa moto, matumizi ya nishati safi na uanzishaji na usimamizi wa kitalu cha miti kwa washiriki 18 kutoka TFS, TAWA, Halmashauri za Wilaya ya Arusha na Kyela pamoja na Mashirika ya Reforest Africa na Biore Foundation. Vilevile, Chuo kimetoa elimu ya ugani ya uhifadhi misitu, utunzaji wa miti na kilimo ikolojia kwa wananchi 400 katika vijiji vya Olmotonyi, Ekenywa na Olkokola vinavyopakana na shamba la miti la Chuo.

**157. Mheshimiwa Spika,** katika kuongeza kasi ya uhifadhi wa misitu na upandaji miti, Chuo kimezalisha miche ya miti 100,000 ya jamii mbalimbali ambapo miche 20,188 imeshapandwa katika shamba la miti la Chuo na viunga vya

Chuo kupitia kampeni za **27 YA KIJANI** na **Wiki ya Upandaji Miti**. Aidha, Chuo kimeanza majaribio ya kuotesha miche ya miti ya mbegu bora aina ya misindano iliyoboreshwa (Pinus tecunumanii) (miche 300) na mikaratusi iliyoboreshwa (Eucalyptus urograndis) (miche 7,000) katika shamba la miti la Chuo kwa lengo la kuona ufanisi wake kwenye ukuaji, uimara, umbo na ustahimilivu wa magonjwa katika Ukanda wa Kaskazini mwa nchi. Matokeo ya majaribio haya yatasaidia kuongeza upatikanaji wa mbegu bora za miti za jamii hiyo katika ukanda wa kaskazini na upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda vya mbao.

**158. Mheshimiwa Spika,** katika kuhamasisha jamii inayozunguka Chuo kushiriki kikamilifu katika uhifadhi wa misitu, Chuo kinashirikiana na vijiji vinavyopakana na shamba la miti la Chuo katika kusimamia msitu wa Chuo kupitia mfumo wa Taungya. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, jumla ya wananchi 400 wamenufaika kwa kuruhusiwa kupanda mazao ya mahindi na maharage katika shamba hilo.

**159. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utendaji kazi, Chuo kimewawezesha watumishi watatu (3) kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu ya misitu na watumishi 25 kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi katika nyanja mbalimbali. Aidha, Chuo kimeshiriki katika matukio na maonesho saba (7) ya ndani na nje ya nchi yakiwemo Sabasaba, Nanenane, Siku ya Misitu, Siku ya Wanyamapori na Maonesho ya Teknolojia za Misitu (Woodex in Africa) nchini Afrika ya Kusini, kwa lengo la kujifunza na kujitangaza.

#### 5.3.2.8 *Chuo cha Viwanda vya Misitu Moshi - FITI*

**160. Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Viwanda vya Misitu Moshi kina jukumu la kutoa mafunzo na ujuzi katika matumizi endelevu ya rasilimali za misitu na teknolojia za viwanda vya misitu. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Chuo kimedahili wanafunzi 396 ambao ni sawa na asilimia 79.2 ya lengo katika teknolojia ya Viwanda vya Misitu kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada. Aidha, Chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi katika maeneo ya biashara ya kaboni, Kuzuia Mioto Msituni, Upimaji ubora wa

mazao ya misitu, Ufundi seremala, Viwanda vya kuchakata magogo kwa washiriki 210 kutoka mikoa ya Katavi, Kagera, Tabora, Arusha na Kilimanjaro. Vilevile, Chuo kimefanya tafiti tano (5) na kutoa ushauri wa kitaalam katika matumizi endelevu ya mazao ya misitu, teknolojia ya viwanda vya misitu na uhifadhi wa mazingira.

**161. Mheshimiwa Spika,** Chuo kimeendelea kufanya maboresho ya miundombinu ya kujifunzia na kufundishia ikiwa ni pamoja na kuanza ujenzi wa hosteli ya wanafunzi wa kike 200 uliofikia asilimia 30, na kukarabati madarasa mawili (2) na mabweni mawili (2). Aidha, Chuo kimenunua mtambo wa kukaushia mbao, mtambo wa kutibu mbao pamoja na vifaa vya kisasa vya maabara ya kupima ubora wa mazao ya misitu kwa lengo la kuimarisha mafunzo ya ufundi sanifu na ufundi stadi na kukuza ubunifu na biashara za mazao ya misitu.




*Mashine za kuchakata, kukausha, kutibu na kupima ubora wa mbao.*




*Kushoto ni Wajumbe wa Bodi wakikagua kuanza kwa ujenzi wa bweni la wasichana chini ya ufadhili wa TaFF Kulia ni Muonekano wa Jengo la Bweni la wasichana litakapokamilika.*

**162. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utendaji kazi, Chuo kimewezesha watumishi wanne (4) kupata mafunzo ya muda

mrefu, wawili (2) ndani ya nchi na wengine wawilli (2) nje ya nchi. Watumishi 33 wamepata mafunzo ya muda mfupi katika fani za ufundishaji, masuala ya kijinsia na maadili. Aidha, Chuo kimeendelea kutangaza huduma zake katika maonyesho na makongamano mbalimbali ndani na nje ya nchi ikiwa ni pamoja na mitandao ya kijamii na vyombo vya habari. Vilevile, kupitia mradi wa kukuza ujuzi unaofadhiliwa na Jumuiya ya Umoja wa Ulaya, Chuo kimeratibu na kuendesha warsha iliolenga kuboresha mitaala ya ufundi stadi wa misitu na viwanda vya misitu kwa nchi za Tanzania na Zambia.

#### *5.3.2.9 Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki, Tabora – BTI*

**163. Mheshimiwa spika;** Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki, Tabora kina majukumu makuu matatu (3) ambayo ni; kutoa Mafunzo kwa wadau mbalimbali katika mnyororo mzima wa Ufugaji Nyuki nchini, kutoa ushauri wa kitaaluma na kufanya tafiti za nyuki na ufugaji nyuki na mazingira. Kwa upande wa mafunzo, Chuo kinatoa Mafunzo ya muda mrefu ya Astashahada na Stashahada ya ufugaji nyuki. Vilevile, Chuo kinatoa Mafunzo ya muda mfupi ya ufugaji nyuki na uhifadhi wa mazingira. Mafunzo yanayotolewa yanalenga kuwajengea uwezo wadau kuzalisha mazao ya nyuki kwa ubora unaokidhi viwango, mahitaji ya soko na kuongeza thamani ya mazao ya nyuki na uhifadhi wa nyuki.

**164. Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki kimeendelea na jukumu la kutoa elimu na ujuzi katika fani ya ufugaji nyuki. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Chuo kimedahili wanafunzi 284 kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada. Aidha, Chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau 748 wa ufugaji nyuki, kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu ufugaji nyuki kwa wananchi 1,563 na kufanya tafiti mbili (2) kuhusu uhifadhi wa nyuki na uzalishaji wa mazao ya nyuki. Vilevile, Chuo kimekamilisha ujenzi wa Bweni la Wasichana lenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi wapatao 170 kwa wakati mmoja. Kwa upande mwingine, Chuo kimekamilisha ujenzi wa jengo la mihadhara lenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 500 kwa wakati mmoja. Aidha, Chuo kimeendelea kushirikiana na TFS katika kutekeleza mradi wa Usimamizi Shirikishi wa Miombo. Kupitia mradi huo, mafunzo yametolewa kwa wafugaji wa nyuki 156 katika wilaya za

Kaliua na Urambo na mizinga ya nyuki 500 imegawiwa.



*Jengo la Mihadhara katika Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora - BTI.*

**165. Mheshimiwa Spika**, Chuo kimeendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa kukarabati nyumba mbili (2) za watumishi, kununua vitendea kazi vya kufundishia kwa njia kidijitali. Vilevile, kimewezesha mtumishi mmoja (1) kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 15 kushiriki mafunzo ya muda mfupi.

**5.3.2.10 *Kituo cha Mafunzo ya Misitu na Viwanda vya Misitu - FWITC***

**166. Mheshimiwa Spika,** Kituo Cha Mafunzo ya Misitu na Viwanda Vya Misitu kilianzishwa kwa lengo la kutoa mafunzo na kuwajengea uwezo wakulima wa miti, vikundi vya upandaji miti na wachakataji wa mazao ya misitu. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kituo kimedahili wanafunzi 85 (wasichana 44 na wavulana 41) sawa na asilimia 106 ya lengo wa ngazi ya I - III ya ufundi stadi katika fani ya uhudumu misitu, uchakataji mazao ya misitu na useremala. Kituo kimetoa mafunzo ya muda mfupi na ushauri wa kitaalam katika matumizi endelevu ya mazao ya misitu na nishati mbadala kwa wananchi 130 kutoka Mikoa ya Ruvuma, Iringa, Njombe na Kagera.



*Wanafunzi wa fani ya uchakataji mazao ya misitu, wakifanya mafunzo kwa vitendo kwa kutumia mashine ya kisasa ya uchanaji mbao, Mafinga.*

**167. Mheshimiwa Spika**, Sambamba na hilo, Kituo kimeendelea kufanya maboresho ya mazingira ya kujifunzia kwa kuanza ujenzi wa bweni moja (1) lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 208. Aidha, katika kuimarisha ufanisi wa utendaji kazi, Kituo kimewezesha Watumishi 11 kufanya mafunzo ya muda mrefu na watumishi saba (7) wamepata mafunzo ya muda mfupi. Vilevile, Kituo kimeshiriki katika maonesho mbalimbali ya kitaifa na kimataifa kama vile Saba Saba, Nane Nane, maadhimisho ya siku ya Misitu Duniani, Siku ya Wanawake Duniani na Maonesho ya Teknolojia za Misitu (Woodex in Africa) nchini Afrika ya Kusini kwa lengo la kujitangaza.



*Wananchi wakishiriki katika mafunzo kwa vitendo ya namna ya kuzima mto wa msituni.*

**168.** **Mheshimiwa Spika**, katika kuhamasisha jamii kupanda miti kwa kutumia vipando vilivyoboreshwa, kuhifadhi na kulinda misitu, Kituo kimezalisha miche 400,000 ambayo imepandwa katika mashamba ya miti ya wananchi. Aidha, Kituo kimetoa mafunzo ya usimamizi jumuishi wa moto wa msituni kwa Maafisa Misitu na Mazingira 83 kutoka mikoa ya Iringa na Njombe.

### *5.3.3 Sekta ya Utalii*

**169.** **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Utalii ina jukumu la kusimamia, kuendeleza na kutangaza utalii ndani na nje ya nchi. Utekelezaji huo unaongozwa na Sera ya Taifa ya Utalii ya Mwaka 1999, Sheria ya Utalii Sura ya 65 na Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania Sura ya 364. Sekta hii inajumuisha Idara ya Utalii inayosimamia maendeleo ya utalii, udhibiti wa ubora na huduma; Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) yenye dhamana ya masuala ya utangazaji utalii; na Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT) kinachotoa mafunzo katika fani ya utalii na ukarimu, kufanya tafiti na kutoa huduma za ushauri wa kitaalam.

#### *5.3.3.1 Idara ya Utalii*

**170.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha usimamizi wa Sekta ya Utalii nchini, Wizara imeendelea kufanya marekebisho ya Sheria ya Utalii Sura ya 65 pamoja na Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania Sura ya 364 kwa lengo la kuhamisha majukumu ya kiutendaji kutoka Idara ya Utalii kwenda Bodi ya Utalii Tanzania ili kuongeza ufanisi, uwajibikaji na kasi ya utekelezaji wa majukumu ya sekta. Marekebisho hayo yaliwasilishwa Bungeni kupitia Muswada Maalum wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2026 uliosomwa kwa mara ya kwanza tarehe 6 Februari, 2026. Sambamba na hilo, Wizara imekamilisha mapitio ya Kanuni za Tozo ya Maendeleo ya Utalii (TDL) na kuzitangaza kupitia Gazeti la Serikali Tangazo Na. 524 la tarehe 15 Agosti, 2025 kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa tozo hiyo.

**171.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuhakikisha Sekta ya Utalii inachangia kukuza uchumi, kuongeza fursa za ajira

na uwekezaji kupitia mnyororo wa thamani na huduma za utalii. Katika kufanikisha hilo, Wizara kwa kushirikiana na Wadau wa Sekta za Umma na Binafsi imeendelea kutekeleza mikakati ya kuongeza wigo wa mazao ya utalii nchini kwa kuendeleza mazao mbadala kulingana na kanda za utalii kijiografia pamoja na fursa za soko la utalii wa kimataifa ili kupunguza utegemezi kwenye zao la utalii wa wanyamapori. Aidha, Wizara imefanya zoezi la kubaini na kusajili vivutio vya utalii 214 vikihusisha utalii wa utamaduni, michezo, miamba, misitu na dini katika maeneo mbalimbali ikiwemo mikoa ya Mtwara (19), Lindi (33), Mbeya (29), Songwe (16), Katavi (8), Kigoma (16), Iringa (21), Njombe (25), Ruvuma (33) na Rukwa (14). Usajili huo umehusisha pia viwanja vya mchezo 17 katika mikoa ya Dar es Salaam (3), Mwanza (1), Tabora (1), Arusha (1), Kigoma (1), Tanga (1), Mtwara (1), Morogoro (1), Dodoma (1), Mbeya (1), Shinyanga (1), Ruvuma (1), Kagera (1), Pwani (1) na Iringa (1) vyenye historia ya nchi yetu na fursa za utalii. Mathalan, kupitia zoezi hilo la kubaini vivutio vya utalii, eneo mojawapo la vivutio vya dini vilivyoibuliwa ni pamoja na Misikiti ya Karne ya 15 ya Kilwa na Mikindani pamoja na eneo alililoishi Papa Leo XVI akiwa hapa nchini katika Nyumba ya Malezi ya Shirika la Mtakatifu Agustino iliyopo Mahanje Jimbo Kuu Katoliki Songea Mkoani Ruvuma. Hatua hii itatanua wigo wa mazao ya utalii na kutoa fursa kwa wadau wa Sekta za Umma na Binafsi kuwekeza katika uendelezaji wa mazao hayo na huduma mbalimbali za utalii.

**172. Mheshimiwa Spika,** katika hatua za uendelezaji wa mazao ya utalii ya kimkakati nchini yakiwemo mazao ya utalii wa fukwe, meli, mikutano na matukio, Wizara imeandaa Mkakati wa Maendeleo Endelevu ya Utalii katika Ukanda wa Pwani na Bahari (2026 - 2036). Mkakati huo unalenga kufungua fursa mpya za uwekezaji, kuboresha miundombinu ya utalii pamoja na kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali zilizopo katika Ukanda wa Pwani na Bahari. Kupitia utekelezaji wake, Tanzania inatarajiwa kuimarisha ushindani wake kama kitovu cha utalii wa fukwe na bahari katika Ukanda wa Afrika Mashariki, hatua itakayosaidia kuongeza mvuto kwa watalii wa kimataifa hususan wanaotumia meli kubwa za kitalii duniani.

**173. Mheshimiwa Spika,** Wizara pia imeshiriki mikutano

mikubwa ya kimataifa ambayo ni mahsusi kuendeleza zao la utalii wa mikutano na matukio ikiwemo Meet Global MICE Congress uliofanyika Jijini Moscow Urusi Desemba, 2025 na warsha ya China Ready iliyofanyika sambamba na Onesho la WTM Africa nchini Afrika Kusini mwezi Aprili, 2026 ambapo Wizara ilipata fursa ya kuwa miongoni mwa wazungumzaji wakuu katika matukio hayo. Hatua hiyo imewezesha kuutangaza utalii wa Tanzania katika nyanja za kimataifa. Vilevile, kupitia warsha ya China ready, Tanzania imetambuliwa kama nchi ya nne (4) Barani Afrika yenye idadi kubwa ya watalii kutoka soko la China.

Aidha, Wizara ilishiriki Onesho la 47 la International Tourism Fair lililofanyika Jijini Belgrade - Serbia, Februari 2026 ambapo ilipata fursa ya kukutana na kujadiliana na wadau wakubwa wa Sekta ya Utalii kutoka nchi za Balkan (Albania, Bosnia-Herzegovina, Bulgaria, Croatia, Greece, Kosovo, Montenegro, North Macedonia, Serbia, Slovenia na Romania). Miongoni mwa wadau hao ni Bodi ya Utalii Serbia, Shirika la Ndege Serbia na Wakala mkubwa wa utalii nchini humo (KonTiki Travel & Service doo). Majadiliano na wadau hao pamoja na masuala mengine, yalilenga kuanzisha mashirikiano ya kukuza utalii hatua ambayo italeta manufaa kwa kuvutia wageni zaidi kutoka soko la utalii la kimataifa.

**174. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Wizara imeendelea kutumia watu mashuhuri na wenye ushawishi kutoka masoko mbalimbali duniani kuitangaza Tanzania kimataifa. Mathalan, Wizara iliandaa ziara ya Bwana Braydon Bent, mtangazaji maarufu wa televisheni kutoka Uingereza, ambaye pia ni mwanablogu wa michezo na shabiki mashuhuri wa timu ya mpira wa miguu ya Manchester City mwenye wafuasi zaidi ya 128,000. Ziara hiyo ilifanyika mwezi Januari, 2026 ambapo alitembelea vivutio mbalimbali ikiwemo Hifadhi za Taifa Serengeti na Arusha, Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na Zanzibar. Hatua hiyo ililenga kuitangaza Tanzania na kuvutia watalii zaidi kutoka soko la Uingereza na Duniani kwa ujumla. Kupitia ziara hiyo, Tanzania imeandikwa na waandishi wapatao 169 kutoka nchi mbalimbali zikijumuisha Marekani, India, Uturuki, Uganda, Kenya, Ufaransa na Uingereza. Vilevile, taarifa kuhusu ziara hiyo imefikia watu wapatao milioni 57.2 kuanzia Januari 19 hadi 13 Aprili, 2026.

**175.** **Mheshimiwa Spika,** katika juhudi za kuboresha utoaji wa huduma za utalii na kuimarisha shughuli za uhifadhi nchini, Wizara iliandaa Tuzo za Kimataifa za Serengeti Awards 2025 kwa lengo la kuwatambua, kuwaenzi na kusherehekea mchango wa wadau katika uhifadhi na uendelezaji utalii. Kupitia tuzo hizo, Wizara imelenga kuhamasisha ubora, uwajibikaji na ushiriki mpana wa wadau katika kulinda na kuhifadhi maliasili na malikale kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho. Katika kipindi cha mchakato wa kuwapata washindi, jumla ya wananchi 789,000 walitembelea tovuti ya The Serengeti Awards ambapo kati yao, 159,487 walishiriki kupiga kura. Hatua hiyo imeonesha mwitikio mkubwa wa umma na kuimarika kwa ushiriki wa wadau katika masuala ya utalii na uhifadhi.



*Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb.), akikabidhi Tuzo ya Uhifadhi na Utalii ya Serengeti kwa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye aliipokea kwa niaba ya Mheshimwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutambua mchango wake katika kukuza utalii na uhifadhi wa maliasili.*

**176.** **Mheshimiwa Spika,** zoezi la kuhakiki na kupanga huduma za malazi katika daraja za ubora wa nyota limeendelea kufanyika nchini, ikiwa ni hatua muhimu ya kuhakikisha viwango vya kimataifa vinazingatiwa kukidhi mahitaji na ushindani wa soko

la utalii. Zoezi hilo lilihusisha huduma saba (7) za malazi zilizofanyiwa tathmini kwa kutumia mfumo wa kielektroniki wa kutathmini na kupanga daraja za ubora (AserT) katika Majiji ya Arusha, Mwanza, Dar es Salaam pamoja na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Hatua hii imefanya jumla ya huduma za malazi zilizopangwa katika daraja za ubora wa nyota kufikia 310 nchini.

**177. Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Wizara kupitia Gazeti la Serikali Tangazo Na. 556 la tarehe 5 Septemba, 2025 ilitangaza orodha ya huduma za malazi ambapo idadi imeongezeka kutoka 10,432 mwaka 2021 hadi 12,470 mwaka 2025 ikiwa ni ishara ya ukuaji mkubwa wa sekta na kuongezeka kwa uwekezaji. Hatua hizi zinaimarisha ushindani wa Sekta ya Utalii na tasnia ya ukarimu, kuongeza imani kwa watalii wa ndani na kimataifa wanaotumia huduma za malazi, sambamba na kuongeza wigo wa mapato ya Serikali kupitia Tozo ya Kitanda Siku (Bed Night Levy).

**178. Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa jukumu la usimamizi na udhibiti wa biashara za utalii nchini, Wizara imefanya kaguzi katika kanda nne (4) za utalii zikihusisha wakala 1,918 katika mikoa ya Arusha (905), Dar es Salaam (204), Mtwara (23), Dodoma (47), Iringa (27), Mbeya (35) na Mara (677) pamoja na malango ya wageni katika Hifadhi ya Taifa Serengeti. Aidha, Wizara imetoa elimu na uhamasishaji kwa wadau wa utalii 14,354 kwa lengo la kuhamasisha uendeshaji wa biashara ya utalii pamoja na kuboresha viwango vya utoaji huduma. Matokeo ya jitihada hizi ni pamoja na kuongezeka kwa idadi ya wakala wa biashara za utalii wenye leseni kutoka 11,597 mwaka 2025 hadi kufikia 12,248 Februari 2026 sawa na ongezeko la asilimia 5.6. Hatua hii imewezesha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kuongezeka kufikia jumla ya Shilingi 10,363,854,055 katika kipindi cha mwezi Aprili, 2026.

**179. Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kuboresha huduma katika Sekta ya Utalii nchini, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa Sekta Binafsi hususan, Chama cha Wasafirishaji Watalii Tanzania (TATO) waliendesha mafunzo kwa waongoza watalii wapatao 2,228. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo katika fani za uongozaji watalii, ukarimu, huduma ya kwanza, usalama na utoaji

huduma kwa viwango vya kimataifa, maadili ya utalii, mawasiliano, sheria na wajibu katika maeneo ya hifadhi na matengenezo ya dharura ya magari wakati wa safari. Hii ni hatua muhimu kwa Tanzania ambayo ni nchi mwenyeji wa matukio makubwa ya kimataifa yakiwemo Mashindano ya AFCON 2027, Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (Inter-parliamentary Union - IPU), World Travel Awards 2026 na Miss World 2027. Vilevile, Wizara imetoa mafunzo kwa wadau 300 katika mikoa ya Iringa na Njombe kuhusu uendelezaji wa vivutio vya utalii na fursa za uwekezaji ili kuimarisha utalii katika Nyanda za Juu Kusini.

**180.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kushiriki katika mikutano mbalimbali ya Kimataifa inayohusu maamuzi yanayowezesha ustawi wa utalii endelevu. Utekelezaji huo ni pamoja na kushiriki Mkutano Mkuu wa 26 wa Shirika la Utalii Duniani (UN Tourism) uliofanyika kuanzia tarehe 7 hadi 11 Novemba, 2025 Jijini Riyadh, Saudi Arabia ambapo Tanzania ilipata uzoefu wa matumizi ya Akili Unde (AI) katika uendelezaji wa Sekta ya Utalii na mabadiliko ya kidijitali kama nyenzo ya utangazaji utalii na uwekezaji. Aidha, Wizara ilishiriki katika Mkutano Mkuu wa 25 wa Baraza la Usafiri na Utalii Duniani (WTTC) uliofanyika Jijini Rome, Italia kuanzia tarehe 28 hadi 30 Septemba, 2025. Wizara pia imeendelea kushiriki Mikutano ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) inayohusu ushirikiano wa Kikanda kwenye Sekta ya Utalii, ikiwemo Mkutano wa Ngazi ya Mawaziri uliofanyika Jijini Arusha tarehe 12 Septemba, 2025.
Katika hatua nyingine, mnamo mwezi Septemba, 2025 kupitia ushirikiano na Taasisi ya Kimataifa ya Aotearoa Astrotourism Academy ya New Zealand, Dark Sky International na Center for Astrophysics Harvard za Marekani pamoja na Chuo Kikuu Huria hapa nchini, Tanzania ilipata fursa za kujenga uwezo kwa wataalam saba (7) wa Wizara katika eneo la uendelezaji wa zao la utalii wa anga (astro-tourism). Vilevile, kupitia ushirikiano na Jamhuri ya India wataalam wanne (4) wa Wizara walipata fursa ya kujengewa uwezo katika eneo la usimamizi na uendelezaji utalii.

### *5.3.3.2 Tozo ya Maendeleo ya Utalii – TDL*

**181. Mheshimiwa Spika,** Tozo ya Maendeleo ya Utalii (TDL) ilianzishwa chini ya Kifungu cha 60(1) cha Sheria ya Utalii Sura ya 65 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2023. Lengo kuu la kuanzisha TDL ni kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zinazohusiana na maendeleo ya utalii (Kanuni ya 10 ya Kanuni za TDL, iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2025). Jukumu kuu la TDL ni kuwezesha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za uendelezaji utalii nchini ikiwa ni pamoja na: kubuni na kuendeleza mazao ya utalii; kuboresha miundombinu ya utalii; kudhibiti ubora wa huduma na biashara za utalii; kutangaza utalii ndani na nje ya nchi; kujenga uwezo na kufanya tafiti katika Sekta ya Utalii nchini.

**182. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara kupitia TDL imeendelea kuwezesha fedha kwa ajili ya maboresho ya miundombinu mbalimbali nchini katika maeneo ya kimkakati ikiwemo makutano ya barabara ya Seronera kuelekea Ndabaka yenye urefu wa kilomita 121.4 ikijumuisha ujenzi wa vivuko vidogo nane (8); ujenzi wa madaraja makubwa matatu (3) (mto Banagi, Bona na Mokasi) katika barabara ya Seronera kuelekea lango la Ikoma; ujenzi wa daraja kubwa eneo la viboko vya Naabi; makalavati matano (5) katika barabara ya Seronera – Naabi; ujenzi wa madaraja makubwa mawili (2) mto Orangi Juu na Orangi Chini katika barabara ya Lobo kuelekea Banagi katika Hifadhi ya Taifa Serengeti. Aidha, TDL imewezesha fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kilomita 38 ya kiwango cha changarawe kutoka linapojengwa lango jipya la kuingia Hifadhi ya Taifa Mikumi upande wa Kilosa hadi makao makuu ya hifadhi kwa lengo la kuunganisha watalii wanaowasili kwa Treni ya SGR na Hifadhi ya Taifa Mikumi. Vilevile, TDL imewezesha ujenzi wa barabara ya kilomita 55.7 katika Pori la Akiba Wami-Mbiki. Kwa upande mwingine, TDL imewezesha fedha za ujenzi wa Kituo cha Taarifa cha Nandete -Kilwa mkoani Lindi ambapo vita vya majimaji vilianzia na ujenzi umefikia asilimia 76.

**183. Mheshimiwa Spika,** ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya AFCON 2027, TDL imewezesha fedha kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya kutolea huduma kupitia ujenzi wa geti moja (1),

kambi moja (1) ya wageni, eneo moja (1) la kuangalia wanyama (Hideout) na eneo moja (1) la kupumzikia katika Hifadhi ya Wanyamapori Makuyuni mkoani Arusha. Aidha, ujenzi wa bwawa la kuogelea na viwanja vya michezo ikiwemo mpira wa miguu, tennis, mpira wa kikapu na wavu katika Pori la Akiba Pande unaendelea. Vilevile, TDL imewezesha fedha za ujenzi wa maeneo ya kupumzikia na njia ya mbao (boardwalk) katika Msitu wa Mikoko wa Sahare, Mkoani Tanga. Sambamba na hilo, TDL imewezesha fedha za mafunzo kwa waongoza watalii (Tour guides) wapatao 2,228 yaliyofanyika mkoani Arusha kwa lengo la kuboresha huduma kwa watalii kabla, wakati na baada ya mashindano ya AFCON 2027.

**184.** **Mheshimiwa Spika,** utangazaji utalii ndani na nje ya nchi ni kichocheo cha kuvutia watalii kutembelea vivutio vyetu nchini. TDL imewezesha fedha kwaajili ya kutangaza vivutio vya utalii vya Tanzania kupitia ushiriki katika maonesho mbalimbali ikiwemo INDABA nchini Afrika Kusini na ITB - Berlin nchini Ujerumani. Vilevile, TDL imewezesha fedha za ununuzi wa vifaa vya kukamilisha Kituo cha Kutolea Habari Kidijitali (DDMCC) kwa ajili ya kutangaza utalii kidijitali.

**185.** **Mheshimiwa Spika,** TDL pia imewezesha fedha kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya vyuo vya utalii nchini kupitia ujenzi wa darasa linalohamishika katika Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT) Kampasi ya Temeke na kukamilisha ukarabati wa hosteli na ujenzi wa darasa kwa ajili ya wanafunzi katika Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii - Likuyu Sekamaganga - CBCTC. Jitihada hizi zinalenga kuboresha mazingira ya kujifunzia kwa wataalam wa utalii nchini.

#### ***5.3.3.3 Bodi ya Utalii Tanzania - TTB***

**186.** **Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Utalii Tanzania ilianzishwa kwa Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania Sura Na. 364. Sheria hiyo imeainisha majukumu makuu manne (4) ambayo ni: kutumia mbinu mbalimbali za utangazaji ili kuifanya Tanzania iwe kituo mojawapo mashuhuri cha utalii duniani; kuhamasisha uendelezaji wa miundombinu ya utalii; kufanya tafiti kwa ajili ya kuboresha Sekta ya Utalii nchini; na kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu

wa utalii na manufaa yake kiuchumi.

**187. Mheshimiwa Spika,** Bodi imeendelea kuhamasisha na kutangaza utalii katika masoko mbalimbali ya kikanda na kimataifa kwa kuratibu ushiriki wa wadau katika maonesho sita (6) ambayo yalitembelewa na wageni 42,801. Maonesho hayo ni WTM London ya nchini Uingereza (7,234), Qatar Travel Mart nchini Qatar (5,576), Akwaaba African Travel Market nchini Nigeria (1,907), OTM nchini India (10,508), FITUR nchini Uhispania (6,812) na ITB Berlin nchini Ujerumani (10,764). Ushiriki wa Tanzania katika maonesho hayo umeendelea kuchangia ongezeko la watalii kutoka nchi husika. Sambamba na hilo, Bodi kwa kushirikiana na wadau wa utalii 30 wa sekta binafsi imeshiriki katika tukio la msafara wa utangazaji utalii kimataifa la My Tanzania Roadshow kwenye nchi za Ujerumani, Sweden, Norway na Denmark, lililofanyika mwezi Machi, 2026 ambapo iliweza kukutana na wanunuzi na wafanyabiashara wa utalii wapatao 173 waliopata fursa ya kuvifahamu vivutio na vifurushi vya mazao ya utalii vilivyopo nchini. Hatua hizo zimekuwa na mchango katika kuitangaza Tanzania na kuvutia watalii wengi ikiwemo soko la Ujerumani, ambapo idadi yake imeongezeka kutoka watalii 102,798 mwaka 2024 hadi kufikia watalii 114,615 mwaka 2025 sawa na ongezeko la asilimia 11.5.

**188. Mheshimiwa Spika,** Bodi pia imeratibu ziara tatu (3) za mafunzo (FAM Trips) kwa washiriki 166 kutoka masoko ya utalii ya kimataifa ya India (6), Urusi (36) na Marekani (124) iliyojumuisha wakala wa safari za utalii na waandishi wa habari kwa lengo la kuwajengea ufahamu wa vivutio na mazao ya utalii yaliyopo nchini ili kuyatangaza katika masoko yao. Ziara hizo zilifanyika katika Hifadhi za Taifa za Ruaha, Serengeti na Mikumi; Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro; Pori la Akiba Mpanga Kipengere; Makumbusho ya Taifa Dar es Salaam; na Zanzibar. Jitihada hizo zinachangia kuongeza idadi ya watalii kutoka masoko hayo. Mathalan, Watalii kutoka Urusi waliongezeka kutoka 12,314 hadi kufikia 17,100 kati ya mwaka 2024 na 2025 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 38.9.

**189. Mheshimiwa Spika,** Bodi imeendelea kushirikiana na Ofisi za Balozi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zilizopo Nigeria,

Qatar, Afrika Kusini, India, Ufaransa, Uingereza, Ujerumani, China na Urusi kwa kuzipatia nyenzo mbalimbali za utangazaji utalii zikiwemo QR codes zenye taarifa za vivutio vya utalii, picha jongefu za vivutio na huduma za utalii, na vipeperushi. Katika ushirikiano huo, Bodi kupitia Ubalozi wa Tanzania nchini Nigeria ilishiriki Onesho la Akwaaba lililofanyika mwezi Agosti, 2025 Jijini Lagos. Onesho hilo lilitembelewa na wageni 1,907 vikiwemo vyombo vya habari, wakala wa biashara za utalii na wawakilishi wa mashirika ya ndege. Aidha, Bodi ilishiriki katika tukio la uzinduzi wa safari za kimataifa za Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kutoka Dar es Salaam kwenda Jijini Lagos, Nigeria kupitia Accra, Ghana. Juhudi hizi zimechangia ongezeko la watalii kutoka ukanda wa soko la Afrika Magharibi wanaotembelea Tanzania ambapo idadi ya watalii kutoka nchini Nigeria imeongezeka kutoka watalii 7,644 mwaka 2024 hadi kufikia watalii 10,030 mwaka 2025 hii ikiwa ni ongezeko la asilimia 31.2. Vilevile, takwimu zinaonesha jumla ya watalii 57,969 kutoka soko la Afrika Kusini walitembelea Tanzania katika kipindi cha mwaka 2025 ikilinganishwa na watalii 53,737 mwaka 2024 ikiwa ni ongezeko asilimia 7.9.

**190.** **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kuhakikisha kuwa vivutio vya utalii Tanzania vinafahamika duniani, Bodi imeendelea kuhamasisha na kupokea wageni mashuhuri kutoka mataifa mbalimbali na kuwatembeza katika vivutio vya utalii ili wawe mabalozi wazuri wa kutangaza Tanzania kwa wafuatiliaji wao. Hadi kufikia Aprili 2026, Tanzania imepokea watu mashuhuri tisa (9) wakiwemo Bwana Jericho Rosales, mwigizaji mashuhuri wa filamu na tamthilia kutoka Ufilipino anayejulikana zaidi kwa uhusika wake kama Angelo katika tamthilia ya Pangako Sa 'Yo (The Promise) ya mwaka 2000; Sydney Sweeney, mwigizaji maarufu wa Marekani anayejulikana kupitia vipindi vya televisheni kama Euphoria na The White Lotus; na Mauro Icardi, Mwanasoka maarufu kutoka Argentina. Wageni hawa walipata fursa ya kutembelea vivutio vya utalii katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Hifadhi ya Taifa Serengeti na Zanzibar. Hadi kufikia Aprili, 2026 walifanikiwa kuchapisha maudhui ya utalii wa Tanzania katika majukwaa ya kidigitali ambapo maudhui hayo yamefikia watu zaidi ya milioni 105.

**191.** **Mheshimiwa Spika,** katika kukuza jitihada za utangazaji

utalii kidijitali, Bodi imeimarisha Kituo cha Utangazaji Utalii Kidigitali ambacho kinawezesha watalii kupata taarifa muhimu za utalii. Aidha, Bodi imeendelea na ujenzi wa mfumo wa Travel Companion wenye Booking Platform unaoambatana na matumizi ya Akili Unde (AI) itakayotoa mwongozo wa papo kwa papo kwa wataliii kwa lugha za kimataifa zaidi ya 56 na kuwezesha watalii kutoka nchi masoko kupata taarifa muhimu kuhusu mazao na vivutio vya utalii nchini Tanzania. Lengo la mfumo ni kumrahisishia mtalii kuandaa safari yake yote kuanzia hatua ya maandalizi, kipindi awapo hapa nchini, na anaporejea nchini kwake. Mfumo huu pia unajumuisha taarifa za utalii zikiwemo maeneo ya hifadhi, fukwe, shughuli za kitalii, matukio, huduma za malazi na usafiri, ramani ya kidijitali na taratibu za kuingia nchini, ambapo unapatikana kupitia tovuti ya www.destinationtanzania.tz. Aidha, mfumo utaendelea kuboreshwa ili kuendana na mahitaji ya soko la kimataifa na mabadiliko ya teknolojia kwa lengo la kuiweka Tanzania katika nafasi ya ushindani wa juu katika utangazaji utalii wa kidijitali duniani. Vilevile, Bodi imeendelea na juhudi zake za kutangaza utalii kupitia mitandao ya kijamii kwa kutengeneza na kurusha maudhui kwenye majukwaa mbalimbali ikiwemo YouTube, Facebook, Instagram, Linkedin, X na TikTok. Kupitia juhudi hizi Bodi imefanikiwa kupata jumla ya wafuatiliaji milioni 2.9 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ikilinganishwa na wafuatiliaji milioni 2.7 kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, hii ni sawa na ongezeko la asilimia 7.4.

**192. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Bodi imeendelea kutangaza na kukuza fursa za mazao ya utalii wa utamaduni, meli na mikutano. Katika kukuza zao la utalii wautamaduni, Bodi imefanya mafunzo kwa vikundi 25 vya utalii wa kitamaduni (cultural tourism enterprises) kuhusu namna bora ya kutangaza, kusimamia na kuendesha vituo vya utalii wa Utamaduni. Mafunzo hayo yalifanyika katika mikoa ya Pwani (4), Singida (12), Mwanza (3), Mara (3) na Dodoma (3) na kufanya idadi ya vikundi vilivyopatiwa mafunzo hayo kufikia 103 mwezi Aprili, 2026 kutoka 78 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 32.05. Pia, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa utalii wa meli, Bodi imepokea meli za utalii (cruiseships) tisa (9) zenye jumla ya watalii 2,508. Meli hizo ni MS Hebridean Sky, Seabourn Sojourn, Crystal Symphony, MV. Europa,

MS Island Sky, Le Bellot, MS Seven Seas Voyager, Silver Cloud na SH Diana. Meli hizo zimeleta watalii kutoka Marekani, Canada, Ubelgiji, Australia, Ujerumani, Urusi na Uingereza. Aidha, watalii hao walipata fursa ya kutembelea vivutio vilivyopo nchini kama vile Hifadhi ya Taifa Nyerere, Bagamoyo, Makumbusho ya Taifa Jijini Dar es Salaam pamoja na Eneo la Urithi wa Dunia la Kilwa Kisiwani na Songomnara.

**193.** **Mheshimiwa Spika,** Bodi imeendelea kutumia fursa za vyombo vya usafiri hususan, Treni ya Mwendokasi ya SGR kutangaza utalii wa Tanzania. Utekelezaji huo umefanyika kupitia uoneshaji wa picha mjongeo tatu (3) zenye maudhui ya utalii ili kuhamasisha wasafiri kutembelea vivutio vilivyopo nchini. Treni hii husafirisha wastani wa abiria 8,500 kwa siku kati ya mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma. Vilevile, Bodi imeendelea kutangaza utalii kupitia ndege za Shirika la Ndege Tanzania ambayo huruka katika nchi 10 za Afrika, nchi tatu (3) nje ya Afrika na mikoa 14 ya Tanzania kwa kutumia Jarida la Twiga kwa kuweka QR codes zenye taarifa kuhusu utalii wa Tanzania. Bodi pia ilitumia mashindano ya CHAN 2024 yaliyofanyika nchini mwezi Agosti, 2025 kutangaza utalii wa Tanzania kupitia kampeni ijulikanayo kama Tinga CHAN, Tinga Tanzania iliyofikia wafuatiliaji milioni 37.9 kupitia mitandao ya kijamii.

**194.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuhamasisha utalii wa ndani, Bodi imeendelea kuratibu na kushiriki katika matukio ya ndani ya nchi yanayohusisha wadau mbalimbali na kufikia watu zaidi ya 900,000 ikiwa ni pamoja na Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba), Maonesho ya Wakulima (Nanenane), Lake Zone Tourism International Marathon, East Africa Trade Fair, Majimaji Festival, Selous Marathon, Zanzibar International Trade Fair (ZITF), Rombo Marathon, Kili International Marathon na Same Utalii Festival. Mathalan, wakati wa Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam 2025, wageni 676,298 walitembelea Banda la Wizara ya Maliasili na Utalii ili kupata taarifa kuhusu utalii, biashara, uhifadhi, kuona wanyamapori hai, kuona vivutio vya urithi wa utamaduni na malikale, kupata huduma za vyakula ikiwemo nyamapori na kununua mazao ya misitu na nyuki.

**195. Mheshimiwa Spika,** pamoja na hayo, Bodi kwa kushirikiana na Wadau wa utalii, waliandaa vifurushi vya safari za utalii wa ndani ambapo wageni 446 walipata fursa ya kutembelea vivutio mbalimbali vikiwemo Hifadhi ya Taifa Mikumi (289), Hifadhi ya Taifa ya Tarangire (72), Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro (53) na Msitu wa Mazingira Asilia Pugu Kazimzumbwi (32). Aidha, Bodi iliratibu programu ya Funga Mwaka Kijanja, Talii na kampeni maalum za huduma mkoba (outreach programs) 48 kwa makundi mbalimbali ya kijamii vikiwemo vyuo, shule za sekondari na shule za msingi ambapo wadau 31,289 walifikiwa na kuhamasishwa kutembelea vivutio vya utalii.

#### *5.3.3.4 Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii - NCT*

**196. Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT) kilianzishwa chini ya Sheria ya Wakala Namba 30 ya mwaka 1997 kikiwa na dhamana ya kutoa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa huduma za ushauri wa kitaalam katika fani za Utalii na Ukarimu. Chuo kina Kampasi nne (4) ambazo ni Bustani, Temeke, Arusha na Mwanza. Chuo kinatoa mafunzo kwa mfumo wa Umahiri (Competence Based Education and Training - CBET) katika ngazi ya Astashahada na Stashahada katika kozi za Ukarimu (Hospitality Management), Mapishi (Food Production), Uokaji (Pastry and Bakery), Uratibu wa Matukio (Events Management), Usafirishaji na Utalii (Travel and Tourism Operations) na Uongozaji Watalii (Tour Guiding Operations). Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Chuo kiliongeza udahili wa wanafunzi kutoka 1,397 kwa Mwaka wa Masomo 2024/2025 hadi wanafunzi 1,653 kwa Mwaka wa Masomo 2025/2026 sawa na ongezeko la asilimia 18.3. Vilevile, Chuo kinatoa mafunzo ya Uanagenzi katika fani za Ukarimu ambapo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 jumla ya wanafunzi 228 walipata mafunzo haya, kati ya hao wanafunzi 170 walifadhiliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Mahusiano.

**197. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Chuo kilitoa mafunzo ya muda mfupi kwa lengo la kuwajengea uwezo wadau katika mnyororo wa thamani wa utalii. Jumla ya washiriki 6,928 wa kada mbalimbali walifaidika na mafunzo hayo

wakiwemo Wanafunzi wa Chuo cha Polisi Moshi 4,868; Maafisa Uhamiaji 220; waongoza watalii Wilayani Mafia 16 na Arusha 1,339; watumishi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) 73; watumishi wa Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) 32; wahudumu katika sehemu za malazi Mkoani Shinyanga 178; na waratibu wa matukio 40. Aidha, Vijana 162 watoa huduma za vinywaji kwenye Mkoa wa Arusha walipata mafunzo ya programu maalum ya "Learning for Life" yaliyotolewa na Chuo kwa kushirikiana na Kampuni ya Serengeti Breweries LTD (SBL). Vilevile, Chuo kimeendelea kutoa huduma za ushauri elekezi katika Sekta ya Utalii na ukarimu nchini ikijumuisha huduma ya ushauri iliyotolewa wilayani Mafia kuhusu uanzishwaji wa vivutio vya utalii wa utamaduni (Cultural Tourism Entreprise - CTE) yaliyofadhiliwa na WWF kwa kuratibiwa na taasisi ya Whale Shark Tour Operators Network of Tanzania (WATONET), jumla ya vivutio vinne (4) tayari vimeanzishwa na kusajiliwa ambavyo ni Kilindoni Cultural Tourism Entreprise, Tuvuli Cultural Tourism Entreprises, Rasta House Cultural Tourism Enterprise pamoja na Rabii's Eco Cultural Mafia Island. Pia, wanafunzi 56 walishiriki kutoa huduma (Ushers) katika mashindano ya CHAN 2024 yaliyofanyika mwezi Agosti, 2025.

**198. Mheshimiwa Spika,** Chuo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kimefanikiwa kuwezesha ufanyaji wa tafiti za kitaaluma 14 zilizojikita katika mbinu za kuimarisha huduma za ukarimu; mbinu za uendelezaji mafunzo ya umahiri katika Sekta ya Utalii; utalii endelevu; pamoja na matumizi ya teknolojia. Tafiti hizo zimekuwa na mchango katika uboreshaji wa mafunzo kwa taasisi za elimu na kuboresha huduma kwa watalii. Tafiti zinazofanyika zimewasilishwa kwa wadau kupitia makongamano, machapisho na majukwaa mbalimbali ikiwemo maonesho, warsha pamoja na mfumo wa chuo wa kidijitali wa kukusanya na kuhifadhi machapisho ya kitaaluma. Vilevile, Chuo kimeendelea kuwajengea uwezo watumishi katika kuandika maandiko na kufanya tafiti ambapo jumla ya watumishi 58 wamepata mafunzo hayo.

**199. Mheshimiwa Spika,** Chuo kimeendelea na ujenzi wa jengo jipya la taaluma la ghorofa tano (5) katika Kampasi ya Arusha lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,212 likiwa na

miundombinu mbalimbali ikiwemo madarasa, kumbi za mikutano, hoteli ya mafunzo na migahawa ambapo ujenzi wa jengo hilo umefikia asilimia 95 na linatarajiwa kuanza kutumika katika Mwaka wa Masomo 2026/2027. Vilevile, Chuo kimeendelea na ujenzi wa darasa linalohamishika katika kampasi ya Temeke lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 250, ambapo hadi sasa ujenzi umefikia asilimia 40.



*Jengo la taaluma la ghorofa tano (5) linaloendelea kujengwa katika Chuo cha Taifa cha Utalii, Kampasi ya Arusha.*

**200. Mheshimiwa Spika,** Chuo kimeendelea na utekelezaji wa mikakati mbalimbali ya kujitangaza. Mikakati hiyo ni pamoja na huduma mkoba (outreach programs) kwa kutembelea shule za sekondari 80 zilizopo katika Kanda ya Ziwa, Kaskazini na Pwani, katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Simiyu, Mwanza na Mara zikihusisha washiriki 11,500. Aidha, Chuo kimeshiriki matukio mbalimbali ikiwemo Mkutano wa International Congress and Convention Association (ICCA) nchini Ureno pamoja na Future Leaders Challenge - Dubai katika Falme za Kiarabu kwa lengo la kujitangaza na kutanua wigo wa fursa kwa wahitimu katika fani mbalimbali. Vilevile, Chuo kimejitangaza kupitia mitandao ya kijamii pamoja na vipindi vya televisheni na redio vya Channel 10, Azam TV, Manyara FM na FADECO FM.

**201. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha watumishi wanakuwa na ujuzi stahiki, Chuo kimefanikiwa kutekeleza mpango wa mafunzo kwa kuwezesha watumishi 15 kupata mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi katika ngazi ya shahada (2), uzamili (10) na uzamivu (3). Aidha, jumla ya watumishi 57 wamewezeshwa kupata mafunzo ya muda mfupi katika fani za utalii, ukarimu na mbinu za ufundishaji.

### *5.3.4 Sekta ya Mambo ya Kale*

**202. Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Mambo ya Kale inajumuisha Idara ya Mambo ya Kale, Shirika la Makumbusho ya Taifa la Tanzania na Mfuko wa Taifa wa Mambo ya Kale. Sekta hii ina jukumu la kusimamia uhifadhi, utafiti na uendelezaji wa rasilimali za malikale. Utekelezaji wa jukumu hilo unazingatia Sera ya Malikale ya Mwaka 2008; Sheria ya Mambo ya Kale, Sura ya 333; na Sheria ya Makumbusho ya Taifa, Sura ya 281.

**203. Mheshimiwa Spika**, Malikale zinajumuisha rasilimali za urithi wa utamaduni, zinazoshikika na zisizoshikika; zinazohamishika na zisizohamishika zilizo nchi kavu na majini zenye umri wa miaka 100 na kuendelea au zile ambazo kutokana na umuhimu wake kitaifa, zimeainishwa na kutangazwa na Waziri mwenye dhamana kuwa Urithi wa Taifa. Rasilimali hizi ni pamoja na majengo ya kihistoria, miji ya kihistoria, makazi ya kijadi, michoro ya miambani, maeneo ya Wapigania uhuru, makaburi yenye historia maalumu, minara ya kihistoria, vifaa vya utamaduni, mabaki ya mimea, wanyama na zamadamu. Kutokana na utajiri mkubwa wa malikale, Tanzania imetambulika kimataifa kama kitovu cha tafiti za malikale kwani maeneo haya yametoa ushahidi muhimu wa kisayansi ambao umejidhihirisha kupitia vielelezo vya chimbuko, maendeleo na uwezo wa binadamu pamoja na mabadiliko ya mazingira, jambo linaloifanya Sekta ya Malikale kuwa na thamani kubwa kitaifa na kimataifa.

#### *5.3.4.1 Idara ya Mambo ya Kale*

**204. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha uhifadhi, kuboresha mnyororo wa thamani na kuvutia uwekezaji kwenye

Sekta ya Mambo ya Kale, Wizara imekamilisha maboresho ya Kanuni za Uhifadhi na Usimamizi wa Malikale na kuzitangaza kupitia tangazo la Serikali Na. 581 la tarehe 26 Septemba, 2025. Kanuni hizo zinahusu utafiti, usafirishaji wa malikale nje ya nchi, kuuza na kubadilishana malikale na uteuzi wa wahifadhi malikale wa heshima. Aidha, Wizara imekamilisha Mwongozo wa Vigezo na Taratibu za Kutangaza Malikale kuwa Urithi wa Taifa. Vilevile, Wizara imekamilisha Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Malikale ya mwaka 2008 ambao utatumika kwa kipindi cha mwaka 2025-2035.

**205. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa jukumu la kudumisha uhifadhi endelevu wa maeneo yenye sifa za kipekee ambayo ni urithi wa Dunia na kuimarisha diplomasia ya kimataifa, Wizara imeratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano Mkuu wa 25 wa nchi wanachama wa Mkataba wa UNESCO wa mwaka 1972 unaohusu ulinzi na uhifadhi wa urithi wa Dunia uliofanyika Novemba, 2025 Paris - Ufaransa. Kupitia mkutano huo, Tanzania imechaguliwa kuwa Mjumbe wa Kamati ya Urithi wa Dunia inayojumuisha nchi 21 kati ya nchi 195 kwa kipindi cha miaka minne (4) kuanzia mwaka 2025 hadi 2029. Hii ni mara ya tatu (3) kwa Tanzania kuchaguliwa kushika nafasi hiyo ambayo imewahi kupata kwa vipindi vya mwaka 1985 hadi 1991; na 2015 hadi 2019. Pamoja na kujiimarisha kiuhifadhi na kidiplomasia, fursa hiyo itatumika kutangaza vivutio vya utalii nchini na kusukuma ajenda za matumizi endelevu ya maeneo ya urithi wa dunia hususan, kipindi hiki ambacho Taifa letu linafanya mageuzi makubwa ya kiuchumi ikiwemo ujenzi wa miundombinu mikubwa ya kimkakati.

**206. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Wizara imeandaa na kuliwasilisha UNESCO Andiko la kuomba kuorodhesha maeneo yenye Michoro ya Miambani yaliyopo Kanda ya Ziwa Victoria katika mikoa ya Kagera, Mwanza na Mara katika Orodha ya Urithi wa Dunia. Andiko hilo limeandaliwa kwa kushirikiana na nchi za Uganda na Kenya ambapo Tanzania imewasilisha maeneo 47, Uganda 27 na Kenya matatu (3). Vilevile, kwa kushirikiana na Ofisi ya UNESCO Dar es Salaam, Wizara imetoa mafunzo kwa watumishi 12 ya kuwajengea uwezo wa kuandaa maandiko ya kuingiza maeneo katika Orodha ya Urithi wa Dunia. Lengo la hatua hizo ni kuhakikisha kuwa Tanzania

inaendelea kuongeza maeneo katika Orodha ya Urithi wa Dunia na kunufaika na fursa zilizopo katika ngazi hiyo.

**207. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa maeneo ya malikale yanalindwa kisheria, kuendelezwa na kutumika kiutalii, Wizara imetangaza maeneo 16 ya malikale kuwa Urithi wa Taifa kupitia matangazo ya Serikali Na. 580 na 582 ya tarehe 26 Septemba, 2025. Hatua hiyo imeongeza idadi ya maeneo ya Urithi wa Taifa kutoka 142 hadi 158. Maeneo yaliyotangazwa yana taarifa za kihistoria zinazohusu ustaraabu wa maisha ya Waswahili na uhusiano wao na jamii za kigeni, chimbuko na kuenea kwa ukristo; tawala za kikoloni na mikakati waliyotumia kujenga uchumi wao; harakati za jamii za Tanganyika kupinga uvamizi wa wakoloni, uasisi na ujenzi wa Tanzania huru; mchango wa Tanzania katika ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika; na ushahidi wa awali wa mawasiliano ya binadamu wa kale kupitia sanaa ya uchoraji wa picha miambani.

**208. Mheshimiwa Spika,** maeneo 16 yaliyotangazwa kuwa urithi wa Taifa ni Boma la Mjerumani, Jengo la Hospitali na Mahakama ya Kihistoria Maposeni na Kanisa la Roman Katoliki Benedictine Abbey, Peramiho – Songea; Michoro ya Miambani ya Msule A na B, Pango la Mgugumu - Isanzu A, Pango la Mgugumu - Isanzu B, Pango la Sumbilila (Kirumi)- Isanzu C – Singida; Mnara wa Kumbukumbu ya Hayati Edward Moringe Sokoine, Kambi ya wapigania Uhuru wa Chama cha ANC cha Afrika ya Kusini iliyopo Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Kampasi ya Solomon Mahlangu, Mazimbu – Morogoro; Shule ya Sekondari Samora Machel ambayo ilikuwa Kambi ya wapigania Uhuru wa Chama cha FRELIMO cha Msumbiji – Mbeya; Makazi ya Watemi Fundikira na Isike – Tabora; Mji wa Kihistoria wa Kilwa Kivinje – Lindi; Kambi ya Wapigania Uhuru wa nchi ya Afrika ya Kusini Kihesa Mgagao, Kilolo – Iringa; na majengo ya kihistora: Sisal House na Hospitali ya Afya ya Akili, Kanisa la KKKT Lutindi na Kituo cha Hija Magila Msalabani - Tanga.

**209. Mheshimiwa Spika,** sambamba na kutangaza maeneo 16 kuwa urithi wa Taifa, Wizara imekusanya taarifa za maeneo 25 ili kuendelea kuhuisha urithi huo. Kati ya maeneo 25 ambayo taarifa zake zimekusanywa, taratibu za kisheria zinazohusu

maeneo 15 yaliyopo katika mikoa ya: Njombe (2), Tanga (2), Arusha (1), Kilimanjaro (1), Mwanza (2), Kagera (4), Mara (2) na Manyara (1) zimekamilika kwa ajili ya kutangazwa kuwa Urithi wa Taifa. Maeneo hayo ni Msitu wa Nyumbanitu na Kaburi la Mashujaa wa Vita vya Majimaji Sawala – Njombe; Kituo cha Amani Medical Research na Jengo la Tanga Old School – Tanga; Nyayo za Zamadamu wa Engarasero – Arusha; Handaki la Mengwe na eneo la kihistoria Mreye Namsera Kati - Kilimanjaro; Michoro ya Miambani Kigongo, Bukumbi na Nyankila Chole – Mwanza; Michoro ya miambani Kigarama, Bukurungo, Bugandika, Bwanjai na Ihangiro - Kagera; na Michoro ya Miambani Kyamajoje na Kasoma - Mara.

**210.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa Urithi wa Taifa unafahamika miongoni mwa wadau na kutumika kwa manufaa ya kijamii na kiuchumi, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa imefanya tathmini ya hali ya uhifadhi na matumizi endelevu ya maeneo tisa (9) ya malikale yaliyopo katika mikoa ya Arusha (6), Mara (1), Shinyanga (1) na Geita (1) ambayo yanajumuisha Makaburi ya Kale ya Naberera na Msalala; Nyayo za Zamadamu Laetoli; eneo la miamba makazi ya Mumba; eneo la Bonde la Olduvai; magofu ya Engaruka; na kilima cha Fort Ikoma. Tathmini hiyo ililenga kuandaa mipango ya usimamizi na uendelezaji kwa ajili ya kuboresha maeneo hayo kwa kuyawekea miundombinu ya uhifadhi na utalii. Matokeo ya tathmini hiyo yamebainisha kuwa maeneo nane (8) yapo katika hali nzuri za uhifadhi na eneo la makaburi ya Naberera lililopo Mkoani Arusha linahitaji kufanyiwa ukarabati.

**211.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha uhifadhi na ulinzi wa malikale, Wizara imefanya ukaguzi wa hali za uhifadhi wa maeneo ya malikale matatu (3), makumbusho tisa (9) na kutatua mgogoro mmoja (1). Maeneo yaliyokaguliwa yanajumuisha Magofu ya Tongoni- Tanga; majengo 39 yenye historia ya utawala wa kijerumani yaliyopo Chuo cha Misitu Olmotonyi-Arusha na Kituo cha Hifadhi ya Mazingira Asili Amani - Tanga. Aidha, ukaguzi umefanyika katika maeneo yafuatayo: Utawala wa jadi Busiya Wilayani Kishapu - Shinyanga, Makumbusho ya Tiba Asili, Bukigi Wilayani Maswa - Simiyu; Makumbusho ya Chuo Kikuu

cha Mtakatifu Agustino – Mwanza; Makumbusho ya Kumbukumbu ya Chifu Ndaskoi - Arusha na Makumbusho ya Mkumbavana - Kilimanjaro. Kupitia kaguzi hizo, ushauri umetolewa kuhusu hatua muhimu za kuchukua ili kuhakikisha rasilimali za malikale zinakuwa endelevu na kuleta tija kwa jamii na Taifa kwa ujumla. Vilevile, mgogoro mmoja (1) wa matumizi ya ardhi katika kituo cha Makumbusho ya Mtwa Mkwawa - Iringa umetatuliwa.

**212.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeratibu na kushiriki katika matamasha matatu (3) ya kumbukumbu kwa lengo la kuhamasisha urithishaji wa historia ya Taifa kutoka kizazi kimoja kwenda kingine na kuongeza mazao ya utalii kupitia matumizi ya urithi usioshikika. Matamasha hayo ni Kumbukizi ya Vita ya Majimaji, Songea – Ruvuma; Entabuko Wilayani Misenyi - Kagera; na Maadhimisho ya Kumbukizi ya Miaka 104 ya Mwl. Nyerere yaliyofanyika mwezi Aprili, 2026 jijini Dodoma ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Miaka Kumi wa Kuenzi na Kutangaza Urithi wa Baba wa Taifa Mwl. Julius Kambarage Nyerere.




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi, akiweka shada la maua kwenye kaburi la shujaa wa vita vya Majimaji katika Kumbukizi ya Vita hiyo iliyofanyika Mjini Songea, mwezi Februari 2026.*

### *5.3.4.2 Mfuko wa Mambo ya Kale - NFA*

**213. Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Mambo ya Kale – NFA ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mambo ya Kale, Sura ya 333 kwa lengo la kuwezesha majukumu ya uhifadhi, utafiti na uendelezaji wa malikale. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mfuko umewezesha fedha kwa ajili ya maandalizi ya Kanuni za Uhifadhi na Usimamizi wa Malikale; Mwongozo wa Vigezo na Taratibu za Kutambua na Kutathimini maeneo ya Malikale yanayofaa kuwa Urithi wa Taifa; tathmini ya hali ya uhifadhi wa mji wa kihistoria Mikindani, uratibu wa vikao vya kujadili uendelezaji wa eneo la Makumbusho ya Mtwa Mkwawa, Kalenga – Iringa, usimamizi wa eneo la Nyayo za Zamadamu Engaresero; na utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Kuenzi na Kusherehekea Urithi wa Mwl. Nyerere. Vilevile, Mfuko umewezesha fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Tanzania kushinda katika kinyang'anyiro cha uwakilishi wa Kamati ya Urithi wa Dunia.

### *5.3.4.3 Shirika la Makumbusho ya Taifa la Tanzania- NMT*

**214. Mheshimiwa Spika,** Shirika la Makumbusho ya Taifa la Tanzania lina jukumu la kuhifadhi, kutafiti, kuendeleza na kuelimisha jamii kuhusu urithi wa utamaduni na wa asili wa Taifa. Vilevile, Shirika linasimamia na kuendeleza vituo saba (7) vya Makumbusho ya Taifa na maeneo 107 ya malikale yaliyopo sehemu mbalimbali Tanzania Bara.

**215. Mheshimiwa Spika,** Shirika limeimarisha uhifadhi wa malikale kwa kutekeleza hatua mbalimbali za kulinda, kukarabati na kuboresha miundombinu ya maeneo ya urithi wa Taifa. Katika jitihada hizo, Shirika limejenga nyumba za asili mbili (2) kwa jamii ya Wamasai na kufanya ukarabati wa nyumba za asili 20 kwa Kaya zinazowakilisha jamii mbalimbali ikiwemo Wahehe (1), Wakinga (2), Wabena (1), Wazanaki (3), Wasukuma (1), Wanyakyusa (2), Wamwera (2), Wasafwa (2), Wabembe (2), Wangoni (3) na Wamakua (1) katika Kijiji cha Makumbusho. Pia, ukarabati wa majenzi ya kale 17 umefanyika katika maeneo ya Mbuamaji (10), Majimaji (5) na Mikindani (2).

**216. Mheshimiwa Spika,** Shirika limeendelea kuimarisha tafiti

za malikale na makumbusho ili kuongeza mikusanyo na uelewa kuhusu historia, mila, desturi na urithi wa Taifa. Jumla ya tafiti 18 zimefanyika katika maeneo ya malikale na makumbusho kwa kushirikisha wadau wa uhifadhi na uendelezaji malikale nchini. Kupitia tafiti hizo, machapisho matatu (3) ya kisayansi yameandaliwa na vibali 11 vya utafiti vimetolewa kwa wananchi waliopo maeneo ya Kahama, Mpwapwa, Moshi, Korogwe, Tanga, Morogoro na Bagamoyo. Aidha, Shirika limeratibu warsha mbili (2) za kitafiti kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Chuo Kikuu cha Hannover cha Ujerumani na kusimamia kazi miradi 521 iliyofanywa na wanafunzi wa shule za sekondari 150 zilizopo mikoa ya Dar es Salaam (43), Lindi (20) Arusha (25), Ruvuma (32) na Mara (30).

**217.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha kumbukumbu za Taifa na kuhifadhi ushahidi wa kihistoria, Shirika limeongeza wigo wa uhifadhi wa historia na malikale kwa kukusanya mikusanyo mipya 678 inayohusiana na historia, mila, akiolojia, palaentolojia na biolojia hivyo kufanya idadi ya mikusanyo iliyopo Makumbusho ya Taifa kufikia 628,135. Kati ya mikusanyo hiyo iliyokusanywa, 287 ni noti za kale, 10 ni mikusanyo ya baiolojia, 152 ni mikusanyo ya Paleontolojia, 14 ni mikusanyo kutoka Meli ya Kihistoria ya MV Liemba, 214 ni mikusanyo ya mila. Pia, Shirika lilipokea mkusanyo wa gari moja (1) aina ya Mercedes-Benz iliyotumiwa na Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu, katika kipindi cha pili cha utawala wake (2000-2005).

**218.** **Mheshimiwa Spika,** Shirika limefanya uchambuzi wa mikusanyo 143,693 yenye asili ya Akiolojia na Palaentolojia na kuiorodhesha katika kanzidata. Mikusanyo hiyo imetokana na tafiti zilizofanyika katika maeneo ya Ziwa Eyasi, Ngorongoro, Seronera, Ndutu, Mumba, Kilwa Kisiwani, Mafia Kisimani, Tongoni na Pangani. Aidha, kati ya mikusanyo hiyo iliyochambuliwa, mikusanyo 306 imesajiliwa katika mfumo wa kidijitali wa usimamizi na uhifadhi wa kumbukumbu unaojulikana kama Digital Records and Archives Management Preservation System -DRAMPS unaorahisisha uhifadhi na upatikanaji wa haraka wa taarifa za Malikale.

**219.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha jamii inashiriki

kikamilifu katika uhifadhi wa urithi wa Taifa, Shirika limeratibu na kuendesha mikutano 32 ya wadau wa uhifadhi malikale. Mikutano hiyo ilifanyika katika Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni (5), Nandete (3), Mtwara Mikindani (2), Majimaji Songea (6), Lindi Mjini (3), Tendaguru (2), Arusha (6), Kua Mafia (1), Mbuamaji (1), Pangani (1), Kilimanjaro (1) na Ujiji-Kigoma (1). Aidha, Shirika limewezesha jamii za kitanzania kukutana katika Kijiji cha Makumbusho - Dar es Salaam ili kuenzi na kutunza mila na desturi zao. Jamii tano (5) zikiwemo za Wamasai, Wasambaa, Wabembe, Wafipa na Wanyakyusa zimekutana na kujadili namna ya kuendelea kutunza desturi zao ikiwa ni sehemu ya utalii wa utamaduni. Moja ya mikakati ya jamii hizo ni kuhifadhi na kuenzi utamaduni wa usanifu wa jadi katika ujenzi wa nyumba za asili kwa kaya zao, kufanya matamasha ya jamii zao na kuwasilisha mikusanyo katika Kijiji cha Makumbusho.

**220. Mheshimiwa Spika,** Shirika limeendelea kuhamasisha umma wa watanzania kuhifadhi historia zao na kuzirithisha kutoka kizazi kimoja kwenda kingine. Katika kutekeleza jukumu hilo, Shirika limetoa ushauri kwa Taasisi sita (6) na jamii sita (6) kuanzisha Makumbusho binafsi. Taasisi zilizohamasishwa zinajumuisha; Wizara ya Nishati kuhusu uanzishwaji wa Makumbusho ya historia ya mradi wa Bwawa la kufua Umeme la Mwalimu Julius Nyerere, Mahakama Kuu ya Tanzania kuhusu kuanzisha Makumbusho ya Mahakama, Mkoani Dodoma; Chuo cha Ulinzi cha Taifa kuhusu historia ya Ulinzi nchini, Wilaya ya Maswa kuhusu kuanzisha Makumbusho ya tiba asili katika kijiji cha Bukigi,Wilaya ya Ukerewe kuhusu kuanzisha Makumbusho ya Historia na Utamaduni na Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino kuhusu kuanzisha makumbusho ya historia ya chuo hicho.

**221. Mheshimiwa Spika,** Jamii zilizohamasishwa zinajumuisha jamii ya Wazaramo kuhusu uhifadhi wa historia yao; Tawala za jadi za Ndaskoi, Arusha na Busiya, Shinyanga katika kuhifadhi historia ya tawala zao; Jamii mbili za Mkoani Kilimanjaro katika kuendeleza uhifadhi kupitia makumbusho za utamaduni. Aidha, katika kuimarisha hilo, Shirika limeandaa Mwongozo wa kitaalamu wa uanzishaji Makumbusho nchini.

**222. Mheshimiwa Spika,** katika kuelimisha jamii na

kuhamasisha watalii wa ndani na nje ya nchi kutembelea Makumbusho, Shirika limekamilisha Onesho Jipya la kudumu la ndege ya kwanza ya Serikali aina ya Jet, Fokker-28-5H-CCM iliyotumiwa na Marais wa nchi kwa Awamu Tano kuanzia mwaka 1978 hadi 2018. Vile vile, Shirika limeandaa na kuendesha maonesho ya muda ya kimakumbusho 10 yaliyotembelewa na wageni 102,420 yakiwemo Onesho la Fahari ya Tanzania katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba); Onesho la Picha za Msanii Doreen Mandawa msanii Maarufu raia wa Scotland alieishi Tanzania kwa miongo 5 akifundisha na kukuza kizazi cha wasanii wa uchoraji; Onesho la mapishi ya asili ya kitanzania Cke Patch Picnic Tourism in Museum; Onesho la Chakula cha asili cha Japani I Love Sushi kwa ushirikiano na Serikali ya Japan; Onesho la historia ya ujezi wa reli ya TAZARA kwa kushirikiana na Makumbusho ya Taifa la China kupitia Ubalozi wa China nchini; Onesho la Mchango wa Urusi katika Harakati za Ukombozi wa Afrika kwa kushirikiana na Kituo cha Utamaduni cha Ubalozi wa Urusi nchini; na Onesho la Ubunifu 9th Edition of the Day of the Italian Photo Design in the World. Shirika limeshiriki maonesho ya kitalii ya ITB Berline. Aidha, maudhui ya kidijitali matano (5) yameandaliwa na kuwekwa kwenye vifaa vya kidijitali vilivyopo kwenye Onesho la Kudumu la Mwl. Nyerere, Butiama.

**223. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Shirika limeanza maboresho ya mifumo ya kutoa huduma ya kidijitali ambapo linajenga Mfumo Jumuishi wa Huduma za Makumbusho Self Service Portal utakaorahisisha upatikanaji wa huduma kwa wageni. Mfumo huu utatoa huduma nane (8) kwa wageni ambazo ni vibali vya utafiti, viingilio, kupiga picha mnato na mjongeo, huduma ya kufanya utafiti ndani ya makumbusho, huduma ya kuongoza watalii, ukodishaji wa kumbi na maombi ya kuanzisha makumbusho ambapo moduli za Vibali vya utafiti na Viingilio zimekamilika.

**224. Mheshimiwa Spika,** Shirika limeendesha matamasha matatu (3) na matukio sita (6) ya kuhamasisha uhifadhi na utalii wa malikale likiwemo Tamasha la Kumbukizi ya Vita vya Majimaji Songea, Tamasha la Jamii ya Wazaramo katika Kijiji cha Makumbusho na Tamasha la Entabuko Mkoani Kagera. Aidha,

programu 15 za kimakumbusho zimefanyika ikiwemo programu ya Museum Art Explosion, programu kwa wanafunzi wa vyuo vikuu (University Museum Hub) na programu ya simulizi za kimakumbusho (Museum Talk) inayorushwa kupitia mitandao ya kijamii. Vilevile, maudhui za kutangaza mazao ya utalii wa malikale yamerushwa kupitia vipindi 30 vya redio, televisheni (41) na Makala (39) katika mitandao ya kijamii. Pia, programu 61 za uhamasishaji zimefanyika katika shule za sekondari zilizopo Mkoa wa Dar es Salaam (30), Arusha (6), Ruvuma (11), Mara (8) na Mtwara (6) ikiwemo ushiriki wa Mikutano ya Wakuu wa Shule za Sekondari (TAHOSSA), Shule za Msingi (TAPSHA) na Chama cha Walimu (CWT). Kupitia matamasha na programu hizi watu 116,015 wamefikiwa na kupata elimu kuhusu uhifadhi, matumizi endelevu ya malikale na kujenga uzalendo.

Aidha, Katika kuenzi urithi wa Mwalimu Nyerere shirika limeadhimisha Siku ya Mwalimu Nyerere na Siku ya Azimio la Arusha, pia limeanzisha mashirikiano na Taasisi mbalimabali kwa ajili ya kutekeleza programu mbalimbali ikiwepo Kituo cha Urithi wa Harakati za Ukombozi, Taasisi ya Mfuko wa Mwalimu Nyerere, Chuo cha Uongozi cha Mawalimu Nyerere, Jasiri Arts.

**225.** **Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine Shirika limepata fursa ya kuweka Onesho la kudumu ndani ya meli ya MV Liemba linaloelezea historia ya meli hiyo katika kukuza biashara na uchumi katika ukanda wa Ziwa Tanganyika na historia ya jamii ya watu wa Kigoma. Hatua hiyo, itawezesha abiria wanaosafiri na meli hiyo kupata fursa ya kufanya utalii wa Malikale kwa kutembelea onesho hilo na kupata historia adhimu. Aidha, onesho hili ni zao jipya la utalii wa meli hususan katika masuala ya Malikale na Makumbusho. Kwa upande mwingine, Shirika linaendelea na utekelezaji wa mradi wa Makumbusho ya Marais, Dodoma ambapo usanifu wa michoro na makadirio ya gharama za awali za ujenzi wa Makumbusho umefanyika.

**226.** **Mheshimiwa Spika,** katika kufungua utalii wa malikale kwenye Mikoa ya Kusini mwa Tanzania, Shirika linaendelea na ujenzi wa Kituo cha Kumbukumbu na Taarifa eneo la Nandete-Kilwa, Mkoani Lindi mahali ambapo vita vya Majimaji vilianzia mwaka 1905 na kuenea katika mikoa mingine. Hatua hii, inalenga

kuweka taarifa sahihi za mnyororo wa historia ya vita hiyo na kutumika kama zao la utalii tangu vilipoanza, maeneo vilipofanyika hadi vilipohitimishwa mwaka 1907 Mkoani Ruvuma. Ujenzi wa kituo hicho umefikia asilimia 76 na unatarajiwa kukamilika Julai 2026. Aidha, Shirika kwa kushirikiana na Jeshi la Wananchi wa Tanzania limekamilisha Ujenzi wa Kituo cha Kumbukumbu na Taarifa kilichopo Songea katika eneo ambalo mashujaa 67 wa vita vya Majimaji walinyongwa. Kituo hicho kinatumiwa na Baraza la Mila na Desturi za Mkoa wa Ruvuma kwa ajili ya kufungamanisha utalii wa malikale na utamaduni. Vilevile, kazi ya uboreshaji wa Sanamu 12 za mashujaa wa vita vya Majimaji zilizopo katika viwanja vya Makumbusho ya Majimaji, Songea unaendelea ambapo kukamilika kwake kutatoa tafsiri halisi ya taswira za mashujaa hao na mchango wao katika kuasisi ukombozi wa Taifa la Tanzania.



*Ujenzi wa Jengo la Kituo cha Kumbukumbu ya Vita vya Majimaji - Nandete, Kilwa.*

### *5.3.5 Utekelezaji wa Masuala Mtambuka*
### Kuimarisha Utendaji wa Wizara (Utawala na Rasilimaliwatu)

**227. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa kwa kutekeleza Awamu ya Nne ya Mpango wa Taifa wa Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa ulioandaliwa na Wizara. Aidha, Wizara imeendeleza jitihada za kupambana na kudhibiti rushwa kwa kuwahimiza watumishi kutoa huduma kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, taratibu, maadili ya utumishi wa Umma, uwajibikaji pamoja na utekelezaji wa majukumu wakizingatia Mkataba wa Huduma kwa Mteja. Sambamba na hilo, Wizara imetoa elimu kwa watumishi kuhusu rushwa na maadili ambapo jumla ya watumishi 3064 wamepatiwa mafunzo.

**228. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuratibu upatikanaji wa watumishi kulingana na mahitaji ambapo katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara imeajiri watumishi 1140 wa kada mbalimbali na watumishi 96 walihamia kutoka taasisi mbalimbali. Aidha, Wizara imewawezesha watumishi 3153 kupata mafunzo ambapo watumishi 546 walipatiwa mafunzo ya muda mrefu, watumishi 1879 kupata mafunzo ya muda mfupi na watumishi 728 kupata mafunzo ya jeshi la uhifadhi. Mafunzo hayo yamekusudiwa kuwajengea uwezo watumishi kumudu majukumu yao kwa ufanisi zaidi, kupata sifa za kimuundo ili kuwawezesha kupata sifa za kupanda vyeo pamoja na kuwaandaa watumishi wanaotarajia kustaafu kwa kuwapa elimu ya ujasiriamali itakayowawezesha kumudu maisha baada ya kustaafu. Vilevile, watumishi 1589 wa kada mbalimbali wamepandishwa vyeo.

**229. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kushiriki katika mapambano dhidi ya VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY) kwa kuwahudumia watumishi waliojiweka wazi kwa kuwapa posho maalum kwa ajili ya lishe bora na kuwahudumia watumishi wenye ulemavu. Aidha, Wizara inaendelea kutoa vifaa kinga kwa watumishi wa Wizara na kuwaelimisha kuhusu umuhimu wa kutunza afya zao kupitia vipeperushi na vikao rasmi vya Wizara. Mathalan, watumishi 4170 wamepatiwa mafunzo ya afya ya akili, VVU na UKIMWI.

**230. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutoa stahili za watumishi kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo. Aidha, katika kutekeleza azma ya Serikali ya kufanya mazoezi mahala pa kazi. Vilevile, Wizara imeendelea kutekeleza mwongozo huo unaolenga kuimarisha afya za watumishi kwa kushiriki michezo mbalimbali ikiwemo michezo ya SHIMIWI iliyofanyika Mkoani Mwanza Oktoba, 2025; SHIMMUTA iliyofanyika Mkoani Morogoro Novemba, 2025 pamoja na Bunge Marathon 2026. Vilevile, Wizara ilishiriki katika michezo ya maadhimisho ya Mei Mosi iliyofanyika Kitaifa Aprili, 2026 mkoani Njombe. Katika mashindano hayo, Wizara ilishinda kombe moja (1) na medali saba (7). Ushiriki wa Michezo hiyo umekuwa chachu ya kuhamasisha watumishi kufanya mazoezi ya viungo, kuimarisha afya na kupunguza hatari ya kupata magonjwa yasiyoambukiza.

**231. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maliasili na Utalii imeendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi kwa kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi kwa watumishi ikiwemo ukarabati wa nyumba 183 za watumishi, ununuzi wa magari 76 na ununuzi wa samani mbalimbali za ofisi.

### *5.4 Miradi ya Maendeleo*

**232. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara iliidhinishwa **Shilingi 82,286,546,000.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ya Wizara na Taasisi. Fedha hizo zinajumuisha **Shilingi 32,476,051,000.00** fedha za ndani na **Shilingi 49,810,495,000.00** fedha za nje. Aidha, fedha za Maendeleo zinajumuisha **Shilingi 34,348,073,903.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali chini ya Wizara na **Shilingi 47,938,472,097.00** za Miradi inayotekelezwa na Taasisi za TANAPA, TAWA, TFS, TTB, TAWIRI, TAFORI, NMT, NCT, BTI, FTI na FITI. Hadi kufikia Aprili 2026, Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 46,860,039,339.02** sawa na **asilimia 56.95** ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 11,995,880,728.30** ni fedha za ndani na **Shilingi 34,864,158,610.72** ni fedha za nje. Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa ni kama ifuatavyo: -

**(i) *Mradi wa Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (Public Finance Management and Reform Programme VI)***

**233. Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma Awamu ya Sita (PFMRP VI) ni mradi wa ubia wa maendeleo baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Benki ya Dunia. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 jumla ya **Shilingi 977,476,764.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi mbalimbali za mradi. Hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya **Shilingi 756,705,180.00** zimetolewa ambazo ni sawa na asilimia 77.4 ya fedha zilizoidhinishwa. Kazi zilizofanyika ni pamoja na: kujenga na kusambaza Mfumo wa Faru kwa ajili ya ubadilishanaji wa taarifa kwa kukusanya na kuandaa mahitaji ya usanifu wa mfumo. Aidha, ujenzi wa mfumo na uandaaji wa nyaraka za matumizi unaendelea.

**(ii) *Mradi wa Kuendeleza Utalii Kusini mwa Tanzania Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za ndani***

**234. Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unatekelezwa katika maeneo Kusini mwa nchi zikiwemo Hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba na Misitu ya Asili. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, mradi ulitengewa jumla ya **Shilingi 18,682,561,593.00** kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili 2026, jumla ya **Shilingi 4,193,570,732.88** zimepokelewa na kutumika, ikiwa ni sawa na asilimia 22.4. Katika utekelezaji wa miundombinu ya kimkakati, mradi unaendelea na ukamilishaji wa jengo la Kituo cha Utangazaji Utalii Kusini mwa Tanzania (Southern Tanzania Destination Marketing Center) katika eneo la Kihesa Kilolo – Iringa, ambapo ujenzi umefikia asilimia 69.



*Ujenzi wa jengo la Kituo cha Utangazaji Utalii Kusini mwa Tanzania, Kihesa Kilolo-Iringa.*

**(iii) *Mradi wa Kukabiliana na Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara (Combating Poaching and Illegal Wildlife Trade in Tanzania)***

**235. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) inatekeleza Mradi wa kupambana na ujangili na biashara haramu ya nyara unaofadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira (Global Environmental Facility – GEF). Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, jumla ya **Shilingi 2,586,276,000.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi mbalimbali. Hadi Aprili 2026, jumla ya **Shilingi 1,324,079,000.00** zimetolewa ambazo ni sawa na asilimia 51.2 ya fedha iliyoidhinishwa. Baadhi ya kazi zilizofanyika ni pamoja na kuwezesha mafunzo ya uchunguzi wa kisayansi (forensic investigation) kwa maafisa 34 (28 wa kiume na Sita (6) wa kike) kutoka Kikosi Kazi Taifa Dhidi ya Ujangili (NTAP), Idara ya Wanyamapori, Kanda 10 za Ki-Ikolojia za Kuratibu Doria (TCGS) na Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu; Kuwezesha doria tatu (3) za ushirikiano (concurrent operations) kati ya Tanzania na Zambia katika mpaka wa Tunduma – Nakonde, na doria mbili kati ya Tanzania na Kenya katika eneo la mpaka kwenye mifumo ikolojia ya Serengeti – Mara pamoja na Tsavo – Mkomazi.

**236. Mheshimiwa Spika,** mradi pia umewezesha mafunzo ya matumuzi ya mifumo ya kubadilishana taarifa za uhalifu (Wildlife Trade Information System -WiTIS) na EAC-TWIX kwa maafisa wa

Wizara na Kanda 10 za kiikolojia za kuratibu doria (TCGS) na kuwaunganisha na maafisa wengine kutoka Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na DRC ili kubadilishana taarifa kupitia mitandao husika. Aidha, mradi umewezesha mafunzo kwa maafisa 81 (74 wa kiume na saba (7) wa kike) kutoka Idara ya Wanyamapori na TCGs kuhusu usimamizi wa maeneo ya uhalifu ulipofanyika, uchambuzi wa uhalifu wa kimitandao pamoja na namna ya kuchukua sampuli kwa ajili ya uchunguzi wa kisayansi; Kuwezesha maandalizi ya Mpango wa Kanda wa Usimamizi wa Rasilimali (Resource Zone Management Plan) ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Jamii -Ikungi; Kuwezesha mafunzo kwa Bodi ya Udhamini ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori Chamwino ili kuwajengea uwezo kuhusu utekelezaji wa majukumu yao; na kuwezesha doria za ki-intelijensia katika Mfumo Ikolojia wa Katavi/Rukwa, Selous Kusini na Burigi Biharamulo.

**(iv)** ***Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi na Mafunzo ya Misitu na Ufugaji Nyuki (Capacity Building in Forestry and Beekeeping)***

**237.** **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mradi wa kujenga Uwezo wa Taasisi za Mafunzo ya Misitu na Ufugaji Nyuki uliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 570,403,992.00** fedha za ndani. Hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya **Shilingi 100,000,000.00** zimetolewa sawa na asilimia 17.53 kwa ajili kuanza ujenzi wa maabara ya kisayansi kwenye Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora. Aidha, ujenzi wa maabara hiyo umeanza na umefikia asilimia 20.

**(v)** ***Programu ya Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Nyuki (Support to Beekeeping Value Chain Programme - BEVAC)***

**238.** **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Umoja wa Ulaya. Mradi unatekelezwa katika Mikoa ya Singida, Katavi, Tabora, Shinyanga na Kigoma kwa upande wa Tanzania Bara na Mkoa wa Pemba kwa upande wa Zanzibar. Hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya **Shilingi 1,842,401,666.00** zilizoidhinishwa zimepokelewa na kutumika sawa na asilimia 100 ya fedha

iliyoidhinishwa. Shughuli zilizotekelezwa ni: kukamilisha ujenzi wa bweni la wasichana lenye uwezo wa kulaza wanafunzi 148 pamoja na ununuzi wa samani (vitanda, meza na viti) katika Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki, Tabora. Vilevile, mradi umewezesha ununuzi wa vifaa vya maabara awamu ya pili kwa ajili ya Maabara ya Kitaifa ya Utafiti wa Nyuki - Njiro; kujenga vituo vitatu (3) vya kukusanyia asali katika Wilaya za Uyui na Urambo Mkoa wa Tabora pamoja na Itigi Mkoa wa Singida; kujenga uzio na kuweka matenki ya maji vituo tisa (9) vya kukusanyia asali katika wilaya za Ushetu, Sikonge, Kaliua, Urambo, Uyui, Itigi, Tanganyika, Nsimbo na Mlele; kugawa mizinga ya nyuki 2,755 kwa halmashauri za wilaya 15 za Tanzania Bara ambapo mradi unatekelezwa na mizinga ya nyuki 500 kwa Wilaya ya Chakechake, Mkoani, Wete na Micheweni- Pemba.

**239.** **Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, mradi umewezesha wakufunzi wawili (2) wa Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki, Tabora kushiriki mafunzo ya tiba ya nyuki (Apitherapy) yaliyotolewa na Taasisi ya Apitherapy Consulting & Trading International Ltd nchini Romania. Vilevile, mradi umewezesha mapitio ya mtaala wa Skuli ya Kilimo ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar na hivyo kujumuisha kozi ya msingi ya ufugaji nyuki kwenye Shahada ya Kilimo inayotolewa na Chuo hicho. Mradi umewezesha Taasisi ya Utafiti Zanzibar (ZALIRI) kufanya utafiti juu ya maadui na visumbufu vya nyuki; kuwezesha TAFORI kufanya utafiti kwa ajili ya kuandaa Itifaki Sanifu za Kuhifadhi Makoloni ya Nyuki Wasiouma nchini Tanzania; na kuandaa mwongozo wa utalii wa nyuki (Apitourist's Guide Book) unaoeleza maeneo ambayo utalii wa nyuki unaweza kufanyika nchini.

**240.** **Mheshimiwa Spika**, kwa lengo la kuwezesha wafugaji nyuki kuwa na maeneo rasmi ya kufugia nyuki, mradi umewezesha uanzishwaji wa hifadhi za nyuki 35 za vijiji (hifadhi 28 kwa Tanzania Bara na 7 Pemba) zenye ukubwa wa hekta 94,960 zikijumuisha hekta 11,835 za uoto wa vichaka vya Itigi. Pia, mradi umewezesha uanzishwaji wa ukanda wa kufugia nyuki wenye ukubwa wa hekta 474,288.06 ndani ya Hifadhi ya Msitu Kigosi. Katika hatua nyingine, Mradi umewezesha mapitio ya Kanuni za Jumla za Ufugaji Nyuki za Mwaka 2005 pamoja na kuchapisha nakala ngumu 20,300 za miongozo inayohusu ufugaji nyuki.

**241. Mheshimiwa Spika**, kwa lengo la kuendelea kuwajengea uwezo wadau wa sekta binafsi wanaojishughulisha na sekta ya ufugaji nyuki, mradi umewezesha maandalizi ya mipango ya biashara kwa vituo tisa (9) vya kukusanyia asali vilivyopo Wilaya za Ushetu, Sikonge, Kaliua, Uyui, Itigi, Urambo, Tanganyika, Nsimbo na Mlele; kuwezesha makampuni matatu (3) kuanza taratibu za kupata alama ya ubora ya TBS; kuwezesha makampuni mawili (2) na vyama vya ushirika sita (6) kuanza mchakato wa kupata cheti cha uuzaji wa asali mahuluku (Organic Certificate) kinachotambulika katika masoko ya kimataifa; na viwanda sita (6) vya kuchakata asali kupata cheti cha uthibiti wa ubora wa chakula (HACCP). Vilevile, mradi umewezesha mafunzo kwa wafanyabiashara 30 kuhusu mbinu za utafutaji wa masoko ya asali kimataifa. Kwa upande mwingine, mradi umekamilisha ujenzi wa Kituo cha kuuzia mazao ya nyuki kilichopo Wilaya ya Wete-Pemba Kaskazini pamoja na kukarabati jengo la kituo cha kuchakata mazao ya nyuki cha SIDO-Singida pamoja na kununua mashine za kuchakata asali.

**(vi) *Mradi wa Usimamizi wa Mifumo ya Chakula, Matumizi Bora ya Ardhi na Urejeshaji wa Uoto wa Asili Tanzania (Food Systems, Land Use and Restoration in Tanzania's Landscapes – FOLUR)***

**242. Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatekelezwa kupitia ufadhili wa Mfuko wa Mazingira Duniani (Global Environmental Facility – GEF). Mradi una lengo la kukuza usimamizi jumuishi wa rasilimali za ardhi, maji na misitu nchini na unatekelezwa katika kongani ya Kilombero kwa upande wa Tanzania Bara na Kaskazini A na B kwa upande wa Zanzibar. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 jumla ya **Shilingi 3,664,636,331.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi. Hadi kufikia Aprili 2026, **Shilingi 2,269,282,506.92** zimetolewa na kutumika sawa na asilimia 62. Baadhi ya kazi zilizofanyika ni pamoja na kununua magari matatu (3) kwa ajili ya shughuli za mradi; kuandaa mipango ya urejeshaji na uongoaji wa maeneo yaliyoharibiwa ya misitu saba (7) ya Vijiji vya Rufulu (1), Udagaji (1), Ching'anda (1), Chisano (2), Mgugwe (1) and Merera (1) iliyoko katika Halmashauri ya Mlimba; Mipango ya urejeshaji saba (7) katika Misitu inayosimamiwa na Jamii ya

Tumbatu – Jiongoe na Kinyasini pamoja na misitu inayosimamiwa na Serikali ambayo ni misitu ya Kiwengwa na Chaani na misitu ya mikoko iliyoko Mkokotoni, Bumbwini na Fungurefu – Zanzibar. Aidha, mradi umefanikiwa kutoa Hati za Kimila za umiliki wa Ardhi (CCRO) 485 na kuandaa mipango mitatu (3) ya matumizi ya ardhi katika vijiji vya Luvirikila, Isago na Mkangawalo vilivyoko Halmashauri ya Mlimba.

**243.** **Mheshimiwa Spika,** mradi huu umewezesha kukamilika kwa Mwongozo wa uzalishaji wa zao la mpunga pamoja na utoaji wa mafunzo ya mbinu bora na za kisasa za uzalishaji wa mpunga kwa Maafisa Ugani 21 kutoka Halmashauri za Mlimba na Maafisa Ugani 20 kutoka Zanzibar. Pia, mafunzo kama hayo, yametolewa kwa Wakulima Viongozi (Lead farmers) 46 kutoka Halmashauri ya Mlimba na 38 kutoka Wilaya ya Kaskazini A na B Zanzibar ikiwa ni pamoja na kuanzisha mashamba darasa matatu (3) ya zao la mpunga katika Halmashauri ya Mlimba na mawili (2) Zanzibar. Vilevile, Mradi umeanzisha na kuwezesha jukwaa la Wadau (Multisectoral Platform – MSP) lenye lengo la kuwaleta pamoja wadau wote wa usimamizi wa rasilimali jumuishi za maji, ardhi na misitu ili kujadili na kuimarisha uhifadhi katika Wilaya ya Kaskazini A na B Zanzibar.

**(vii)** ***Mradi wa Kusimamia Uhifadhi wa Misitu, Matumizi Bora Ardhi na Kuongeza Thamani ya Mazao ya Misitu (Forest, Land Use and Value Chain Development Tanzania – FORLAND)***

**244.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Ufini inatekeleza Mradi wa Kusimamia Uhifadhi wa Misitu, Matumizi bora Ardhi na Kuongeza Thamani ya Mazao ya Misitu. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Jumla ya **Shilingi 4,001,200,000.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi. Hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya **Shilingi 3,550,762,336.04** zimepokelewa na kutumika sawa na asilimia 89. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: ununuzi wa magari mawili (2) kwa ajili ya shughuli za mradi; kuboresha mtambo wa kukaushia mbao uliopo katika Kituo cha Mafunzo ya Misitu na Viwanda vya Misitu (FWITC); kuanzisha mashamba ya miti ya mfano katika shule tano (5) katika Mkoa wa Njombe (woodlots) ambapo jumla ya miche ya

miti 5,000 ilipandwa; kutoa elimu ya upandaji miti kwa wanafunzi 629 na walimu 15 katika Mkoa wa Iringa na Njombe; kuwezesha usimamizi wa mashamba ya mfano ya mbegu bora za miti yanayomilikiwa na jamii pamoja na kuvuna mbegu za aina ya Pinus maximinoi (kilo 300), Tecunumanii (kilo 25) na Pinus Oocarpa (kilo 5). Hatua hii inawezesha jamii kuwa na uhakika wa kupata mbegu bora za miti kutoka katika mashamba yao.

**245. Mheshimiwa Spika**, mradi umetoa mafunzo kuhusu masuala ya jinsia, watu wenye mahitaji maalum na ujumuishaji wa makundi mbalimbali ya jamii, mazingira na bioanuai, pamoja na mafunzo ya tathmini na ufuatiliaji kwa wafanyakazi wa ugani na washirika 200 wa utekelezaji wa mradi katika Halmashauri 19 kwenye Mikoa ya Njombe, Iringa, Ruvuma, Dodoma na Lindi. Aidha, jumla ya maafisa ugani 37 na wakufunzi wa FWITC walipata mafunzo ya usimamizi shirikishi wa kukabiliana na moto. Vilevile, kupitia mradi huu tani 30 za magogo ya mbao ya aina 10 za mbao zisizojulikana (lesser-known timber) kwa ajili ya kutengeneza bidhaa za mbao ili kupanua wigo wa matumizi ya mbao zaidi ya Mninga na Mkongo zimenunuliwa. Sambamba na hilo, mradi umewezesha ununuzi wa vifaa vya uvunaji wa mbegu za miti katika mashamba yenye jumla ya hekta 210 katika Mikoa ya Iringa, Njombe na Ruvuma; na kuwezesha mafunzo ya usimamizi wa rasilimali za misitu na mnyororo wa thamani wa mazao hayo kwa maafisa misitu 20 kutoka katika Mikoa ya Njombe, Iringa, Ruvuma na Lindi. Pia, mradi umewezesha kufanyika kwa tathmini ya soko la venia ili kubaini changamoto na namna bora ambayo nchi inaweza kunufaika zaidi kupitia zao hilo.

**(viii)** ***Mradi wa Kujenga Uwezo na Kuimarisha Chuo Cha Taifa Cha Utalii (The National College of Tourism Capacity Building and Institutional Strengthening)***

**246. Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatekelezwa na Serikali kwa kutumia fedha za ndani. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, mradi uliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,654,595,091.00** fedha za ndani kwa ajili ya ujenzi wa jengo la taaluma katika Kampasi ya Arusha. Hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya **Shilingi 1,239,384,648.35** zimepokelewa na kutumika sawa na asilimia 75. Mradi huo kwa sasa umefikia asilimia 92 ya utekelezaji.

(ix) *Miradi ya TANAPA*

**247.** **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Shirika limeendelea kutekeleza miradi mbalimbali kwa kutumia fedha za nje ambapo miradi iliyotekelezwa ni pamoja na Mradi wa Msaada wa Dharura wa Urejeshaji wa Bioanuai Tanzania; Mradi wa Maendeleo na Uhifadhi wa Mfumo wa Ikolojia wa Serengeti awamu ya kwanza na ya pili; na Mradi wa Uhifadhi wa Ikolojia ya Hifadhi za Taifa za Katavi, Mahale na Ushoroba wa Uunganishi. Miradi hii yote inafadhiliwa na Serikali ya Ujerumani kupitia benki ya maendeleo ya KfW ambapo hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya **Shillingi 16,686,284,857.00** zilitumika sawa na asilimia 90 ya **Shilingi 18,489,000,000.00** zilizotengwa.

**248.** **Mheshimiwa Spika,** kupitia mradi wa msaada wa dharura wa urejeshaji wa bioanuai nchini Tanzania (ERB), shughuli mbalimbali zimefanyika ikiwa ni pamoja na ununuzi wa magari ya doria nane (8) ambayo kwa sasa yako bandarini pamoja na ununuzi wa ndege moja aina ya Cessna 206 iliyowasili nchini mwezi Machi 2026. Aidha, mradi umewezesha kugharamia shughuli za doria za askari kwa kutumia magari na ndege, ikijumuisha ununuzi wa sare, mafuta ya magari na ndege, pamoja na matengenezo ya magari 79 (Serengeti 51 na Nyerere 28). Vilevile, mifumo mipya ya nishati imewekwa katika eneo la Seronera, ukarabati wa karakana moja (1), Ujenzi wa mifumo ya kukusanya na kuchakata taka ngumu, Hifadhi ya Taifa Serengeti, visima viwili (2) vya maji vimechimbwa katika vituo vya askari na kisima kipya cha mafuta kimejengwa katika Hifadhi ya Taifa Nyerere. Mradi pia umewezesha kuondolewa kwa mimea vamizi katika eneo la jumla ya hekta 3,055 na kusimikwa mitego ya mbung'o 2,000 katika Hifadhi ya Taifa Nyerere. Aidha, uwekaji wa mfumo wa mawasiliano ya redio katika Hifadhi ya Taifa Nyerere umefikia asilimia 95 ya utekelezaji. Kupitia mradi huu, wananchi 7,923 wamepata elimu ya uhifadhi, na vikundi 15 vya shughuli za kiuchumi katika Wilaya za Busega, Meatu na Itilima vimewezeshwa na kuendelezwa.

**249.** **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Maendeleo na Uhifadhi wa Mfumo wa Ikolojia wa Serengeti (SEDCP I) - Awamu ya Kwanza umetekeleza Miradi ya ukarabati wa barabara za

mchepuko yenye urefu wa kilomita 77 (Serengeti km 31 pamoja na box culvert 5, na Ngorongoro km 46) imekamilika na kukabidhiwa kwa TARURA na Halmashauri husika. Ukarabati mkubwa wa Kituo cha Taarifa kwa Wageni Seronera (SVIC) unaotekelezwa na Mkandarasi DF Mistry unaendelea na unatarajiwa umekamilika Aprili 2026. Jumla ya miradi ya kijamii 58 (SCIPs) inaendelea kutekelezwa katika wilaya za Serengeti na Ngorongoro. Miradi 15 iliyotekelezwa na Mkandarasi DF Mistry imekamilika na kukabidhiwa. Miradi 14 Serengeti na 11 Ngorongoro iliyotekelezwa na Mkandarasi Humphrey imekamilika na ipo katika kipindi cha matazamio (DLP) hadi Agosti 2026. Miradi 18 ya Ujirani Mwema chini ya Mkandarasi OSAKA ipo katika hatua za ukamilishaji. Aidha, utekelezaji wa miradi nane (8) ya mabwawa ya maji kwa matumizi ya binadamu na mifugo katika Wilaya za Serengeti na Ngorongoro unaendelea.

**250.** **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Maendeleo na Uhifadhi wa Mfumo wa Ikolojia ya Serengeti (SEDCP II): Mradi huu ulihusisha tafiti za topografia na hidrojia kwa ajili ya ujenzi wa Daraja la Kogatende pamoja na ukamilishaji wa usanifu na makisio ya gharama za utekelezaji. Aidha, ulijumuisha ukarabati wa Ofisi za Fort Ikoma, uchimbaji wa visima na uwekaji wa mifumo ya uvunaji wa maji ya mvua. Mchakato wa kupata wakandarasi wa miradi ya Daraja la Kogatende na Ofisi za Fort Ikoma umekamilika na taarifa kuwasilishwa TANAPA na KfW kwa hatua za idhini. Maandalizi ya awali ya miradi ya maji, ikiwemo tafiti na nyaraka za zabuni, yamekamilika na kujumuishwa katika mpango wa manunuzi Awamu ya Pili.

**251.** **Mheshimiwa Spika,** Pia, mradi umefanikisha ukamilishaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika Vijiji 18 vya Wilaya za Bariadi, Tarime na Bunda. Jumla ya mawe ya mipaka 1,080 na mabango 300 yamewekwa pamoja na kuandaliwa na kukabidhi vyeti 3,014 vya haki za kimila za ardhi (CCROs). Aidha, vikundi 66 vya COCOBA vyenye wanachama 1,294 katika vijiji 33 vimeanzishwa na kupatiwa mafunzo ya ufugaji nyuki. Vilevile, mizinga ya nyuki 350 imenunuliwa na kugawiwa kwa vikundi vya COCOBA ili kuimarisha shughuli za kiuchumi za jamii.

**252.** **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Uhifadhi wa Ikolojia ya

Hifadhi za Taifa za Katavi, Mahale, na Ushoroba wa Uunganishi (KAMACO): Kupitia mradi huu, mradi umefanikisha kununua magari matano (5) (Hifadhi ya Taifa Mahale - 2 na Hifadhi ya Taifa Katavi - 3), engine boat 3, ujenzi wa jengo la utawala na kuendelea kusaidia uzoeshaji wa sokwe na kuondoa mimea vamizi kwenye eneo lenye ukubwa wa ekari 218 katika Hifadhi ya Taifa Mahale; kuanza ujenzi wa nyumba 10 za watumishi katika Hifadhi ya Taifa Katavi; na madarasa 10, zahanati tatu (3) na nyumba za watumishi wanne (4) katika Wilaya ya Uvinza na Tanganyika. Vilevile, mradi umefanikiwa kununua vitendea kazi mbalimbali ikiwemo Mahema 18, kompyuta 17 na simu za kukusanyia taarifa 26.

**253.** **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa shughuli za kijamii mradi umeendelea kukamilisha mipango bora ya matumizi ya ardhi katika Vijiji 23, kuanzisha na kusimamia vikundi 194 vya COCOBA, kusimika mabango 121 katika maeneo mbalimbali ya vijiji vya Lagosa, Ndele na Igalula ambayo yamefanyiwa mipango bora ya matumizi ya ardhi, kupeleka mafunzo VGS 50, kuweka vigingi 22 katika eneo la mpaka kati ya Hifadhi ya Taifa Katavi na Kijiji cha Kabage na kutoa hati miliki za kimila 2084 katika vijiji vya Sibwesa na Kaseganyama.

**(x)** ***Miradi ya TAWA***

**254.** **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mamlaka ilidhinishiwa kutumia kiasi cha **Shilingi 12,004,877,017.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo kiasi cha **Shilingi 7,487,896,003.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 4,516,981,014.00** fedha za nje. Hadi Kufikia Aprili 2026, jumla ya **Shilingi6,563,178,511.89** zimepokelewa ambapo **Shilingi 1,217,248,255.41** ni fedha za nje na **Shilingi 5,345,930,256.48** ni fedha za ndani.

**255.** **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo: Ujenzi wa barabara yenye kilomita 20 kati ya kilomita 30 katika Pori la Akiba Mpanga Kipengere umekamilika; Ujenzi wa vizimba vinne (4) katika Wilaya za Bunda (1), Buchosa (2) na Sengerema (1) umekamilika; Uwekaji wa mageti madogo sita (6) ya kukusanya mapato katika Mapori Tengefu Mto wa Mbu na

Ziwa Natron umekamilika; Ujenzi wa barabara yenye kilomita 35 kati ya kilomita 65 katika Pori la Akiba Wamimbiki umekamilika; Ujenzi wa barabara yenye Kilomita 11 kati ya Kilomita 30 katika Pori a Akiba Pande umekamilika; Ujenzi wa vivuko 68 kati ya vivuko 96 katika Pori la Akiba Selous-Kingupira umekamilika; na Upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa madaraja mawili (2) katika Pori la Akiba Selous umekamilika.

## 6.0 MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**256. Mheshimiwa Spika,** Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 umezingatia miongozo mbalimbali ikiwemo: Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027; Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050; Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/2027 - 2030/2031); Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2025; Sera na Sheria mbalimbali; Mpango Mkakati wa Wizara wa Mwaka 2026/2027 - 2030/2031; maagizo mbalimbali ya Viongozi Wakuu wa Serikali; Maoni na Ushauri wa Kamati za Kudumu za Bunge pamoja na Mikataba ya Kikanda na Kimataifa.

**257. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara itatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maeneo ya vipaumbele kama ifuatavyo: -

i. Kuimarisha utangazaji wa utalii ndani na nje ya nchi kwa kutumia mikakati mahsusi ya masoko (market-driven strategies), hususan katika masoko ya kimkakati na mapya ikiwemo Mashariki ya Mbali na Mashariki ya Kati;

ii. Kuendeleza na kuboresha mazao ya utalii ya kimkakati ikijumuisha utalii wa meli, mikutano na matukio (MICE), fukwe, michezo, anga na tiba pamoja na kutambua na kusajili mazao mapya yatakayopanua wigo wa fursa za uwekezaji, ajira na mapato;

iii. Kuimarisha miundombinu wezeshi katika maeneo ya utalii na hifadhi ikiwemo barabara, viwanja vya ndege, mawasiliano na huduma za kijamii;

iv. Kuimarisha ulinzi, uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori, misitu, nyuki na malikale kwa kuimarisha ushiriki wa jamii, kupunguza migongano ya binadamu na wanyamapori, kukabiliana na ujangili na kuzuia uharibifu wa mazingira;

v. Kuimarisha uzalishaji, uongezaji thamani na masoko ya mazao ya misitu na nyuki kwa kuzingatia usimamizi endelevu wa rasilimali, ili kuongeza mchango wa sekta katika uchumi wa Taifa, kukuza ajira na kipato cha jamii;

vi. Kuimarisha matumizi ya teknolojia za kisasa katika usimamizi wa rasilimali, ulinzi, ufuatiliaji, ukusanyaji wa mapato, pamoja na utangazaji wa utalii;

vii. Kufanya mapitio ya sera, sheria, kanuni na miongozo ili kuendana na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kiteknolojia, kuimarisha mazingira rafiki kwa uwekezaji;

viii. Kuimarisha Utafiti, Ubunifu na Maendeleo ya Rasilimaliwatu kwa kuratibu masuala ya utafiti na ubunifu, kuimarisha taasisi za mafunzo na kujenga uwezo wa watumishi na wadau wa sekta kwa lengo la kuongeza utaalam, tija na uendelevu wa sekta ya maliasili na utalii; na

ix. Kuboresha mazingira ya kazi, mifumo ya usimamizi wa utendaji na uwajibikaji ili kuongeza motisha kwa watumishi, ubora wa huduma kwa wananchi na thamani ya fedha za umma.

### 6.1 *Ukusanyaji wa Maduhuli*

**258.** **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara inakadiria kukusanya maduhuli ya **Shilingi 1,486,502,065,176.69** kutoka kwenye Idara na Taasisi zake.

### 6.2 *Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo*

**259.** **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027,

Wizara inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi 334,345,870,000.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 272,044,425,000.00** zitagharamia Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 62,301,445,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha Mishahara **Shilingi 144,691,490,000.00** na Matumizi Mengineyo **Shilingi 127,352,935,000.00.** Fedha za Miradi ya Maendeleo zinajumuisha **Shilingi 23,134,770,000.00** fedha za ndani na **Shilingi 39,166,675,000.00** fedha za nje.

**260.** **Mheshimiwa Spika**, fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 272,044,425,000.00** zinajumuisha **Shilingi 32,605,599,383.00** kwa ajili ya Wizara na **Shilingi 239,438,825,617.00** kwa ajili ya taasisi zilizo chini ya Wizara. Kati ya fedha za Wizara, **Shilingi 10,267,106,968.00** ni Mishahara na **Shilingi 22,338,492,415.00** ni Matumizi Mengineyo. Fedha za taasisi zinajumuisha **Shilingi 134,424,383,032.00** za Mishahara na **Shilingi 105,014,442,585.00** za Matumizi Mengineyo.

### 6.3 *Kazi zitakazotekelezwa na Wizara na Taasisi zake*

#### 6.3.1 *Sekta ya Wanyamapori*

**261.** **Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Wanyamapori ina jukumu la kuhifadhi, kusimamia, kutoa mafunzo pamoja na kufanya tafiti kuhusu rasilimali za wanyamapori ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa. Majukumu haya yanatekelezwa na Wizara kupitia Idara ya Wanyamapori na Taasisi za uhifadhi ambazo ni Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania (TWPF), Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Afrika - Mweka (CAWM), Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori - Pasiansi (PWTI) pamoja na Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii - Likuyu Sekamaganga (CBCTC).

##### 6.3.1.1 *Mikakati ya Utatuzi wa Migongano baina ya Binadamu na Wanyamapori*

**262.** **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027,

Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kusimamia Utatuzi wa Migongano baina ya Binadamu na Wanyamapori wa Mwaka 2025/2026 - 2035/2036. Kazi zitakazotekelezwa na Wizara kupitia Taasisi zake ni pamoja na kujenga vituo 30 vya askari; kujenga vizimba 72 katika maeneo yenye changamoto ya mamba na viboko; na kuchimba mabwawa 30 kwenye maeneo ya hifadhi.

**263.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara itaendelea kutumia teknolojia katika kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu kwa kununua ndege nyuki 100, visukuma mawimbi 100 kwa ajili ya ufuatiliaji wa mienendo ya wanyamapori, mabomu baridi 50,000 na virushio 252, magari 11 ya doria na kukamilisha ununuzi wa helikopta mbili (2) kwa ajili ya kuimarisha ulinzi na udhibiti wa wanyamapori wakali na waharibifu.

**264.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara itakamilisha ujenzi wa uzio wa umeme wenye urefu wa kilomita 53 katika Hifadhi ya Taifa Serengeti kutoka Tabora B hadi Mto Mara (km 38) na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro (km 15) kutoka shamba la Acacia Hills Limited (Mang'ola juu) hadi kijiji cha Makhoromba kitongoji cha Endawishi. Vilevile, Wizara itajenga uzio wa umeme wenye urefu wa kilomita 99 kutoka Kijiji cha Ming'ong'wa hadi Mto Guya Kijiji cha Ihusi (km 84) katika mpaka wa Pori la Akiba Maswa na kutoka Loduare kuelekea Mbulumbulu (km 15) katika mpaka wa Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro.

**265.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara itaendelea kushirikisha jamii katika utatuzi wa migongano baina ya binadamu na wanyamapori kwa kuwajengea uwezo Askari Wanyamapori wa Vijiji (VGS) 500 katika Halmashauri za Wilaya 50; kutoa mafunzo ya Mfumo wa PAIS kwa Maafisa Ugani 612 wa Halmashauri za Wilaya 51; na kutoa elimu kuhusu mbinu rafiki za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu kwa wananchi katika Halmashauri za Wilaya 112. Sambamba na hilo, Wizara itaendelea kulipa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi watakaoathirika na matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu kwa mujibu wa Kanuni za Kifuta Jasho na Kifuta Machozi za mwaka 2011 na marejeo yake ya mwaka 2024.

**266. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi na kuongeza uwajibikaji, Wizara itaanzisha Kituo cha Huduma kwa Wateja kitakachowezesha wananchi kuwasilisha kwa urahisi malalamiko, maoni, ushauri na taarifa mbalimbali zinazohusu huduma za sekta hii ikiwemo changamoto za wanyamapori wakali na waharibifu, shughuli za utalii, uhifadhi wa maliasili na malikale. Hatua hii inalenga kuimarisha mawasiliano kati ya Serikali na wananchi, kuongeza ufanisi katika utatuzi wa changamoto kwa wakati pamoja na kuwezesha utoaji wa msaada wa haraka ili kulinda maisha ya wananchi, mali zao na kuendelea kujenga imani ya wananchi kwa Serikali yao. Aidha, kituo hicho kitakuwa dirisha muhimu la kupokea mrejesho wa wananchi na wadau kwa lengo la kuendelea kuboresha huduma na maendeleo ya utalii na uhifadhi.

***6.3.1.2 Idara ya Wanyamapori***

**267. Mheshimiwa Spika**, Idara ya Wanyamapori ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za uhifadhi wa rasilimali za wanyamapori nchini. Katika kuimarisha ulinzi na uhifadhi wa wanyamapori, Wizara kupitia Taasisi zake za Uhifadhi itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kupambana na Ujangili wa Mwaka 2023 - 2033 kwa kufanya doria za Kanda za Kiikolojia (TCGs) na kuwezesha doria maalum za Kikosi Kazi cha Taifa Dhidi ya Ujangili (NTAP) zinazoongozwa na taarifa za kiintelijensia ili kuvunja mitandao ya ujangili. Aidha, Wizara itafanya mapitio ya Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori Sura ya 283 na Kanuni zake kwa lengo la kuimarisha uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori.

**268. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha ushiriki wa jamii katika uhifadhi, Wizara itaendelea kuwezesha uanzishaji wa Jumuiya nne (4) za Hifadhi za Wanyamapori (WMA) za MAWIMA (Uvinza), MANYARU (Kilolo), Kipamba (Mkalama), na JUHIZINA (Longido); na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya uendeshaji wa shughuli za Jumuiya 10 za Hifadhi za Wanyamapori. Aidha, Wizara itaendelea kujenga uwezo kwa WMA mpya na zilizopo kwa kuziwezesha vitendea kazi ikiwemo pikipiki 15 kwa ajili ya kuimarisha ulinzi wa wanyamapori. Vilevile, Wizara itaendelea kuandaa miongozo mbalimbali kwa ajili ya kutatua changamoto za usimamizi wa WMAs nchini.

**269. Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, Wizara itaendelea kutekeleza Mikataba ya Kikanda na Kimataifa (CBD, CITES, AEWA, ETIS, MIKE, LATF, RAMSAR, SADC, CMS, EAC, AU) ambayo Tanzania imeridhia; kuandaa Mkutano wa 24 wa Jukwaa la Uhifadhi wa Wanyamapori Barani Afrika utakaofanyika nchini mwezi Novemba 2026 unaotarajiwa kuwa na washiriki zaidi ya 200 na kutekeleza programu ya ufuatiliaji wa uwindaji wa Chui na Simba ikiwa ni utekelezaji wa Mkataba wa CITES. Aidha, Wizara itatoa elimu ya uhifadhi na mbinu rafiki za kukabiliana na matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu; kuadhimisha Siku ya Wanyamapori Duniani na Siku ya Askari wa Wanyamapori Duniani; kutatua migogoro ya mipaka kati ya maeneo ya hifadhi; na kukamilisha tathmini ya Mapori Tengefu 23 kwa lengo la kujiridhisha kama bado yana sifa za kiikolojia na kuendelea kuwa na hadhi hiyo.

#### 6.3.1.3 *Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania – TWPF*

**270. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Mfuko utaendelea kuwezesha utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Migongano Baina ya Binadamu na Wanyamapori (2025/2026 - 2035/2036) kwa kuziwezesha Taasisi za TANAPA, TAWA, NCAA na TAWIRI kujenga vizimba (30); kuchimba mabwawa (5); kujenga vituo (10) vya askari; kununua vitendea kazi mbalimbali ikiwemo visukuma mawimbi (40), ndege nyuki (50), mabomu baridi (35,000) na virushio (200) vya mabomu baridi. Aidha, Mfuko utawezesha fedha kwa ajili ya mafunzo kwa Askari Wanyamapori wa Vijiji (VGS) 100 kutoka Halmashauri za Wilaya 10 kwa ajili ya kuimarisha udhibiti wa wanyamapori wakali na waharibifu; na mafunzo ya Mfumo wa PAIS kwa Maafisa Ugani 612 wa Halmashauri za Wilaya 51 kwa ajili ya kuwajengea uwezo katika ukusanyaji na uwasilishaji wa taarifa za matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu. Vilevile, Mfuko utanunua pikipiki (43) za Maafisa Wanyamapori wa Wilaya ili kuimarisha udhibiti wa wanyamapori wakali na waharibifu.

**271. Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Mfuko utawezesha fedha za ujenzi wa uzio wa umeme wenye urefu wa

kilomita 99 kutoka Kijiji cha Ming'ong'wa hadi Mto Guya Kijiji cha Ihusi (km 84) katika mpaka wa Pori la Akiba Maswa na kutoka Loduare kuelekea Mbulumbulu (km 15) katika mpaka wa Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Vilevile, Mfuko utawezesha tafiti za kimkakati za utatuzi wa migongano baina ya binadamu na wanyamapori pamoja na Miradi inayoendelea ya Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI); Ujenzi wa Mradi wa Bweni la wanafunzi katika Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori, Pasiansi; Ujenzi wa Maktaba ya Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka; kukamilisha ujenzi wa nyumba mbili (2) za watumishi, ujenzi wa bweni na kukamilisha ukarabati wa bweni, darasa, bwalo na jengo la utawala katika Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii - Likuyu Sekamaganga. Hatua hizo zimelenga kuimarisha uwezo wa taasisi husika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**272.** **Mheshimiwa Spika**, katika hatua nyingine, Mfuko utaendelea kuwezesha utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Ujangili wa Mwaka (2023-2033). Katika kutekeleza mkakati huo, Wizara itaendelea kufanya doria za kuzuia na kupambana na ujangili na biashara haramu ya nyara na mazao ya misitu, kukusanya taarifa za intelijensia kuhusu wahalifu na mitandao yao, kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa kesi za makosa ya wanyamapori na misitu na kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika kukabiliana na ujangili na biashara haramu ya nyara zinazovuka mipaka ya nchi. Vilevile, Mfuko utawezesha uanzishaji wa Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori (WMAs); uratibu na usimamizi wa Mikataba ya Kikanda na Kimataifa ambayo Tanzania imeridhia; na uratibu wa Matumizi Endelevu ya Rasilimali za Wanyamapori. Kazi nyingine zitakazowezeshwa ni pamoja na kutoa elimu ya uhifadhi kupitia matukio ya Kitaifa na Kimataifa nchini; utatuzi wa migogoro ya mipaka baina ya vijiji na maeneo ya hifadhi; ufuatiliaji wa utekelezaji wa masuala ya Kisera, Sheria na Miongozo mbalimbali ya Serikali kuhusu rasilimali za wanyamapori nchini; na kuandaa Mkakati wa Ustahimilivu wa Mfuko Kifedha.

#### 6.3.1.4 *Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania – TANAPA*

**273.** **Mheshimiwa Spika,** Shirika lina jukumu la kulinda na

kuhifadhi wanyamapori, mimea, na mifumo ya ikolojia katika Hifadhi za Taifa ili kuhakikisha uhifadhi endelevu; usimamizi na uendelezaji wa utalii endelevu kwa kusimamia na kukuza shughuli za utalii na malikale kwa kuzingatia ubora wa huduma, usalama wa wageni na uhifadhi wa mazingira.

**274.** **Mheshimiwa Spika,** Shirika litaendelea kuimarisha ulinzi wa rasilimali za wanyamapori na mifumo ya ikolojia katika hifadhi za Taifa kwa kufanya jumla ya doria 51,058. Aidha, Shirika litaimarisha ulinzi wa faru kwa kuweka alama kwa faru 73 katika Hifadhi za Taifa Serengeti (53) na Mkomazi (20); na kuendelea na ukarabati wa uzio wa faru katika Hifadhi ya Taifa Mkomazi pamoja na uwekaji wa mifumo ya kisasa ya ulinzi na ufuatiliaji wa ikolojia katika Hifadhi za Taifa Serengeti na Mkomazi. Vilevile, Shirika litapanua uzio wa boma la faru katika Hifadhi za Taifa za Mkomazi na kujenga uzio mpya wa boma la faru katika Hifadhi ya Taifa Burigi-Chato. Sambamba na hilo, Shirika litakamilisha ununuzi wa helikopta moja (1) na ndege nyuki 20 kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika shughuli za doria na ufuatiliaji wa mienendo ya wanyamapori wakali na waharibifu. Pia, Shirika litajenga chumba cha kuratibu mawasiliano (control room) na kufunga mfumo wa redio katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kwa ajili ya kuboresha mawasiliano. Ili kuimarisha ulinzi na kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu, Shirika litakamilisha ujenzi wa vituo sita (6) vya askari katika wilaya za Mbarali, Kalambo, Bariadi, Bunda, Serengeti na Kilwa na kujenga vituo saba (7) katika hifadhi za Taifa Ibanda-Kyerwa (1), Mto Ugalla (2), Mikumi (1), Rumanyika-Karagwe (1), Ziwa Manyara (1) pamoja na Wilaya ya Karagwe (1).

**275.** **Mheshimiwa Spika**, katika kutatua migongano baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu, Shirika litaendelea kuimarisha upatikanaji wa maji kwa wanyamapori ili kuwezesha wanyamapori kutumia muda mwingi ndani ya hifadhi kwa kuchimba mabwawa 20 katika hifadhi za Taifa Katavi (5), Nyerere (3), Mikumi (3), Serengeti (5), Saadani (1), Ruaha (1), na Mkomazi (2). Aidha, Shirika litachimba visima virefu saba (7) katika Hifadhi za Taifa Mkomazi (2), Tarangire (3) na Mto Ugalla (2). Vilevile, Shirika litaondoa mimea vamizi katika eneo lenye ukubwa wa hekta 4,889.17 ili kuongeza nyanda za malisho kwa

wanyamapori katika Hifadhi za Taifa Kitulo (5), Rumanyika-Karagwe (25), Ziwa Manyara (720), Kisiwa cha Rubondo (101.17), Milima Udzungwa (33.9), Saadani (120), Katavi (60), Nyerere (2000), Mikumi (150), Arusha (283.3), Kilimanjaro (20), Gombe (5), Mto Ugalla (40), Burigi-Chato (60), Tarangire (25), Ibanda-Kyerwa (22.8), Saanane (18), Serengeti (100), Mkomazi (400) Milima ya Mahale (300) na Ruaha (400). Sambamba na hilo, Shirika litafunga visukuma mawimbi kwa tembo 20 viongozi wa makundi katika hifadhi za Taifa Mikumi (2), Ruaha (3), Mkomazi (2), Tarangire (2), Burigi-Chato (2), Serengeti (2), Mto Ugalla (2), Nyerere (3) na Kilimanjaro (2) kwa ajili ya kufuatilia mienendo yao.

**276.** **Mheshimiwa Spika**, Shirika litajenga vizimba 21 vya kuzuia mamba katika wilaya za Bunda (3), Busega (3), Namtumbo (2), Liwale (1), Ulanga (1), Rufiji (1), Chato (2), Uvinza (2), Kyerwa (4), Morogoro (1) na Pangani (1). Vilevile, Shirika litaendelea kutoa elimu ya uhifadhi na mbinu za kukabiliana na wanyamapori kwa jamii zinazozunguka maeneo ya hifadhi ambapo jumla ya mikutano 4,500 inatarajia kufanyika. Pia, Shirika litawezesha mafunzo kwa askari wa vijiji (VGS) 100 ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa kwa ajili ya kutekeleza mbinu za kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu. Halikadhalika, Shirika litanunua mabomu baridi 5,000 kwa ajili ya kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu.

**277.** **Mheshimiwa Spika**, katika kuendelea kuimarisha ushiriki wa jamii katika uhifadhi, Shirika litaendelea kutekeleza sera ya ujirani mwema kwa kutoa elimu ya uhifadhi, kuanzisha na kutekeleza mahitaji ya huduma za kijamii kwa wananchi wanaoishi pembezoni mwa Hifadhi. Shirika litawezesha utekelezaji wa miradi ya ujirani mwema inayoanzishwa na jamii ambayo ni pamoja na ujenzi wa bwawa la samaki Mpanda; ujenzi wa bwawa la kunyweshea mifugo katika wilaya ya Kondoa; vizimba vinne (4) vya samaki katika wilaya ya Nyamagana (1) na Chato (3); ujenzi wa zahanati katika wilaya ya Kigoma na ukamilishaji wa zahanati tatu (3) katika wilaya za Karagwe, Bunda na Tarime; ujenzi wa choo cha matundu mawili (2) katika zahanati ya Arumeru; nyumba za madaktari 2 katika wilaya za Karatu na Bunda; ujenzi wa mabweni katika shule za sekondari tatu (3) wilaya za Chunya, Kyerwa na Namtumbo; ujenzi wa vyoo vyenye

matundu 28 katika shule za msingi tatu (3) wilaya za Rungwe (8), Karatu (12) na Simanjiro (8); kufunga mfumo wa gesi ya kupikia katika shule saba (7) za sekondari katika wilaya za Siha (1), Moshi (3), Longido (1) na Rombo (1).

**278.** **Mheshimiwa Spika,** vilevile, Shirika litajenga madarasa tisa (9) katika wilaya za Kyerwa (2), Tarime (2), Kilosa (2) na Handeni (3); nyumba mbili (2) za walimu katika wilaya za Simanjiro na Babati; ofisi mbili (2) za vijiji katika Wilaya za Simanjiro na Kilombero; uzio wa shule ya sekondari katika Wilaya ya Same; na kituo cha Polisi katika Wilaya ya Uvinza na kukamilisha ujenzi wa jengo la kutengenezea dawa katika Wilaya ya Mpanda. Pia, Shirika litakarabati madarasa mawili (2) Wilaya ya Hai; kutoa madawati 400 kwa shule nne (4) za sekondari katika wilaya za Kaliua (2) na Urambo (2) pamoja na kuchimba kisima kirefu cha maji katika Wilaya ya Mkinga.

**279.** **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha huduma za utalii, Shirika litaendelea kuboresha miundombinu ya utalii ili kuongeza ubora wa huduma kwa watalii na kuvutia wageni zaidi. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa barabara mpya za utalii zenye urefu wa kilomita 252 katika Hifadhi ya Taifa Nyerere (200), Ibanda-Kyerwa (37) na Mto Ugalla (15). Vilevile, Shirika litafanya ukarabati wa barabara za utalii zenye urefu wa kilomita 4,301 katika Hifadhi za Taifa Nyerere (200), Milima ya Udzungwa (42), Arusha (20), Kilimanjaro (24), Ziwa Manyara (249), Mkomazi (60), Tarangire (200), Katavi (473), Kitulo (20), Ruaha (310), Burigi-Chato (2,000), Ibanda-Kyerwa (51), Milima ya Mahale (5), Rubondo (20), Serengeti (517) na Mto Ugalla (110).

**280.** **Mheshimiwa Spika,** Shirika litaboresha miundombinu ya utalii kwa kujenga barabara ya kilomita 6.69 ya tabaka gumu ili kuunganisha lango kuu la Hifadhi ya Taifa Tarangire na barabara ya lami eneo la Kibaoni. Ujenzi wa njia mpya za watalii zenye urefu wa kilomita 55 utafanyika katika Hifadhi za Taifa Milima ya Udzungwa (45) na Mto Ugalla (10). Aidha, Shirika litafanya ukarabati wa njia za watalii zenye urefu wa kilomita 227 katika Hifadhi za Taifa Milima ya Udzungwa (70), Arusha (7), Kilimanjaro (51), Ziwa Manyara (35), Katavi (54) na Milima ya Gombe (10). Vilevile, Shirika litafanya ukarabati wa maeneo 10 ya kupumzikia

wageni katika Hifadhi za Taifa Nyerere (4), Kilimanjaro (3) na Serengeti (3).

**281.** **Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Shirika litajenga nyumba mpya nne (4) za kupumzikia wageni katika Hifadhi za Taifa Arusha (1), Ibanda-Kyerwa (2), Kisiwa cha Rubondo (1) pamoja na ukarabati wa nyumba 36 za kupumzikia wageni katika hifadhi za Taifa Nyerere (2), Saadani (7), Gombe (3), Kisiwa cha Saanane (3), Kisiwa cha Rubondo (8) na Serengeti (14). Aidha, Shirika litajenga vyoo vipya 10 katika Hifadhi za Taifa Nyerere (1), Milima ya Udzungwa (1), Saadani (1), Arusha (1), Kilimanjaro (6) pamoja na ukarabati wa vyoo 19 katika Hifadhi ya Taifa Serengeti. Vilevile, Shirika litafanya ukarabati katika viwanja vya ndege 17 katika Hifadhi za Taifa Nyerere (4), Tarangire (2), Katavi (1), Milima ya Mahale (1), Kisiwa cha Rubondo (1), Serengeti (7) na Mto Ugalla (1).

**282.** **Mheshimiwa Spika,** katika kukuza utalii wa Malikale, Shirika litafanya usanifu na kutekeleza awamu ya kwanza ya ujenzi wa Kituo cha Makumbusho ya Mwl. Nyerere katika Eneo la Magomeni, Jijini Dar es Salaam na kufanya ukarabati wa vituo vya malikale ikiwemo Caravan Serai (Bagamoyo), Isimila (Iringa), Dr. Livingstone (Kigoma) na Fort Ikoma (Serengeti). Vilevile, Shirika litaendelea kutangaza fursa za uwekezaji katika maeneo 72 ya uwekezaji kwenye hifadhi za Taifa Mikumi (2), Nyerere (42), Ruaha (21) na Saadani (7) kulingana na mpango wa ujumla wa hifadhi husika.

**283.** **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha mifumo ya ukusanyaji mapato pamoja na kuboresha huduma kwa wageni, Shirika litaweka malango janja 15 katika Hifadhi za Taifa Serengeti (8), Manyara (1), Arusha (2), Mkomazi (2), Mikumi (1) na Tarangire (1); na kujenga malango mapya matatu (3) katika Hifadhi za Taifa Nyerere, Saadani na Rumanyika-Karagwe. Katika kuboresha huduma na kuimarisha mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi, Shirika litakarabati nyumba 195 katika Hifadhi za Taifa Nyerere (75), Saadani (4), Kilimanjaro (10), Manyara (12), Mkomazi (14) Milima ya Gombe (23), Milima ya Mahale (18), Kisiwa cha Rubondo (39) na Ofisi (2) za Kanda ya Kaskazini (1) na Hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Saanane (1).

**284.** **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha mikakati ya kutangaza vivutio vilivyopo ndani ya hifadhi za Taifa pamoja na kukuza taswira ya nchi kama kitovu cha utalii duniani, Shirika litashiriki matukio ya Kimataifa ikiwemo IFTM – Top Resa (Paris), My Tanzania Road Show – Southern Europe, ITB Berlin, WTM London, Qatar Travel Mart, FITUR – Spain, Outbound Travel Mart (OTM India), Indaba Africa – Afrika ya Kusini pamoja na Magical Kenya Travel Expo. Aidha, Shirika litashiriki matukio ya kitaifa yakiwemo maonesho ya Sabasaba, Nanenane, Karibu KILIFAIR, Karibu Kusini, Great Ruaha Marathon, Serengeti Marathon, Mkutano wa IPU na Shangwe la Sikukuu na TANAPA. Matukio haya ya kitaifa na kimataifa yataendelea kutumika kama majukwaa muhimu ya kutangaza vivutio vilivyopo pamoja na fursa za uwekezaji zinazopatikana katika Hifadhi za Taifa.

**285.** **Mheshimiwa Spika**, Shirika litaanzisha mradi wa kurusha matangazo ya moja kwa moja awamu ya kwanza katika Hifadhi ya Taifa Serengeti; kuendelea kutumia TANAPA Go App kwa ajili ya watalii kupata taarifa za vivutio vilivyopo hifadhini na namna ya mtalii kufika katika hifadhi. Taarifa hizo zinapatikana kwenye mfumo huo kupitia lugha Kiswahili, Kiingereza, Kijerumani, Kispaniola, Kichina na Kirusi; kuendelea kutumia mitandao ya kijamii; na vyombo vya habari vikiwemo Televisheni ya Taifa (TBC), ZBC, ITV, Pori TV, Global TV, Azam TV, Millard Ayo, Mwananchi, Channel 10, Clouds TV, Wasafi TV, Imani TV, Star TV na Safari channel. Vilevile, Shirika litaendelea kutumia Redio ya Taifa (TBC), Redio One, Clouds FM, Redio Free Afrika, Wasafi Redio, Abood Redio, Redio Kwizera, Redio Maria na Redio Imani ili kuhamasisha wananchi kutembelea Hifadhi za Taifa kwa wingi.

**286.** **Mheshimiwa Spika**, kuelekea mashindano ya mpira wa miguu Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), Mkutano wa Umoja wa Mabunge Duniani (Inter Parliamentary Union - IPU) na Mashindano ya Ulimbwende "Miss World 2027", Shirika linaendelea na uboreshaji wa miundombinu ya utalii ndani ya hifadhi za Taifa kwa kuboresha barabara, viwanja vya ndege, maeneo ya kupumzikia wageni, njia za milimani pamoja na huduma za mtandao wa intaneti katika hifadhi za Taifa Serengeti, Kilimanjaro, Arusha, Ziwa Manyara, Tarangire, Mikumi, Saadani, Milima Udzungwa na Nyerere kwa lengo la kurahisisha

watalii kufika hifadhini, kuongeza uzoefu wa watalii na siku za kukaa hifadhini. Aidha, Shirika limepanga kuweka matangazo ya vivutio vya utalii kwa kuweka mabango katika Jiji la Dar es salaam, Arusha na Zanzibar. Vilevile, Shirika litatoa matangazo katika maeneo ya kimkakati hususan viwanja vya ndege vya Arusha, Dar es Salaam na Kilimanjaro, kumbi za mikutano za AICC na JNICC na viwanja vya mpira vya Arusha na Dar es Salaam. Halikadhalika, Shirika limepanga kufanya vipindi maalum kwenye vyombo vya habari na kutumia mitandao ya kijamii kutangaza vivutio vya utalii katika hifadhi za Taifa. Pia Shirika limepanga kufanya kampeni kidijitali za kutangaza vivutio vya hifadhi za Taifa, kutumia watu maarufu nchini kwa ajili ya kufanya matangazo yenye kuhamasisha watalii nchini na nje ya nchi kutembelea Hifadhi za Taifa.

**287.** **Mheshimiwa Spika**, sambamba na hilo, Shirika limejipanga kurusha matangazo ya moja kwa moja "Live streaming" kutokea Hifadhi ya Taifa Serengeti kwa kutumia gari maalum litakalokuwa linachukua matukio makubwa ya kuvutia ikiwamo tukio la uhamaji wa Nyumbu. Aidha, Shirika litaweka matangazo kwenye mabasi ya mwendo kasi na treni ya SGR. Vilevile, litashiriki maonesho na misafara ya watalii "road shows" za kimkakati kwenye nchi za Afrika zitakazo shiriki michezo ya AFCON kwa lengo la kutangaza nchi yetu kama "Destination Tanzania" kwa wageni wa AFCON na kuongeza mwamko wa kimataifa kuhusu vivutio vinavyopatikana nchini. Halikadhalika, Shirika kwa kushirikiana na wadau wa sekta binafsi limepanga kuongeza maeneo ya malazi yatakayoongeza idadi ya vitanda 714 ndani ya hifadhi hasa zilizo karibu na maeneo ambayo michezo ya AFCON inafanyika.

**288.** **Mheshimiwa Spika**, Shirika litawezesha mafunzo kwa watumishi 1,213 ambapo mafunzo ya muda mrefu yatatolewa kwa watumishi 63 na mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 234. Aidha, watumishi 400 wa ajira mpya watapatiwa mafunzo ya ulinzi kwa ajili ya kuwaandaa kufanya kazi kwenye Hifadhi za Taifa. Vilevile, watumishi 516 watapatiwa mafunzo ya uongozi ili kuwaongezea ujuzi na kuboresha utendaji kazi.

### 6.3.1.5 *Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania – TAWA*

**289. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ina jukumu la kusimamia rasilimali za wanyamapori nje ya maeneo ya Hifadhi za Taifa na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro ili kudhibiti ujangili, uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa na biashara haramu ya nyara sambamba na kusimamia na kuendeleza utalii kwa manufaa ya jamii zinazozunguka maeneo ya hifadhi na Taifa kwa ujumla.

**290. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Mamlaka itaendelea kudhibiti ujangili na biashara haramu ya nyara kwa kufanya doria 19,228. Aidha, Mamlaka itanunua boti tatu (3) kwa ajili ya kuimarisha doria katika maeneo yenye maziwa, mito na ardhioevu. Vilevile, Mamlaka itaendelea kuimarisha mwitikio wa haraka katika kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu kwa kununua magari nane (8), kujenga vituo 14 vya askari katika wilaya za Madaba (1), Liwale (1), Kilwa (1), Chunya (1), Bariadi (1), Chalinze (1), Chunya (1), Longido (1), Ngorongoro (1), Ulanga (1), Nachingwea (1), Kisarawe (1), Simanjiro (1), na Kongwa (1); kujenga vizimba 15 vya kudhibiti mamba katika Halmashauri za wilaya za Bunda (3), Buchosa (2), Sengerema (2), Kilosa (2), Busega (2), Ukerewe (1), Lindi Vijijini (1), Nkasi (1) na Nyasa (1); kuchimba mabwawa nane (8) katika Mapori ya Akiba Rungwa (2), Lwafi (1), Ugalla (1), Ikorongo (1), Liparamba (1), Msanjesi (1) na Swagaswaga (1); na kununua mahema 500 ya doria, ndege nyuki (drones) 10 na visukuma mawimbi (GPS Satellite Collars) 10; mabomu baridi 5,000 na virushio vya mabomu baridi (launchers) 22.

**291. Mheshimiwa Spika**, sambamba na hilo, Mamlaka itaendelea kuwatumia Askari Wanyamapori wa Vijiji (VGS) 187 kutoka Wilaya 37 katika doria za mwitikio wa haraka na kuwezesha mafunzo kwa VGS 100. Aidha, Mamlaka itajenga uzio wa umeme wenye urefu wa kilomita 84 katika mpaka wa Pori la Akiba Maswa kutoka Kijiji cha Ming'ong'wa hadi Mto Guya Kijiji cha Ihusi utakaosaidia kudhibiti wanyamapori wasitoke nje ya hifadhi hususan tembo katika vijiji vinavyopakana na Pori hilo. Halikadhalika, elimu ya uhifadhi na namna bora ya kuepuka madhara ya wanyamapori wakali na waharibifu itaendelea

kutolewa kwa wananchi katika Wilaya 59 zinazopakana na maeneo ya hifadhi na maeneo mengine yenye changamoto hiyo.

**292. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha miundombinu ya uhifadhi na utalii, Mamlaka itajenga barabara zenye urefu wa kilomita 184.7 katika Pori la Akiba Rukwa (km 17), Hifadhi ya Wanyamapori Makuyuni (km 22), Pori la Akiba Swagaswaga (km 90) na Pori la Akiba Wami-Mbiki (km 55.7). Sambamba na hilo, Mamlaka itajenga gati dogo kwa ajili ya utalii katika Kisiwa cha Lundo; na kujenga lango moja (1) la utalii, eneo la kupumzikia wageni, kujenga eneo la kutazama wanyamapori (animal observation hide-out) na kambi moja (1) ya utalii katika Hifadhi ya Wanyamapori Makuyuni. Vilevile, Mamlaka itajenga bwawa la kuogelea na miundombinu ya michezo mbalimbali ikiwemo uwanja mdogo wa mpira wa miguu, uwanja wa tenisi, mpira wa wavu, mpira wa kikapu na kujenga eneo la michezo ya watoto katika Pori la Akiba Pande; kujenga kambi moja (1) ya utalii na eneo la kupumzikia wageni na kukarabati eneo la kupumzika wageni katika Pori la Akiba Wami-Mbiki; kujenga uzio wa ukuta wenye urefu wa kilomita 1.5 na njia ya waenda kwa miguu yenye urefu wa kilomita 1.2 katika Bustani ya Wanyamapori Tabora; na kukarabati hosteli katika Pori la Akiba Swagaswaga.

**293. Mheshimiwa Spika,** maboresho ya miundombinu yanayofanyika yanalenga kuiwezesha Mamlaka kunufaika na fursa za matukio makubwa yatakayofanyika nchini ikiwemo Mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani - IPU, World Travel Awards - WTA, Shindano la Mlimbwende wa Dunia na Mkutano wa 24 wa Jukwaa la Uhifadhi wa Wanyamapori Barani Afrika. Aidha, Mamlaka imeainisha maeneo manne (4) ya kimkakati kwa ajili ya kuhamasisha wageni watakaoshiriki kwenye matukio makubwa kutembelea kwenye vivutio hivyo. Maeneo hayo ni Hifadhi ya Wanyamapori Makuyuni, Mapori ya Akiba Pande na Wami - Mbiki pamoja na Magofu ya Kunduchi. Vilevile, Mamlaka itaandaa vifurushi mahsusi vya safari za utalii; kutangaza fursa za uwekezaji kwa Sekta Binafsi kwa ajili ya kuwekeza katika miundombinu ya malazi yenye takriban vitanda 400 katika Hifadhi za Makuyuni (300), Pande (50) na Wami-Mbiki (50); kuendelea

kurajamu (branding); na kutangaza vivutio vya utalii katika miji ambapo matukio hayo yatafanyika sambamba na kuanzisha mazao mapya ikiwemo utalii wa michezo katika maeneo ya hifadhi.

**294.** **Mheshimiwa Spika**, Mamlaka itashiriki katika maonesho ya Kitaifa, Kimataifa na Kikanda kwa lengo la kutangaza fursa za uwekezaji pamoja na utalii wa picha, uwindaji na utalii wa meli - cruise ship tourism. Miongoni mwa maonesho hayo ni Abu Dhabi International Hunting & Equestrian Exhibition (ADIHEX, 2026), Dallas Safari Club, Safari Club International - USA, ITB Berlin, FITUR – Spain, Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba) na Maonesho ya Siku ya Wakulima (Nanenane). Aidha, Mamlaka itaendelea kuandaa na kuhamasisha wananchi kushiriki katika matukio ya utalii wa ndani ikiwemo Funga Mwaka Kijanja na TAWA, Nyamapori Choma Festival, Nyerere Day, Siku ya Utalii Duniani, Siku ya Wanawake Duniani, Siku ya Maporomoko Duniani na Siku ya Wanyamapori Duniani.

**295.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuepusha migogoro ya mipaka kati ya wananchi na maeneo ya hifadhi, Mamlaka itaweka alama za mipaka (maboya 80) katika Pori la Akiba Uwanda na kutengeneza barabara ya mpaka (mkuza) yenye urefu wa kilomita 172 katika Pori la Akiba Inyonga. Aidha, Mamlaka itaendelea kushirikisha jamii katika shughuli za uhifadhi kwa kutoa vibali vya uvuvi kwa wananchi 24,500 katika Mapori ya Akiba Kilombero, Uwanda, Ugalla, Rukwa, Igombe na Luganzo pamoja na kutoa vibali vya ufugaji nyuki kwa wananchi 500 katika Mapori ya Akiba Ugalla na Moyowosi. Vilevile, Mamlaka itaongeza maeneo mapya sita (6) kwa ajili ya uwindaji wa wenyeji ambayo ni Ipembampazi, Kisarawe, Kimbanda, Tunduru/Nalika, Kisungule na Namawe-Magingo hivyo kuwa na jumla ya maeneo nane (8) ya uwindaji wa wenyeji. Ongezeko hili litaongeza wigo wa upatikanaji wa kitoweo kwa wananchi kupitia mabucha ya nyamapori. Sambamba na hilo, Mamlaka inaendelea kufanya tathmini ya maeneo mengine saba (7) kwa lengo la kubaini kama kiikolojia yanaweza kutumika kwa uwindaji wa wenyeji. Halikadhalika, Mamlaka inatarajia kurejesha takriban shilingi Bilioni 17.91 kwa wanufaika wa shughuli za utalii ikiwemo

Halmashauri za Wilaya, vijiji na WMAs ambazo shughuli za utalii zinafanyika.

**296. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka itaendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi kwa kujenga vituo vya burudani na michezo (indoor games) katika Mapori ya Akiba Piti na Kilombero. Aidha, Mamlaka itanunua magari mawili (2); kuanza ujenzi wa jengo la Makao Makuu Jijini Dodoma; kuchimba visima sita (6) vya maji; na ununuzi wa samani za ofisi kwa ajili ya Mapori ya Akiba Kilombero, Rukwa, Ugalla, Inyonga na Magofu ya Kunduchi. Vilevile, Mamlaka itawezesha mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 577 na muda mrefu kwa watumishi 126 pamoja na watumishi kushiriki katika mashindano ya SHIMMUTA.

#### 6.3.1.6 *Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro – NCAA*

**297. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro ina jukumu la kuendeleza uhifadhi wa maliasili na malikale; kuendeleza utalii na kutoa huduma kwa jamii. Aidha, Mamlaka inasimamia na kuendeleza maeneo ya urithi wa kiutamaduni ya mapango ya Amboni, Kimondo cha Mbozi, mabaki ya Engaruka Monduli-Arusha, maeneo ya historia ya zama za mawe Eyasi (Mumba Rock-Shelter) yaliyopo Wilayani Karatu pamoja na Pori la Akiba Pololeti.

**298. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Mamlaka itaendelea kuimarisha ulinzi na uhifadhi wa wanyamapori kwa kufanya doria za kawaida 4,200 na doria za pamoja 12 kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama. Aidha, Ujenzi wa kituo kimoja (1) cha askari katika Eneo la Kakesio; ujenzi wa jiko la kisasa kwenye Kituo cha Mafunzo ya Kijeshi Mlele-Katavi; ukarabati wa vituo (2) vya askari maeneo ya Loduare na Zahanati ya Ngorongoro; na ukarabati wa vituo vitatu (3) vya uangalizi katika ukingo wa kreta. Kwa upande mwingine, Mamlaka itanunua visukuma mawimbi 15 na kufunga kwenye faru 15 ili kuendelea kuimarisha mienendo yao ndani ya Hifadhi. Kwa upande mwingine, Mamlaka itatoa elimu ya uhifadhi kwa jamii ndani na nje ya hifadhi kwa kufanya mikutano 54, kuandaa

vipindi 10 kwa njia ya redio. Hatua hizi zitaimarisha ulinzi na uhifadhi wa wanyamapori na maliasili nyingine ndani ya hifadhi.

**299. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Mamlaka itatekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Migongano Baina ya Binadamu na Wanyamapori wa Mwaka 2025/2026 - 2034/2035 kwa kufanya doria 720 za mwitikio, kujenga uzio wa umeme kutoka lango la Loduare kuelekea Mbulumbulu kilomita 15, vituo vitatu (3) vya askari katika wilaya za Manyoni, Kilosa na Morogoro vijijini, ndege nyuki 10, mabomu baridi 5,000, virushio vya mabomu baridi 30, magari matatu (3), Kununua na kufunga visukuma mawimbi 10, kuchimba mabwawa mawili (2), kujenga vizimba (11) vya kuzuia mamba na kiboko, kutoa mafunzo kwa VGS 100, kutoa elimu kwa wananchi katika Halmashauri za Wilaya nne (4) zinazozunguka eneo la Hifadhi kuhusu uhifadhi na mbinu rafiki za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu, kuwezesha mafunzo ya urubani wa ndege nyuki kwa watumishi 7. Aidha, mamlaka itasafisha mpaka wenye urefu wa kilomita 200 na kuweka vigingi 150 kwa lengo la kuepusha migororo ya mipaka na changamoto ya mioto holela. Hatua hizi zinalenga kupunguza migongano ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu.

**300. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka itaendelea kuboresha nyanda za malisho kwa kuondoa mimea vamizi katika eneo lenye ukubwa wa hekta 1,200. Vilevile, Mamlaka itachoma hekta 8,000 kupitia moto mpango ili kuboresha nyanda za malisho katika maeneo hayo. Katika hatua nyingine, Mamlaka itazalisha jumla ya miche ya miti 100,000 itakayopandwa kwenye eneo la mamlaka na kuigawa kwa wadau mbalimbali na jamii zinazopakana na hifadhi kwa lengo la kuimarisha uoto wa asili. Utekelezaji wa hatua hizi unalenga kuboresha maeneo ya malisho ya wanyamapori pamoja na mazingira kwa ujumla.

**301. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza mapendekezo ya tathmini ya mpango wa matumizi bora ya ardhi katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Mamlaka itashiriki katika utekelezaji wa Mpango wa Makazi Mbadala kwa jamii inayoishi ndani ya hifadhi; kutengeneza mfumo wa kieletroniki kwa ajili ya kusajili na kuhifadhi taarifa za wakazi, makazi na mifugo; kutoa elimu kwa jamii kuhusu mapendekezo ya tathmini ya mpango wa matumizi

bora ya ardhi; na kushirikiana na wadau mbalimbali katika kukamilisha afua za kuweka uwiano wa shughuli za kiuhifadhi na kibinadamu.

**302. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka itaendelea na jukumu la kutoa ufadhili wa ada, fedha za kujikimu na nauli kwa wanafunzi wanaotoka katika jamii inayoishi ndani ya hifadhi. Katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Mamlaka imetenga jumla ya Shilingi 937,482,160 kwa ajili ufadhili wa wanafunzi 978 katika ngazi ya sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu. Sambamba na hilo, Mamlaka itaendelea na ugawaji wa unga na sukari kwa ajili ya uji katika shule 26 za msingi zilizopo ndani ya Hifadhi. Aidha, Mamlaka itawezesha utekelezaji wa miradi ya kijamii katika shule za sekondari ndani ya Hifadhi na maeneo yanayozunguka Hifadhi. Pamoja na hayo, Mamlaka itaendelea na utoaji wa huduma za afya kwa wakazi ndani ya Hifadhi katika zahanati ya Mamlaka. Vilevile, Mamlaka itawezesha mafunzo ya ufugaji nyuki, uongezaji thamani mazao ya nyuki pamoja na masoko kwa vikundi nane (8) vilivyopo ndani ya hifadhi na vinavyozunguka hifadhi. Hatua hizi zinalenga kuimarisha mahusiano na ustawi wa jamii inayoishi ndani ya hifadhi.

**303. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha miundombinu ya utalii, Mamlaka itaendelea na ujenzi wa kilomita 29.5 za barabara ya Loduare hadi Golini kwa kiwango cha tabaka gumu la zege. Aidha, Mamlaka itafanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ufunguaji wa barabara ya Engaruka kupitia Kapenjiro hadi Empakaai yenye urefu wa kilomita 33; na barabara ya Endamagha kupitia Endulen hadi Ndutu yenye urefu wa kilomita 32. Vilevile, Mamlaka itafanya ukarabati wa mtandao wa barabara wenye urefu wa kilomita 368.5 na ukarabati wa viwanja viwili (2) vya ndege vya Ngorongoro na Ndutu. Kwa upande mwingine, Mamlaka itakarabati chanzo cha maji cha Lerai pamoja na uchimbaji wa visima 10 katika maeneo ya Nasera Rock, Garlus, Malambo, Ndorobo, Kiroma, Matiti, Masamburai, Ereko, Sendui na Laetoli. Hatua hizi zitaboresha usafiri na urahisi wa kufikia vivutio vya utalii ndani ya hifadhi na kuongeza mvuto kwa watalii.

**304. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha shughuli za utalii, Mamlaka itaongeza mazao mapya ya utalii yakiwemo kutembea

kwenye madaraja ya kamba juu ya miti (Canopy Walking), kuteleza kwenye waya (Zip line), harusi hifadhini na kupanda mlima (hiking). Aidha, Mamlaka itaboresha njia za watembea kwa miguu katika Eneo la Eyasi kupitia Empakai hadi Nasera. Vilevile, Mamlaka itaanzisha matumizi ya teknolojia ya kuona vivutio kwenye uhalisia kupitia mfumo wa Virtual Reality na kutangaza kupitia mfumo wa mubashara (live streaming). Katika hatua nyingine, Mamlaka itaainisha maeneo mapya ya kupumzikia watalii (Picnic site), utalii wa machweo (Sundowner) na maeneo ya kusimama kwa muda kwa wageni (stop-Over). Pia, Mamlaka itaendelea na mchakato wa ufukuaji wa nyayo za Laetoli pamoja na kutangaza fursa za uwekezaji katika mapango ya Amboni - Tanga kwa lengo la kuboresha maeneo ya mapumziko na maegesho ya magari. Sambamba na hilo, Mamlaka itajenga fensi ya kuzunguka Makumbusho ya Jiopaki ya Ngorongoro - Lengai kwa ajili ya kuimarisha ulinzi. Hatua hizi kwa pamoja zinalenga kuongeza idadi ya watalii na idadi ya siku za watalii kukaa ndani ya hifadhi.

**305. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka itaendelea kutangaza vivutio vya utalii kupitia maonesho 20 ya utalii na uhifadhi ya ndani ya nchi (10) na nje ya nchi (10). Aidha, Mamlaka itashiriki misafara mitatu (3) ya utalii, kampeni tano (5) za ndani za kuhamasisha utalii wa ndani na kuandaa matukio matano (5) ya utalii. Vilevile, Mamlaka itaweka mabango 10 ya kidijitali katika maeneo ya Kiwanja cha ndege Arusha, Dodoma, Njia panda ya Uwanja wa Ndege - KIA, Himo, Namanga, Makuyuni, Morogoro, Zanzibar, Karatu na Mwanza. Aidha, katika kutumia fursa za Mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON, 2027), Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), World Travel Awards (WTA), Shindano la 74 la Ulimbwende Duniani. Mamlaka kwa kushirikiana na wadau, itajenga kambi za muda 30 zitakazo ongeza idadi ya vitanda 900 ndani ya Hifadhi; kuandaa vifurushi maalum vya utalii; kutoa mafunzo maalum ya huduma kwa wateja na ukarimu kwa watumishi; na kuhamasisha wadau kujenga maeneo ya burudani katika eneo la Karatu ili kuwawezesha wageni watakaolala nje ya Hifadhi ya Ngorongoro kuangalia mashindano hayo kabla na baada ya kuingia hifadhini.

**306.** **Mheshimiwa Spika,** katika kulifanya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro kuwa kivutio kikuu cha watalii wengi zaidi nchini Tanzania na barani Afrika (Premium Safari Destination-PSD), Mamlaka itaendelea kuimarisha matumizi ya mifumo ya kidijitali katika kutangaza vivutio vinavyopatikana ndani ya Hifadhi, kuboresha mifumo ya TEHAMA ili kuwawezesha wageni kutumia muda mfupi wakati wa kupata huduma; uundwaji wa mifumo ya kukusanya na kuhifadhi takwimu mbalimbali. Vilevile, Mamlaka itaendelea kutumia mitandao ya kijamii ikiwemo Instagram, YouTube, TikTok, WhatsApp, Thread, na Facebook kutangaza vivutio katika Eneo la Hifadhi. Katika hatua nyingine, Mamlaka itaweka mfumo wa kidijitali katika lango la Loduare kwa ajili ya kukusanya mrejesho wa watalii baada ya kupata huduma ndani ya hifadhi. Jitihada hizi zinalenga kuboresha utoaji wa huduma na kuongeza hadhi ya hifadhi kimataifa.

**307.** **Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi, Mamlaka itawezesha watumishi 35 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 260 kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi. Aidha, Mamlaka itaendelea kuwapa mafunzo ya ulinzi wa rasilimali za wanyamapori na utalii maafisa na askari kwa lengo la kuwajengea uwezo na kuimarisha utendaji kazi pamoja na nidhamu.

#### 6.3.1.7 *Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania – TAWIRI*

**308.** **Mheshimiwa Spika**, Taasisi ina jukumu la kufanya, kuratibu na kusimamia tafiti za wanyamapori nchini kwa lengo la kuishauri Serikali na wadau namna bora ya kusimamia na kuendesha shughuli za uhifadhi na utalii endelevu.

**309.** **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Taasisi itaendelea kufanya tafiti zitakazojikita katika kutatua changamoto za uhifadhi na maendeleo ya utalii, zikiwemo tafiti za kutatua migongano baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu; matumizi ya teknolojia mbalimbali katika uhifadhi; afya za wanyamapori na mifumo ikolojia; nyuki na mazao yake; mahusiano ya viumbe na ikolojia zao; uhifadhi wa bioanuwai; matumizi ya mimea vamizi kama nishati safi na

urejeshwaji wa spishi za wanyamapori zilizotoweka katika mifumo ikolojia mbalimbali. Aidha, Taasisi itafanya sensa ya wanyamapori jamii ya Kanivora kwenye mifumo ikolojia nchini pamoja na kuendelea kufanya ufuatiliaji wa mienendo ya wanyamapori. Vilevile, Taasisi itaendelea kusimamia na kuratibu watafiti waliosajiliwa na wapya ikiwemo ufuatiliaji wa miradi iliyopitishwa pamoja na kupokea maombi mapya.

**310. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha tafiti zinazofanyika zinaleta tija katika uhifadhi na utalii nchini, Taasisi itafanya tathmini ya ufanisi wa mbinu na teknolojia mbalimbali zinazotumika zikiwemo; matumizi ya vizimba vya kudhibiti mamba na viboko; matumizi ya ndege nyuki; matumizi ya mabomu baridi; na matumizi ya mabwawa ya maji na uzio wa umeme. Aidha, Taasisi itaendelea kubuni teknolojia mpya; kufanya tathmini ya maeneo ya kipaumbele kwa ajili ya uzio wa umeme; tathmini ya mahitaji na idadi ya mabwawa nchini na utambuzi wa visababishi na mbinu mahsusi za kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu kikanda.

**311. Mheshimiwa Spika**, sambamba na tafiti katika kupunguza kadhia ya wanyamapori wakali na waharibifu, Taasisi itajenga vizimba 15 katika maeneo mbalimbali yenye changamoto za mamba na viboko; ununuzi na uvalishaji wa visukuma mawimbi (GPS Satellite Collars) 10 kwa ajili ya kufuatilia mienendo ya wanyamapori viongozi wa makundi pamoja na makundi ya tembo yaliyo nje ya maeneo ya hifadhi kwa muda mrefu; na kufanya tafiti mbili (2) za kimkakati za ubunifu wa mbinu mpya kwa ajili ya utatuzi wa migongano baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu. Aidha, Taasisi itaendeleza na kufuatilia mienendo ya makundi ya wanyamapori waliovalishwa visukuma mawimbi nchini.

**312. Mheshimiwa Spika**, pamoja na kufanya tafiti, Taasisi ina jukumu la kusambaza matokeo ya utafiti kwa watumiaji. Katika kufanikisha hilo, Taasisi itasambaza matokeo ya tafiti kwa Mamlaka za Uhifadhi, wadau wa uhifadhi na utalii kwa njia mbalimbali ikiwemo majarida ya kisayansi, vipindi vya redio na televisheni, pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu uhifadhi na mbinu za kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu.

**313. Mheshimiwa Spika,** Taasisi itaendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi na kutoa huduma bora kwa wadau kwa kuendelea na Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Ofisi za Makao Makuu ambao unajumuisha ofisi za watafiti, maabara na kumbi za mikutano na jengo hilo litakuwa na uwezo wa kutumiwa na jumla ya watu 950 kwa wakati mmoja litakapokamilika. Aidha, Taasisi itakarabati majengo katika Kituo cha Utafiti Serengeti yakiwemo ofisi, maktaba, maabara, hostel ya wanafunzi na nyumba ya kulala watafiti (rest house). Vilevile, Taasisi itaendelea kuwapa watumishi stahiki zao, kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao ikiwemo ununuzi wa gari moja (1), vifaa vya maabara na samani za ofisi kwa ajili ya watumishi wapya vituoni na Makao Makuu, kupandisha vyeo watumishi 28, kuwapatia mafunzo ya muda mrefu watumishi 20 na mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 45. Sambamba na hilo, Taasisi itaendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utendaji kazi kwa lengo la kuongeza ufanisi.

### 6.3.1.8 *Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka - CAWM*

**314. Mheshimiwa Spika,** Chuo kina jukumu la kutoa mafunzo kuanzia Cheti cha Msingi, Cheti cha Ufundi, Stashahada, Shahada ya kwanza na Shahada ya Uzamili. Aidha, Chuo kina jukumu la kufanya tafiti na kutoa huduma za ushauri wa kitaalam na ugani katika nyanja za usimamizi wa wanyamapori na utalii.

**315. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza jukumu la utoaji mafunzo, Chuo kitadahili wanafunzi wapatao 1,498 katika fani za Usimamizi wa Wanyamapori na Utalii; Usimamizi wa Mazingira na Udhibiti wa Taka pamoja na Usimamizi wa Maliasili. Kozi hizo zitatolewa katika ngazi ya Cheti cha Msingi hadi Shahada ya Uzamili. Aidha, Chuo kitatoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi katika Nyanja za Usimamizi wa Wanyamapori, Usimamizi wa Utalii, na Usimamizi wa Mazingira na Maliasili. Sambamba na hilo, Chuo kitatoa mafunzo ya udereva kwa wanafunzi wanaosoma kozi za muda mfupi na mrefu katika fani za utalii ili kuongeza sifa za kuajiriwa na kujiajiri wanapohitimu masomo yao. Vilevile, Chuo kitaendesha mafunzo ya muda mfupi kwa wapagazi na waongoza utalii wa mlima ili

kuwapa stadi stahiki za kuhudumia wageni hususan kwa wageni watakaoshiriki mashindano ya AFCON 2027.

**316.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha utoaji wa mafunzo na kuchangia utatuzi wa changamoto zinazokabili Sekta za Wanyamapori na Utalii nchini, Chuo kitaendelea kufanya tafiti tano (5) katika nyanja za bioanuwai, uhifadhi wa mazingira, uhifadhi wa wanyamapori, magonjwa ya wanyamapori, usimamizi wa utalii pamoja na migongano baina ya wanyamapori na binadamu. Aidha, Chuo kitaendelea kutekeleza jukumu la kutoa huduma za ushauri wa kitaalam na ugani kwa wadau mbalimbali.

**317.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi na kujifunzia kwa watumishi na wanafunzi, Chuo kitajenga Maktaba yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000, kujenga chumba kimoja (1) cha mihadhara, kununua gari moja (1) kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo pamoja na kujenga ghala moja (1) la silaha na uzio wa ukuta katika Kampasi ya Chuo. Aidha, Chuo kimepanga kuendeleza eneo la Kihesa Kilolo lililopo katika Manispaa ya Iringa kwa kujenga miundombinu ya mafunzo ili kuwezesha kuanza kutoa mafunzo ya muda mfupi katika nyanja ya Usimamizi wa Utalii, hatua itakayowezesha kutoa fursa ya ajira kwa vijana wa mikoa ya nyanda za juu kusini. Vilevile, Chuo kitakarabati mabweni matano (5), vyumba nane (8) vya madarasa, nyumba tano (5) za watumishi, ofisi nane (8) na kujenga njia za ndani zenye urefu wa kilomita 0.5 katika Kampasi ya Mweka. Pia, Chuo kitanunua na kufunga vifaa vya TEHAMA, mahema 100 kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi na seti 100 za vifaa vya maabara.

**318.** **Mheshimiwa Spika**, katika hatua nyingine, Chuo kitafanya mapitio ya programu zake za mafunzo katika nyanja za usimamizi wa wanyamapori na usimamizi wa utalii ili ziendane na mahitaji ya sasa ya soko la ajira na kuchangia kutatua changamoto za Sekta za Wanyamapori na Utalii nchini. Vilevile Chuo kitafanya mapitio ya muundo ili uendane na mahitaji ya sasa ya uendeshaji.

**319.** **Mheshimiwa Spika**, ili kuwajengea watumishi uwezo wa

kufanya kazi kwa weledi na kuongeza tija, Chuo kitawawezesha watumishi 32 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na 50 ya muda mfupi na kuajiri watumishi wapya 15 ili kukidhi mahitaji ya utendaji na kuendelea kutoa stahiki kwa watumishi wa Chuo kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Taratibu na miongozo iliyopo.

#### 6.3.1.9 *Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii - Likuyu Sekamaganga (CBCTC)*

**320. Mheshimiwa Spika,** Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii – Likuyu Sekamaganga kina jukumu la kuijengea jamii uwezo kwa njia ya mafunzo ili iweze kushiriki kikamilifu katika uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za maliasili. Kituo kinatoa mafunzo ya muda mfupi ya kozi za Uaskari Wanyamapori wa Vijiji (VGS), Askari wa Misitu wa Vijiji (VFG), Vikosi vya Ulinzi wa Fukwe pamoja na Viongozi na Wajumbe wa Kamati za Maliasili za Vijiji. Aidha, kituo kinatoa mafunzo ya muda mrefu ya kozi ya Utalii na Uongozaji Watalii kwa ngazi ya Astashahada ya Awali, Astashahada na Stashahada.

**321. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Kituo kitatoa mafunzo kwa wanafunzi 624. Kati yao wanafunzi 100 watapatiwa mafunzo ya muda mrefu ya Utalii na Uongozaji Watalii na wanafunzi 524 watapatiwa mafunzo ya muda mfupi ambapo 500 watapatiwa mafunzo ya Uaskari Wanyamapori wa Vjijiji (VGS) na wanafunzi 24 ambao ni Viongozi na Wajumbe wa Kamati za Maliasili za Vijiji watapatiwa mafunzo ya usimamizi shirikishi wa maliasili. Aidha, Kituo kitaendelea kushiriki katika maonesho na matukio mbalimbali kwa ajili ya kutangaza shughuli za kituo na kutoa elimu.

**322. Mheshimiwa Spika**, Kituo kitaendelea kuboresha miundombinu ya mafunzo kwa kukamilisha ujenzi wa nyumba mbili (2) za watumishi, kuanza ujenzi wa bweni moja (1) la ghorofa lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 300, kukamilisha ukarabati wa majengo ikiwemo bweni moja (1), darasa moja (1), bwalo na jengo la utawala. Aidha, kituo kitanunua vifaa vya mafunzo na malazi ikiwemo basi moja (1) lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 40, kompyuta 35 na meza zake, madawati 80, vitanda (double decker) 32, magodoro 64, meza 32 na viti 64.

Vilevile, Kituo kitafanya mapitio ya mitaala mitatu (3) ya kozi ya Utalii na Uongozaji Watalii.

**323.** **Mheshimiwa Spika**, ili kuwajengea watumishi uwezo wa kufanya kazi kwa weledi na kuongeza tija, Kituo kitawawezesha watumishi 10 kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi na watumishi wawili (2) ya muda mrefu na kuendelea kutoa stahiki kwa watumishi wa kituo kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Taratibu na miongozo iliyopo.

#### 6.3.1.10 *Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi - PWTI*

**324.** **Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi ina jukumu la kutoa mafunzo ya Askari Wahifadhi wa Wanyamapori na Waongoza Watalii katika ngazi ya Astashahada ya Awali, Astashahada na Stashahada. Vilevile, taasisi hutoa mafunzo ya muda mfupi kwa Askari Wanyamapori wa Vijiji (VGS), Askari wa Misitu ya vijiji (VFG) na Vikosi vya Ulinzi wa Fukwe.

**325.** **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Taasisi inatarajia kudahili wanafunzi 681 wa kozi za muda mrefu na 200 wa kozi za muda mfupi. Taasisi itafanya mapitio ya mitaala yake ya kozi za muda mrefu na muda mfupi. Aidha, Taasisi itakamilisha ujenzi wa bweni lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 400, kujenga vyumba vinne (4) vya madarasa, mfumo wa maji na umeme katika mabweni manne (4) ya kituo cha mafunzo kwa vitendo Matongo wilayani Bariadi na kukarabati vyumba vinne (4) vya madarasa. Vilevile, ili kuimarisha matumizi ya teknolojia katika utoaji mafunzo, Taasisi itanunua Ndege Nyuki tatu (3), Kamera-mtego (Camera traps-5), Viona mbali (15), Redio za mawasiliano (10), GPS (30) na mahema (30). Sambamba na hilo, Taasisi itanunua gari moja (1) aina ya KAMAZ kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo. Sambamba na hilo, Taasisi itaendelea kusimamia kampuni ya ulinzi ya Pasiansi Wildlife Security Company Limited - PASCO ili kuongeza mapato. Halikadhalika, Taasisi itaendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kuwezesha watumishi wawili (2) kuendelea na mafunzo ya muda mrefu na watatu (3) mafunzo ya muda mfupi.

### 6.3.2 *Sekta ya Misitu na Nyuki*

**326. Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Misitu na Nyuki ina jukumu la kusimamia uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu na nyuki. Utekelezaji wa shughuli za sekta unasimamiwa na Sheria ya Misitu, Sura ya 323; Sheria ya Ufugaji Nyuki, Sura ya 224; Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania, Sura ya 270 (TAFORI); pamoja na kanuni na miongozo mbalimbali.

#### 6.3.2.1 *Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Ufugaji Nyuki kwa Tanzania Iliyo Bora (Achia Shoka, Tundika Mzinga)*

**327. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara kupitia Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Ufugaji Nyuki kwa Tanzania Iliyo Bora itawezesha mafunzo ya mbinu bora za ufugaji nyuki na uongezaji thamani ya mazao ya nyuki kwa vikundi 145 vyenye wafugaji nyuki 2,175 na mizinga 10,375 pamoja na mavazi ya kinga 430. Aidha, mafunzo kwa mafundi seremala 100 kuhusu utengenezaji wa mizinga ya kisasa na washonaji 10 wa mavazi ya kinga yatatolewa. Vilevile, jumla ya pikipiki 15 zitanunuliwa kwa ajili ya ufuatiliaji na ugani katika vikundi vya wafugaji nyuki. Pia, Mpango utawezesha ununuzi wa vifaa vya utafiti wa nyuki kwa ajili ya kuboresha shughuli za utafiti. Katika hatua nyingine, Wizara itawezesha ujenzi wa viwanda vitatu (3) vya kuchakata na kufungasha mazao ya nyuki katika wilaya za Njombe, Urambo na Chato pamoja na kusimika mitambo ya kuchakata mazao ya nyuki katika viwanda hivyo. Sambamba na hilo, Wizara itatenga maeneo maalum ya utafiti na uzalishaji wa makundi ya nyuki kwa ajili ya kugawa kwa wafugaji nyuki walio jirani na maeneo ya hifadhi.

#### 6.3.2.2 *Idara ya Misitu na Nyuki*

**328. Mheshimiwa Spika**, Wizara itaendelea na utekelezaji wa Sera, Kanuni na Miongozo ya misitu na nyuki ikiwa ni pamoja na kuendelea kukamilisha tathmini ya Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Misitu na kuanza tathmini ya Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki. Aidha, Wizara itaandaa Mwongozo wa Uthibitishaji wa Misitu, Mwongozo wa

Kitaifa wa Ufuatiliaji wa Mazao ya Nyuki, Mwongozo wa Uwekezaji katika Sekta ya Misitu na kuidhinisha Mipango ya Usimamizi wa Misitu 70. Vilevile, Wizara itasimamia utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Utafiti wa Misitu, Mpango Kabambe wa Utafiti wa Ufugaji Nyuki, Mkakati wa Ufugaji Nyuki na Uhifadhi wa Misitu ya Ukanda wa Miombo, Mkakati wa Uzalishaji wa Mbegu Bora za Miti na Urejesheaji Miti ya Ukanda wa Miombo na Mpango Kazi wa Usimamizi wa Mazao yasiyo Timbao.

**329.** **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara itatoa mafunzo kwa wadau mbalimbali kuhusu mbinu za uongezaji thamani na uvunaji endelevu wa mazao ya misitu na fursa za huduma za ikolojia ikiwa ni pamoja na biashara ya Kaboni. Wizara itafanya mikutano miwili (2) na wadau wa Sekta za Misitu na Ufugaji Nyuki kujadili fursa zilizopo katika Sekta ya Misitu na Nyuki. Vilevile, Wizara itawezesha uanzishwaji wa Misitu ya hifadhi yenye ukubwa wa hekta 500,000; hifadhi za nyuki 10; na kanda nne (4) za ufugaji nyuki ndani ya hifadhi za misitu.

**330.** **Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hilo, Wizara itafanya vikao vinne (4) vya kisheria kwa kila Kamati za Misitu na Ufugaji Nyuki ambazo ni Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya Ufugaji Nyuki (NABAC); Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya Misitu (NAFAC); Kamati ya Uendeshaji ya Mazao ya Misitu yaliyohandisiwa (EWP) na Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Kilimo Misitu (NAAC). Vilevile, Wizara itaratibu maadhimisho ya Siku ya Kitaifa ya Upandaji Miti, Siku ya Misitu Duniani na Siku ya Nyuki Duniani. Pia, Wizara itashiriki mikutano na matukio mbalimbali ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa yakiwemo Kampeni ya 27 YA KIJANI, Siku ya Mazingira Duniani, EAC, SADC, AU, Congo Basin, Nairobi Convention, Miombo Declaration, APIMONDIA (2026 na 2027), UNEA na COFO. Aidha, Wizara itaendelea kushiriki katika utekelezaji wa mikataba ya kimataifa ikiwemo UNCBD, UNCCD, UNFCCC, CITES na Ramsar Sites.

### 6.3.2.3 *Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania – TFS*

**331.** **Mheshimiwa Spika**, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) ulianzishwa kwa lengo la kusimamia, kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za misitu na nyuki zilizo chini ya Serikali Kuu.

Wakala unatekeleza majukumu mbalimbali yakiwemo kusimamia hifadhi za misitu ya asili, hifadhi za mikoko, hifadhi za nyuki za Serikali Kuu, mashamba ya miti, mashamba ya nyuki na manzuki; na kusimamia rasilimali za misitu na nyuki katika ardhi ya jumla.

**332.** **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wakala utaimarisha usimamizi na ulinzi wa rasilimali za misitu na nyuki kwa kuandaa mipango ya usimamizi wa misitu 99 ya hifadhi yenye ukubwa wa hekta 2,341,350.43. Aidha, utaimarisha mipaka ya hifadhi za misitu 128 kwa kusafisha kilomita 1,486 za mipaka, kuhakiki kilomita 895.93 za mipaka, kusimika vigingi 727, mabango 374 pamoja na kupanda miti 23,700 kwenye mipaka. Vilevile, Wakala utalinda mashamba ya miti 26 yenye hekta 692,270, hekta 13,841,900 za misitu ya asili na hekta158,100 za mikoko kwa kufanya doria 2,439 katika kanda saba (7).

**333.** **Mheshimiwa Spika,** Wakala utaendelea kuzuia na kupambana na matukio ya moto kwa kufanya kampeni 295 za kuzuia moto katika vijiji 337 pamoja na kuunda vikundi 49 vyenye jumla ya watu 588 kwa ajili ya kuzuia na kudhibiti moto kwenye hifadhi za misitu. Aidha, Wakala utafungua kilomita 114 za njia mpya za kuzuia moto na kusafisha kilomita 4,376 za njia za kuzuia moto katika mashamba 26 ya miti. Vilevile, Wakala utendelea kusimamia minara 19 ya kuangalizia moto na kujenga minara mipya mitatu (3) katika Mashamba ya miti Silayo na Buhigwe pamoja na Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia Pugu/Kazimzumbwi. Pia, Wakala utaendelea kufanya ufuatiliaji wa moto nchi nzima kwa kutumia satellite ili kubaini matukio ya moto mapema na kuukabili kabla ya kuenea na kusababisha madhara zaidi.

**334.** **Mheshimiwa Spika,** Wakala utapanda miti katika eneo la hekta 7,321 na kurudishia miti katika hekta 2,001, kupalilia hekta 39,871, kupogolea hekta 12,126 na kupunguzia hekta 5,443. Aidha, Wakala utajenga kilomita 61.28 za barabara mpya, kukarabati kilomita 2,883 za barabara, kusimika mabomba ya maji 26 (culverts); na kukarabati madaraja 45 na njia za kuvuka mito. Vilevile, Wakala utaendeleza mashamba matatu (3) ya nyuki na manzuki 82; kuzalisha tani 60 za asali; tani tano (5) za nta; kusimamia viwanda vitatu (3) vya mazao ya nyuki vilivyopo

Manyoni, Sao Hill na Nzega pamoja na kutoa elimu kwa wafugaji nyuki. Sambamba na hilo, Wakala utaendelea kusimamia na kuendeleza vyanzo 118 vya mbegu za miti pamoja na kuanzisha vyanzo vipya 15. Pia, tani tisa (9) za mbegu za miti na miche milioni 37.4 ya miti ya aina mbalimbali itazalishwa.

**335. Mheshimiwa Spika,** Wakala utaendelea kuboresha shughuli za utalii pamoja na kushiriki maandalizi ya matukio makubwa ya Kimataifa yatakayofanyika nchini ikiwemo mashindano ya AFCON, Mkutano wa Mabunge Duniani (IPU) na Mashindano ya Walimbwende Duniani. Katika kutekeleza hili, Wakala utakamilisha ujenzi wa miundombinu ya kambi za watalii nane (8) katika misitu ya Rau (1), West Kilimanjaro (1), Meru (1), Mlima Hanang (1), North Kilimanjaro (1), Pugu/Kazimzumbwi (1), Vikindu (1) na Ziwa Ngosi (1). Aidha, Wakala utawezesha uwekezaji wa miundombinu ya malazi na burudani kupitia sekta binafsi katika misitu ya Ziwa Duluti, Magamba, Pugu/Kazimzumbwi, West Kilimanjaro na ujenzi wa Mabanda (Cottages) 26 yenye jumla ya vitanda 54 katika hifadhi ya mikoko iliyopo Sahare - Tanga, Ras Kilomoni - Dar es Salaam, Pugu/Kazimzumbwi na Vikindu - Pwani. Sambamba na hilo, Wakala utanunua Boti mbili za kitalii ambazo zitatumika kwa shughuli za kitalii katika misitu ya mikoko ya Sahare na Ras Kilomoni. Vilevile, Wakala utaimarisha shughuli za utalii katika vituo vya Malikale kwa kukamilisha ukarabati wa jengo la Kale la Ngome Kongwe mjini Bagamoyo, kuimarisha kambi za watalii kwa kununua mahema 30 kwa ajili ya vituo vya michoro ya miambani Kondoa, magofu ya Tongoni na Kaole.

**336. Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, Wakala utazalisha nakala 17,032 za matangazo; kuandaa na kurusha video mjongeo 16, programu 117 za vipindi vya redio na 116 za televisheni, video fupi 120; kushiriki katika matukio 27 ya Kitaifa na Kimataifa ya utalii; na kuandaa matukio 24 ya michezo ya utalii ndani ya hifadhi za misitu. Vilevile, Wakala utaweka mabango ya kidigitali ya matangazo ya vivutio katika jengo la mpingo, Dar es Salaam na mzunguko wa barabara ya Impala jijini Arusha.

**337. Mheshimiwa Spika,** Wakala utaendelea kuimarisha

utawala bora na maslahi ya watumishi kwa kuwajengea watumishi uwezo katika kutekeleza majukumu yao kwa kuwezesha mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 75 na muda mfupi kwa watumishi 564; kununua magari 12, ndege nyuki 8 na pikipiki 33; Ujenzi wa jengo la Makao Makuu katika eneo la Njedengwa, Jijini Dodoma na kukamilisha ujenzi wa majengo mawili (2) ya ofisi na ghala moja (1). Aidha, Wakala utajenga ofisi mbili (2), vituo 15 vya ulinzi, nyumba tano (5) za watumishi na jengo la bustani ya miche (nursery).

**338. Mheshimiwa Spika,** Wakala utaendelea kuwezesha miradi ya maendeleo kwa jamii zinazopakana na misitu kwa kutoa vifaa vya ujenzi ikiwemo mifuko ya saruji 1,100, mabati 700 na mbao 300 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa na zahanati; kutoa madawati 400, meza 125 na viti 125 kwa shule za Msingi na Sekondari. Pia, Wakala utawezesha mizinga ya nyuki 330 na miche ya miti 13,324,464 kwa jamii.

#### 6.3.2.4 *Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania – TAFORI*

**339. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, TAFORI itaendelea kutekeleza jukumu la kufanya, kusimamia na kuratibu tafiti za misitu na nyuki na kutoa ushauri wa kitaaluma kuhusu matumizi ya teknolojia bora na uendelezaji wa misitu na nyuki nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo, TAFORI itafanya jumla ya tafiti 10 na kuratibu tafiti 24. Aidha, tafiti zitakazofanyika ni pamoja na: -

i. Utafiti wa tathmini ya hali ya sasa ya matumizi ya nishati safi nchini pamoja na kupima ufanisi wa majiko banifu;
ii. Utafiti wa kubaini fursa na changamoto kwenye biashara ya kaboni katika misitu ya vijiji;
iii. Utafiti wa uzalishaji wa makundi bora ya nyuki yatakayokuwa na uwezo mkubwa wa kuzalisha mazao ya nyuki;
iv. Utafiti wa ufanisi wa mizinga ya nyuki wasiodunga katika maeneo nane (8) ya majaribio (Rufiji, Mkinga, Siha, Kondoa, Manyoni, Mpanda, Biharamulo, Mbeya);
v. Kuendelea na utafiti wa ukuaji na ubora wa mazao ya nyuki katika manzuki tano (05) za majaribio (TAFORI - Morogoro,

Chamwino - Dodoma, Kongwa - Dodoma, Mufundi - Iringa na Rondo - Lindi); na

vi. Kuendelea na utafiti wa kuchunguza athari za mizunguko ya ukuaji wa miti jamii za misindano na mikaratusi kwenye uzalishaji na ubora wa mbao zinazozalishwa.

**340.** **Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, TAFORI itashirikiana na wadau kufanya tafiti mbalimbali zikiwemo: -

i. Utafiti wa kuangalia jinsi wadudu wachavushao wanavyoathiriwa na mabadiliko ya hali ya hewa kwenye milima ya Uluguru na Udzungwa Mkoani Morogoro; na
ii. Utafiti wa kubaini aina za miti na malighafi nyinginezo za biomasi zenye kiwango kikubwa cha nishati kwa ajili ya uzalishaji wa mkaa mbadala ili kuendeleza juhudi za Serikali za matumizi ya nishati safi ya kupikia.

**341.** **Mheshimiwa Spika,** TAFORI kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kuimarisha ushirikiano katika Sekta ya Misitu na Kilimo kwa kutoa ushauri wa kitaalamu na kuwajengea uwezo watekelezaji wa mradi kuhusu kilimo misitu (agroforestry), upandaji miti (afforestation), na usimamizi shirikishi wa misitu ya jamii (CBFM) kupitia mradi wa Kujenga Ustahimilivu Dhidi ya Mabadiliko ya Tabia Nchi katika Mandhari ya Mkoa wa Kigoma. Aidha, TAFORI itashirikiana na Shirika la Kuhifadhi Mpingo na Maendeleo itatengeneza mfumo wa kidijitali wa ufuatiliaji na uthibitishaji wa mnyororo wa thamani wa mbao kwa ajili ya kuimarisha usimamizi endelevu wa misitu na biashara ya jamii za miti zilizoorodheshwa chini ya Mkataba wa CITES.

**342.** **Mheshimiwa Spika**, TAFORI itaendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kuendelea na ukarabati wa jengo la Makao Makuu na ujenzi wa Kituo cha Utafiti wa Misitu cha Tabora. Aidha, Taasisi itaendelea kuwapatia watumishi stahiki zao kwa kuwapandisha madaraja watumishi 27 wanaostahili, kuwezesha watumishi 15 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu, watumishi 12 kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi na kuajiri watumishi wapya 51 wa kada mbalimbali. Sambamba na hilo, Taasisi itaendeleza shamba darasa la miti lenye ukubwa wa hekta 112 katika Halmashauri ya Madaba, Mkoa wa Ruvuma kwa

kujenga nyumba ya mtumishi, ofisi, miundombinu ya bustani na kupanda miti kwenye eneo la hekta 15. Vilevile, Taasisi itaendelea kuimarisha uwezo wa kitalu cha miti kwa kuboresha teknolojia ya uzalishaji wa miche ya miti katika Kituo cha Utafiti wa Misitu cha Kibaha ili kuongeza upatikanaji wa vipando bora vya miti.

#### 6.3.2.5 *Mfuko wa Misitu Tanzania – TaFF*

**343.** **Mheshimiwa Spika**, Mfuko utaendelea kutekeleza jukumu la kuwezesha na kugharamia shughuli na miradi ya kuboresha uhifadhi, usimamizi na uendelezaji rasilimali za misitu na nyuki. Katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Mfuko utatoa ruzuku kwa miradi 302 ambayo utekelezaji wake unaendelea na miradi mipya 90. Mfuko utawezesha upandaji miti katika mashamba ya miti matatu (3) yenye ukubwa wa hekta 697, kuwezesha uanzishwaji wa vitalu vya miti katika shule 25 na miradi minne (4) ya nishati mbadala ikiwemo matumizi ya biogas, majiko banifu pamoja na utengenezaji na matumizi ya briketi. Sambamba na hilo, Mfuko utawezesha fedha kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Ufugaji Nyuki kwa Tanzania iliyo bora kwa kuwezesha miradi ya kimkakati ikiwemo ujenzi wa viwanda viwili (2) katika Wilaya ya Njombe na Chato pamoja na ununuzi wa mitambo ya kuchakata asali katika Wilaya ya Urambo.

**344.** **Mheshimiwa Spika**, katika hatua nyingine, Mfuko utaendelea kujenga uwezo wa vyuo vya mafunzo vya kati vya misitu, viwanda vya misitu na ufugaji nyuki kwa kuwezesha ujenzi wa bweni la wasichana lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 200 katika Chuo cha FITI; ujenzi wa bweni la wanafunzi katika Kituo cha FWITC lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 208; na ujenzi wa bweni la wanafunzi katika chuo cha Misitu Olmotonyi lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500. Vilevile, Mfuko utawezesha ukarabati wa jengo la TAFORI Makao Makuu, ujenzi wa jengo la Ofisi ya Kituo cha Utafiti wa Misitu Tabora na ununuzi wa samani za jengo la mihadhara katika Chuo cha BTI. Pia, Mfuko utaendelea kugharamia masomo ya Shahada ya Uzamili na Uzamivu kwa fani ambazo zina watalaam wachache katika masuala ya misitu na nyuki hapa nchini. Aidha, Mfuko utaendelea kuhamasisha vijana kusomea fani za misitu na ufugaji nyuki kwa kutoa ufadhili wa masomo na tuzo kwa wanafunzi 27

watakaofanya vizuri zaidi katika ngazi ya Astashahada na Stashahada ya Misitu, Viwanda vya Misitu na Ufugaji Nyuki, pamoja na Stashahada ya Kwanza ya Misitu.

**345.** **Mheshimiwa Spika**, Mfuko utaimarisha mazingira ya utendaji kazi kwa kuanza ujenzi wa jengo la Ofisi za Mfuko katika eneo la Nzuguni 'C' Jijini Dodoma; kuendelea na utekelezaji wa muundo kwa kuongeza idadi ya watumishi ili kuwezesha Mfuko kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi; na kuwezeshamafunzo ya muda mrefu kwa mtumishi mmoja (1) na muda mfupi kwa watumishi 10.

### *6.3.2.6 Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki, Tabora – BTI*

**346.** **Mheshimiwa spika,** Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki, Tabora kina majukumu makuu matatu (3) ambayo ni; kutoa Mafunzo kwa wadau mbalimbali katika mnyororo mzima wa Ufugaji Nyuki nchini, kutoa ushauri wa kitaaluma na kufanya tafiti za nyuki na ufugaji nyuki na mazingira. Katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Chuo kitadahili wanafunzi 400 wa mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya Stashahada na Astashahada. Aidha, Chuo kitatoa mafunzo ya muda mfupi ya ufugaji nyuki na uhifadhi wa mazingira kwa washiriki 540. Vilevile, Chuo kitatoa huduma za ugani kwa shule 12 za Msingi na Sekondari katika Manispaa ya Tabora, Wilaya ya Uyui na Sikonge. Aidha, Chuo kitafanya tafiti mbili za kuboresha uzalishaji na matumizi ya teknolojia za ufugaji nyuki nchini.

**347.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha mazingira ya mafunzo, Chuo kitaendelea na ujenzi wa awamu ya pili ya jengo la bweni la wasichana, ujenzi wa maabara, pamoja na uwekaji wa uzio kuzunguka eneo la Chuo. Aidha, Chuo kitaweka samani katika jengo la mihadhara, kufanya ukarabati wa bwalo la chakula na bweni la wavulana. Vilevile, Chuo kitatoa huduma za kutengeneza mizinga ya nyuki 500 pamoja na kutoa huduma za ugani kwa wafugaji nyuki 1500. Pia, Chuo kitawezesha mtumishi mmoja (1) katika mafunzo ya muda mrefu na watumishi 12 katika mafunzo ya muda mfupi.

### 6.3.2.7 *Chuo cha Viwanda vya Misitu - FITI*

**348. Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Viwanda vya Misitu Moshi kina jukumu la kutoa mafunzo, utafiti na ushauri wa kitaalamu katika matumizi endelevu ya rasilimali za misitu na teknolojia za viwanda vya misitu. Katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Chuo kitatoa mafunzo katika ngazi ya Astashahada na Stashahada ya teknolojia ya viwanda vya misitu kwa kudahili wanafunzi 500 na wanafunzi 100 katika ngazi ya ufundi stadi (I – III) wa uchakataji magogo (wood processing) na Useremala (Carpentry and Joinery). Vilevile, Chuo kitatoa mafunzo ya muda mfupi kwa watu 280, kufanya tafiti 2 na kutoa ushauri kwa wananchi 1,200 juu ya teknolojia za viwanda vya misitu, matumizi endelevu ya mazao ya misitu na biashara ya kaboni.

**349. Mheshimiwa Spika,** Chuo kitaendelea kufanya maboresho ya miundombinu ya kujifunzia na kufundishia ikiwa ni pamoja na kukamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa hosteli ya wanafunzi wa kike yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 200, ukarabati wa darasa na mabweni mawili (2) katika kituo cha mafunzo West Kilimanjaro, ukarabati wa karakana ya useremala, kununua vitendea kazi na kuimarisha mifumo ya TEHAMA.

**350. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utendaji kazi, Chuo kitawezesha watumishi sita (6) kupata mafunzo ya muda mrefu na kuwajengea uwezo watumishi 34 katika maeneo mbalimbali. Aidha, Chuo kitaendelea kutangaza huduma zake kupitia maonesho mbalimbali ya ndani na nje ya nchi yakiwemo Sabasaba, Nanenane, Siku ya Nyuki, Siku ya Misitu, Tukacharu Rau na West Kili. Vilevile, kupitia mradi wa kukuza ujuzi unaofadhiliwa na Jumuiya ya Umoja wa Ulaya, Chuo kitapeleka wakufunzi wanne (4) nchini Estonia kwa mafunzo ya muda mfupi ya viwanda vya misitu. Katika hatua nyingine, Chuo kitaendeleza mashirikiano na wadau mbalimbali wa misitu na mazingira katika kukuza ujuzi na ubunifu kwa vijana ili kuongeza fursa na kipato katika mnyororo mzima wa mazao ya misitu.

### 6.3.2.8 *Chuo cha Misitu, Olmotonyi – FTI*

**351. Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Misitu, Olmotonyi kina

majukumu ya kutoa mafunzo ya ufundi sanifu ya uhifadhi wa misitu, mafunzo ya muda mfupi na ushauri wa kitaalam wa uhifadhi misitu na mazingira. Katika mwaka wa Fedha 2026/2027, Chuo kitadahili na kutoa mafunzo ya Astashahada na Stashahada ya Uhifadhi wa Misitu, Misitu ya Mjini na Jioinfomatiki kwa wanafunzi 930. Sambamba na hilo, Chuo kitatoa mafunzo ya muda mfupi ya uhifadhi wa misitu na mazingira kwa washiriki 100 kutoka taasisi mbalimbali. Aidha, Chuo kitatoa elimu ya ugani ya uhifadhi misitu, utunzaji wa miti na kilimo ikolojia kwa wananchi 400 katika vijiji vya Olmotonyi, Ekenywa na Olkokola vinavyopakana na shamba la miti la Chuo. Pia, Chuo kitatoa ushauri wa kitaalam wa upandaji miti na uhifadhi wa misitu kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari tano (5) katika wilaya za Arumeru na Arusha.

**352.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuongeza kasi ya uhifadhi wa misitu na upandaji miti, Chuo kitazalisha miche ya miti 100,000 ya jamii mbalimbali ambapo itapandwa katika shamba la miti la Chuo na viunga vya Chuo kupitia kampeni za **27 YA KIJANI**, Wiki ya Upandaji Miti na Siku ya Misitu Duniani. Aidha, Chuo kitaendelea na uangalizi wa majaribio ya kuotesha miche ya miti ya mbegu bora aina ya misindano na mikaratusi iliyoboreshwa katika shamba la miti la Chuo kwa lengo la kupima ufanisi katika ukuaji, uimara, umbo na ustahimilivu wa magonjwa katika Ukanda wa Kaskazini.

**353.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi na wanafunzi, Chuo kitajenga miundombinu ya utalii ikolojia kwenye msitu wa asili wenye ukubwa wa hekta 19 katika eneo la chuo ili kuboresha mafunzo ya utalii ikolojia. Ujenzi utajumuisha; njia ya watembea kwa miguu yenye urefu wa kilometa 1, daraja la miti, kambi ya watalii, jengo la mapokezi ya wageni na mabanda (3). Vilevile, Chuo kitaanza ujenzi wa bweni la wanafunzi lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500. Aidha, Chuo kitakarabati bwalo la chakula la wanafunzi, chumba cha maabara, chumba cha kuhifadhi sampuli za mimea, nyumba sita (6) za watumishi, barabara za moto zenye urefu wa kilometa 8 na barabara za ndani ya chuo zenye urefu wa kilomita 1. Sambamba na hilo,

Chuo kitanunua na kufunga vifaa vya TEHAMA na mahema 10 kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi.

**354. Mheshimiwa Spika,** katika kuhamasisha jamii inayozunguka Chuo kushiriki kikamilifu katika uhifadhi wa misitu, Chuo kitaendelea kushirikiana na vijiji vya Olmotonyi, Ekenywa na Olkokola vinavyopakana na shamba la miti la Chuo katika kuhudumia msitu wa Chuo kupitia mfumo wa Taungya. Katika mwaka wa fedha 2027/2026, jumla ya wananchi 400 wataendelea kuwezeshwa kupanda mazao ya mahindi na maharage kwenye shamba la miti la chuo.

**355. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utendaji kazi, Chuo kitawajengea uwezo wakufunzi 23 katika eneo la uandaaji wa mitaala na ufundishaji kwa kushirikiana na Chuo cha Misitu cha Zambia, Chuo cha Misitu cha Estonia, Chuo cha Viwanda vya Misitu na Chuo Kikuu cha HAMK (UFINI). Aidha, Chuo kitawezesha watumishi wanne (4) kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu ya misitu na kujenga uwezo watumishi 35 katika nyanja mbalimbali. Vilevile, Chuo kitashiriki katika matukio mbalimbali ikiwemo michezo na maonesho kwa lengo la kujifunza na kujitangaza.

#### 6.3.2.9 *Kituo cha Mafunzo ya Misitu na Viwanda vya Misitu – FWITC*

**356. Mheshimiwa Spika,** Kituo Cha Mafunzo ya Misitu na Viwanda Vya Misitu kilianzishwa kwa lengo la kutoa mafunzo na kuwajengea uwezo wakulima wa miti, vikundi vya upandaji miti na wachakataji wa mazao ya misitu. Kwa mwaka wa Fedha 2026/2027, Kituo kitadahili wanafunzi 95 kwa fani ya Uhudumu Misitu, Uchakataji wa mazao ya Misitu na Ufundi seremala ngazi ya I-III ya ufundi stadi. Aidha, Kituo kitaendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na ushauri wa kitaalam katika matumizi endelevu ya mazao ya misitu na nishati mbadala kwa wananchi 200. Vilevile, Kituo kitatoa mafunzo ya usimamizi jumuishi ya moto wa msituni kwa wananchi 200, Maafisa Misitu na Mazingira 150 kutoka mikoa ya Ruvuma, Njombe, Lindi na Iringa. Sambamba na hilo, Kituo kitaanzisha programu atamizi kwa wahitimu wa Mafunzo ya

misitu na wajasiriamali wadogo na wa kati wa mazao ya Misitu katika kuanzisha na kuendeleza shughuli za ujasiriamali.

**357. Mheshimiwa Spika,** Kituo kitaendelea kufanya maboresho ya mazingira ya wanafunzi kujifunzia ikiwa ni pamoja na ujenzi wa bweni la wanafunzi lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 208; upanuzi wa karakana ya uchakataji mazao ya misitu, ununuzi wa mitambo na mashine za kisasa za mazao yaliohandisiwa (EWP), ukarabati wa majengo ya madarasa na ununuzi wa basi moja (1). Vilevile, Kituo kitaboresha kitalu cha uzalishaji miche na kuzalisha miche 500,000 itakayogawiwa kwa wananchi kwa ajili ya kupanda kwenye maeneo yao.

**358. Mheshimiwa Spika,** Kituo kitaendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kununua vifaa vya Tehama, kuwezesha watumishi 26 kupata mafunzo katika nyanja mbalimbali ikiwemo ufundishaji, ukusanyaji na utunzaji wa mbegu, uchakataji wa mazao ya misitu na useremala. Vilevile, Chuo kitashiriki maonesho mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa kwa ajili ya kujitangaza na kuhabarisha umma kuhusu mafunzo ya ufundi stadi maonesho hayo ni kama Sabasaba, Nanenane, Siku ya kitaifa ya Upandaji Miti, Siku ya Misitu Duniani, Mei Mosi na Siku ya Nyuki Duniani.

### 6.3.3 *Sekta ya Utalii*

**359. Mheshimiwa Spika,** utalii ni mojawapo ya sekta muhimu za kiuchumi nchini ambapo imekuwa ikichangia zaidi ya asilimia 17 ya Pato la Taifa, kuzalisha fursa za ajira milioni 2.7 pamoja na asilimia 25 ya mapato ya fedha za kigeni. Katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara itafanya mapitio ya Sera, Sheria, Kanuni na nyenzo za kisera zinazolenga kuimarisha na kukuza Sekta ya Utalii nchini hususan, katika udhibiti wa sekta na ukusanyaji maduhuli, uendelezaji wa vivutio na mazao ya utalii, utangazaji utalii, uboreshaji wa huduma na miundombinu ya utalii pamoja na utoaji wa mafunzo katika tasnia ya ukarimu. Aidha, utekelezaji huo utahusisha kutumia kikamilifu fursa zinazotokana na ukuaji wa sekta. Halikadhalika, uwepo wa matukio makubwa ya kimataifa ambayo Tanzania itakuwa nchi mwenyeji. Hatua hizo, zitachangia katika kuimarisha Sekta ya Utalii na kuongeza idadi ya watalii kufikia milioni nane (8) mwaka 2030.

**360.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza kukuza Sekta Utalii, Wizara imeanzisha ufadhili wa mafunzo ya ukarimu na utalii utakaojulikana kama Samia Tourism Scholarship itakayokuwa inatolewa kila mwaka kuendeleza ujuzi na weledi kwenye huduma za ukarimu na utalii. Ufadhili huu utalenga maeneo ya uhitaji maalum na yanayohitajika kwenye mnyororo wa kuongeza thamani kwenye soko la utalii. Hatua hiyo inatarajiwa kuongeza tija katika kuboresha ubora wa huduma za utalii pamoja na kuchochea maendeleo ya uchumi jumuishi na endelevu.

**6.3.3.1 *Idara ya Utalii***

**361.** **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Utalii ina jukumu la kusimamia maendeleo na udhibiti wa Sekta ya Utalii nchini. Katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Wizara itafanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Sheria ya Utalii Sura ya 65 na Kanuni zake ili kuimarisha udhibiti wa biashara za utalii na ubora wa huduma nchini, kuandaa mikakati ya motisha za kuvutia uwekezaji wa biashara za utalii katika kanda nne (4) za utalii zikiwemo Kanda ya Kaskazini, Nyanda za Juu Kusini, Pwani na Kanda ya Ziwa pamoja na kufanya mapitio ya Mwongozo wa Biashara za Utalii. Aidha, Wizara itaratibu usajili wa Wataalamu wa utalii na ukarimu ili kuwa na kanzidata itakayowezesha kufanya tathmini na kuweka mipango stahiki ya uendelezaji wa wataalamu katika kada za Sekta ya Utalii na ukarimu nchini.

**362.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara itaandaa Mpango Kabambe wa Uendelezaji Utalii Nchini (Tourism Master Plan) unaotoa mwelekeo wa kukuza sekta kwa kuainisha ushiriki wa wadau wa utalii kutoka Sekta za Umma na Binafsi. Pia, kufuatilia utekelezaji wa mikakati endelevu ikijumuisha utalii wa kimataifa katika kanda nne (4) za utalii nchini. Katika hatua nyingine, Wizara itatekeleza jukumu la usimamizi na udhibiti wa Sekta ya Utalii kwa kufanya kaguzi za biashara za utalii nchini, kupanga huduma za malazi na chakula katika daraja za ubora, kuibua na kuendeleza vivutio na mazao mapya ya utalii. Vilevile, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kushiriki mikutano, maonesho na matukio ya kitaifa, kikanda na kimataifa yenye fursa za kukuza utalii. Wizara pia itafanya tafiti za utalii zitakazowezesha uendelezaji na kubaini masoko yenye tija na yanayoweza kunufaisha wadau na sekta kiujumla.

**363.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara itaratibu vikao vinne (4) vya Kamati ya Kitaalamu ya Ushauri katika Masuala ya Utalii ikiwa pia ni utekelezaji wa matakwa ya kisheria na kisera ili kukuza utalii endelevu. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa Sekta ya Utalii, ikiwa ni pamoja na kuratibu vikao vinne (4) vya kujadili masuala yanayohusu uibuaji na uendelezaji wa mazao ya utalii ya kimkakati ya fukwe, meli, utalii na matukio yenye fursa za kukuza uchumi na uwekezaji katika soko la utalii. Hatua hiyo itahusisha pia utekelezaji wa Mkakati wa Maendeleo Endelevu ya Utalii katika Ukanda wa Pwani na Bahari (2026 - 2036).

**6.3.3.2** ***Tozo ya Maendeleo ya Utalii - TDL***

**364.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Tozo ya Maendeleo ya Utalii (Tourism Development Levy - TDL) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 itaendelea kuwezesha fedha kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya utalii, ambayo inajumuisha ukamilishaji wa ujenzi wa barabara ya kilometa 38 na geti la kimkakati la kuunganisha watalii wanaowasili kupitia treni ya SGR na Hifadhi ya Taifa Mikumi upande wa Kilosa, mkoani Morogoro. Pia, itawezesha ukamilishaji wa ujenzi wa awamu ya kwanza wa hoteli ya nyota tatu (3) iliyopo Chato Mkoani Geita. Aidha, TDL itawezesha fedha za ukarabati wa njia za kurukia ndege katika Hifadhi ya Taifa Mahale na uwanja cha ndege cha Ndutu katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Vilevle, itawezesha ujenzi wa njia ya mbao (boardwalk) katika Hifadhi ya Kitulo, na ukarabati wa nyumba za watalii (bandas) na barabara ya kilomita 20 kwa kiwango cha changarawe katika Hifadhi ya Taifa Katavi.

**365.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuelekea mashindano ya AFCON 2027, Wizara kupitia TDL itawekeza nguvu kubwa katika maeneo yatakayopokea wageni ikiwa ni pamoja na kuwezesha fedha za kukamilisha njia za mbao (boardwalks) na mabanda 26 ya malazi (cottages) katika Msitu wa Mikoko wa Sahare Tanga (10) na Ras Kilomoni, Kinondoni – Dar es Salaam (6), Pugu Kazimzumbwi (5) na Vikindu (5). Ukamilishaji huu utaenda sambamba na ununuzi wa boti mbili (2) ya utalii zenye sakafu ya kioo zitakayokuwa Sahare na Ras Kilomoni Mkoani Tanga na Dar es salaam.

**366.** **Mheshimiwa Spika**, katika kuhifadhi historia na utamaduni wetu, TDL itawezesha fedha za ukamilishaji wa ujenzi wa Kituo cha Dinasoria kilichopo Tendaguru, Lindi na ukarabati wa Makumbusho ya Majimaji, mkoani Ruvuma. Miradi hii inaenda sambamba na uboreshaji wa Kijiji cha Makumbusho mkoani Dar es Salaam ambapo mifumo ya kidijitali itawekwa ili kuwapa watalii uzoefu wa kipekee wa maisha ya asili ya Kitanzania.

**367.** **Mheshimiwa Spika,** katika kutangaza utalii wa Tanzania Duniani, TDL itawezesha fedha kwaajili ya kutangaza utalii kidijitali zaidi kwa kutumia majukwaa makubwa kama Trip Advisor, Expedia na Google Ads. Aidha, itawezesha kutumia fursa za kipekee kama Mashindano ya Miss World 2027, matukio ya World Travel Awards na pia kutangaza utalii wetu kupitia mashindano ya kimataifa ya mbio za baiskeli ya Tour De France, yote haya yakiwa na lengo la kuongeza idadi ya watalii nchini.

**368.** **Mheshimiwa Spika,** uwekezaji rasilimali watu na vifaa ni kipaumbele cha Wizara, TDL itafadhili masomo ya utalii na ukarimu kwa wanafunzi 250 kupitia Samia Tourism Scholarship. Pia, TDL itawezesha mafunzo maalum kwa watoa huduma 2,500 wakiwemo mama na baba lishe na madereva taxi ili kuhakikisha wageni kabla, wakati na baada ya AFCON 2027 wanapata huduma bora na za kitaalamu. Aidha, TDL itawezesha ununuzi wa mabasi mawili (2) ya mafunzo kwa vitendo katika Chuo cha Taifa cha Utalii kwenye Kampasi za Temeke na Mwanza na basi moja (1) kwa ajili ya Kituo cha Mafunzo ya Wanyamapori kwa Jamii – Likuyu Sekamaganga.

**369.** **Mheshimiwa Spika,** vilevile, TDL itawezesha kazi ya udhibiti wa ubora kwa kupanga huduma za malazi katika daraja za ubora wa nyota pamoja na kufanya ukaguzi wa wakala wa biashara za utalii katika mikoa sita (6) ya kimkakati ambayo ni Arusha, Dodoma, Mara, Pwani, Mwanza na Mbeya.

#### 6.3.3.3 *Bodi ya Utalii Tanzania - TTB*

**370.** **Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Utalii Tanzania ina majukumu makuu manne (4) ambayo ni: kutumia mbinu mbalimbali za utangazaji ili kuifanya Tanzania iwe kituo mojawapo mashuhuri

cha utalii duniani; kuhamasisha uendelezaji wa miundombinu ya utalii; kufanya tafiti kwa ajili ya kuboresha Sekta ya Utalii nchini; na kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa utalii na manufaa yake kiuchumi. Katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Bodi itafanya tathmini ya chapa ya kutangaza utalii wa Tanzania yaani Tanzania Unforgettable! kwa kushirikiana na wadau ili kuendana na mwelekeo wa nchi wa ukuzaji wa Sekta ya Utalii kama ilivyoelekezwa katika Dira 2050. Chapa hii ina muda wa miaka sita (6) tangu ilipoanza kutumika mwaka 2019. Ni imani yetu kuwa sasa ni wakati muafaka wa kutengeneza utambulisho mpya wa Tanzania (Brand Campaign) kama nchi yenye vivutio vingi na vya kipekee duniani.

**371.** **Mheshimiwa Spika,** katika kukuza jitihada za utangazaji utalii kidijitali, Bodi itaendelea kuimarisha Kituo cha Utangazaji Utalii Kidijitali - DDMCC na mfumo wa Travel Companion wenye Booking Platform kwa kutengeneza maudhui na kuongeza lugha za kimataifa ikiwemo Kiarabu, Kirusi, Kichina (Mandarin), Kihindi, Kifaransa, Kispaniola na Kireno. Pia, kulipia nafasi katika National Internet Data Centre – NIDC na kuongeza uwezo wa uchakataji wa taarifa na kutoa mafunzo kwa wadau juu ya mfumo na namna bora ya kuutumia.

**372.** **Mheshimiwa Spika,** Bodi itaendelea na kutangaza utalii kupitia uandaaji na uratibu wa maonesho ya utalii ndani na nje ya nchi hususan kuandaa Onesho la Tisa (9) la Swahili International Tourism Expo (S!TE 2026). Onesho hili hufanyika mara moja kwa mwaka na kuvutia washiriki zaidi ya 2,000 kutoka ndani na nje ya nchi, ambapo huwakutanisha wafanyabiashara wa utalii kwa ajili ya mazungumzo ya kibiashara (B2B na B2C). Vilevile, S!TE huusisha Jukwaa la Uwekezaji (Tanzania Tourism Investment Forum - TTIF) ambapo wadau hupata taarifa mbalimbali kuhusu fursa za uwekezaji.

**373.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuunga mkono juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alizozifanya kwa uzalendo na umahiri mkubwa kuitambulisha nchi na kutangaza utalii kupitia filamu ya Tanzania - The Royal Tour na Amazing Tanzania. Kwa muktadha huo, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, katika Mwaka

wa Fedha 2026/2027, Serikali itaandaa filamu nyingine yenye viwango vya kimataifa kutangaza utalii wa Tanzania ili kuendelea kuvutia watalii wengi zaidi hususan, kufikia idadi ya watalii milioni nane (8) ifikapo mwaka 2030. Kupitia filamu hii, Bodi itaweza kuongeza wigo mpana wa kutangaza mazao mapya ya Utalii kijiografia kama utalii wa dini, utalii wa historia, utalii wa utamaduni, ikolojia, michezo, mikutano na matukio. Aidha, Bodi itaendelea kuandaa na kusambaza maudhui ya utalii wa Tanzania kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kidijitali maarufu duniani ikiwemo Expedia, National Georgraphic, Ctrip, Wechart na Xiachongsh.

**374.** **Mheshimiwa Spika,** Bodi itaendelea kutangaza utalii kwa kushirikiana na watu mashuhuri na wenye ushawishi, wakala wa utalii, waandishi wa habari kutoka ndani na nje ya nchi hususan, katika masoko ya kimkakati duniani ili kuitangaza vyema Tanzania na vivutio vyake. Bodi itaandaa ziara za mafunzo kwa kuwapeleka wageni hawa katika vivutio mbalimbali na kukutana na viongozi wetu ili kupata taarifa za upekee wa Tanzania katika Sekta ya Maliasili na Utalii. Katika kutekeleza jukumu hili, Bodi pia itashirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Ofisi za Ubalozi wa Tanzania katika nchi husika.

**375.** **Mheshimiwa Spika,** Bodi itatangaza utalii wa Tanzania kupitia matukio makubwa ya kimataifa yatakayofanyika hapa nchini ikijumuisha Matukio makubwa manne ambayo ni: -

i. Bodi itaandaa Tukio la 33 la Tuzo za World Travel Awards ambalo litafanyika Tanzania mwezi Desemba, 2026. Tuzo hizi huwaleta viongozi na wakuu wa taasisi zilizo katika mnyororo wa thamani wa Sekta ya Utalii ikiwemo, watoa huduma za malazi, wakala wa Utalii, mashirika makubwa ya ndege, viwanja vya ndege, huduma za usafiri, wawekezaji na bodi za utalii, taasisi za uhifadhi, wawakilishi wa mataifa mbalimbali duniani kushiriki kupokea tuzo;

ii. Katika kuhakikisha Tanzania inanufaika kikamilifu na Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (Inter-Parliamentary Union Assembly - IPU) utakaohudhuriwa na washiriki zaidi ya 1,500 wakiwemo Maspika 183 kutoka nchi mbalimbali duniani. Bodi

itaendelea kutekeleza mikakati ya kuwashawishi washiriki kutembelea maeneo ya utalii wa Tanzania kabla, wakati na baada ya Mkutano huo. Hatua hiyo ni pamoja na kuendelea kushirikiana na wadau wa utalii kuandaa vifurushi vya safari na kuvitangaza kwenye tovuti ya IPU. Aidha, Bodi itaweka mabanda ya taarifa za utalii katika eneo la Mkutano ili kuhamasisha washiriki kutembelea vivutio vyetu kipindi na baada ya kushiriki mkutano;

iii. Bodi itafanya utangazaji utalii kupitia Mashindano ya Ulimbwende ya Dunia (Miss World 2027) yatakayofanyika nchini, ambayo uhusisha takriban watu 20,000 wakiwemo washindani 120 kutoka nchi mbalimbali Duniani. Katika kufanikisha hilo, Bodi itaandaa ziara ya mafunzo kwa kuwapa fursa walimbwende na waandishi wa habari kutembelea maeneo ya vivutio (FAM Trip) kabla na wakati wa shindano kwa lengo la kukuza uelewa wa vivutio vyetu na kurusha maudhui hayo kwenye mitandao yao ya kijamii pamoja na kuvitangaza katika vyombo vya habari mbalimbali duniani. Pia, itaweka mabanda ya kutangaza utalii na kutoa taarifa kwa watalii ndani ya maeneo yatakapo fanyika mashindano na kuendelea kutumia maudhui ya mashindano hayo, ikiwemo yatakayomhusu Mshindi wa Mashindano ya Miss World kujitangaza zaidi duniani. Aidha, washindi wa juu watano wa shindano hilo watateuliwa kuwa mabalozi wa hiari wa utangazaji utalii wa Tanzania; na

iv. Bodi itatumia fursa za Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa Nchi za Afrika (AFCON 2027) kutangaza utalii wa Tanzania. Mashindano hayo yanayohusisha timu 24 za Taifa kutoka Afrika, watazamaji wa viwanjani milioni 1.8, wafuatiliaji katika televisheni bilioni 1.9 kupitia vituo vya utangazaji zaidi ya 185. Katika kufanikisha hilo, Bodi itawatumia watu maarufu na wenye ushawishi mkubwa kama vile wanamichezo, wanahabari na wanamuziki mashuhuri duniani kwa kuandaa ziara maalum ambapo maudhui mbalimbali yenye kulenga kuitangaza Tanzania yatarekodiwa na kurushwa kwenye tovuti mbalimbali sambamba na mitandao ya kijamii ya watu hao kama vile Instagram, LinkedIn, Tiktok, Facebook na mtandao wa X. Pia, Bodi itaweka matangazo yenye maudhui ya utalii wa Tanzania katika viwanja vitakavyotumika ili kuwahamasisha mashabiki

kutembelea vivutio vya utalii hapa nchini. Hatua hiyo, itaenda sambamba na kutangaza vifurushi maalum vya safari za utalii, kuhamasisha mashabiki kupitia maeneo maalum ya ufuatiliaji mashindano mubashara (fan zones) katika maeneo ya kimkakati ikiwemo Dar es Salaam, Arusha, Kilimanjaro, Dodoma, Mwanza, Mbeya na Morogoro. Vilevile, kushirikiana na wadau kuandaa ziara za mafunzo kwa watu wenye ushawishi watakaokuwa nchini kuangalia mechi za mpira.

**376.** **Mheshimiwa Spika,** katika juhudi za kuimarisha uwezo wa watumishi ili kutekeleza majukumu yao ipasavyo, Bodi itapeleka watumishi 40 kwenye mafunzo ya muda mfupi na watumishi sita (6) katika mafunzo ya muda mrefu. Aidha, watumishi 25 wa kada mbalimbali wamekasimiwa kwa ajili ya kupandishwa vyeo. Vilevile, katika kuboresha utendaji kazi wa Taasisi unaolenga katika kuongeza tija na ufanisi, Bodi itaajiri watumishi wapya 23.

#### 6.3.3.4 *Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii - NCT*

**377.** **Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT) kina dhamana ya kutoa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa huduma za ushauri wa kitaalam katika fani za Utalii na Ukarimu. Chuo kinatoa mafunzo katika ngazi ya Astashahada na Stashahada katika kozi za Ukarimu, Utalii na Uratibu wa Matukio.

**378.** **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Chuo kitaendelea kutekeleza majukumu yake ya kutoa mafunzo ya umahiri kwa kuongeza udahili kutoka wanafunzi 1,653 Mwaka wa Masomo 2025/2026 hadi wanafunzi 1,889 Mwaka wa Masomo 2026/2027. Aidha, Chuo kitaendelea kujitangaza kupitia mitandao ya kijamii, vituo vya televisheni, makala maalumu, kushiriki katika mikutano na maonesho mbalimbali ndani na nje ya nchi pamoja na kutumia baadhi ya wahitimu wa Chuo kuwa mabalozi wake wa hiari kutangaza huduma zake. Pia, Chuo kitatumia fursa za matukio makubwa yatayofanyika nchini, ikiwemo AFCON 2027 kwa kutangaza huduma zake na kutoa mafunzo ya huduma bora kwa mteja, uendelezaji na usimamizi wa biashara za utalii na ukarimu kwa wadau 2,000 katika mnyororo wa thamani wa utalii. Wadau hawa wanajumuisha mama lishe, waongozaji watalii,

wasafirishaji, wahudumu wa migahawa, hoteli na sehemu za starehe katika mikoa ya Dar es salaam, Arusha na Kilimanjaro ili kuwezesha utoaji wa huduma bora kwa wageni. Vilevile, Chuo kitaendelea kuimarisha uwezo wa kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalam kwa waendesha biashara za utalii na ukarimu nchini.

**379. Mheshimiwa Spika,** Chuo kitaendelea kuimarisha miundombinu na kununua vitendea kazi na vifaa muhimu katika utoaji wa mafunzo kwa vitendo ikijumuisha ununuzi wa mabasi mawili (2) pamoja na gari moja (1) kwa ajili ya usimamizi wa shughuli za mafunzo. Aidha, Chuo kitaendelea kukamilisha ujenzi wa jengo la taaluma lililopo katika Kampasi ya Arusha ikiwemo kuweka samani, mifumo ya TEHAMA na vifaa vya mafunzo. Vilevile, Chuo kitaanza ujenzi wa jengo kwa ajili ya huduma za malazi ya wanafunzi wakike 600 katika Kampasi ya Arusha pamoja na kufanya ukarabati wa miundombinu katika Kampasi za Bustani na Temeke.

**380. Mheshimiwa Spika,** katika juhudi za kuendelea kuimarisha uwezo wa watumishi kufanya kazi kwa weledi na kuongeza tija, Chuo kitawawezesha watumishi nane (8) kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 60 ya muda mfupi. Vilevile, Chuo kitaajiri watumishi wapya 21 ili kukidhi mahitaji ya utendaji na kuendelea kutoa stahiki kwa watumishi wa Chuo kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo.

### 6.3.4 *Sekta ya Mambo ya Kale*

#### 6.3.4.1 Idara ya Mambo ya Kale

**381. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Wizara itatangaza maeneo 10 ya malikale kuwa Urithi wa Taifa, itaandaa kanuni za usimamizi na uendeshajiwa makumbusho binafsi, miongozo ya uhifadhi wa majengo ya kihistoria; na itakamilisha Mwongozo wa Kutwaa na Kuhamisha Umiliki wa Rasilimalikale kutoka wadau ambao hawana uwezo wa kuziendeleza. Aidha, Wizara itafanya mapitio na kuhuisha Orodha ya Urithi wa Taifa katika mikoa ya Tanga, Arusha na Pwani; na tathmini ya uhifadhi na uendelezaji wa maeneo 10 ya malikale na

makumbusho saba (7). Vilevile, Wizara itawezesha vikao vinne (4) vya kitalaam vya kujadili urejeshwaji wa malikale za Tanzania zilizopo nje ya nchi. Pia, Wizara itaratibu maandalizi ya mipango minne (4) ya usimamizi, uhifadhi na uendelezaji wa maeneo ya malikale.

**382. Mheshimiwa Spika,** katika kuhamasisha uhifadhi na matumizi endelevu ya malikale, Wizara itaanzisha Jukwaa la Wadau wa Malikale, itafanya vikao viwili (2) vya wadau kuhusu utekelezaji wa Sera ya Malikale ya Mwaka 2008 na tathmini ya makumbusho binafsi 10 nchini. Kazi nyingine zitakazotekelezwa ni kushiriki katika mikutano ya kikanda na kimataifa kwa lengo la kutekeleza matakwa ya mikataba inayohusiana na malikale na kushiriki katika maonesho na matamasha ya Kitaifa kwa ajili ya kuhamasisha matumizi endelevu ya malikale. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara itashiriki Mkutano wa 48 wa Kamati ya Urithi wa Dunia kwa lengo la Utekelezaji wa Mwaka wa Urithi wa Dunia wa mwaka 1972. Aidha, Wizara itaandaa Andiko la kuomba kuorodhesha Njia ya Kati ya Biashara ya Utumwa na Vipusa katika Orodha ya Urithi wa Dunia.

#### 6.3.4.2 *Mfuko wa Taifa wa Mambo ya Kale – NFA*

**383. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Mfuko wa Taifa wa Mambo ya Kale utawezesha uandaaji wa mipango minne (4) ya usimamizi na uendelezaji wa maeneo ya malikale; tathmini ya hali ya uhifadhi wa maeneo 30 ya Urithi wa Taifa na tafiti za kimkakati. Aidha, Mfuko utawezesha uratibu na usimamizi wa mikataba ya Kikanda na Kimataifa; na maandalizi ya Andiko la kuomba kuorodhesha michoro ya miambani iliiyopo Kanda ya Ziwa Victoria katika Orodha ya Urithi wa Dunia na uwekaji wa nembo za utambulisho wa urithi wa Taifa katika maeneo 10 ya malikale.

**384. Mheshimiwa Spika,** Katika hatua nyingine, Mfuko utawezesha uhifadhi wa Nyayo za Zamadamu zilizopo Laetoli na Engarasero mkoani Arusha; na utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Kuenzi na Kusherehekea Urithi wa Mwl. Nyerere.

#### 6.3.4.3 *Shirika la Makumbusho ya Taifa - NMT*

**385.** **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Makumbusho ya Taifa la Tanzania lina jukumu la kuhifadhi, kutafiti, kuendeleza na kuelimisha jamii kuhusu urithi wa utamaduni na wa asili wa Taifa. Vilevile, Shirika linasimamia na kuendeleza vituo saba (7) vya Makumbusho ya Taifa na maeneo 107 ya Malikale yaliyopo sehemu mbalimbali Tanzania Bara.

**386.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Shirika litaendelea kulinda na kuhifadhi urithi wa malikale na mikusanyo kwa kuandaa mpango wa uhifadhi na uendelezaji wa malikale katika vituo vya Mbuamaji na Pangani, pamoja na kuandaa miongozo miwili (2) ya uhifadhi wa mikusanyo katika vituo vya makumbusho. Shirika litafanya ukarabati wa majenzi ya kale na miundombinu ya uhifadhi katika vituo vinne (4), kukusanya na kuhifadhi mikusanyo 800 ya asili na kiutamaduni na kuisajili katika mfumo wa kidijitali wa usimamizi na uhifadhi wa kumbukumbu unaojulikana kama Digital Records and Archives Management Preservation System (DRAMPS).

**387.** **Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Shirika litafanya tafiti tano (5) za masuala ya urithi wa utamaduni wa asili katika maeneo ya malikale; baadhi ya tafiti hizo zinahusu chimbuko la Mwanadamu (Zamadamu), Mji wa kale wa karne ya kwanza (Rhapta) unaosadikika kuzama katika pwani ya bahari ya Hindi, na Madhara ya mabadiliko ya tabianchi katika pwani ya Afrika ya Mashariki na Laetoli. Tafiti hizi zitasaidia kupata matokeo mapya yatakayosaidia kuhifadhi na kuendeleza urithi wa Taifa. Pia, Shirika litaandaa muongozo wa huduma za ushauri na utafiti, mfumo wa kuhifadhi nyaraka za kitafiti, na mfumo wa kuchakata vibali vya utafiti.

**388.** **Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Shirika litaendelea kuelimisha jamii kuhusu malikale kwa kutumia maonesho, programu za kielimu, na programu za kuhamasisha jamii. Shirika litaweka maonesho ya kudumu sita (6) katika vituo vya Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni Dar es Salaam (2), Tendaguru (1), Nandete (1), nyumba za asili kwa mfumo wa kaya katika Kijiji cha Makumbusho Dar es Salaam (2) na

kukarabati nyumba za asili (7). Vilevile, Shirika litaweka maonesho 10 ya muda katika vituo vya makumbusho nchini, kuratibu kazi mradi 336 za wanafunzi wa sekondari, na kuendesha programu 240 za kuelimisha jamii kuhusu urithi wa malikale. Aidha, Shirika litaendelea kuhamasisha jamii kuhusu utalii wa malikale kwa kufanya matamasha matatu (3) yakiwemo; Tamasha la Siku ya Utamaduni wa Mtanzania-Kijiji cha Makumbusho na Matamasha ya Majimaji Nandete na Songea. Pamoja na kutekeleza Mpango wa Miaka 10 wa Kuenzi na Kuhifadhi Urithi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.Vilevile, matukio 11 yatafanyika yakiwemo Mbio za Mwalimu Nyerere, Azimio la Arusha, Siku ya Zinji, warsha na programu. Aidha, Shirika litafanya vipindi 113 vya redio na 62 vya televisheni, na kushirikisha wadau na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuhifadhi na matumizi endelevu ya maeneo ya malikale.

**389. Mheshimiwa Spika,** katika kuelekea Mashindano ya AFCON 2027 na Ulimbwende (Miss World 2027), Shirika limejipanga kuboresha miundombinu ya utalii katika vituo vya Makumbusho ya Taifa kwa kuweka Onesho la Historia ya Mpira wa Miguu katika Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni, Onesho la Mila katika Kijiji cha Makumbusho, Onesho la lugha ya Kiswahili Azimio la Arusha na maonesho ya Ikolojia, Historia na chimbuko la mwanadamu Elimu Viumbe Arusha. Aidha, Shirika litazindua Makumbusho yanayotembea katika Jiji la Arusha na Dar es Salaam ili kuwafikia wageni katika maeneo mbalimbali yenye mikusanyiko ya watu. Pia Shirika litaandaa matukio ya burudani kama Usiku wa AFCON, Kijiji Soko, Museum Art Explosion na Kona za Mashabiki (Fun Zones). Vilevile, Shirika litaendelea kuimarisha mifumo ya TEHAMA katika shughuli za uhifadhi na utalii na kukamilisha ujenzi wa mfumo jumuishi wa utoaji huduma. Pia Shirika litafanya maboresho katika mfumo wa usajili wa mikusanyo unaojulikana kama Digital Records and Archives Management Preservation System (DRAMPS) na kuweka mifumo ya kidijitali katika maonesho kama QR Code, Augmented Reality na Virtual Reality.

**390. Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Shirika litaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa Makumbusho ya Marais, Dodoma kwa kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwemo

kufanya tafiti, kukusanya, na kuhifadhi taarifa na vifaa vinavyohusiana na viongozi wakuu wa nchi na tawala zao. Aidha, Shirika litasimamia kazi ya usanifu wa mpangilio wa maonesho katika Makumbusho ya Marais pamoja na kuanza taratibu za kumpata mshauri elekezi katika usimamizi wa ujenzi wa Makumbusho. Ujenzi wa makumbusho hiyo utatufanya tuandike historia kwa mitazamo ya Kitanzania na kuweka kumbukumbu sahihi za mifumo, falsafa na mchango wa viongozi kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni ili kukuza uelewa kuhusu utambulisho wa Taifa na kujenga uzalendo, msikamano na maadili mema. Katika hatua nyingine, Shirika litakamilisha ujenzi wa onesho la Dinosaria katika kituo cha Taarifa cha Palontolojia Tendaguru. Vilevile, Shirika litawezesha watumishi watano (5) kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu, watumishi 20 mafunzo ya muda mfupi na kuajiri watumishi wapya 22 wa kada mbalimbali.

### 6.3.5 *Masuala Mtambuka*

**391. Mheshimiwa Spika,** Wizara itaendelea kushiriki katika mapambano dhidi ya VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY) kwa kuwahudumia watumishi waliojiweka wazi kwa kuwapa posho maalum kwa ajili ya lishe bora na kuwahudumia watumishi wenye ulemavu. Pia, Wizara itaendelea kutoa vifaa kinga kwa watumishi wa Wizara na kuwaelimisha kuhusu umuhimu wa kutunza afya zao kupitia vipeperushi na vikao rasmi vya Wizara. Wizara inatarajia kutoa elimu kwa watumishi 6528 kuhusu masuala afya ya akili, VVU na UKIMWI. Aidha, itawawezesha watumishi wenye mahitaji maalum kwa kuwapatia mahitaji yao na kuratibu ushiriki wao katika Siku ya Watu wenye Ulemavu.

**392. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa kwa kufanya vikao vinne (4) vya Kamati ya Uadilifu. Aidha, Wizara itaratibu utoaji wa elimu kwa watumishi 5665 kuhusu uelewa wa masuala ya mapambano dhidi ya rushwa na maadili na kuwahimiza watumishi kutoa huduma kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, taratibu, maadili ya Utumishi wa Umma, uwajibikaji pamoja na utekelezaji wa majukumu wakizingatia Mkataba wa

Huduma kwa Mteja. Vilevile, Wizara itaratibu na kuandaa mpango kazi wa Wizara wa kupinga masuala ya rushwa ya ngono mahala pa kazi.

**393. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utendaji kazi wa watumishi na kuwajengea uwezo wa kumudu majukumu yao kwa ufanisi, Wizara itawawezesha jumla ya watumishi 5,283 kupata mafunzo ya muda mrefu (382); muda mfupi (2,954); na mafunzo ya Jeshi la Uhifadhi (1,947). Vilevile, Wizara itaendelea kuratibu upatikanaji wa stahili za watumishi kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo, kununua vitendea kazi kwa ajili ya kuweka mazingira wezeshi kwa watumishi katika kutekeleza majukumu yao. Sambamba na hilo, Wizara itaratibu na kuandaa Mpango wa urithishanaji madaraka; kuhuisha Mkataba wa Huduma kwa Mteja. Katika kutekeleza azma ya Serikali ya kuimarisha afya za watumishi, Wizara itaendelea kuhimiza na kuwawezesha watumishi kufanya mazoezi; kushiriki michezo ya SHIMIWI, SHIMMUTA, Mei Mosi na Mabonanza ya wafanyakazi; na kuratibu ushiriki wa watumishi wa Wizara katika sherehe za maadhimisho ya Kitaifa.

**394. Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kukabiliana na upungufu wa watumishi, Wizara itaendelea kuratibu upatikanaji wa watumishi kulingana na mahitaji, ambapo katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Wizara inatarajia kuajiri watumishi wa kada mbalimbali 1,180 na kupandisha vyeo watumishi 2,594. Aidha, itawezesha upatikanaji wa magari 35, pikipiki 33, vitendea kazi pamoja na samani za ofisi. Vilevile, itawezesha ujenzi wa nyumba nane (8) na ukarabati wa nyumba 195 za watumishi.

### 6.4 *Miradi ya Maendeleo*

**395. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 62,301,445,000.00** kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 23,134,770,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 39,166,675,000.00** ni fedha za nje. Fedha za maendeleo zinajumuisha **Shilingi 13,686,497,742.00** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Idara na Vitengo vilivyo chini ya Wizara; na **Shilingi 48,614,947,258.00** za Miradi itakayotekelezwa na Taasisi (TANAPA, TAWA, TFS, NMT, NCT na TAWIRI).

**396.** **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara itatekeleza miradi ya maendeleo kama ifuatavyo:-

**(i)** ***Mradi wa Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (Public Finance Management and Reform Programe VI)***

**397.** **Mheshimiwa Spika,** mradi huu ni wa ubia baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki ya Dunia. Katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 mradi utatumia **Shilingi 57,476,764.00** fedha za ndani kwa ajili ya kuwezesha mafunzo kwa watumishi sita (6) kuhusu Usimamizi wa Fedha na Miradi ya maendeleo.

**(ii)** ***Mradi wa Kuendeleza Utalii Kusini mwa Tanzania***

**398.** **Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 mradi utatumia **Shilingi 9,341,280,593.00** fedha za ndani kuboresha miundombinu ya utalii. Aidha, Serikali itatekeleza miradi muhimu ikiwemo:-

a. Ukamilishaji wa jengo la Kituo cha Utangazaji Utalii Kusini mwa Tanzania (Southern Tanzania Destination Marketing Center) katika eneo la Kihesa Kilolo – Iringa;
b. Kuwezesha huduma za ushauri elekezi katika ujenzi wa Kituo cha Utangazaji Utalii Kusini mwa Tanzania katika eneo la Kihesa Kilolo-Iringa;
c. Ukamilishaji wa ujenzi wa daraja la juu ya miti (canopy walkway) katika hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa;
d. Ujenzi wa banda (4 in one) katika Hifadhi ya Kitulo; na
e. Ujenzi wa vibanda vitano (5) vya kioo (Spacedoms) katika Pori la Akiba la Mpanga Kipengere.

**(iii)** ***Mradi wa Kujenga Uwezo wa Maeneo ya Hifadhi, Mapori ya Akiba na Kikosi Dhidi ya Ujangili (Capacity Building in Game Reserves)***

**399.** **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unatekelezwa kwa fedha za ndani, kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 mradi utatumia **Shilingi 1,114,138,124.00** kutekeleza shughuli zifuatazo:-

a. Kuwezesha hatua ya mchoro wa ghala la Taifa la kuhifadhi nyara za Serikali na ujenzi wa ukuta kuzunguka eneo la uwanja;

b. Kununua vitendea kazi kwa ajili ya kuimarisha shughuli za uhifadhi;

c. Kununua visukuma mawimbi 50 pamoja na mabomu baridi 20,000; na

d. Kufanya ukarabati wa vyumba vinne (4) vya madarasa, ujenzi wa bwalo la chakula na kumalizia mfumo wa maji na umeme katika mabweni manne (4) kituo cha mafunzo kwa vitendo Matongo, wilayani Bariadi kupitia Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi.

**(iv) *Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi na Mafunzo ya Misitu na Ufugaji Nyuki (Capacity Building in Forestry and Beekeeping)***

**400. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 mradi huu utatumia **Shilingi 570,403,992.00** fedha za ndani kutekeleza shughuli zifuatazo:-

a. Kuendelea na ujenzi wa maabara ya mafunzo kwenye Chuo cha Ufugaji Nyuki - Tabora (BTI);
b. Kukarabati madarasa matatu (3), mabweni mawili (2) na karakana ya useremala FITI;
c. Kukarabati Bwalo la chakula, jengo la sampuli za mimea, maabara na nyumba tano (5) za watumishi FTI; na
d. Kukarabati maabara ya utafiti iliyopo Makao Makuu ya TAFORI Morogoro.

**(v) *Mradi wa Usimamizi wa Mifumo ya Chakula, Matumizi Bora ya Ardhi na Urejeshaji wa Uoto wa Asili Tanzania (Food Systems, Land Use and Restoration in Tanzania's Landscapes - FOLUR)***

**401. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unafadhiliwa na Mfuko

wa Mazingira wa Dunia (Global Enviromental Facility – GEF) na katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 utatumia **Shilingi 1,694,218,836.00** fedha za nje kutekeleza shughuli zifuatazo: -

a. Kuwezesha uongoaji wa hekta 10,000 za ardhi iliyoharibika katika misitu, maeneo oevu na ardhi ya uzalishaji kwa kuzingatia mipango ya Usimamizi Shirikishi wa Mandhari (ILM) kwa mandhari ya Kilombero na Zanzibar;

b. Kuwezesha jamii katika maeneo ya kipaumbele ya uhifadhi kutekeleza mipango mahususi ya usimamizi na utendaji wa jukwaa la wadau mbalimbali wa Mandhari ya Kilombero na Unguja;

c. Kuandaa mifumo ya kifedha itakayosaidia usimamizi endelevu wa mandhari na urejeshaji kwa wakulima wadogo wadogo na sekta binafsi;

d. Kufanya warsha za mashauriano kati ya wadau kuhusu Mfumo wa Usimamizi Shirikishi wa Mandhari katika vijiji 10 vya Kilombero na Unguja kupitia majukwaa ya Wadau;

e. Kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 15 kwa kuzingatia maeneo ya kipaumbele yaliyobainishwa na Kufanya mafunzo na kujenga uwezo kuhusu Usimamizi Shirikishi wa Mandhari (ILM) katika vijiji 15 vya Kilombero na Zanzibar;

f. Kutoa mafunzo kuhusu mbinu za uzalishaji endelevu wa zao la mpunga kwa maafisa ugani na vikundi 17 vya wakulima;

g. Kuwezesha utekelezaji wa mipango endelevu ya mnyororo wa thamani wa zao la mpunga katika vijiji vitano (5) katika sekta ya uzalishaji kwa Mandhari ya Kilombero na Zanzibar;

h. Kuwezesha utekelezaji wa maandiko na mipango ya biashara katika mnyororo wa thamani wa uzalishaji endelevu wa mpunga kupitia wadau wa mradi;

i. Kuwezesha utekelezaji wa mapendekezo ya maandiko ya sera kwa ajili ya kuboresha mifumo ya umiliki wa ardhi na usimamizi wa rasilimali za maji; na

j. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mradi.

**(vi) *Mradi wa Kuimarisha Usimamizi wa Mashamba ya Miti ya Serikali (Enhancing Management of State Forest Plantations)***

**402. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Ufaransa na katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 utatumia **Shilingi 10,410,020,174.00** fedha za nje kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

a. Kuendeleza mashamba matatu (3) ya miti ya Silayo, Mtibwa na Wino;

b. Kuotesha miche ya miti 6,444,300 itakayopandwa katika eneo la hekta 4,500;

c. Kujenga miundombinu ya barabara kilomita 125.1 na vifaa vya kuzuia moto; na

d. Kujenga vituo vya ulinzi vinne (4), ununuzi wa magari nane (8) na ununuzi wa mitambo mitatu (3) kwa ajili ya mashamba hayo matatu (3).

**(vii) *Mradi wa Uendelezaji wa Utalii wa Mikutano na Matukio (MICE Tourism Development Project)***

**403. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unatekelezwa kwa fedha za ndani na kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 utatumia **Shilingi 908,979,433.00** kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

a. Kufanya maandalizi ya Michoro ya kina ya Ukumbi wa Mikutano na Matukio (Detailed Designs), tathmini ya athari za Kijamii (ESIA) na Kimazingira (EIA), pamoja na makadiro ya gharama (Bill of Quantities) za ujenzi kwa mradi wa MICE; na

b. Kuimarisha DDMCC na mfumo wa Destination Portal kwa kutengeneza maudhui na kuongeza lugha za kimataifa zikiwemo lugha za (Kiarabu, Kirusi, Kichina (Mandarin), Kihindi, Kifaransa, Kihispania na Kireno), kulipia nafasi ya kutunza data katika NIDC na kuongeza uwezo wa GPU, kutoa mafunzo kwa wadau juu ya mfumo na namna bora ya kuutumia pamoja na kuendeleza Kituo cha Utangazaji Utalii Kidijitali kupitia mfumo wa "Travel Companion".

**(viii)** ***Mradi wa Kujenga Uwezo na Kuimarisha Chuo cha Taifa cha Utalii (The National College of Tourism Capacity Building and Institutional Strengthening)***

**404.** **Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 mradi huu utatumia fedha za ndani kiasi cha **Shilingi 1,654,595,091.00** kwa ajili ya ukamilishaji wa shughuli za ujenzi wa jengo la taaluma Kampasi ya Arusha.

**(ix)** ***Mradi wa Ujenzi wa Makumbusho ya Marais, Dodoma***

**405.** **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, mradi huu utatumia jumla ya **Shilingi 1,000,000,000.00** kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

a. Kuratibu na kufanya tafiti zinazohusiana na kukusanya, kusajili na kuhifadhi taarifa na vifaa vinavyohusiana na viongozi wakuu wa nchi na tawala zao; na

b. Kufanya usanifu wa mpangilio wa maonesho katika Makumbusho ya Marais.

**(x)** ***Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya TAWIRI***

**406.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Nchini (TAWIRI) katika kuimarisha mazingira rafiki ya kufanyia kazi kwa watumishi, Taasisi imetengewa fedha za ndani **Shilingi 1,000,000,000.00** kwa ajili ya kuendelea na mradi wa ujenzi wa jengo la Makao Makuu. Aidha, jengo hili litakuwa na miundombinu ya ofisi za watumishi, maabara za wanyamapori na kumbi za mikutano.

**(xi)** ***Miradi ya TANAPA***

**407. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) litatumia kiasi cha **Shilingi 27,062,435,990.00** fedha za nje chini ya ufadhili wa Benki ya watu wa Ujerumani (KfW) ili kutekeleza miradi ya kimkakati inayolenga kuimarisha uhifadhi, kuboresha huduma za jamii na vitendea kazi. Miradi itakayotekelezwa ni pamoja na Mradi wa Dharura wa Urejeshaji wa Bioanuai Tanzania; Mradi wa Kuendeleza na Kuhifadhi Mfumo wa Ikolojia ya Serengeti awamu ya I na II; Mradi wa Kuhifadhi Ikolojia ya Hifadhi za Taifa Katavi, Mahale na Ushoroba Unganishi; pamoja na Mradi wa Kuboresha Mawasiliano katika Hifadhi ya Taifa Serengeti. Miradi hii inatekelezwa katika Hifadhi za Taifa za Serengeti, Nyerere, Katavi na Milima ya Mahale pamoja na Wilaya za Serengeti, Ngorongoro, Uvinza na Tanganyika, ikiwa imelenga kuimarisha ulinzi wa rasilimali za asili na kuongeza ufanisi wa usimamizi wa hifadhi.

**408. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha miundombinu ya uhifadhi na utalii kupitia Mradi wa Dharura wa Urejeshaji wa Bioanuai Tanzania, Shirika litajenga na kuimarisha vituo vya usimamizi na ulinzi ikiwemo wildlife holding boma katika mradi wa faru Moru ndani ya Hifadhi ya Taifa Serengeti; ujenzi wa vituo vitatu (3) vya askari vya kuhamishika (Miradi ya faru Ndasiata – 2 na Nyamalumbwa - 1); ujenzi wa karakana ya ndege Hifadhi ya Taifa Nyerere; ujenzi wa nyumba ya walimu (2 in 1) katika kijiji cha Iharara (Serengeti); ujenzi wa matenki mawili (2) ya kuhifadhia maji Matambwe na kukamilisha uchimbaji wa visima vinne (4) vya maji katika vituo vya askari vya Bomaulanga, Likuyu Sekamaganga, Liwale na Kalulu katika Hifadhi ya Taifa Nyerere.

**409. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha huduma za jamii kupitia Mradi wa Kuendeleza na Kuhifadhi Mfumo wa Ikolojia ya Serengeti Awamu ya I na II Shirika litajenga zahanati katika kijiji cha Maalon; nyumba tatu (3) za madaktari (2 in 1) katika vijiji vya Njoroi, Naan na Yosamditu katika wilaya ya Ngorongoro; na ukuta wa shule ya sekondari Loliondo katika Wilaya ya Ngorongoro. Vilevile, Shirika litachimba mabwawa mawili (2) katika vijiji vya Nyamandicha Wilaya ya Serengeti na Piyaya Wilaya ya

Ngorongoro pamoja na kuweka mifumo ya nishati ya jua katika zahanati saba (7) ili kuboresha huduma za afya katika kata ya Samunge, Soitsambu, Enguserosambu na Maalon katika Wilaya ya Ngorongoro. Sambamba na hilo, katika kuboresha makazi ya watumishi Shirika litajenga nyumba za askari na ofisi tano (5) eneo la Fort Ikoma katika Hifadhi ya Taifa Serengeti, kuboresha miundombinu ya upatikanaji wa maji hifadhini kwa kuchimba visima na kujenga mifumo ya kuvuna maji ya mvua katika lango la Ndabaka Hifadhi ya Taifa Serengeti. Sambamba na hilo, Shirika litajenga ofisi ya Mkuu wa Hifadhi eneo la Seronera, ofisi za watumishi katika viwanja vya ndege vya Lobo na Kusini; pamoja na malango ya Naabi na Ndutu. Shirika litajenga daraja la Kogatende na barabara unganishi katika Hifadhi ya Taifa Serengeti ambalo ni muhimu kwa shughuli za utalii.

**410. Mheshimiwa Spika,** kupitia Mradi wa kuhifadhi ikolojia ya hifadhi za Taifa Katavi, Milima Mahale na ushoroba unganishi (KAMACO) unaotekelezwa katika hifadhi za Taifa Katavi na Milima Mahale, Shirika litajenga madaraja ya Mongwe na Kapirula pamoja na nyumba ya askari katika Hifadhi ya Taifa Katavi; kufungua barabara ya kilomita 77 kutoka Ikamba hadi Lufubu ili kuboresha miundombinu ya hifadhi na kuongeza ufanisi wa ulinzi wa rasilimali katika eneo la Mashariki mwa Hifadhi ya Taifa Milima Mahale. Vilevile, Shirika litajenga nyumba moja (1) ya watumishi na rest house kwa ajili ya wageni katika Hifadhi ya Taifa Milima Mahale.

**411. Mheshimiwa Spika,** kupitia Mradi wa kuboresha mawasiliano Hifadhi ya Taifa Serengeti (Digital Traffic Management System-DTMS), Shirika litajenga minara 10 ya mawasiliano na taarifa katika hifadhi za Taifa Serengeti (4), Ngorongoro (1), Ziwa Manyara (2), Tarangire (2) pamoja na Ofisi ya Makao Makuu ya Shirika (1). Vilevile, Shirika litanunua na kufunga mfumo wa kufuatilia magari ya wageni na kujenga vyumba vya mawasiliano (control rooms) ili kuboresha usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za utalii.

**(xii) *Miradi ya TAWA***

**412. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania itatumia kiasi cha **Shilingi 7,487,896,003.00** kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo: -

a. Ujenzi wa vituo vitano (5) vya askari katika Wilaya za Madaba (1), Liwale (1), Kilwa (1), Chunya (1) na Bariadi (1);

b. Ujenzi wa vizimba 10 katika Wilaya za Bunda (2), Buchosa (2), Sengerema (2), Kilosa (2), Busega (1) na Nyasa (1);

c. Uchimbaji wa mabwawa matatu (3) katika Mapori ya Akiba Lwafi (1), Ugalla (1) na Ikorongo (1);

d. Ujenzi wa kilomita 17 za barabara katika Pori la Akiba Rukwa;

e. Ujenzi wa gati dogo katika eneo la utalii Kisiwa cha Lundo;

f. Kuanza ujenzi wa jengo la Makao Makuu Jijini Dodoma;

g. Ujenzi wa vituo vya burudani na michezo mbalimbali kwa watumishi katika Mapori ya Akiba Piti na Kilombero; na

h. Ununuzi wa vitendea kazi ikiwemo magari mawili (2), boti tatu (3), ndege nyuki (drones) 10, visukuma mawimbi-GPS Satellite Collars 10, mahema 500 ya doria, mabomu baridi 5,000, virushio vya mabomu baridi (launchers) 22 na samani za ofisi kwa ajili ya ofisi za Mapori ya Akiba Kilombero, Rukwa, Ugalla na Inyonga.

## 7.0 SHUKURANI

**413.** **Mheshimiwa Spika,** ninatumia nafasi hii kutoa pongezi na shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake thabiti, miongozo yenye tija na maelekezo muhimu anayoyatoa katika Sekta ya Maliasili na Utalii, ambayo yameiwezesha sekta hii kuendelea kuimarika, kupanuka na kutoa mchango mkubwa katika ustawi wa wananchi pamoja na maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Aidha, napenda pia kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti wa Bunge na Kamati zake za Kudumu, kwa ushirikiano wenu muhimu katika kuliongoza kwa ufanisi Bunge letu Tukufu.

**414. Mheshimiwa Spika,** kabla ya kufunga hoja yangu, ninapenda kuchukua nafasi hii kumpongeza na kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa ushirikiano wake wa karibu anaonipatia katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, ninatoa shukrani za dhati kwa Katibu Mkuu pamoja na Naibu Katibu Mkuu kwa mchango wao, ushauri na uongozi imara katika kuendesha shughuli za Wizara na taasisi zake. Vilevile, nawapongeza na kuwashukuru Wakurugenzi wa Idara, Wakuu wa Vitengo, Wenyeviti wa Bodi zilizo chini ya Wizara, Viongozi wa Taasisi pamoja na watendaji wote kwa ushirikiano na juhudi zao zisizo na kikomo katika kutekeleza majukumu ya kila siku ya Wizara.

**415. Mheshimiwa Spika,** ninapenda kutumia nafasi hii kutoa shukrani zangu za kipekee kwa wadau wote wa Wizara yetu, wakiwemo Washirika wa Maendeleo, kwa mchango wao mkubwa katika utekelezaji wa programu, miradi na mipango mbalimbali ya Wizara. Ushiriki wao umeendelea kuimarisha jitihada za Serikali katika kuhakikisha wananchi wanapata ustawi na maendeleo endelevu. Ninawathibitishia kuwa Wizara inaelewa na kuuthamini mchango wenu muhimu. Pia, Wizara itaendelea kufungua milango ya ushirikiano zaidi kwa lengo la kuleta maendeleo endelevu ya sekta yetu na Taifa zima.

**416. Mheshimiwa Spika,** ninapenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Nchi rafiki, Jumuiya za Kikanda, Mashirika ya Kimataifa, Taasisi za Serikali pamoja na wadau wengine wakiwemo sekta binafsi kwa mchango wao wa kipekee katika kukuza na kuendeleza sekta ya Maliasili, Malikale na Utalii. Ushirikiano wao umeendelea kuwa nguzo muhimu katika kuharakisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya taifa letu. Aidha, ninatoa shukrani maalum kwa Serikali za Canada, China, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Korea Kusini, Marekani, Morocco, Namibia, Norway, Ubelgiji, Ufaransa, Ufini, India, Ujerumani, Uswisi, Oman, Italia, Japan, Urusi, Iran, Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Jumuiya ya Umoja wa Nchi za Ulaya kwa kuendeleza ushirikiano wao nasi.

**417. Mheshimiwa Spika,** ninaomba kwa namna ya kipekee

kuyashukuru na kuyatambua Mashirika na Taasisi za Kimataifa ambazo zimeendelea kushirikiana na Serikali katika kuimarisha Sekta ya Maliasili na Utalii. Mashirika na Taasisi hizo ni pamoja na: EU, AfDB, AWF, AWHF, ENABEL, FAO, FZS, GEF, GIZ, ICCROM, ICOM, ICOMOS, ILO, IMF, ITC, IUCN, KfW, NORAD, RTI, PAMS Foundation, Trade Aid, UNDP, UNESCO, UN-Tourism, IORA, USAID, UNEP, Honey Guide Foundation, CIFOR, ICRAF, INBAR, GATSBY, FOREST-FARM FACILITY, SIX RIVERS, WCS, WHC, WTTC, TNC, UNOPS, SADC-TFCA, TPW, OIKOS East Africa, Fredkin Conservation Fund, Grumet Fund, STEP, World Bank, Wild Aid, WMF, WWF, CIFOR, APIMONDIA, National Museum of China, Humboldt Forum - Berlin na CYARC-USA. Ushirikiano wao umeendelea kuwa nguzo muhimu katika kuhifadhi, kulinda na kuendeleza rasilimali zetu kwa maendeleo ya Taifa.

**418. Mheshimiwa Spika,** ninaomba pia nitumie fursa hii kuwashukuru wadau wote wa ndani wa Sekta ya Maliasili na Utalii wakiwemo: TCT, TATO, HAT, TAHOA, TLTO, TTGA, KGA, NTSGS, IGS, TGS, KTGA, NGTF, KPA, TPO, TACTO, TAOA, TAHA, TAWTO, TWEA, CWMAC, TABEDO, TAF, TTGAU, API-SUPPORT, HEAT, SHIVIMITA, TASOTA, FGCI, TPA, STTGS, ADEA, DARCH, Fahari Yetu, Kilwa Division Development Association (KIDDA), Urithi Wetu, Makumbusho ya Kanyigo, Taasisi ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino (SAUT), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Makumbusho ya Wasukuma na Kituo cha Taarifa Bujora, Dr. Salim Ahmed Salim Foundation, Benki Kuu ya Tanzania, BASATA, TAFCA, Beegreen, Misitu Jamii, Nature Tanzania na wadau wote wanaoshiriki kikamilifu katika shughuli za uhifadhi wa maliasili, malikale, uendelezaji na utangazaji utalii ikiwemo ofisi zetu za Ubalozi nje ya Nchi.

**419. Mheshimiwa Spika,** kwa heshima na moyo wa unyenyekevu, ninapenda kuthamini mchango wa Viongozi wetu wa Dini na Viongozi wa Kimila katika kuielimisha jamii, kuongoza na kushiriki kikamilifu katika juhudi za uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za nchi yetu, zikiwemo wanyamapori, misitu na malikale. Viongozi hawa wamekuwa mstari wa mbele katika kuelimisha, kuhamasisha jamii kulinda na kuhifadhi maliasili za taifa, kupambana na ujangili, kuzuia ukataji holela wa miti,

kulinda malikale dhidi ya uharibifu, pamoja na kuhimiza utalii wa ndani unaozingatia mila, desturi na uhifadhi wa mazingira. Aidha, ninatambua kwa dhati mchango mkubwa wa taasisi za elimu ikiwemo vyuo vikuu, vyuo vya kati, shule za sekondari na msingi kwa juhudi zao katika kulinda rasilimali za misitu na nyuki kupitia uanzishaji wa vitalu vya miti na miradi ya ufugaji nyuki. Vilevile, napongeza mchango wa taasisi za utafiti kwa ushirikiano wao kwa Wizara katika kubuni na kutoa suluhisho la changamoto mbalimbali zinazoikabili Sekta ya Maliasili na Utalii. Sambamba na hilo, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa vyombo vya ulinzi na usalama, taasisi za himasheria pamoja na vyombo vya habari kwa ushirikiano wao endelevu kwa Wizara ya Maliasili na Utalii katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yetu.

**420.** **Mheshimiwa Spika,** ninaomba nitumie fursa hii kuwashukuru tena Watanzania wote kwa kuendelea kuunga mkono jitihada za kuendeleza Sekta ya Maliasili na Utalii. Aidha, ninawapongeza kwa ushiriki wao katika shughuli za uhifadhi wa Maliasili, Malikale pamoja na kuendeleza Sekta ya Utalii. Nitumie fursa hii kuwaomba wadau wote kuendelea kutoa ushirikiano kwa Wizara ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Ninawahakikishia kuwa Wizara inatambua na kuthamini mchango wenu na itaendelea kuimarisha na kufungua milango ya ushirikiano zaidi kwa maendeleo ya sekta yetu na Taifa kwa ujumla.

## 8.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2026/2027

**421.** **Mheshimiwa Spika,** ili Wizara iweze kutekeleza malengo na vipaumbele iliyojiwekea, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 334,345,870,000.00** kwa matumizi ya Fungu 69 kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 272,044,425,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 62,301,445,000.00** ni za Miradi ya Maendeleo.

**422.** **Mheshimiwa Spika,** fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha **Shilingi 144,691,490,000.00** za Mishahara na **Shilingi 127,352,935,000.00** za Matumizi Mengineyo. Fedha za Miradi ya Maendeleo zinajumuisha **Shilingi 23,134,770,000.00** fedha za ndani na **Shilingi 39,166,675,000.00** fedha za nje.

## 9.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** ninapenda kuhitimisha kwa kutoa rai kwa Watanzania wote kuendelea kushiriki kikamilifu katika uhifadhi na uendelezaji endelevu wa Maliasili, Malikale na Utalii, ambazo ni nguzo muhimu za uchumi wa Taifa letu na urithi wa vizazi vijavyo. Uhifadhi wa rasilimali hizi si jukumu la Serikali pekee, bali ni wajibu wa kila Mtanzania katika kulinda na kuendeleza urithi wa Taifa letu. Aidha, ninaomba tena kutoa shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

**423.** **Mheshimiwa Spika,** Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maliasili na Utalii: www.maliasili.go.tz

**424.** **Mheshimiwa Spika,** ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, hoja imetolewa na hoja imeungwa mkono. Nimwite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava. *(Makofi)*

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 121(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2025, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii Fungu 69, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea niombe taarifa yetu yote ya Kamati iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa mezani kwako mapema leo asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza ni utangulizi inayotoa msingi wa uchambuzi na mawanda ya uchambuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili inatoa uchambuzi na tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2025/2026, pamoja na uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027, sehemu ya tatu inafafanua maoni na ushauri wa Kamati unaotolewa kwa Serikali pamoja na kuhitimisha taarifa ya uchambuzi wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa uchambuzi. Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Katika hatua hiyo, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na kuja na matokeo kama yalivyoainishwa katika taarifa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi uliofanywa na Kamati uligusa maeneo yafuatayo:-

(i) Utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2026/2026;

(ii) Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 202026/2027;

(iii) Makadirio ya Mapato;

(iv) Mambo muhimu yanayogusa sekta ya maliasili na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uchambuzi, Kamati iliongozwa na kigezo cha asilimia pamoja na kufanya tathmini ya jumla ya ulinganisho wa mambo mbalimbali ambayo yaliwezesha Kamati kubaini hatua iliyofikiwa katika utekelezaji na mantiki ya mpango na makadirio kwa mwaka fedha unaokuja 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi na tathmini. Uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120 (1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilichambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya maliasili na utalii baada ya kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha. Sehemu hii inafafanua mambo manne muhimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ni uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati. Katika kulisaidia Bunge lako Tukufu kutekeleza jukumu lake na kuishauri Serikali, tarehe 19 Mei, 2025, wakati wa uwasilishwaji wa hotuba ya mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kamati ilitoa maoni na ushauri kuhusu mambo nane. Ili kupima tija ya Bunge kuendelea kuishauri Serikali, Kamati ilitaka kubaini iwapo ushauri uliotolewa umezingatiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 26 Machi, 2026, Waziri wa Maliasili na Utalii alifika mbele ya Kamati kuwasilisha taarifa kuhusu hatua iliyofikiwa katika kuzingatia ushauri wa Kamati. Kamati ilichambua taarifa na kubaini kwamba Wizara imezingatia ushauri wa Kamati kwenye maeneo manne na utekelezaji wake uko katika hatua mbalimbali. Aidha, Kamati haikuridhika na utekelezaji na uzingatiaji wa ushauri wa Kamati katika maeneo mengine manne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzingatiwaji usioridhisha wa maoni na ushauri wa Kamati katika kutimiza majukumu ya Wizara unaweza kupunguza ufanisi na kupelekea kuzorotesha ustawi wa wananchi kinyume na lengo la Serikali katika Ibara ya 8(1)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa miradi ya maendeleo. kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120(1), Kamati ilifanya ziara katika Mikoa mitatu ya Manyara, Arusha, na Kilimanjaro, ili kukagua baadhi ya miradi inayotekelezwa na Wizara ya Maliasili na Utalii. Kamati ilikagua jumla ya miradi minne, ambayo ni mradi wa ujenzi wa lango la kuingilia Hifadhi ya Taifa ya Tarangire, ujenzi wa makumbusho ya Jiopaki ya Ngorongoro, mradi wa ujenzi wa

jengo la mafunzo katika Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka, na mradi wa Faru Weusi katika Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yatokanayo na ukaguzi wa miradi. Katika ziara ya ukaguzi wa miradi inayotekelezwa na Wizara ya Maliasili na Utalii, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa miradi na kuona hali halisi kwenye maeneo ya utekelezaji wa miradi husika, lengo likiwa ni kulinganisha na kubaini iwapo taarifa zilizowasilishwa na Wizara zinawiana na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji pamoja na madhumuni ya miradi inayohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua iliyofikiwa katika ukusanyaji wa maduhuli. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 1,185,584,115,330, hadi kufikia Februari, 2026 Wizara ilikuwa imekusanya shilingi 895,818,665,714, sawa na 75% ya lengo la makusanyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia takwimu hizi, Kamati imewianisha muda wa utekelezaji wa bajeti na hatua iliyofikiwa katika ukusanyaji wa maduhuli na kubaini kuwa mwenendo huu wa makusanyo unaonyesha kuwa lengo linaweza kufikiwa ifikapo mwishoni mwa mwaka wa fedha. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii. Taswira kamili ya hali ya ukusanyaji wa mapato ni kama inavyoonekana kwenye kielelezo Namba Moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi kutoka Hazina. Utekelezaji wa bajeti unategemea upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara iliidhinishiwa kutumia shilingi 336,518,895,000 kwa ajili ya Matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Februari, 2026, Wizara ilikuwa imepokea shilingi 206,903,257,247, sawa na 62% tu ya fedha iliyoidhinishwa. Taswira halisi ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina ni kama inavyoonekana kwenye kielelezo Namba Mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa mpango na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027; Kamati ilichambua na kujadili mpango wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa

mwaka wa fedha 2026/2027. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo:-

(i) Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2026/2027;

(ii) Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027;

(iii) Ulinganisho wa bajeti ya Wizara na Bajeti ya Taifa na mambo muhimu yanayogusa sekta ya maliasili na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kwa kutambua uwiano uliopo kati ya mapato na matumizi, Kamati ilipokea ufafanuzi kuhusu lengo la maduhuli kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ambapo Wizara ya Maliasili na Utalii Fungu 69 inakadiriwa kukusanya maduhuli ya shilingi 1,468,724,740,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati ilifanya uchambuzi wa kuzingatia uzoefu uliopatikana katika ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha unaokwisha. Taswira ya ulinganisho wa makusanyo na maduhuli kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ni kama inavyoonekana kwenye kielelezo namba saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli yameongezeka kwa 24% ikilinganishwa na mwaka wa fedha unaokwisha. Aidha, kwa mtiririko wa makusanyo kwa mwaka unaoisha, unaonyesha kuwa lengo la ukusanyaji wa maduhuli unaweza kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taswira ya ulinganisho wa makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ni kama inavyoonekana kwenye kielelezo namba nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa mambo mahsusi katika sekta ya maliasili na utalii. Changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu. Pamoja na mafanikio yanayopatikana katika sekta ya maliasili na utalii, migongano baina ya binadamu na wanyamapori ni moja ya changamoto kubwa inayoikabili

sekta hii kwa sasa. Katika Halmashauri 184 nchini, Halmashauri 91 sawa na 49.5% zinakabiliwa na changamoto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanyama wanaoleta changamoto hii kwa sehemu kubwa ni pamoja na tembo, mamba, viboko, nyumbu, ngedere, na nyani, huku taarifa zikionyesha kwamba 80% ya migongano hiyo inasababishwa na mnyama tembo. Madhara yanayotokana na changamoto hiyo ni pamoja na vifo, ulemavu wa muda na ulemavu wa kudumu na wananchi kujeruhiwa, uharibifu wa mali za wananchi kama vile mazao, miundombinu ya makazi, maji na barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifahamishwa kuwa sababu za migongano baina ya binadamu na wanyamapori ni kukosekana au kutozingatiwa kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi, kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu, mabadiliko ya tabianchi na ongezeko la mimea vamizi katika maeneo yaliyohifadhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifahamishwa jitihada za Serikali kupambana na changamoto hii ambazo ni kuongeza doria za kudhibiti wanyamapori, ununuzi wa pikipiki za doria, ujenzi wa vizimba, uchimbaji wa visima na mabwawa katika maeneo ya hifadhi, ujenzi wa vituo vya Askari, ufungaji wa visukuma mawimbi kwa wanyamapori ambao ni viongozi wa makundi ya wanyama, pamoja na uvunaji wa wanyama mbalimbali. Kielelezo namba sita kinaonyesha utekelezaji wa mpango na jitihada za Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada za Serikali, Kamati imebaini kwamba changamoto hii ni kubwa na athari, madhara na malalamiko yake ni dhahiri. Hali hii inawaumiza wananchi, inaharibu uchumi na kuwachonganisha na Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupunguza maumivu ya changamoto hii, Serikali iliweka utaratibu wa kutoa kifutajasho na kifutamachozi kwa wananchi wanaokumbwa na changamoto hii. Hata hivyo, Kamati inaona bado kasi ya kutenga na kulipa fedha

za kifutajasho na kifutamachozi hairidhishi, na hivyo wananchi wengi waliohakikiwa madai yao kutolipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalan, hadi tarehe 21 Januari, 2026 Wizara ilikuwa imepokea madai kutoka kwa wananchi 62,446 yenye jumla ya shilingi bilioni 18.67 kutoka katika Halmashauri 56 nchini. Hadi kufikia tarehe 20 Machi, 2026 Wizara ilikuwa imelipa madai kwa wananchi 15,153 tu yenye thamani ya shilingi bilioni 7.2, huku wananchi 47,293 wakiwa hawajalipwa madai yao ambayo ni shilingi bilioni 11.47 na baadhi ya madai yamekuwepo kwa zaidi ya miaka miwili. Ucheleweshaji huu wa malipo unapoteza maana halisi ya kifutajasho na kifutamachozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inatenga na kutoa fedha ili kulipa madai ya kifutajasho na kifutamachozi kwa wakati, ifanye utafiti wa kina juu ya changamoto hii, na iendelee kuchukua hatua mbalimbali za utatuzi wa changamoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii wa malikale. Utalii wa malikale nchini unahusisha kutembelea maeneo ya kihistoria kama vile michoro ya mambo ya kale, magofu, mapango, mifupa ya wanyama wakali na makumbusho ili kujifunza utamaduni na historia. Tanzania imebarikiwa kuwa na maeneo mengi ya malikale ambayo Kamati inaona hayajawekewa mikakati ya kutosha kutangazwa ili kuvutia na kuongeza watalii wa ndani pamoja na watalii wa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Utalii Tanzania *(TTB)* ni taasisi ya umma iliyoanzishwa kwa Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania Sura ya 364 kama ilivyo rejewa mwaka 2002, ikitakiwa kuchukua majukumu ya liliyokuwa Shirika la Utalii Tanzania. Sheria iliyounda *TTB* inaainisha majukumu ya *TTB* ambayo kimsingi ni kutangaza na kuendeleza aina zote za utalii nchini. Kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania kinaeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya uchambuzi wa taarifa mbalimbali ziliwasilishwa na Serikali kwa lengo la kupima ufanisi katika utendaji wa Bodi ya Utalii Tanzania. Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa pamoja na hatua za

Serikali kuendelea na mchakato wa kufanya mapitio ya sheria ya uanzishwaji wa bodi hii ili kuihuisha iendeane na mahitaji ya sasa, bado bodi imekabiliwa na changamoto kubwa ya ufinyu wa bajeti katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna mwingiliano mkubwa wa kimajukumu baina yake, Wizara na Taasisi nyingine ndani ya Wizara. Vilevile Bodi inakabiliwa na upungufu wa wataalam wa kutosha wenye uzoefu, ujuzi na ubobevu katika kutangaza utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2025 - 2030 katika ukurasa wa 18 imeweka lengo la kuongeza mchango wa sekta ya utalii katika pato la Taifa kutoka 17% mwaka 2025 hadi 20% mwaka 2030. Moja ya mipango iliyojiwekea ni kuimirisha mikakati ya kutangaza na kuvutia watalii wa ndani na wa nje kwa kuanzisha kampeni maalum ya kufikisha idadi ya watalii 8,000,000 kwa mwaka ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati haioni ni namna gani bodi hii inaweza kuchangia kufikia malengo yaliyowekwa kwenye Ilani ya uchaguzi ya kufikia watalii 8,000,000 ifikapo mwaka 2030 ikiwa changamoto zilizoainishwa hazitapatiwa ufunguzi wa haraka na wa kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya maeneo muhimu katika kufanikisha shughuli za utalii ni miundombinu ikiwemo barabara, madaraja na uwanja wa ndege. Kamati ilibaini kuwa hali ya miundombinu hasa ya barabara na madaraja katika baadhi ya maeneo ya vivutio vyetu siyo ya kuridhisha na haikidhi mahitaji ya huduma za shughuli za utalii na kufanya baadhi ya vivutio kutofikika au kufikika kwa shida, hasa nyakati za mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa hali ya miundombinu katika Hifadhi ya Serengeti iliyoharibika kiasi cha kupunguza kasi ya utalii na kuleta taswira mbaya kipindi cha mvua, na hali hii imekuwa ikijirudia mara kwa mara. Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati mahsusi ya kuipatia changamoto hii, ufumbuzi wa kudumu ili kuboresha mazingira ya utalii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo ya maendeleo ya utalii, *(TDL)* ili kutimiza azma yake ya kukuza na kuendeleza sekta ya utalii nchini, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliridhia kurejeshwa kwa tozo ya maendeleo ya utalii nchini *TDL* ambayo ilikuwa imesitishwa. Bunge lako Tukufu lilifanya marekebisho kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2024 ili kuruhusu asilimia sita ya mapato ghafi ya taasisi za *TANAPA* na Ngorongoro kuwa chanzo cha tozo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake ambao unalenga kukuza sekta ya utalii nchini. Aidha, uamuzi wa kuidhinisha kiasi hicho cha fedha unaonyesha nia ya dhati ya Bunge lako Tukufu katika kuunga mkono juhudi za Serikali kwenye kuleta maendeleo ya sekta ya utalii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa tangu kuanza kwa utekelezaji wa tozo hii, kumekuwa na changamoto kwenye vipaumbele, mgawanyo, utekelezaji na usimamizi wa shughuli zinazotekelezwa kwa kutumia tozo hii. Kamati inaona mgawanyo wa matumizi ya fedha hizi hautokani na hali, mahitaji, mahitaji halisi ya sekta, wala mipango madhubuti ya kutangaza na kukuza utalii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya mipaka na utwaaji wa ardhi katika maeneo ya uhifadhi ni changamoto ya muda mrefu inayochochewa na ushindani wa matumizi ya ardhi kati ya shughuli za binadamu na malengo ya uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro mingi inatokana na kutokuwepo kwa alama za kudumu katika mipaka kati ya ardhi za vijiji na maeneo ya hifadhi, jambo linalopelekea kuingiliana kwa shughuli za kiuchumi na uhifadhi, hasa ukizingatia kuwa ongezeko la watu limesababisha ongezeko la uhitaji wa ardhi kwa ajili ya shughuli za kibinadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kumekuwa na mazoezi ya utwaaji wa ardhi kwa ajili ya shughuli za uhifadhi kwenye baadhi ya maeneo. Utwaaji huo umesababisha migogoro na malalamiko

ya wananchi kucheleweshewa malipo ya fidia na kutoridhika na viwango vya fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kazi kubwa iliyofanywa na Kamati ya Mawaziri Nane wa kisekta iliyozunguka maeneo mengi nchini kutatua migogoro ya ardhi. Kamati inashauri Serikali kuendelea kutatua migogoro ya mipaka kati ya maeneo ya hifadhi na maeneo ya vijiji ili kuendelea kulinda rasilimali za nchi yetu. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inalipa fidia stahiki na kwa wakati inapotwaa maeneo kwa ajili ya shughuli za uhifadhi kama Katiba na Sheria za Ardhi inavyoelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya uchambuzi kuhusu utekelezaji wa bajeti pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii, sasa ninaomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri katika maeneo mahsusi wa Wizara ya Maliasili na Utalii. Hali ya upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo. Kamati inashauri kuwa Serikali ihakikishe fedha za miradi iliyotengwa na kuidhinishwa na Bunge zinatolewa kwa wakati ili miradi iliyokusudiwa ikamilike kama ilivyopangwa, lakini pia kuepuka kuzalisha gharama za ziada. Kamati inashauri kuwa Serikali kupitia timu ya usimamizi na ukaguzi wa miradi ihakikishe thamani ya fedha katika miradi iliyotekelezwa inapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu, Kamati inashauri kuwa, Serikali ifanye utafiti wa kina wa sababu, athari na mbinu za kukabiliana na changamoto hii ili kupata suluhisho la kudumu. Serikali iandae na kuboresha mkakati mpya wa Kitaifa wa kushughulika na migongano kati ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu ili kupata suluhisho la kudumu la changamoto hiyo kwa kushirikiana na wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke mpango mahsusi wa kulipa kwa wakati kifutajasho na kifutamachozi kwa wananchi walioathiriwa na wanyamapori ili kuleta maana halisi ya

kifutajasho na kifutamachozi. Serikali iweke mkakati wa kuhakikisha kuwa maeneo yote yenye changamoto kubwa ya mwingiliano yanawekewa uzio wa umeme ili kuondokana na changamoto hiyo. Serikali ihakikishe inaendelea kuimarisha ulinzi katika hifadhi na mapori yetu ili kutokomeza ujangili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utalii wa malikale, Kamati inashauri kuwa Serikali iongeze na kuweka mikakati ya kuibua, kuanzisha na kutangaza utalii wa malikale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali ya miundombinu ya vivutio vya utalii. Kamati inashauri kuwa, Serikali ihakikishe inaandaa mpango madhubuti na mahsusi wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ili kupata ufumbuzi wa kudumu na kuwezesha maeneo ya vivutio vya utalii kufikika wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kuwa, Serikali iweke na iboreshe, mfumo utakaoiwezesha Bodi ya Utalii Tanzania *(TTB)* kufanya shughuli zote za utangazaji utalii bila kuingiliwa kama yalivyo madhumuni ya uanzishwaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kuwa,

(i) Serikali iweke/iboreshe mfumo utakaoiwezesha *TTB* kufanya shughuli zote za utangazaji utalii bila kuingiliwa kama yalivyo madhumuni ya uanzishwaji wake;

(ii) Serikali iongeze uwekezaji katika kutangaza utalii na fedha zinazotengwa zitolewe kwa wakati ili kufanikisha utangazaji wa kimkakati;

(iii) Serikali iifanyie *TTB* mageuzi makubwa ya kimuundo na kimajukumu ikiwa ni pamoja na kuipa wataalamu wenye ujuzi na ubobevu kwenye kutangaza utalii;

(iv) Serikali iweke mikakati ya kuiwezesha Bodi ya Utalii Tanzania kuwa huru, kujiendesha na kujitegemea kimapato ikiwa ni pamoja na kufanya uwekezaji na kuongeza vyanzo vya mapato;

(v) Serikali iongeze nguvu ya utangazaji wa utalii kwenye masoko ya kimkakati ili kuendelea kuongeza idadi ya watalii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tozo za maendeleo ya utalii; Kamati inaishauri Serikali kutafakari upya malengo, mgawanyo na usimamizi wa fedha hizi ili tija iliyokusudiwa iweze kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ya mipaka na utwaaji wa ardhi, Kamati inashauri kuwa:-

(i) Serikali iendelee kutatua migogoro ya mipaka nchini kati ya wananchi na hifadhi;

(ii) Serikali ihakikishe wananchi wanalipwa fidia stahiki na kwa wakati kama Katiba na sheria za ardhi zinavyoelekeza pale inapotoa ardhi kwa ajili ya shughuli za Uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika *(AFCON);* Kamati inashauri kuwa, Serikali ihakikishe inaweka mikakati ya kutumia vizuri fursa ya uwepo wa mashindano haya ili kutangaza vivutio vya utalii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; kwa niaba ya Kamati, ninapenda kutumia fursa kuwapongeza na kuwashukuru Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, wewe Mheshimiwa Mwenyekiti na pamoja na Wenyeviti wengine wa Bunge, kwa namna ambavyo mmekuwa mkitimiza majukumu yenu kwa weledi mkubwa na hivyo kuliwezesha Bunge letu Tukufu kutimiza wajibu wake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutumia fursa hii pia kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote cha ziara za ukaguzi wa miradi na uchambuzi wa bajeti ya wizara ya hii. Ninaomba majina yao yatambuliwe na kuingizwa kwenye Kumbukumbu Rasmi ya Bunge kama yanavyoonekana kwenye taarifa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, ninapenda kutumia fursa hii kuwashukuru Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji na Naibu Waziri Mheshimiwa Hamad Chande kwa ushirikiano wao mkubwa ambao umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi katika sekta hii. Aidha, ninawashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara Dkt. Hassan Abbas.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini si kwa umuhimu, kwa namna ya pekee ninawashukuru watumishi wa Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Leonard.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili taarifa hii pamoja na taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii, Fungu 69 kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kama ilivyowasilishwa hapo awali na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 MAELEZO YA JUMLA

### 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 121(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii **(Fungu 69)** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, pamoja na Maoni ya

Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** ili kurahisisha mtiririko wa maudhui pamoja na kuzingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge yanayohusu taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu kama ifuatavyo: -

(i) Sehemu ya kwanza ni utangulizi inayotoa Msingi wa Uchambuzi na Mawanda ya Uchambuzi;

(ii) Sehemu ya pili inayotoa uchambuzi na tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; pamoja na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2026/2027; na

(iii) Sehemu ya tatu inayofafanua Maoni na Ushauri wa Kamati unaotolewa kwa Serikali pamoja na kuhitimisha taarifa ya uchambuzi wa bajeti.

## 1.2 Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Kamati wa kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii ni Masharti ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ambapo Kanuni ya 6(8)(b) ikisomwa kwa pamoja na Kanuni ya 7(1)(a) zinatoa jukumu hilo kwa Kamati. Aidha, Kanuni ya 121(4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya wizara hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika,** ili kukidhi masharti hayo, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Katika hatua hiyo, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na kuja na matokeo kama yalivyoainishwa katika taarifa hii.

## 1.3 Mawanda ya Uchambuzi wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Kamati inahusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii **(Fungu 69)** kwa mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi uliofanyika uligusa maeneo yafuatayo: -

(i) Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(ii) Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027;

(iii) Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027; na

(iv) Mambo muhimu yanayogusa Sekta za Maliasili na Utalii.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa uchambuzi, Kamati iliongozwa na kigezo cha asilimia pamoja na kufanya tathmini ya jumla na ulinganisho wa mambo mbalimbali. Mambo hayo yaliwezesha Kamati kubaini hatua iliyofikiwa katika utekelezaji na mantiki ya mpango na makadirio kwa mwaka wa fedha unaokuja.

### SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI

## 2.1 MAELEZO YA JUMLA

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja ya Waziri wa Maliasili na Utalii. Uchambuzi ulijielekeza katika maeneo mawili ambayo ni Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa

Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

## 2.2 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120 (1) na ya Kanuni za Bunge, Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii baada ya ziara ya Ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha. Madhumuni ya sehemu hii ni kupata uelewa utakaolisaidia Bunge katika majadiliano yake kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hii. Aidha, sehemu hii inafafanua mambo manne yafuatayo: -

(i) Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri uliotolewa na Kamati wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(ii) Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa fedha na Bunge;

(iii) Hali ya ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali; na

(iv) Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi kutoka Hazina.

**Mheshimiwa Spika,** mambo hayo kwa pamoja yameweka msingi wa kuliwezesha Bunge lako Tukufu kupata uwiano utakaolisaidia katika kufanya uamuzi baada ya mjadala wa Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

### 2.2.1 Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** katika kulisaidia Bunge kutekeleza jukumu lake la kuishauri Serikali, tarehe 19 Mei, 2025, wakati wa uwasilishwaji wa Hotuba ya Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilitoa Maoni na Ushauri kuhusu mambo nane

(08). Ili kupima tija ya Bunge kuendelea kuishauri Serikali, Kamati ilitaka kubaini iwapo ushauri uliotolewa umezingatiwa.

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 26 Machi, 2026, Waziri wa Maliasili na Utalii alifika mbele ya Kamati kuwasilisha taarifa kuhusu hatua iliyofikiwa katika kuzingatia ushauri wa Kamati. Kamati ilichambua taarifa na kubaini kwamba, baadhi ya ushauri umezingatiwa na utekelezaji wake uko katika hatua mbalimbali. Kamati inaipongeza wizara kwa hatua hiyo na kuendelea kusisitiza kuzingatia maoni na ushauri unaotolewa na Kamati na Waheshimiwa Wabunge katika kuboresha utekelezaji wa majukumu ya wizara. Aidha, Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa maoni yafuatayo:-

(i) Pamoja na Serikali kuanza kutumia Mfumo wa kielektroniki (PAIS) katika ulipaji wa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi walioathirika na Wanyamapori wakali na waharibifu, bado Kamati inaona kasi ya ulipaji ni ndogo kulingana na mahitaji. Vilevile, kasi ndogo katika kuchukua hatua stahiki za muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu katika kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazosababishwa na muingiliano baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu kwa lengo la kunusuru maisha ya watu, wanyamapori na kuzuia uharibifu wa mali unaotokana na migongano hiyo;

(ii) Pamoja na maelezo ya wizara kuhusu matumizi ya fedha za TDL, Kamati inaona bado malengo, mgawanyo, usimamizi na matumizi ya fedha hizo hauoneshi mwelekeo wa kuleta tija iliyokusudiwa kwa kuzingatia sababu au malengo hasa ya kurejeshwa kwa fedha hizi;

(iii) Serikali kushindwa kuchukua hatua za haraka kurudisha hoteli na loji toka kwa wamiliki waliobinafsishiwa hoteli na loji za Serikali ambao wamekiuka masharti ya mikataba ya kuziboresha na kuziendeleza; na

(iv) Serikali kushindwa kuiwezesha TTB kutekeleza majukumu yake kikamilifu kama chombo kilichopewa majukumu ya kutangaza na kuvutia utalii ndani na nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** uzingatiaji usioridhisha wa Maoni na Ushauri wa Kamati katika kutimiza majukumu ya wizara, unaweza kupunguza ufanisi na kupelekea kuzorotesha ustawi wa wananchi kinyume na lengo la Serikali katika Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### 2.2.2 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha

#### 2.2.2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya ziara katika mikoa mitatu **(3)** ya Manyara, Arusha na Kilimanjaro ili kukagua baadhi ya miradi inayotekelezwa na Wizara ya Maliasili na Utalii. Kamati ilikagua jumla ya miradi minne (04) ambayo ni: -

**(a) Mradi Na. 4314: Mradi wa Ujenzi wa Lango la Kuingilia katika Hifadhi ya Taifa Tarangire Eneo la Mamire**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ulitekelezwa kwa thamani ya **Shilingi 3,921,704,476.60** ikiwa ni fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Mradi ulipangwa kutekelezwa kwa kipindi cha miezi 28 kuanzia tarehe 10 Machi, 2023 hadi tarehe 30 Juni, 2025. Hata hivyo, wakati Kamati ilipotembelea mradi ilibaini kuwa, muda wa kukamilisha mradi umeongezeka hadi tarehe 14 Aprili, 2026.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 13 Machi, 2026, ambapo Kamati ilitembelea na kufanya ukaguzi wake, mradi ulikuwa umepokea **Shilingi 2,833,048,952.15** sawa na **asilimia 71.8** ya fedha zote za mradi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa, kutokana na changamoto ya upatikanaji wa fedha, mradi huu umeongezwa muda wa utekelezaji wake (*extension*) mara 10. Ongezeko la muda wa utekelezaji linaweza kuambatana na ongezeko la

gharama kutokana na kupanda kwa gharama za mradi lakini pia kuchelewesha manufaa yaliyokusudiwa.

**(b) Mradi Na. 4814: Mradi wa Ujenzi wa Makumbusho ya Jiopaki (Geopark), Ngorongoro**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ulitengewa **Shilingi Bilioni 32** kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya utalii na ujenzi wa makumbusho ya kisasa ya Jiopaki. Utekelezaji wa Mradi ulianza mwezi Juni, 2022 na ulitakiwa kutekelezwa ndani ya miezi 35 kuanzia Juni, 2022 hadi Mei, 2025.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ziara na kukagua mradi huo tarehe 13 Machi, 2026 na ilikuta mradi ukiwa umekamilika kwa **asilimia 100**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kukamilisha mradi huu wa makumbusho ya kisasa ambao kukamilika kwake kunatoa taswira halisi ya eneo la Hifadhi ya Ngorongoro pamoja na kuongeza uelewa kwa jamii juu ya thamani ya urithi wa jiolojia kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuboresha mazingira ya eneo hili kwa kuweka vivutio vya aina mbalimbali kama vile maonesho ya tamaduni za makabila mbalimbali, maduka ya asili na maeneo ya huduma, hali itakayofanya watalii wavutiwe kukaa muda mrefu katika eneo hilo. Vilevile, Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati ya kutangaza makumbusho hii ili kuongeza watalii.

**(c) Mradi Na. 4812: Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Mafunzo katika Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka (CAWM)**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu umetokana na ongezeko la wanafunzi mwaka hadi mwaka katika chuo hiki uliopelekea chuo kutenga **Shilingi3,799,982,716.9** kutoka vyanzo vya ndani kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la mafunzo. Utekelezaji wa mradi huu ulianza tarehe 01Juni, 2022 hadi tarehe 31Mei, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 14 Machi, 2026 ambapo Kamati ilifanya ukaguzi wake, mradi ulikuwa umekamilika kwa **asilimia 100** na jengo limeanza kutumika rasmi mwaka wa masomo 2025/2026. Kukamilika kwa mradi huu kunatarajia kukiwezesha chuo kutoa mafunzo katika mazingira bora na yenye tija.

**(d) Mradi Na. 4313: Mradi wa Faru Weusi katika Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi, Same**

**Mheshimiwa Spika,** mradi wa Faru Weusi katika Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi Mkoani Kilimanjaro, umegawanyika kwenye miradi miwili ya kuzalisha Faru Weusi na Mbwambitu pamoja na Mradi wa Utalii wa Faru Weusi. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, mradi ulitarajia kupanua uzio kwa kilomita za mraba 10 kwa lengo la kukabiliana na ongezeko la faru. Hata hivyo, Kamati ilifahamishwa kuwa mradi huo haukutekelezwa kutokana na kupungua kwa fedha za miradi za TANAPA kutoka **Shilingi Bilioni 144** hadi **Shilingi Bilioni 70.** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inatoa fedha za miradi kama zilivyoidhinishwa na Bunge ili kutekeleza miradi iliyokusudiwa na kwa wakati. Vilevile, Serikali iweke mpango wa kutumia teknolojia ili kurahisisha upatikanaji wa faru (*tracking*) wakati wa utalii. Aidha, kwa kuzingatia ukubwa na ugumu wa kazi inayofanywa na wahifadhi wetu katika maeneo yote nchini, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaboresha maisha na maslahi yao kama sehemu ya motisha.

### 2.2.2.2 Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi

**Mheshimwa Spika,** Katika ziara za ukaguzi wa miradi inayotekelezwa na Wizara ya Maliasili na Utalii, Kamati ilipokea taarifa za utekelezaji wa miradi na kuona hali halisi kwenye maeneo ya utekelezaji wa miradi husika. Lengo likiwa ni kulinganisha na kubaini iwapo taarifa zilizowasilishwa na wizara zinawiana na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji pamoja na madhumuni ya miradi inayohusika. Tathmini ya kina, imebainisha yafuatayo: -

(i) Kumekuwa na ucheleweshaji katika utekelezaji wa miradi mingi ya wizara hali inayoweza kupelekea

kuongezeka kwa gharama na kupunguza tija inayotokana na miradi husika;

(ii) Hali ya upatikanaji wa fedha za miradi kutoka hazina sio ya kuridhisha na Serikali inaweza kupata hasara ya kudaiwa riba na wakandarasi wanaotekeleza miradi hiyo. Mathalani katika utekelezaji wa Mradi Na. 4313 - Mradi wa Faru Weusi katika Hifadhi ya Mkomazi, kulikuwa na mpango wa kupanua uzio kwa kilomita za mraba 10 ambao haukufanyika kutokana na kutopatikana kwa fedha. Mradi Na. 4313 wa ujenzi wa Lango la Mamire pamoja na miundombinu yake katika Hifadhi ya Tarangire, umechukua muda mrefu kukamilika kutokana na upatikanaji hafifu wa fedha za utekelezaji; na

(iii) Uwiano wa thamani ya fedha na miradi; Katika eneo hili, Kamati ilibaini uwepo wa uwiano wa thamani ya fedha na miradi kwa baadhi ya miradi lakini kwa upande mwingine uwiano wa thamani ya fedha na miradi ulikosekana. Kamati inaipongeza timu ya usimamizi ya Mradi Na. 4814: Ujenzi wa Makumbusho ya Jeopaki ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ambapo utekelezaji wake na thamani ya fedha vinaonekana wazi ukilinganisha na miradi mingine ambayo Kamati ilikagua. Kwa mfano, Mradi Na. 4313 - Ujenzi wa Lango la Mamire na miundombinu yake katika Hifadhi ya Tarangire, ulikosa uwiano wa thamani ya fedha na mradi. Kamati ilipotembelea mradi huu, ilifahamishwa kuwa utekelezaji wake umefikia **asilimia 98.** Kamati haikuridhishwa na hali ya Mradi kwani ulionekana dhahiri una upungufu; kwa mfano, choo chenye matundu saba (7) kilichojengwa kwa **shilingi milioni 107**; Kamati inaona hakina thamani hiyo na lango lenyewe haliakisi thamani halisi. Mradi huu pamoja na kuwa ulitumia fedha nyingi, lakini pia uliongezewa muda wa utekelezaji wake. Jambo hili linaweza kuambatana na ongezeko la gharama za ziada kutokana na kupanda kwa gharama za mradi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mambo hayo mahsusi yaliyobainika, Kamati pia ilibaini kuwa hali ya miundombinu ya barabara katika Hifadhi za Taifa sio ya kuridhisha, hali inayosababisha vivutio vingi kushindwa kufikika hasa nyakati za mvua. Mfano halisi ni Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ambayo miundombinu yake kwa kiasi kikubwa iliharibiwa na mvua kiasi cha Kamati kushindwa kwenda kukagua Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Gofu katika eneo la Fort IKoma; na barabara kutoka Babati kuelekea Lango la Mamire na sehemu ya kutoka Lango la Mamire kuingia Hifadhini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuandaa mpango mkakati wa kuhakikisha maeneo yote korofi katika miundombinu ya hifadhi yanapatiwa ufumbuzi wa kudumu ili yapitike nyakati zote. Sekta hii ya Utalii ambayo inachangia asilimia 17 ya pato la Taifa inapaswa kupewa kipaumbele katika kuhakikisha inapata mahitaji muhimu ya kuiwezesha kuendelea kuongeza tija.

### 2.2.3 Hatua iliyofikiwa katika Ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, Lengo la uchambuzi wa taarifa za makusanyo ya maduhuli ni kuliwezesha Bunge kubaini iwapo lengo la makusanyo lililoidhinishwa na Bunge limefikiwa, lakini pia kutumia uzoefu unaopatikana kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na kubaini uhalisia unavyostahili kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ilipangiwa kukusanya **Shilingi 1,185,584,115,330.55**. Hadi kufikia Februari, 2026, Wizara ilikuwa imekusanya **Shilingi 895,818,665,714.85** sawa na **asilimia 75** ya lengo la makusanyo lililokusudiwa. Kiwango hicho kinaashiria mwenendo mzuri wa ukusanyaji wa maduhuli.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati katika eneo la ukusanyaji wa maduhuli ulionesha kuwa ukusanyaji wa kutumia MNRT portal, umefikia **asilimia 65** ya lengo, huku ukusanyaji wa kutumia TRA umefikia **asilimia 79** ya lengo. Kupitia takwimu hizi, Kamati imewianisha muda wa utekelezaji wa bajeti na hatua

iliyofikiwa katika ukusanyaji wa maduhuli na kubaini kuwa mwenendo huu wa makusanyo unaonesha kuwa lengo linaweza kufikiwa ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha. Taswira kamili ya hali ya ukusanyaji inaonekana katika **Kielelezo Na. 1.**

**Kielelezo Na. 1: Ukusanyaji wa Maduhuli hadi Februari, 2026**

| Fungu 69 | % ya Makadirio | Makadirio (A) | Makusanyo (B) | Ufanisi (lengo vs makusa |
|---|---|---|---|---|
| *MNRT Portal* | 27.45 | 325,478,017,370.65 | 216,203,800,995.54 | 66.42 |
| TRA (TANAPA& NCAA) | 72.55 | 860,106,097,959.74 | 679,614,864,719.31 | 79.00 |
| **JUMLA** | **100** | **1,185,584,115,330.55** | **895,818,665,714.85** | **75.56** |

***Chanzo**: Randama ya Wizara ya mwaka 2026 na usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** kwa mchanganuo huo ni dhahiri kuwa, Makusanyo ya Taasisi za TANAPA na NCAA ndio yaliyofanikisha kwa kiasi kikubwa makusanyo kufikia **asilimia 75.56**. Kamati inaipongeza wizara kwa hatua ya makusanyo iliyofikiwa. Vilevile, Kamati inaishauri wizara kuongeza mikakati ya usimamizi katika kukusanya mapato kwa Taasisi zinazotumia mfumo wa MNRT Portal ili kuongeza tija katika ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

### 2.2.4 Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Bajeti unategemea upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, wizara iliidhinishiwa kutumia **Shilingi 336,518,895,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 254,232,349,000** sawa na **asilimia 75.5** zilikuwa fedha za Mtumizi ya Kawaida na **Shilingi 82,286,546,000** sawa na **asilimia 24.45** zilikuwa fedha za Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Februari, 2026, wizara ilikuwa imepokea **Shilingi 206,903,257,247.13** sawa na **asilimia 62** tu ya fedha iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **shilingi 163,517,161,157.05** sawa na **asilimia 64.32** zilikuwa za matumizi ya kawaida na **Shilingi**

**43,386,096,090.08** sawa na **asilimia 53** zilikuwa fedha za kugharamia Miradi ya Maendeleo. Taswira ya Upatikanaji wa Fedha inaonekana katika Kielelezo Na. 2.

**Kielelezo Na. 2 Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026**

| Matumizi | | Kilichoidhinishwa | Kilichopokelewa | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Kawaida | **OC** | 123,523,295,000 | 79,714,304,562.27 | 63.82 |
| | **Mishahara** | 130,709,054,000 | 83,775,856,594.78 | 51 |
| | **Jumla (A)** | **254,232,349,000** | **163,490,161,157** | **64** |
| | | | | |
| Maendeleo | **Ndani** | 32,476,051,000 | 8,521,937,479.36 | 26 |
| | **Nje** | 49,810,495,000 | 34,864,158,610.72 | 70 |
| | **Jumla (B)** | **82,286,546,000** | **43,386,096,090** | **53** |
| **JUMLA KUU (A+B)** | | **336,518,895,000** | **206,903,257,247.13** | **61.5** |

***Chanzo:*** *Randama ya Wizara 2026 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** ili kubaini kiwango cha utekelezaji wa bajeti, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kuzingatia mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka hazina ambapo unaonyesha kwamba hadi kufikia mwezi Februari, 2026: -

(i) Upatikanaji halisi ulitakiwa kuwa usiopungua **asilimia 66.67** ya Bajeti yote iliyoidhinishwa ili kuendana na muda wa utekelezaji wa bajeti, lakini wizara ilikuwa imepokea **asilimia 61.5** tu. Hali hii inaweza kuchangia kushuka kwa ufanisi katika kutekeleza majukumu ya wizara; na

(ii) Katika **asilimia 53** ya bajeti iliyopokelewa kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, fedha za ndani ni **asilimia 26** tu, huku fedha za nje zikiwa ni **asilimia 70** ya bajeti iliyoidhinishwa. Mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha za ndani za maendeleo sio wa kuridhisha. Hali hii inaweza kupelekea miradi mbalimbali ya maendeleo na wakandarasi kushindwa kuendelea na kazi.

**Mheshimiwa Spika,** hali isiyoridhisha ya upokeaji wa fedha kutoka hazina kwenye utekelezaji wa shughuli za wizara, ni moja ya kikwazo kikubwa katika kuhakikisha wizara na Taasisi zake zinaendelea kukuza Sekta ya Utalii.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inatoa fedha kama zilivyoidhinishwa na Bunge kwa kuwa ukamilishaji wa Miradi ya Maendeleo unaweza kuleta tija kama Serikali itazingatia utoaji wa fedha za kutosha na kwa wakati kama ilivyotarajiwa.

## 2.3 Uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua na kujadili Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo: -

(i) Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027;

(ii) Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2026;

(iii) Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa; na

(iv) Mambo muhimu yanayogusa Sekta ya Maliasili na Utalii.

### 2.3.1 Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua uhusiano uliopo kati ya Mapato na Matumizi, Kamati ilipokea ufafanuzi kuhusu lengo la maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ambapo Wizara ya Maliasili na Utalii **(Fungu 69)** inakadiriwa kukusanya maduhuli ya **Shilingi 1,468,724,740,725.84.** Aidha, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kuzingatia uzoefu uliopatikana katika ukusanyaji wa maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**.** Taswira ya ulinganisho wa

makusanyo ya maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na 2026/2027 inaonekana katika **Kielelezo Na. 3.**

**Kielelezo Na. 3 Ulinganisho wa Makadirio Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha/2026 na 2026/2027**

| Fungu 69 | 2025/2026 | 2026/2027 | % ongezeko |
|---|---|---|---|
| Maduhuli yanayokwenda Mfuko Mkuu wa Serikali | 113,536,198,276.65 | 139,927,689,307.10 | 23.26 |
| Maduhuli yanayokusanywa na kutumika na taasisi | 1,070,047,917,053.90 | 1,328,797,051,418.74 | 24.18 |
| **JUMLA** | **1,183,584,115,330.55** | **1,468,724,740,725.84** | **24** |

***Chanzo***: *Randama ya Wizara 2026 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umebaini yafuatayo: -

(i) Makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli yameongezeka kwa **Shilingi 214,742,096,850.55** sawa na **asilimia 24** ikilinganishwa na makadirio ya Mwaka wa Fedha 2025/2026. Aidha, kwa mtiririko wa makusanyo kwa mwaka unaoisha, unaonesha kuwa lengo la ukusanyaji wa maduhuli linaweza kufikiwa;

(ii) Makadirio ya Makusanyo ya maduhuli yanayokwenda Mfuko Mkuu wa Serikali yameongezeka kwa **asilimia 23.26** ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2025/2026. Hata hivyo, ili kufikia lengo hili, wizara iimarishe usimamizi wa mikataba ya uwekezaji katika maeneo yanayosimamiwa na TAWA pamoja na usimamizi wa shughuli za kitalii ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa maduhuli;

(iii) Makusanyo ya maduhuli yanayokusanywa na kutumika na taasisi yameongezeka kwa **asilimia 24.18**

ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2025/2026. Ongezeko hilo limetokana na uamuzi wa Serikali kuruhusu baadhi ya taasisi kubaki na makusanyo yake ili kuongeza ufanisi katika kujiendesha; na

(iv) Katika lengo la Makusanyo ya wizara, **asilimia 90.47** ya makusanyo, yatakusanywa na kutumika na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, huku **asilimia 9.53** ya makadirio yatakusanywa na kupelekwa Mfuko Mkuu wa Serikali. Hali hii inaonesha dhamira ya dhati ya Serikali ya kuhakikisha Wizara na Taasisi zake hazikwami katika kutekeleza majukumu yake.

### 2.3.2 Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza mpango na vipaumbele vilivyowekwa katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara ya Maliasili na Utalii **(Fungu 69)** inakadiria kutumia **Shilingi 334,345,870,000** kulinganisha na Makadirio ya Matumizi ya **Shilingi 336,518,895,000** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026. Aidha, masharti ya Kanuni ya 120(2) ya Kanuni za Bunge yamelenga kuliwezesha Bunge kutumia uzoefu wa utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha unaoisha ili kuchambua makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata. Kwa kuzingatia lengo hilo, Kamati imechambua Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kwa kulinganisha makadirio hayo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Taswira ya ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na 2026/2027 inaonekana katika **Kielelezo Na. 4.**

**Kielelezo Na. 4 Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na 2026/2027**

| Mwaka | Matumizi ya Kawaida | | Maendeleo | |
|---|---|---|---|---|
| | PE | OC | Ndani | Nje |
| 2025/26 | 130,709,054,000 | 123,523,295,000 | 32,476,051,000 | 49,810,495,000 |
| 2026/27 | 144,691,490,000 | 127,352,935,000 | 23,134,770,000 | 39,166,675,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Pungufu/ ongezeko | 13,982,436,000 | 3,829,640,000 | (9,341,281,000) | (10,643,820,000) |
| Asilimia % | 10.7 | 3.14 | -28.82 | -21.38 |

***Chanzo**: Randama ya Wizara 2026 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umeonesha kuwa:-

(i) Fedha za mishahara zimeongezeka kwa **Shilingi 13,982,436,000** sawa na **asilimia 10.7** ilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(ii) Fedha za Matumizi Mengineyo yaani (OC) zimeongezeka kwa **Shilingi 3,829,640,000** sawa na **asilimia 3.14** ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2024/2025; na

(iii) Fedha za Miradi ya Maendeleo zimepungua kwa **Shilingi 19,985,101,000** sawa na **asilimia 24** ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2025/2026. Aidha, fedha za ndani kwa Miradi ya Maendeleo zimepungua kwa **asilimia 28.82** huku fedha za nje zikipungua kwa **asilimia 21.38**.

**Mheshimiwa Spika**, upungufu wa **asilimia 24** wa fedha za Miradi ya Maendeleo unaweza kusababisha utekelezaji wa miradi kupunguza ufanisi na hivyo kupoteza tija iliyokusudiwa.

### 2.3.3 Uchambuzi wa Mambo Mahsusi katika Sekta ya Maliasili na Utalii

#### (i) Changamoto ya Wanyamapori wakali na Waharibifu

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yanayopatikana katika Sekta ya Maliasili na Utalii, migongano baina ya binadamu na wanyamapori ni moja ya **changamoto kubwa** inayoikabili sekta hii kwa sasa. Katika halmashauri 184 nchini halmashauri 91 sawa na **asilimia 49.5** zinakabiliwa na changamoto hiyo. Wanyama wanaoleta changamoto hii kwa sehemu kubwa ni

pamoja na tembo, mamba, viboko, nyumbu, ngedere na nyani huku taarifa zikionyesha kwamba asilimia 80 ya migongano hiyo inasababishwa na mnyama tembo. Madhara yanayotokana na changamoto hiyo ni pamoja na vifo, ulemavu wa muda na wakudumu unaosababishwa na wananchi kujeruhiwa, uharibifu wa mali za wananchi kama vile mazao, miundombinu ya makazi, maji na barabara.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifahamishwa kuwa sababu za migongano baina ya binadamu na wanyamapori ni kukosekana au kutozingatiwa kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi, mabadiliko ya tabia ya nchi na ongezeko la mimea vamizi katika maeneo yaliyohifadhiwa, na kamati ilifahamishwa jitihada za Serikali za kupambana na changamoto hii ambazo ni kuongeza doria za udhibiti wa wanyamapori, ununuzi wa pikipiki za doria, ujenzi wa vizimba, uchimbaji wa visima na mabwawa katika maeneo ya hifadhi, ujenzi wa vituo vya askari, ufungaji wa visukuma mawimbi kwa wanyamapori ambao ni viongozi wa makundi ya wanyama, uvunaji wa Wanyama mbalimbali ikiwemo tembo 100, kiboko 197, fisi 171 na mamba 153. Kielelezo kifuatacho kinaonesha utekelezaji wa mipango na jitihada za Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

**Kielelezo Na. 6: Utekelezaji wa Shughuli za kukabiliana na migongano baina ya Wanyamapori na Binadamu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 hadi kufikia Februari, 2026**

| **SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA HADI FEBRUARI, 2026** | | | |
|---|---|---|---|
| **SHUGHULI** | **MPANGO** | **UTEKELEZAJI** | **ASILIMIA YA UTEKELEZAJI** |
| **Ununuzi wa helikopta** | 02 | 0 | 0 |
| **Uchimbaji wa mabwawa** | 12 | 05 | 42 |
| **Ujenzi wa vizimba** | 50 | 45 | 90 |
| **Uchimbaji wa visima** | 18 | 10 | 56 |
| **Ujenzi wa uzio wa umeme** | Km. 53 | 0 | 0 |
| **Ujenzi wa vituo vya askari** | 19 | 20 | 105.3 |
| **Kuwajengea uwezo askari wa wanyamapori wa vijiji** | 100 | 410 | 410 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Ununuzi wa pikipiki** | 22 | 33 | 150 |
| **Ununuzi wa ndege nyuki (drones)** | 12 | 0 | 0 |
| **Ununuzi wa mikanda maalum ya mawasiliano (Visukuma mawimbi)** | 50 | 52 | 104 |
| **Ununuzi wa mabomu baridi** | 40,000 | 0 | 0 |

**Chanzo:** *Randama ya Wizara ya Maliasili na Utali na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na jitihada hizi za Serikali, kamati imebaini kwamba bado changamoto hii ni kubwa sana na athari, madhara na malalamiko yake ni Dhahiri. Hali hii inawaumiza wananchi, kuwakatisha tamaa na kuwachonganisha na Serikali yao.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kupunguza maumivu ya changamoto hii kwa wananchi, Serikali iliweka utaratibu wa kutoa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi wanaokumbwa na changamoto hii. Hata hivyo, Kamati inaona bado kasi ya kutenga na kulipa fedha za kifuta jasho na kifuta machozi hairidhishi na hivyo wananchi wengi waliohakikiwa madai yao kutolipwa kwa wakati. Mathalani, hadi tarehe 21 Januari 2026 wizara ilikuwa imepokea madai kutoka kwa wananchi 62,446 yenye jumla ya **Shilingi Bilioni 18.67** kutoka katika Halmashauri 56 nchini, na hadi kufikia tarehe 20 Machi, 2026 wizara ilikuwa imelipa madai ya wananchi 15,153 tu yenye thamani ya **shilingi bilioni 7.2.** Bado wananchi 47,293 hawajalipwa madai ya **shilingi bilioni 11.47** na baadhi ya madai yamekuwepo kwa zaidi ya miaka miwili. Ucheleweshaji huu wa malipo unapoteza maana halisi ya kifuta jasho na kifuta machozi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inatenga na kutoa fedha ili kulipa madai kwa wakati; ifanye utafiti wa kina juu ya changamoto hii, na iendelee kuchukua hatua mbalimblai za utatuzi kama vile kujenga uzio wa umeme; kuchimba mabwawa kwenye maeneo ya hifadhi ili kupunguza tatizo la Wanyama kuhamahama kwenda kutafuta maji, kuongeza askari, vitendea kazi na kutoa elimu kwa wananchi.

(ii) **Hali ya Ujangili Nchini**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua juhudi za Serikali za kupunguza/kupambana changamoto ya ujangili nchini ambapo katika miaka ya hivi karibuni imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kutumia teknolojia ya mbwa maalum waliofunzwa kunusa nyara katika viwanja vya ndege na mipakani, matumizi ya teknolojia ya kisasa, kuboresha mafunzo, vitendea kazi kwa askari na kuongeza doria. Kupitia jitihada hizo, tumeshuhudia kuongezeka kwa idadi ya wanyamapori adimu kama vile faru. Hata hivyo, bado kuna changamoto ya biashara haramu ya nyara na uwindaji wa wanyamapori katika baadhi ya maeneo.

Kamati ilifahamishwa kuwa kupitia doria mbalimbali zaidi ya nyara 180 zilikamatwa, watuhumiwa wa ujangili 6,431 walikamatwa pamoja na silaha za aina mbalimbali 145 zilizotumika kufanyia ujangili.

**Mheshimiwa Spika**, Hali hii isipodhibitiwa inaweza kurudisha nyuma juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita za kukomesha kabisa ujangili na kuinua utalii. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha hali hii inadhibitiwa kabisa ili kuendelea kulinda rasilimali zetu kwa kuweka sheria kali; kuzisimamia; na kuwawezesha askari kwa kuwapa motisha zaidi ili waendelee kufanya kazi kwa bidii. Utalii wa Malikale

**Mheshimiwa Spika,** utalii wa malikale nchini, unahusisha kutembelea maeneo ya kihistoria kama vile michoro ya mambo ya kale, magofu, mapango, mifupa ya Wanyama wa kale na makumbusho ili kujifunza utamaduni na historia. Tanzania imebarikiwa kuwa na maeneo mengi ya malikale ambayo Kamati inaona hayajawekewa mikakati ya kutosha ya kutangazwa ili kuvutia, kuongeza watalii wa ndani na nje pamoja na kukuza mapato yatokanayo na utalii.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, Kamati inaona kuna fursa ya kukuza utalii na kuongeza mapato ya Serikali kwa kuyapa kipaumbele maeneo ya kihistoria ambayo bado hayajatumika kikamilifu.

(iii) **Bodi ya Utalii Tanzania (*Tanzania Tourist Board-TTB*)**

**Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Utalii Tanzania ni Taasisi ya Umma iliyoanzishwa kwa Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania Sura Na. 364 R.E 2002 ikitakiwa kuchukua majukumu ya lililokuwa Shirika la Utalii Tanzania (*Tanzania Tourist Corporation - TTC*). Sheria hiyo imeainisha majukumu ya TTB ambayo kimsingi ni kutangaza na kuendeleza aina zote za utalii nchini. Kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania kinatamka wazi kuwa, moja ya kazi za Bodi ni: "*kuchukua hatua zote zinazostahili kutangaza na kuitangaza Tanzania kama kivutio maarufu cha utalii*" (*to adopt alls uch measures as it may consider necessary to advertise and publicise Tanzania as a popular tourist destination*).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa taarifa mbalimbali zilizowasilishwa na Serikali kwa lengo la kupima ufanisi katika utendaji wa Bodi ya Utalii Tanzania. Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa, pamoja na hatua za Serikali kuendelea na mchakato wa kufanya mapitio ya Sheria ya Uanzishaji wa Bodi hii ili kuihuisha iendane na mahitaji ya sasa, bado Bodi inakabiliwa na changamoto kubwa ya ufinyu wa bajeti katika kutekeleza majukumu yake. Vilevile, kuna muingiliano wa majukumu baina yake, Wizara na Taasisi nyingine ndani ya Wizara. Vilevile inakabiliwa na upungufu wa wataalam wa kutosha wenye uzoefu, ujuzi na ubobevu katika kutangaza utalii.

**Mheshimiwa Spika,** Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2025/2030 katika ukurasa wa 18 imeweka lengo la kuongeza mchango wa Sekta ya Utalii katika Pato la Taifa kutoka **asilimia 17** mwaka 2025 hadi **asilimia 20** mwaka 2030. Na moja ya mipango iliyojiwekea ni kuimarisha mikakati ya kutangaza na kuvutia watalii wa ndani na nje ya nchi kwa kuanzisha kampeni maalumu ya kufikisha idadi ya watalii milioni nane (8,000,000) kwa mwaka ifikapo mwaka 2030.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haioni ni namna gani Bodi hii inaweza kuchangia kufikia malengo yaliyowekwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya kufikia watalii milioni 8ifikapo 2030 ikiwa changamoto zilizoainishwa hazitapatiwa ufumbuzi wa haraka na wa kudumu. Kamati inaishauri Serikali kuweka mfumo utakaoiwezesha TTB

kufanya shughuli zote za utangazaji utalii. Aidha, TTB iwezeshwe kufikia malengo yake ya kujitegemea ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kupunguza utegemezi wa fedha kutoka Serikalini.

### (iv) Hali ya Miundombinu katika vivutio vya Utalii Nchini

**Mheshimiwa Spika**, Moja ya maeneo muhimu katika kufanikisha shughuli za utalii ni miundombinu ikiwemo barabara, madaraja na viwanja vya ndege. Kamati ilibaini kuwa hali ya miundombinu haswa barabara na madaraja katika baadhi ya maeneo ya vivutio vyetu sio ya kuridhisha na haikidhi mahitaji ya huduma na shughuli za Utalii na kufanya baadhi ya vivutio kutofikika au kufikika kwa shida hasa nyakati za mvua. Mfano, miundombinu katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti iliharibika kiasi cha kupunguza kasi ya utalii na kuleta taswira mbaya kipindi cha mvua na hali hii imekuwa ikijirudia mara kwa mara. Kamati inaishauri Serikali kuweka mkakati mahsusi wa kuipatia changamoto hii ufumbuzi wa kudumu ili kuboresha mazingira ya utalii nchini.

### (v) Tozo ya Maendeleo ya Utalii (TDL)

**Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza sekta ya utalii nchini Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilianzisha Tozo ya Maendeleo ya Utalii (*Tourism Development Levy - TDL*) mwaka 2013 kupitia Sheria ya Utalii, Sheria Na. 29 ya mwaka 2008 Kifungu cha 59(1) na 59(2) ambapo pia vyanzo vya mapato ya mfuko/tozo hiyo viliainishwa kuwa ni asilimia 3 ya mapato ghafi kutoka taasisi za Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA). Kutokana na mabadiliko ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2020 yaliyosababisha mapato ya taasisi hizo za TANAPA na NCAA kukusanywa moja kwa moja na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), TDL ilisitishiwa kupokea fedha.

**Mheshimiwa Spika,** ili kutimiza azma yake ya kukuza na kuendeleza Sekta ya Utalii Nchini, Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliridhia kurejeshwa kwa Tozo ya Maendeleo ya Utalii nchini (TDL), ambayo

ilikuwa imesitishwa. Bunge lako Tukufu lilifanya marekebisho kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2024 ili kuruhusu **asilimia 6** ya mapato ghafi ya taasisi za TANAPA na NCAA kuwa chanzo cha tozo hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa uamuzi wake ambao unalenga kukuza sekta ya utalii nchini. Aidha, uamuzi wa kuidhinisha kiasi hicho cha fedha unaonesha nia ya dhati ya Bunge lako Tukufu katika kuunga mkono juhudi za Serikali kwenye kuleta maendeleo ya Sekta ya Utalii nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa tangu kuanza kwa utekelezaji wa tozo hii, kumekuwa na changamoto kwenye vipaumbele, mgawanyo, utekelezaji na usimamizi wa shughuli zinazotekelezwa kwa tozo/fedha hizi. Kamati inaona mgawanyo na matumizi ya fedha hizi hautokani na hali, mahitaji halisi ya sekta wala mipango madhubuti ya kutangaza na kukuza utalii. Badala yake unagawanywa na kutumiwa kama fedha za dharura zilizokusanywa bila kuwepo kwa mahitaji.

Kamati inaishuri Serikali kutafakari upya malengo, mgawanyo na usimamizi wa fedha hizi ili tija iliyokusudiwa ipatikane.

(vi) **Migogoro ya Mipaka na Utwaaji Ardhi**

**Mheshimiwa Spika,** Migogoro ya mipaka na utwaaji wa ardhi katika maeneo ya uhifadhi nchini ni changamoto ya muda mrefu inayochochewa na ushindani wa matumizi ya ardhi kati ya shughuli za binadamu (kama kilimo na ufugaji) na malengo ya uhifadhi.

**Mheshimiwa Spika**, Migogoro mingi inatokana na kutokuwepo kwa alama za kudumu (vigingi) kati ya ardhi ya kijiji na maeneo ya hifadhi, jambo linalopelekea kuingiliana kwa shughuli za kiuchumi na uhifadhi haswa ikizingatiwa kuwa ongezeko la watu limesababisha ongezeko la uhitaji wa ardhi kwa ajili ya shughuli za kibinadamu. Pia kumekuwa na mazoezi ya utwaaji wa ardhi ya wananchi kwa ajili ya shughuli za uhifadhi kwenye baadhi ya maeneo. Utwaaji huo umesababisha

migogoro na malalamiko ya wananchi kucheleweshewa malipo ya fidia na/au kutoridhika na viwango vya fidia.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kazi kubwa iliyofanywa na Kamati ya Mawaziri nane wa Kisekta iliyozunguka maeneo mengi nchini kutatua migogoro ya ardhi**.** Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutatua migogoro ya mipaka kati ya maeneo yaliyohifadhiwa na wananchi ili kulinda amani, utulivu na uhifadhi wa rasilimali zetu. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inalipa fidia stahiki na kwa wakati inapotwaa maeneo kwa ajili ya uhifadhi kama Katiba na Sheria za Ardhi zinavyoelekeza.

(vii) **Mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2027)**

**Mheshimiwa Spika**, Uwepo wa Mashindano ya mpira wa miguu ya Kombe la Mataifa ya Afrika mwaka 2027 (AFCON 2027) ambayo Tanzania ni moja ya nchi wenyeji ni fursa ya kihistoria kwa Sekta za Uchumi na Utalii. Mashindano haya yanaweza kuwa kichocheo kikubwa kwa Sekta ya Utalii nchini ikiwa fursa hiyo itatumika kikamilifu kwa kuwa yanatarajiwa kutazamwa na kuleta maelfu ya mashabiki, wanahabari, wawekezaji na watalii kutoka Afrika na Duniani kote.

**Mheshimiwa Spika,** wakati Kamati ikichambua bajeti ya Wizara hii, haikuona mikakati mahsusi iliyowekwa na Wizara inayoonesha kushiriki na kutumia fursa ya uwepo wa mashindano haya kutangaza utalii. Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati madhubuti ili kutumia mashindano haya kuitangaza Tanzania na Vivutio vyake na kwa kuwafanya Wageni watakaokuja wakati wa mashindano haya kupata uelewa wa vivutio vyetu, waweze kuvitembelea na kuwa mabalozi wazuri wa Tanzania. Aidha, Serikali ihimize na kusimamia wamiliki wa hoteli kuziweka kwenye hadhi nzuri ili kuwezesha kupokea ugeni huu.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi kuhusu Utekelezaji wa Bajeti pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii, sasa naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati kama ifuatavyo: -

### 3.1 Maoni ya Jumla

(a) Serikali ihakikishe inaendelea kubuni mbinu mpya za kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi ili kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea vivutio hivyo hali itakayochangia kuongeza mapato ya Serikali, kukuza uchumi na kuongeza ajira katika mnyororo wa thamani kwenye shughuli zitokanazo na utalii nchini; na

(b) Serikali iendelee kuibua na kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati, kuboresha miundombinu ya utalii na uhifadhi pamoja na kuimarisha matumizi ya teknolojia za kisasa katika usimamizi wa uhifadhi.

### 3.2 Ushauri wa Kamati katika Maeneo Mahsusi kwa Wizara ya Maliasili na Utalii

#### A. Hali ya Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Ihakikishe fedha za miradi zilizotengwa na kuidhinishwa na Bunge zinatolewa kwa wakati ili miradi iliyokusudiwa ikamilike kama ilivyopangwa lakini pia kuepuka kuzalisha gharama za ziada; na
(ii) Kupitia timu za usimamizi na ukaguzi wa miradi, ihakikishe thamani ya fedha katika miradi inayotekelezwa inaonekana.

**B. Changamoto ya Wanyamapori Wakali na Waharibifu**

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Ifanye utafiti wa kina wa sababu, athari na mbinu za kukabiliana na changamoto hii ili kupata suluhisho la kudumu.

(ii) Iandae na kuboresha Mkakati mpya wa Kitaifa wa kushughulika na mgongano kati ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu ili kupata suluhisho la kudumu la changamoto hiyo kwa kushirikiana na wadau;

(iii) Iweke mpango mahsusi wa kulipa kwa wakati kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi walioathiriwa na wanyamapori ili kuleta maana halisi ya kifuta jasho na kifuta machozi;

(iv) Iweke mkakati wa kuhakikisha kuwa, maeneo yote yenye changamoto kubwa ya muingiliano yanawekewa uzio wa umeme ili kuondokana na changamoto hii; na

(v) Ihakikishe inaendelea kuimarisha ulinzi katika hifadhi na mapori yetu ili kutokomeza ujangili.

**C. Utalii wa Malikale**

Kamati inashauri kuwa, Serikali iongeze na kuweka mikakati ya kuibua, kuanzisha na kutangaza utalii wa malikale.

**D. Changamoto ya Miundombinu ya Utalii**

Kamati inashauri kuwa, Serikali ihakikishe inaandaa mpango Madhubuti na mahususi wa Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ili kupata ufumbuzi wa kudumu na kuwezesha maeneo ya vivuto vya utalii kufikika nyakati zote.

## E. Bodi ya Utalii Tanzania (TTB)

Kamati inashauri kuwa, Serikali: -

(i) Iweke/iboreshe mfumo utakaoiwezesha TTB kufanya shughuli zote za utangazaji utalii bila kuingiliwa kama yalivyo madhumuni ya uanzishwaji wake;

(ii) Iongeze uwekezaji katika kutangaza utalii na fedha zinazotengwa zitolewe kwa wakati ili kufanikisha utangazaji wa kimkakati;

(iii) Iifanyie TTB mageuzi Makubwa ya kimuundo na kimajukumu ikiwa ni pamoja na kuipa wataalamu wenye ujuzi na ubobevu kwenye kutangaza utalii;

(iv) Iweke mikakati ya kuiwezesha Bodi ya Utalii Tanzania kuwa huru, kujiendesha na kujitegemea kimapato ikiwa ni pamoja na kufanya uwekezaji na kuongeza vyanzo vya mapato; na Iongeze nguvu ya utangazaji wa Utalii kwenye masoko ya kimkakati ili kuendelea kuongeza idadi ya watalii nchini.

## F. Tozo za Maendeleo ya Utalii (TDL)

Kamati inashauri Serikali kutafakari upya malengo, mgawanyo na usimamizi wa fedha hizi ili tija iliyokusudiwa ipatikane.

## G. Migogoro ya Mipaka na Utwaaji wa Ardhi

Kamati inashauri kuwa, Serikali: -

(i) Iendelee kutatua migogoro ya mipaka nchini kati ya Wananchi na Hifadhi; na

(ii) Ihakikishe inapotwaa maeneo kwa ajili ya uhifadhi pamoja na shughuli zingine za maendeleo,

wananchi wanalipwa fidia stahiki na kwa wakati kama Katiba na Sheria za Ardhi zinavyoelekeza.

**H. Mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2027)**

Kamati inashauri kuwa, Serikali ihakikishe inaweka mikakati ya kutumia vizuri fursa ya uwepo wa mashindano haya ili kutangaza vivutio vya utalii nchini.

## 3.3 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa namna ambavyo mmekuwa mkitimiza majukumu yenu kwa weledi mkubwa na hivyo kuliwezesha Bunge letu Tukufu kutimiza wajibu wake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutumia fursa hii pia kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote cha Ziara za Ukaguzi wa Miradi na Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya hii. Kutokana na ufinyu wa muda sitaweza kuwataja kwa majina, lakini naomba majina yao yaingizwe katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo:

1. Mhe. Timotheo Paul Mnzava, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Mary Masanja, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Festo R. Sanga, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Haidary Hemed Sumry, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Cosmas Mtesigwa Bulala, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Fadhili Fabian Ngajilo, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Silvery Luboja Salvatory, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Yannick Ikayo Ndoinyo, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Chiku Athuman Issa, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Rashid Mohamed Mtima, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mb - Mjumbe
12. Mhe.Selina Henry Kingalame, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Mvita Mustafa Ali, Mb - Mjumbe

14. Mhe. Asia Abdulkarimu Halamga, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Khamis Ali Vuai, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Hadija Shabani Taya, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Joshua Samweli Nassari, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Issa Ally Mchungahela, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Amina Good said, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji (Mb) na Naibu Waziri, Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb) kwa ushirikiano wao mkubwa ambao umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi katika sekta hii. Aidha, nawashukuru pia Watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii chini ya uongozi wa Katibu Mkuu, Dkt. Hassan Abbasi, kwa ushirikiano na mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini si kwa umuhimu, kwa namna ya pekee, nawashukuru Watumishi wa Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge, Ndg. Baraka I. Leonard, kwa kuongoza vyema uratibu wa shughuli za Kamati na Bunge kwa ujumla hadi kukamilika kwa Taarifa hii na kuwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu, lipokee na kuijadili Taarifa hii pamoja na Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii **(Fungu 69),** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwasilisha.

Timotheo Paul Mnzava, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII**
15 Mei, 2026

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa wasilisho lako.

Waheshimiwa Wabunge tutaanza sasa uchangiaji na majina ni mengi sana kwa Wizara hii kama mnavyojua. Tutaanza na Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari, atafuatiwa na Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko ajiandae.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Maliasili na Utalii na zaidi sana nikiwa ni mchangiaji wa kwanza kwenye wizara hii. Awali ya yote, nimshukuru Mungu kwa kusimama tena ndani ya Bunge katika awamu nyingine hii nikiwakilisha Jimbo lile la Watu wa Meru, lakini nikipitia Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia nafasi hii kumshukuru sana Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Taifa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Kamati Kuu na Halmashauri Kuu ya Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi. Zaidi sana ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Arumeru Mashariki ambao wameona ninafaa kurudi hapa kuendelea kuwapigania hata pamoja ya misukosuko ambayo ilitokea hapo nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza kabisa; ninaanza kwa kutoa pongezi zangu kwa wizara. Yapo baadhi ya mageuzi ambayo tunasema mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Pamoja na changamoto nyingi ambazo sitazieleza hapa, lakini yako baadhi ya mageuzi ambayo yamefanyika. Huko nyuma sisi ambao tunatoka kwenye Ukanda wa Kaskazini ambao ni ukanda wa sekta hii, uwekezaji kwenye hifadhi zetu kuweza kuwekeza hoteli na nini ilikuwa ni changamoto kubwa sana. Kwa miaka ya karibuni tumeona mageuzi ambayo yamefanyika ya kuruhusu sekta binafsi kufanya uwekezaji kwenye kwenye *industry* ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumza hapo Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Utalii; ku-*declare interest* mimi ni Mjumbe wa Kamati hiyo. Amezungumzia habari ya miundobinu ya barabara. Sisi ambao tunatoka kaskazini, hususan

Mkoa wa Arusha ambao sehemu kubwa ya shughuli za vijana wetu ni utalii. Kwenye hifadhi zetu tukubaliane wazi kabisa na hizi mvua zilizonyesha na juzi, kila mtu hapa ni shahidi hahitaji kuhadithiwa tuliona kwa picha za kawaida na picha za video namna ambavyo magari yalikuwa amekwama, hususan kwenye *signature destination* tuliyonayo, kwa maana ya Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni lazima tuendelee kuweka msisitizo kwa wizara na hususan wenzetu wa Shirika la Hifadhi za Taifa la *TANAPA* kuendelea kuhakikisha kwamba barabara za ndani ya hifadhi zinapitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, leo tunapozungumza kuna barabara inaitwa Wagara kutoka *Central Serengeti* ukishuka kutoka Kirawira kwenda hadi Geti na Ndabaka ambayo iko *Western Serengeti*. Kwa mwezi huu Mei na mwezi Juni ndiko mahali ambako *migration* inakua; na inajulikana kwamba miongoni mwa kitu kinachouzwa sana kwenye Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ni uhamaji wa wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza Mheshimiwa Cosmas Bulala yuko pale; juzi alikuwa na wageni wake ambao sisi tumewa-*operate* kuwapeleka Serengeti; Kamati yake ya Ulinzi na usalama kwenye jimbo lake kule, wiki iliyopita. Pamoja na kwamba wanatokea Kwimba, watu walilazimika kwenda mpaka, wakazunguka wakaenda hadi Nata, Ikoma wakaenda kuingia kule hadi wakachelewa ilihali wana geti liko jirani, Bunda pale, pembeni ya lami kabisa wangeweza kuingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ni nini? Ni ile barabara ya Kilawira ambayo haipitiki. Miezi hii ya Mei na Juni ndiyo *migration* iliko. Sasa ni kwa nini hadi leo barabara hii haijaguswa ilihali ndiko watu wanakopaswa kwenda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika tumetoka juzi tumeona wageni wakikwama. Ni jambo la kumshukuru Mungu tu kwamba hatukuona mgeni yeyote akichukuliwa na maji; leo sijui tungekuwa tungeficha wapi uso wetu. Kwa hiyo tunataka kuzungumzia habari ya miundobinu na madaraja kule ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika eneo la Kogatende, kuna wakati ilifika hatua hadi ma-*guide* madereva wakapigwa faini pale na wengine kufungiwa kwa sababu wageni walilazimika kushuka ndani ya magari ili waweze kuona kivuko, kwa maana ya *migration* wanapovuka pale kwenye Mto Mara. Sababu ni moja tu, kwamba pale Kogatende daraja ni la chini, mvua ikinyesha kidogo tu maji yanajaa hamuwezi kupita juu watu wote inabidi mbaki upande mmoja; wakati daraja lingekuwa la juu wangeweza kuvuka wakaangalizia kwa upande zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambayo ninapenda kuzungumzia ni idadi ya watalii hapa ndani. Mheshimiwa Rais amepambana sana kunyanyua hii sekta ya utalii na kwa kweli lazima tumpe maua yake. Mpaka ikafika hatua yeye mwenyewe kuamua kutoka ofisini kwenda kufanya kuigiza filamu ya *Royal Tour;* lakini bado kuna namna ambavyo tunamwangusha. Yeye amesema kufikia 2030 anatamani kuona watalii 8,000,000 kwenye nchi hii. Leo hii wizara inatuambia watalii wamefika 5,300,000. Tunashukuru tunawapongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukweli ni kwamba hizi takwimu ukifuatilia, ni takwimu zinazochukuliwa kwenye *border*, kwenye mipaka yetu ya kuingilia. Uhalisia ni kwamba kuna mtu amehesabiwa kwamba ni mtalii katika hao 3,800,000 lakini alikuja pale Mwang'ola Karatu kuja kununua vitunguu kutoka Kenya, naye anaambiwa ni mtalii. Ukienda pale Rombo, kuna watu wanavuka pale kuja kufanya biashara ya mahindi pale Holili na Tarekea na wapi, nao wanahesabiwa kwamba ni watalii katika watalii milioni tano. Huu si ni ujinga? Tunajipongeza wenyewe, yaani tunajitekenya na kucheka. Tunajiambia tumefika watalii 5,000,000 wakati ni takwimu tu. Tunataka takwimu za watalii ambao wanakwenda kweli kwenye *destination* zetu za *tourism* kwa sababu *the country is blessed*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuache kuzungukazunguka hapa. Nchi imebarikiwa na kila kitu ambacho tungekitaka, ina kila kitu ambacho mataifa mengine yanatuonea wivu; lakini bado hatujatangaza ipasavyo. Tunapitwa na watalii, Morocco ukienda tunapitwa, ukienda Afrika Kusini unapitwa, ukienda wapi unapitwa wakati tuna vivutio vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninapenda kulizungumza, ni hii habari ya migogoro; na hili ninaomba nilizungumze nikiwa na uchungu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoka Jimbo la Meru; niliwahi kuzungumza hapa Bungeni wakati huo Kamati yetu ikiongozwa na Mheshimiwa Nape. Miongoni mwa maazimio tulizungumza wakati ule ni kwamba mambo haya ya utwaaji wa maeneo ambayo hifadhi inataka kuyachukua ni lazima ufanyike kwa ushirikishwaji. Nilipoondoka hapa nilipata neema ya kuwa Mkuu wa Wilaya, nimekuwa Mkuu wa Wilaya nne. Kwa hiyo nikageuza kutoka kupigania wananchi kwenda kusimamia shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Bunda, kuna Kata inaitwa Nyatwali, imehamishwa kata nzima tangu mwaka 1996. Serikali imeshindwa kusongeza watu pale, ilikuwa kila wakijaribu ni migogoro imeshindikana, imeshindikana. Jambo lile nimekuja kufanikiwa nikiwa Mkuu wa Wilaya na nilisimamia mwenyewe. Nini nilichofanya? Moja ya jambo nililofanya ni ushirikishwaji. Nilichukua timu ya watu kutoka Serikalini, Ofisi ya Rais ya wapi, nikaomba kuandikiwa *document* ya kuongoza zoezi. Nilivyopewa ile *document*, nikawachukua, nimekwenda kwenye Chama, Kamati ya Siasa ya Wilaya tumefanya wasilisho. Tumekwenda kwenye Halmashauri Kuu ya Kata tumefanya wasilisho, nimeenda nimeitisha mikutano kwa wananchi kwenye vijiji kule tumefanya *awareness* ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walipokuja Waheshimiwa Mawaziri Nane na wako hapa ndani, akina Mheshimiwa Mary Masanja, akina Mheshimiwa Silinde, akina nani wakati ule akiongozwa na Waziri wa Ardhi, alikuwa Mbunge wa Ilemela Mwanza. Alipokuja, baada ya kwenda kwenye mkutano kwa wananchi aliniambia Mheshimiwa Nassari tumekuja kufanya nini mbona kazi imekwisha hapa. Kwa sababu walifika wakakuta tayari wananchi washajiandikisha zaidi ya 100 kuomba wenyewe wafanyiwe uthamini kwa sababu *we engaged them* na tulihakikisha haki zao zinalindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya, nimeondoka Bunda watu wamekubali kufanya zoezi, leo ninaambiwa kuna mgogoro umeibuka pale Nyatwali mpaka leo watu hawajalipwa hela zao. Kwenye eneo linaitwa la Mjapani pale hawajalipwa pesa, unauliza kwa nini, wakati mimi nikiwa *DC* nimekuta *document* kwenye ofisi pale ambayo imekwenda kwa wananchi kuwarudishia eneo la Mjapani baada ya Mjapani kuondoka; lakini mpaka leo hawajalipwa, kwa nini? Kwa nini tunatesa wananchi wetu wenyewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninatoka Meru, pale Meru Ngarenanyuki; na hili ninaliongea kwa uchungu mkubwa; *1951, nine years before independence*, miaka tisa kabla ya uhuru, watu wa Meru walikaa kwenye vikao, wakachanga fedha, kwenye chungu haikuibiwa hata shilingi. Ninaomba tafadhali jambo ni muhimu sana; wakamtuma aliyekuwa Mbunge wetu wa kwanza hapa Mheshimiwa Japhet Kirilo Ayo Ngura, Marekani *New York* wakati wa ukoloni wakati huo, kwa ajili ya ardhi ya Meru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imepata uhuru, miaka mingi imekwenda mbele mpaka leo tunarudi tunakwenda tena kuhamisha wananchi wetu pale. Ninazo *documents* hapa ninaomba mtu wako aje achukue akuletee Mezani hapo, ninaomba kuzi-*register*. Leo kuna wananchi wanalipwa fidia, wanahamishwa kwenye eneo pale Ngarenanyuki, Kitongoji cha Nasura; mtu analipwa shilingi 17,200 anaambiwa ahame kwenye eneo lake, aende wapi? Mtu analipwa shilingi milioni mbili, milioni tatu, *documents are here*, huo si ni umaskini kwenye nchi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo mtu si wanamwachanisha na familia yake; akitoka akaenda mjini akala hiyo milioni tatu ikaisha, si familia imefarakana. Hana nyumba, hajaambiwa aende kwenye eneo lipi, hajahamishwa, analipwa fidia anaambiwa tunakulipa maendelezo, ardhi siyo ya kwako wakati ardhi hii tulinyang'anywa na wakoloni. Wakoloni wameondoka tumekuja kuanzisha hifadhi baadaye. Ninaomba sana, sana, watu wa wizara…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana…

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia. Tafadhali mimi nikiwa Mheshimiwa Mbunge wa watu wa Meru na ninaomba kusema hapa wazi kabisa, tena Mbunge wa Chama Cha Mapinduzi…

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** … moja ya nguzo ya CCM inasema "Nitasema ukweli daima, fitina kwangu Mwiko." Ninaomba kuwaambieni ukweli, hakuna mwananchi wa pale Ngarenanyuki *as long as* mimi ni Mheshimiwa Mbunge wao, atakayeondolewa kwa fidia ya hovyo namna hiyo, hakuna. Hatukatai maendeleo ya uhifadhi, hatukatai lakini *let's do it with dignity…*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana…

**MHE. JOSHUA S, NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, *TTB* na *AFCON* tafadhali sana Mheshimiwa Waziri, maoni ya Kamati yazingatiwe. Ninashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Eric James Shigongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Bahati Ndingo.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba kuanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kunipa nafasi ya kusimama tena ndani ya Bunge hili Tukufu. Kipekee kabisa ninampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri ambayo ameifanya. Msemo wa wazee wetu wa kale "Mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni", katika mambo ambayo Tanzania imefanya vizuri, katika mambo ambayo ninatembea na kujivuna kila ninapokwenda, ni sekta ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepanda, tumeenda kwa kasi na hii ni kwa sababu ya kiongozi aliyeko mbele yetu. Amesimama mbele Mheshimiwa Rais wetu, anatuongoza, mapato

yameongezeka. Ninafuatilia mambo yaliyofanyika katika nchi hii kwa hivi sasa; watalii wameongezeka, mapato yameongezeka, Pato la Taifa mchango wa utalii kwenye pato la Taifa umefikia 17.2%. Jirani zangu hapa, majirani zangu wanawafahamu wana asilimia saba, Rwanda wana asilimia tisa, Uganda wana asilimia 6.7, ni maendeleo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote nimeongea na nitarudia tena leo; njia pekee ya kuisaidia Tanzania kama nchi kutoka kwenye umaskini ni kutumia maliasili ambazo Mungu alitupatia ili mchango wa sekta katika nchi hii uweze kuongezeka kwenye pato la Taifa. Siku tukifanikiwa, sekta zote za uchumi wa nchi hii zikachangia kwenye pato la Taifa, umaskini utaondoka. Hii imeanza kuonekana kwenye utalii, pato limeongezeka; ndani ya miaka mitatu, minne tumetoka shilingi 1,000,000,000 mpaka shilingi 4,000,000,000, tunaelekea shilingi 5,000,000,000. Sasa hii ikifanyika kwenye madini, ikafanyika kwenye kilimo, ikafanyika kwenye uvuvi, umaskini wa nchi yetu utaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda mbele, kuna mambo matatu muhimu sana sitaki kuyasahau. La kwanza, kama alivyozungumza Mheshimiwa Nassari, kule kwangu Buchosa iko shida ya tozo ya kuingia kwenye hifadhi. Nimekwishazungumza sana na Mkurugenzi wa *TFS*, rafiki yangu sana, mtu mzuri, mtu mwema, mkarimu Dos Santos, akaniambia ni kwa mujibu wa sheria. Sisi Waheshimiwa Wabunge si ndiyo tunaotunga sheria? Basi sheria hiyo iletwe Bungeni tuirekebishe. Nikamfuata Mheshimiwa Waziri, nimeongea naye sana dada, shemeji yangu, mtu mkarimu na mtu rahimu, lakini sikupata majibu ya kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuwaje pale Buchosa? Buchosa kuna hifadhi kule Kome inaitwa Hifadhi ya Kome. Upande wa pili wa hifadhi wananchi wamepewa eneo wanafanya shughuli za uvuvi, ni ziwani; lakini wananchi wanaishi eneo kabla hujafika kwenye hifadhi kwa hiyo inawalazimu kila siku kulipa shilingi 3,000 kwenda kufanya shughuli za uvuvi kule upande wa pili. Ili uende kuvua ni lazima upite kwenye hifadhi, unalipa shilingi 3,000, wananchi wanalalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nimepigiwa simu kutoka Kisiwa cha Maisome, wananchi wanapigwa. Nimeshamweleza rafiki yangu Don Santos, anasema kwamba mbona kule chini hamna matatizo, ninamwambia watu wake wanamdanganya, aende mwenyewe akashuhudie, kuna mateso; na wananchi wanavyonisikia hivi sasa wanalalamika. Tukawaambia basi hii tozo waipunguze, shilingi 3,000 kila siku hawawezi kumudu watu wangu, sijapata majibu. Ninaomba suala hilo lizingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kwa Buchosa ni mamba. Watu wangu bado wanaliwa na mamba. Nimekwishazungumza hapa ndani, nimekwishasema sana, nimepoteza watu 32 ndani ya miaka mitano, wameliwa na mamba. Siwezi kukubali watu wangu waendelee kuliwa na mamba nikiwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru sana wizara imetujengea vizimba, lakini vizimba utajenga kila mahali? Wana fedha ya kujenga vizimba Kanyala, Luhama na Kahunda? Haitawezekana. Mimi nimewaeleza, kitu pekee cha kufanya hapa siyo vizimba peke yake, mamba wamezidi, idadi ya mamba imekuwa kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sensa ya mamba imefanyika mwaka 1985, waende wakawavune mamba wapungue, watu wanaliwa. Ukiwaeleza wanasema mamba wanalindwa na sheria za kimataifa. Haki ya kuishi binadamu ni haki ya kwanza. Nani aishi, mamba au aishi binadamu? Aishi binadamu kwanza. Kwa hiyo ninachokiomba, ifanyike sensa halafu mamba hawa wavunwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu; barabara ya lami inajengwa, kaka yangu Mheshimiwa Tabasam yuko hapa, tumepambana tunajenga barabara ya lami toka Sengerema mpaka Nyehunge baadaye Kahunda. Ninaomba, pale Kahunda tufunguliwe geti kwa ajili ya kwenda kwenye Hifadhi ya Rubondo ili watalii watoke Mwanza waende mpaka Kahunda wapite kwenye geti la Kahunda kwenda Rubondo kilomita 50, ni karibu zaidi. Hiyo itasaidia nchi yetu kupata watalii lakini itasaidia halmashauri yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, biashara ya utalii ni kama biashara nyingine yoyote, ni mapambano. Tunapambana na Kenya, tunapambana *South Africa*, tunapambana na n hi nyingine nyingi sana. Ninaomba *TTB* iwe *empowered*, ipewe nguvu, ipewe fedha. Siyo fedha peke yake, wapewe fedha na baadaye wapewe *freedom* ili waweze kufanya kazi kwa akili zao. Tuondoe *political intervention,* tunawatafuta watu wazuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakwambia ukweli, ninamwamini sana Mafuru. Ninamwamini Mafuru tangu akiwa *TBL,* ameenda sukari, amechukuliwa akaenda *South Africa* mambo ya *marketing*, amefanya kazi nzuri mno, lakini tukafika *TTB* pale ninamwona amezubaa tu. Mafuru vipi mbona sikuelewi, ananiambia kaka tunaendelea hivyo hivyo kimjini mjini. Wapeni fedha, wafanye kazi, wana uwezo na wasiingiliwe. Zaidi ya hayo, wa-*invest* sana kwenye *digital marketing*, *marketing* ya leo siyo ya kubandikabandika mabango, watu wako kwenye mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninasoma hapa sasa hivi, nimesema *where to visit in Africa*, hapa tu nimekaa nikakuta Serengeti haijatajwa kama *destination* ya kwanza. Kuna ujanja unafanyika…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dakika moja tu. *Marketing* ya kwenye mtandao siyo tu kwamba inahitaji ku-*post*, kuna *algorithm* unapo-*post* ili uonekane wa kwanza pale juu kwenye *Google* kuna vitu vina inafanyika. *TTB* wanisikilize, watafute watu wenye *influence* duniani wa-*post* mambo yao. Watafute waandishi, *websites, celebrities, influencers* ili hao watu wakitu-*post* leo, mtu akitaka kusafiri duniani; hata Mheshimiwa Mwenyekiti wewe ukitaka kusafiri unaandikaje, ninataka kwenda Tanzania, nitembelee wapi? Majibu utakayoyapata kule, ndiko unakokwenda. *Influence* iko kwenye mtandao.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana…

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Alitumia neno tunapambana, ninadhani alitaka kusema tunashindana. Ninadhani hatupambani na nchi nyingine, tunashindana. Tunaendelea Waheshimiwa, ninamwita sasa Mheshimiwa Bahati Ndingo, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema William Mgaya na Mheshimiwa Mdowe Haji Kombo ajiandae.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kupata fursa. Ninaungana na Waheshimiwa wenzangu kwanza kwa kumpongeza; sina mashaka na Mheshimiwa Waziri na timu yake; ni timu ambayo ninaiamini kama Mheshimiwa Rais alivyowaamini. Lengo la Mheshimiwa Rais ni kurejesha tabasamu kwa wananchi. Ninaamini kupitia Wizara hii ambayo imekuwa chachu ya migogoro mingi ambayo tunayo Mbarali, ni kwamba, sasa watakwenda kurejesha tabasamu kwa Wanambarali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kwamba sisi Wanambarali hatukuomba wakati wa kuzaliwa tujikute tuko karibu na hifadhi, lakini ilitokea babu zetu, bibi zetu, tumekuta wako pale na sisi tukazaliwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa dada yangu Mheshimiwa Dkt. Ashatu Jumatatu atakuja kufanya *wind up* hapa, nimwombe aje na majibu sahihi. Tunafahamu kwa mujibu wa *GN 754*, yako maeneo ambayo yanasubiri wananchi walipwe fidia ili waweze kupisha maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako maeneo mawili wakulima wanaolima mnazi na wanaolima mlonga, *TANAPA* wamewasimamisha kufanya shughuli zozote pale hawajalipwa mwaka wa tatu huu na huwezi kukuta taarifa kwa Mkuu wa Mkoa wala huwezi kukuta taarifa kwa Mkuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatufanyi sawa. Tunazo sheria na ninaomba Jumatatu tupate majibu sahihi. Wamesimamisha maeneo yale bila kuwalipa watu fidia, wananchi hawa

wanauziwa nyumba zao na wamefilisiwa; siyo sawa. Niombe Wizara watuletee majibu Jumatatu hapa nini kimetokea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni lazima ieleweke wazi hakuna Mwanambarali aliyevamia hifadhi, ila ni hifadhi wanafanya utanuzi wa kuja kwa wananchi. Ili kupisha kwa sababu ya uhifadhi, *TANAPA* baada ya *GN* 754 walishaweka zile *beacon*. Ninaomba na ninamwomba Mheshimiwa Waziri wananchi wale bado wana stahiki zao ambapo wao kwa upande wa Serikali hawajatimiza wajibu wao wa kisheria kuwawezesha wale wananchi kuondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe wawaache wananchi wale kwa utaratibu ambao tulikubaliana kama ni kilimo wafanye kilimo kwenye mita zilizokubaliana karibu na pembezoni mwa mto wawaambie. Kama ni kilimo kipindi cha kutotumia maji ya Ruaha wawaelekeze lakini siyo kuwanyanyasa wakati bado Serikali hawajatimiza wajibu wao. Niwaombe sana Mbarali na Wanambarali hatuna tatizo na Serikali ila migogoro mingi wanatusababishia wao kwa kutotimiza wajibu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana sisi Wanambarali sasa hivi hatutaki migogoro wala kuonekana ni wilaya ambayo kila siku inazungumzwa kwa migogoro. Tafadhali sana sana tupate majibu sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane vilevile na ushauri wa Kamati. Sisi ni miongoni mwa watu ambao tuna athari kubwa sana za tembo na tunaishukuru Serikali kwamba wametujengea kituo pale Igava, tunaomba kituo kile basi kimalizike. Kwa sababu tukipata dharura kubwa inayohitaji msaada askari wa wanyamapori wanakaa Iringa kule huku Mbarali tunakosa msaada. Tuwaombe sana kituo kile kikamilike ili wananchi wetu waweze kupata msaada na Askari wa Wanyamapori wawepo pale ili wawasaidie wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la fidia; wanaoliwa mazao haya jamani ni wakulima wadogo ambaye mtaji wake ni eka tano au tatu, lakini anachukua miaka mitatu kulipwa fidia. Yaani anachukua mtaji wake uleule wote wa eka tatu walizolima, eka

tano alizolima, miaka yote hii anasubiria fidia. Leo hii tembo akigongwa barabarani kunakuwa na mshike mshike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii mnyama akigongwa pale Mikumi hiyo mbingembinge lake ni balaa. Hebu tuangalie jamani tuwasaidie wananchi wetu. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan amejipambanua anataka kurejesha tabasamu kwa wananchi. Wizara hii itusaidie, changamoto ni kubwa. Watusaidie wawe na utu na utulivu wakati wa kusaidia wananchi wetu, tunawaomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawaomba sana. Tunapata shida sana, wanatuweka katika wakati mgumu sana na wanachonganisha sana wananchi na Serikali yao. Niwaombe sana yaani (Ee Mungu wangu tusaidie). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia kabisa dada yangu Mheshimiwa Dkt. Ashatu ninamwamini sana, watusaidie Wanambarali. Wanambarali hatuna migogoro, migogoro mingi ni Serikali kushindwa kutimiza wajibu wao. Wanambarali wako tayari kufanya kazi kwa kufuata sheria. Tunaomba watusaidie jamani kila siku Mbarali, Mbarali, Mbarali. Hivi hata kweli na wao hawachoki tu kila siku Mbarali yaani ukisikia Mbarali mpaka Mawaziri wengine wanaogopa kuja Mbarali kwa sababu hawana majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata viongozi wengine wanashindwa kufanya ziara Mbarali hawana majibu. Ukiwauliza huu utaratibu umefuatwa kwa vigezo vipi hawana majibu. Yaani inawezekana tu mtu leo anaamka anaenda kule porini wanafyeka mazao ya watu; siyo sawa hebu watusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wana Mbarali tunahitaji kupata tabasamu ambalo Mheshimiwa Rais ametuahidi. Kazi kubwa ya maendeleo imefanywa Mbarali. Muda wote tuko kwenye migogoro badala ya kueleza kazi kubwa ambazo Mheshimiwa Rais amezifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ninaomba Mheshimiwa Dkt. Ashatu, dada yangu aje na majibu, la sivyo hapa patachimbika Jumatatu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Neema William Mgaya atafutiwa na Mheshimiwa Mdowe Haji Kombo, Mheshimiwa Chiku… (ngoja niwataje hawa wawili kwanza). Endelea Mheshimiwa Neema.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali cha kuweza kusimama mbele ya Bunge hili na kuweza kuchangia hii Hotuba ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji mkubwa alioufanya katika hii Sekta ya Utalii. Vilevile, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na timu yao yote kwa kazi nzuri wanayoifanya katika hii Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitazungumzia sehemu mbili. Sehemu ya kwanza nitazungumzia namna ya kufungua masoko mapya ya utalii na namna bora ya kutafuta masoko kulingana na soko tunalolihitaji kwa sasa hivi. Vilevile, nitazungumzia mashindano ya *AFCON* na fursa za utalii ndani ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa hakuna ambaye hajui kwamba kuna vita vinavyoendelea kati ya Marekani, Israel na Iran. Sisi soko letu kubwa la utalii ni Wamarekani. Vilevile, tujikumbushe Oktoba 29 yale yaliyotokea kulipelekea *travelling ban* za nchi kama Uingereza, Marekani, Italy na Spain na ukiangalia kwamba nchi hizi ndiyo soko letu kubwa liko huko la utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi ninaona Wizara sasa ione namna ya kuweza kutafuta masoko mengine duniani ili tuweze kuendelea kupata watalii wa uhakika na tuweze kufanya biashara yetu vizuri ya utalii. Katika hili nimpongeze Mheshimiwa

Waziri kwenye Hotuba yake nimeona kwamba wamejipanga kutafuta masoko mapya ya utalii Mashariki ya Mbali kama vile Nchi za Asia lakini na Nchi za Ghuba ya Uajemi. Niwapongeze sana kwa hatua hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hatua hizo ambazo Wizara imezichukua ninataka niwashauri katika suala zima la masoko. Ni muda mwafaka sasa kuhakikisha kwamba tunakwenda kutangaza utalii wetu kidijiti. Kwa sababu gani? Ukiangalia mfano wa wasafiri wananchi wa China wakipanga safari zao kwenda nje ya nchi yao asilimia kubwa karibu asilimia 72 wanaandaa, wanafanya maandalizi yao ya safari kupitia njia ya mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kuna kila sababu ya sisi kutumia *digital market* katika kuhakikisha kwamba tunatangaza utalii wetu. Pia, ukifuatilia zaidi asilimia kubwa ya watalii hao *age group* yao ni kati ya miaka 25 mpaka miaka 45 na hao wote wana utaratibu wa kuandaa safari zao kwa kutumia njia ya kidijiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili sioni Bodi ya Utalii kama imeweka kipaumbele kutumia njia ya kidijiti katika kufanya masoko. Dunia sasa hivi ipo kiganjani, mambo yote duniani sasa hivi yapo kiganjani. Hakuna namna tutakwepa kutafuta masoko kwa njia ya kidijiti. Niishauri Bodi ya Utalii iweze kufanya masoko yao kwa kutumia njia ya kidijiti ili tuweze kuendana na soko ambalo tunalihitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimesikiliza Hotuba ya Kamati ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Ninaungana nao katika kusisitiza kwamba kunahitaji mabadiliko ya muundo wa Bodi ya Utalii. Vilevile, wameonesha na kutuambia kwamba kuna upungufu wa wataalamu katika kitengo cha *marketing.* Ukiangalia haya yote yanayoendelea ninaweza kuthibitisha na kuona kwamba kweli tunahitaji waongezewe wataalamu kwenye kitengo cha *marketing* na wataalamu hao watakaoongezewa, basi waweze kuendana na jinsi ulimwengu unavyokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la pili la Mashindano ya *AFCON* na fursa tutakazozipata za utalii ndani ya nchi yetu ya

Tanzania, kuna siku moja nilishangaa sana. Nilimwona Naibu Waziri wa Wizara ya Sanaa na Michezo akijibu swali linalohusiana na upungufu wa malazi kule Arusha pindi itakapofika Mashindano hayo ya *AFCON*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati anajibu swali lile alikiri kwamba kuna mapungufu, lakini nikashangaa akaenda mbali zaidi akasema kwamba kama Wizara ya Sanaa na Michezo wataandaa mfumo wa kuwasajili nyumba za baadhi ya wananchi ili ziingie kwenye mfumo wa *Airbnb* ili ziweze ku-*accommodate* hao watu watakaokwenda kwenye mashindano ya *AFCON*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikajiuliza, Bodi ya Utalii na Wizara ya Utalii ipo wapi? Yaani iweje leo Wizara ya Sanaa na Michezo ifanye kazi hiyo wakati niliangalia Morocco walifanya nini? Morocco masuala ya malazi na *hospitality* yote yalifanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii na wale Wizara ya Sanaa na Michezo wakabaki tu wao kufanya yale mambo ya *technicalities* ya kuangalia kwamba uwanja unakidhi vigezo kutokana na mashindano hayo ya *FIFA,* kuangalia *delegation* za *FIFA delegation* za *CAF,* lakini leo… *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema, malizia.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie. Leo nimepata angalau moyo baada ya kusikia Mheshimiwa Waziri akitaja mikakati mbalimbali waliyojipanga kuweza kukabiliana na hizo fursa za Mashindano ya *AFCON*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Wizara waanze kufanya hiyo mikakati kwa kasi kubwa kwa sababu Juni mwakani siyo mbali. Tulitegemea sasa hivi tuone Bodi ya Utalii ikitangaza vivutio mbalimbali ambavyo hawa watu watakaokuja kushiriki katika mashindano haya ya *AFCON* waanze kuona, waanze kujipanga kwamba nikifika Tanzania nitakwenda kufanya moja, mbili, tatu katika utalii. Si mbaya lakini Wizara nayo…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema, ahsante.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ikaangalia na taasisi zingine nazo ziangalie namna gani ya kutangaza vivutio vyao: *TANAPA,* Ngorongoro, *TAWA, TFS*. Hasa hasa *TFS* jamani tunawategemea sana watangaze utalii wa kiikolojia. Nyanda za juu Kusini tumeachwa mbali sana…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Mgaya, ahsante sana, ninaomba uunge mkono hoja.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba watumie fursa hii, nyanda za juu Kusini watangaze utalii wa kiikolojia. Tuna misitu mizuri, watu wakaone ndege, watu wakatembelee misitu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema, ahsante sana.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimboni kwako Njombe pia waweze kuja. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Mgaya, ahsante sana. Tunaendelea, nimwite sasa Mheshimiwa Mdowe Haji Kombo atafuatiwa na Mheshimiwa Chiku Athman Issa, ninadhani muda utatutosha tutakwenda na Mheshimiwa Ali Khalil Mirza. *(Makofi)*

**MHE. MDOWE HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moyo usiokuwa na shukrani hukausha mema yote. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia leo kukutana hapa tukiwa katika hali ya uzima na afya, lakini nikushukuru nawe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hoja ya Wizara hii muhimu sana kwa mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee sana ninaomba nimpongeze na kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini na kuniteua kuwa mgombea wa Jimbo la Nungwi katika Uchaguzi wa Mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru pia wananchi wenzangu wa Jimbo la Nungwi baada ya kuaminiwa na Chama changu na wao wakakiamini Chama changu na kunichagua

kuwa Mbunge wao nitakayewakilisha sauti zao katika Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi yangu kwao ni ileile ambayo tumekubaliana siku zote, nitakuwa sauti itakayochochea mabadiliko ya kweli katika Jimbo letu la Nungwi. Baada ya shukrani hizo, ninaomba moja kwa moja nijikite katika mchango wangu wa siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya utalii imeendelea kufanya vizuri sana duniani. Sekta hii imekuwa ina ukuaji mkubwa sana unaochochea maendeleo katika nchi ambazo zinajikita katika sekta hii ya utalii. Hata katika Nchi yetu ya Tanzania tunaitegemea sana sekta hii. Kwa mujibu wa taarifa ambazo zinatolewa na Benki ya Dunia na Serikali ya Tanzania zimeonyesha kwamba sekta hii imekuwa ni chanzo kikubwa cha kupata fedha za kigeni katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na mafanikio hayo, lakini bado tuna suala muhimu sana la kujiuliza. Ni kwa namna gani basi sekta hii inachochea na inawanufaisha katika maendeleo ya vijana katika nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijana wa Tanzania, Tanzania hii imekuwa ni Taifa la vijana na kwa nini limekuwa ni Taifa la vijana? Kwa sababu zaidi ya 60% ya wakazi wa nchi hii, ni vijana au ni watu ambao wapo chini ya umri wa miaka 35, lakini ukiangalia bado vijana hawa hawajanufaika ipasavyo na wamebaki kuwa waangaliaji wa sekta hii na siyo washiriki wakuu kwa ajili ya kujiletea maendeleo ya Taifa, lakini na kujiletea maendeleo yao binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaiomba sana sana Serikali yangu kupitia hii Wizara ya Utalii iangalie kwa jicho la tatu vijana wa Tanzania kwa sababu tunaamini kwamba Tanzania wapo vijana ambao wana uwezo, lakini wanayo nia ya kuwekeza katika sekta hii ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mdogo mimi nitatolea; yupo kijana mmoja juzi tu kanitafuta. Yeye baba yake tayari

ameshatangulia mbele ya haki, lakini analo eneo ambalo kaachiwa ni urithi. Eneo lile ana mpango wa kuliendeleza kwamba yeye pale ajenge nyumba za kulaza wageni na asaidie sekta hii ya utalii na yeye mwenyewe apate kujiingizia kipato lakini kitu ambacho kinamkwamisha ni kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba sana Serikali yangu ielekeze zaidi kuanzisha Mfuko ambao utawasaidia vijana ambao wana malengo ya kujiendeleza katika sekta hii ya utalii ili basi waweze kupata mikopo nafuu, lakini waweze kupata ruzuku kwa sababu hiyo ndiyo imekuwa changamoto ya vijana wengi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kuna changamoto sana katika masuala ya elimu yetu ya Tanzania na mwingiliano wa soko letu la ajira. Ninaishauri sana Serikali yangu ya Tanzania ikajikite zaidi kwenda kuangalia elimu ambayo itakwenda kuwasaidia vijana wa Tanzania kuingia moja kwa moja katika soko hili la utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano kuna fani za *hospitality*. Fani hizi zimekuwa bado hazipewi kipaumbele kinachostahiki kwa Taifa letu la Tanzania. Wapo vijana wengi katika Tanzania, lakini wengi wanajikuta hawafikii malengo kwa sababu ya kukosa elimu. Mfano, nitatolea mfano, katika Jimbo letu la Nungwi. Sisi kule Nungwi tumebarikiwa sana kuwa na wawekezaji wa masuala haya ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoteli nyingi sana zimejengwa katika Jimbo letu kule Nungwi, lakini sasa kitu ambacho kinawakwamisha vijana kuingia katika soko lile ni kwamba hawana ujuzi. Kwa hiyo, ninachukua nafasi hii kuiomba Serikali yangu ya Tanzania ituone kwa jicho la tatu ikatujengee chuo ambacho kitawasaidia vijana katika Jimbo letu la Nungwi kunufaika na sekta hii ya utalii na waondokane na ile adha ya kwamba wao wamekuwa ni waangaliaji tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba sasa niunge mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Chiku Athman Issa.

**MHE. CHIKU A. ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niwe mmoja kati ya wachangiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetupa nafasi ya kukutana siku ya leo. Ninamshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya kwa kukuza uchumi wa nchi hii katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya maliasili na utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru Wizara ikiongozwa na mdogo wangu, Waziri wetu Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji. Ninawashukuru pia viongozi wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niende moja kwa moja kwa sababu ya muda nijikite kwenye suala la michezo iliyopo mbele yetu ya *AFCON*. *AFCON* ni fursa kubwa katika nchi yetu, *AFCON* siyo michezo peke yake, *AFCON* inakuja kukuza utalii wa nchi yetu, uchumi, biashara pamoja na ajira kwa vijana na wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi hii kuiomba Wizara ikaitumie *TTB* kama mdau mkubwa ambaye ataenda kusimamia kutangaza na kuratibu shughuli zote za *AFCON* kwa sababu *TTB* imeanzishwa kwa madhumuni hayo. Kumekuwa na mkanganyiko kwa *TTB* kuiona kwamba kama alivyosema ndugu yangu Mheshimiwa Shigongo hapa, *TTB* haionekani inafanya kazi yake kama ambavyo matakwa ya kisheria iliyoanzishwa inataka ifanye hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TTB* iwezeshwe kwa kupewa fedha; *TTB* iwezeshe kwa kupewa *independence*. Ina watu mahiri mashuhuri ambao wamefanya kazi kubwa nchi hii, kwa hiyo, kwa kuwatumia *TTB* waende wakaunganisha utalii na michezo wakati wa *AFCON*; waende wakatangaze *sports tourism* wakati wa *AFCON*; waende kuuza mechi zetu na utalii wakati wa *AFCON*; waende kuhakikisha kwamba kila mtu anajua watakapofika

Tanzania wategemee kukuta kitu gani. Kusiwe na mwingiliano wa sekta nyingine za ndani ya Wizara, itokee *TANAPA* wanaingia wanafanya *marketing*, itokee Ngorongoro wanafanya *marketing*, wakae pamoja wakiwa *coordinated* na *TTB*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha pili kwenye *AFCON*, ninaomba tukaboreshe miundombinu. Barabara, ndege zetu za ndani ziwe *reliable*, ziwe kwa wakati na zifike zinakotakiwa ili wanaokuja kwenye michezo waweze ku-*enjoy* na kutumia pesa ambazo wamezitumia kuja kuongeza furaha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwe na huduma za uhakika za *internet* nchi nzima. Wakati ambapo watalii wapo kwetu hapa nchini, hawa hawa ndiyo watakuwa mabalozi wa kutuma habari zinazoendelea huko duniani. *TTB* na wadau wa utalii wakae chini waje na *special package;* hii *package*, nimemwona ndugu yangu Zahara amekuja, karibu sana, pamoja na timu yake kutoka Moshi. Tunawaomba wakae pamoja waweze kuja na *package* ambayo itakuwa *more attractive*. *(Mkofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa mashindano hayo tuendelee kuitangaza nchi yetu kupitia sanaa, ngoma zetu, chakula, mavazi pamoja na matamasha. Kuna mambo muhimu sana ambayo tunatakiwa kufanya. Moja ni kutoa huduma bora wakati wa mashindano ya *AFCON*; tuhakikishe usalama wa wageni wetu; tuhakikishe usafi wa miji yetu; tuhakikishe hoteli zetu zinatoa huduma nzuri na bora; lugha za watoa huduma ziwe lugha safi zinazoeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, urahisi wa kupata *Visa* pia Serikali iangalie jambo hili. Malipo ya kidijiti, hakuna mtu siku hizi anatembea na pesa. Hii itawafanya wageni wetu waje wa-*enjoy* na warudi waweze kwenda kutumikia. *AFCON* itumike siyo tu kwa mpira pekee, *AFCON* itumike kuwa jukwaa la kutangaza utalii, utamaduni, uwekezaji na biashara duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa watu wangu wa Mkoa wa Arusha, ninawaomba vijana wa Mkoa wa Arusha na wanawake tutoke tuanze kujiandaa, tumechelewa. Tujiandae kwa ajili ya mashindano ya *AFCON*, biashara ambazo tunazifanya

tukaziweke mahali sahihi, tuunganishe nguvu vikundi vyote viweze kufanya kazi kwa pamoja; tuwe na ubunifu wa kutengeneza *Souvenir* ambazo watu wetu wageni wetu watanunua na kuzirudisha nyumbani wanakototа. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ninamwita sasa Mheshimiwa Ali Khalil Mirza. Muda ukiruhusu tutamalizia na Mheshimiwa Musa Godfrey Mbuga.

**MHE. ALI KHALIL MIRZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuchipa nafasi hii ya kuchangia na awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uzima wa kuweza kufanya shughuli yetu ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninapenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri iliojaa maono na yenye nambari zinazoonyesha kwamba Mheshimiwa anajua wapi anakwenda, anajua *true north* yake ilipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita zaidi katika Sekta ya Utalii. Sekta hii ni muhimu katika kuchangia pato letu la Taifa, fedha za kigeni, kuzalisha ajira, lakini pia kuitangaza nchi yetu Tanzania Kimataifa. Utafiti unaonyesha kwamba, mtalii mmoja anayekuja nchini anachangia ajira tatu. Vilevile, fedha zinazoingia nchini huwa zina mwelekeo mkubwa zaidi ya kuchangia moja kwa moja na zaidi zile zilizokuwa zinachangia, siyo moja kwa moja ni *direct* na *indirect*, pamoja na kutanua na ukuaji wa sekta nyingine, huo ndiyo umuhimu wa utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Utalii pamoja na Tanzania kufanya vizuri ni sekta ambayo ina ushindani mkubwa, na ushindani huo haupo tu kikanda lakini pia upo Kimataifa. Hapa ninampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa juhudi aliyochukua kwa kuanzisha na kufanya *Royal Tour*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii lazima utangazwe na kutangazwa ni muhimu kwa sababu utalii *nature* yake unamuuzia mtu *package* ambayo inakuja kwako bila yeye kujua. Wewe inabidi umshawishi kwa kile ambacho unacho. Sasa, suala la kutangaza utalii duniani hilo haliepukiki. Hiyo ni dhamana ya Bodi ya Utalii *(TTB)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya *TTB* haitaki *restructuring*, Boda ya *TTB* inataka kuwezeshwa. Kuwezeshwa kifedha na kuwezeshwa kiutaalamu, hasa katika utaalamu wa masoko na utaalamu wa kujitangaza. Nchi nyingi ambazo zimeendelea kiutalii na wale washindani wetu wame-*invest* sana katika kutangaza utalii. Katika kujitangaza tunaona bado tupo katika yale masoko ambayo tunasema ni *traditional;* Marekani, Ulaya Magharibi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tujikumbushe mwaka 2009 ilipotokezea *credit crunch* Marekani, watalii wengi kutoka Marekani na Ulaya Magharibi walikatiza safari zao mpaka walipo-*recover*. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri ametaja kwamba kuna mipango ya kutanua wigo na kuimarisha masoko Mashariki ya Mbali, lakini Uchina, India na kadhalika hizo ni nchi ambazo sasa hivi zimejitokeza kwamba zinaleta watalii wengi na zina wasafiri wengi sana duniani. Katika kuendeleza utalii wakati tunatanua wigo wa masoko yetu, pia ndani ya nchi na sisi tunatakiwa tujitayarishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, 70% ya watalii wote wanaokuja nchini kwetu wanapitia uwanja wa ndege. Kwa hivyo, lile suala zima la mapokezi wanapokuja na wanapoondoka ni muhimu. Kwa sababu, ile *impression* anayoiacha ndiyo inakuwa *lasting impression* wanapokwenda kwao. Hili suala ambalo limezungumzwa sana katika sekta ya utalii, ni watu wanavyokusifu inakuwa ndiyo wale wanakutangazia kuja kwa watalii wengi. Kwa sababu, kile kinachozungumza kinachotoka mdomoni huwa kinafahamika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, lingine utalii ni *publicly promoted* lakini *private driven* yaani iko chini ya Sekta ya Umma

lakini inaendeshwa na Sekta Binafsi. Hapa ushirikiano ya *PPP* ni muhimu; hawa wenzetu wa *private sector* tuwaone kama ni wenzetu ambao tuko nao pamoja katika kujenga utalii, kwa sababu hoteli zote wanauza misafara na kadhalika, hawa wote wanatokana na *private sector*. Kwa hivyo, sisi lazima tuwasaidie ili wao wanavyotanuka zaidi na sisi ndio tunaweza kupokea zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kufikia watalii 8,000,000 hilo linawezekana kabisa kwa kutazama umahiri wa Tanzania, uzuri wa Tanzania na usalama wa Tanzania. Watalii wanaangalia vitu vitatu; kwanza, usalama wa nchi yako, yaani kiusalama. Pili, wanaangalia usalama wa nchi yako wao wakija wanaweza kutembea, hilo lipo Tanzania. Tatu, salama nchi yako kiafya. Hakuna mtu anakwenda katika *destination* yenye *Ebola* au yenye milipuko. Kwa hivyo, sisi Tanzania tuna *advantage* kubwa, lakini sisi tunatakiwa tuamke tujiamini na kwa *region* hii ya *Sub-Saharan Africa*, ninaona bado tuko vizuri na tutaendelea kwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya hayo, ninaunga mkono hotuba hii mia juu ya mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii ya kuchangia Wizara yetu ya Maliasili na Utalii. Ninapenda kuanza kwa kusema kwamba, sisi ambao tuko Jimbo la Kilombero, tuna Hifadhi ya Nyerere na Hifadhi ya Udzungwa; tuko kama katikati. Kwa hiyo, matunda mengi yanayotokana na Wizara hii yanatusaidia sisi sote katika Mfuko Mkuu wa Serikali, lakini katika wananchi wetu. Kwa hiyo, ni sekta muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kushukuru kwa kazi kubwa ambayo Serikali imeendelea kuifanya katika Wizara hii, kwa maana ya Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, watu wa Hifadhi *TANAPA* na Katibu Mkuu wa Wizara kwa ujumla wanafanya kazi kubwa. Hata kama changamoto zinapotokea basi zinatokea kutokana na mazingira yetu ambayo tunayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kwa kweli kuna hali ya wanyama tembo; tembo wamekuwa ni tatizo kubwa sana kwa Jimbo la Kilombero. Unavyovuka Daraja la Kidatu upande wa kulia unakutana na Hifadhi ya Udzungwa kuna baadhi ya wananchi wanaishi, mpaka unafika karibu kata zangu zote 10 upande mmoja zinapakana na Hifadhi ya Udzungwa na upande wa chini wanapakana na Hifadhi ya Nyerere kama nilivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna mkakati wa Barabara ya Ushiroba ambayo ingesaidia tembo wapite chini ya barabara, lakini haijaleta matunda mazuri. Juzi kuna mwananchi amekufa, imeleta *tension* kubwa sana, ameuawa na tembo. Tulikuwa tukisema mara zote kwamba, tunaomba Serikali ijaribu kuweka nguvu kubwa kwa sababu sisi ni *special case*, kwa maana ya eneo ambalo tupo, tembo wamekuwa wakisumbua watu wengi tu sana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, lingine ni uadilifu wa watu wetu wa *TANAPA* kule chini. Wanakuwa wanawaangusha viongozi wao na ndiyo maana jambo ambalo nimekuwa nikilalamikia. Ninawashukuru sana viongozi wa Wizara, Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu nimemwona, Naibu Waziri na Mkurugenzi Mkuu wa *TANAPA*, wamenijulisha kwamba washachukua hatua. Jambo limetokea muda mrefu na nilikuwa nikilisema, kuna baadhi ya askari wetu wanatumika kisiasa. Hili jambo halipendezi. Kwa kuwa tu ni Mbunge na ni mvumilivu, lakini walitufanyia kitendo ambacho siyo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeenda kusaidia vijana kujenga banda kwenye eneo la *TANROADS,* lakini wamekuja askari, amenikunjakunja na nini na bahati nzuri nina *video* zote. Sasa, nimelifikisha jambo hili vizuri nikataka wachukue hatua kwa sababu haikuleta picha nzuri mbele ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, cha kusikitisha zaidi na Mheshimiwa Waziri ninataka aichukue hii. Nitampa video Mheshimiwa Rais amesimama kwenye eneo nililosimama mimi; wananchi katika kuzungumza na Mheshimiwa Rais wameomba Rais amezungumza kuwajibu wananchi wale. Mheshimiwa Rais

ameshatoa maelekezo pale, ijapokuwa sisi hilo suala la banda halihusiani na eneo la hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la hifadhi Mheshimiwa Rais katoa maelekezo yake na barua imeandikwa na Wizara na Waziri aliyekutangulia, kuhusu eneo la hifadhi kwa wananchi wale, mpaka leo halijatolewa majibu. Kwa hiyo, ninaomba sana walifanyie kazi jambo hili, kwa sababu vinginevyo sisi hapa tunaunga mkono hoja tunapitisha bajeti. Huko mbele ya safari kwa kweli lugha itakuwa tofauti. Hapa ninajitahidi sana kuongea kwa utaratibu, lakini kwa kweli nimefanyiwa kitu ambacho hakifai na hakipendezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ninataka kuzungumza kuhusu Tarafa ya Ifakara Mjini pale. Kwa mfano ukitoka Kidatu kuja Ifakara unakutana na kata 10 ambazo zinapakana na hifadhi zinasumbuliwa na wanyama tembo. Kwa kupitia kule chini pia kuna sehemu ya Iluma, tembo wanapita wanakuja mpaka Ifakara Mjini katika sehemu inaitwa Katindiuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, askari wetu ni wachache wana vifaa vichache, hawawezi kushughulika katika kata 10. Tembo wanakuwa *Msolwa Station* wametoka Nyerere wanakuja *Msolwa Station,* Mkula, Mang'ula A na Mang'ula B, askari hawatoshi na vifaa havitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu, waweke utaratibu kama wenzetu wa jirani, wameweka *fence* za kisasa. Zamani waliweka *fence* za nguzo za miti, ikaonekana tembo wanasukuma, sasa hivi wanaweka nguzo za zege. Wekeni *fence* kuzuia tembo labda Hifadhi ya Mwalimu Julius Nyerere na Hifadhi hii ya Udzungwa, ndiyo itaponyesha tatizo la tembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia pia maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, tumesaini mikataba ya Kimataifa kuhusu wanyama tembo, lakini wananchi wanaathirika na tembo. Siyo kama kila mkataba wa Kimataifa tumeutii. Tumejenga Bwawa la Mwalimu Nyerere mikataba ya Kimataifa haikukubali, sasa, ni vizuri wakatuambia *square meter* ngapi zinahitaji tembo wangapi; tembo wanasumbua watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amekuja Makamu wa Rais kwenye kampeni Mwaya, mkutano mzima watu wana mabango ya tembo. Makamu wa Rais akatoa maelekezo, katika kero zote nilizoziona hapa ni tembo. Sisi ni *special case*, kwa hiyo watuangalie kwa *operation* maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee wanasema zamani walikuwa askari wa halmashauri, wanapiga tembo mmoja risasi wanahama kwa muda mrefu. Sasa hivi wanasema hatuwezi, basi wawabebe, wawatoe wawabebe na helikopta. Tumeona Kenya wanabeba tembo kwa helikopta, wawatoe, tembo wanapunguza kura za chama chetu, hali ni mbaya. Ninazungumza kwa lugha ya kuwa *calm* hapa kwa sababu nilikuja na *tension* kubwa kweli kweli leo. Ninazungumza kwa busara kweli ili watu wasipate sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia ninashukuru kwa nafasi hii, lakini ninataka nimwambie Mheshimiwa Waziri, askari wake walitumika na Mkuu wa Wilaya ya Kilombero kum-*harass* Mbunge, jambo hili si sawa, hatua zichukuliwe. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa tuna dakika chache za matangazo. La kwanza, ni kuendelea kuwatambua wageni ambao tunao kwenye ukumbi wetu wa Bunge. Hawa ni wageni wa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, Mbunge na Waziri wa Maliasili na Utalii.

Tunao ndugu Musa Kuji, huyu ni Kamishna wa Uhifadhi wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA);* Dkt. Eblate Mjingo, huyu ni Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania *(TAWIRI)*; Dkt. Revocatus Mushumbuzi, huyu ni Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania *(TAFORI)*. Karibuni sana kwenye Ukumbi wetu wa Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nimeambiwa niwakumbushe, niwataarifu tena kwa mara ya mwisho kwa sababu ni siku ya mwisho, kuhusiana na huduma ya hati za kusafiria ambapo huduma hizo zinaendelea kwenye viwanja vyetu vya Bunge na

leo ndiyo siku ya mwisho. Ukumbi ni ule ule wa jengo la Utawala, *Ground Floor* ukumbi namba tisa na huduma itakuwepo mpaka saa kumi jioni.

Waheshimiwa Wabunge tutakaporudi watakaoanza kuchangia ni wafuatao: Mheshimiwa Musa Godfrey Mbuga, atafuatiwa na Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao na Mheshimiwa Yannick Ikayo Ndoinyo. Wengine tutawataja kadri muda unavyokwenda.

Baada ya matangazo haya, ninasitisha kikao hiki mpaka saa 11.00 Jioni.

*(Saa 6.57 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tunaendelea na majadiliano. Nitamwita sasa mchangiaji wa kwanza ambaye ni Mheshimiwa Musa Godfrey Mbuga, atafuatiwa na Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas na Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao ajiandae.

**MHE. MUSA G. MBUGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la

Kisesa. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili ya nafasi hii na wakati huu tena kunipa nafasi hii ya kuchangia kwenye hotuba ya bajeti ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana na kumshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa fedha nyingi na kwa nia ya dhati kabisa kwa ajili ya Jimbo la Kisesa. Niwashukuru na kuwapongeza sana Wizara; Waziri wetu Dkt. Ashatu Kijaji, pamoja na Naibu wake mahiri kabisa Mheshimiwa Hamad Chande. Pia, ninawapongeza Katibu Mkuu wa Wizara hii ndugu yangu Dkt. Hassan Abbas na Naibu Katibu Mkuu Nkoba, hawa ni watu mahiri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu makini sana hata kwenye Kanda ya Bunda pale, yupo kamishna Mkuu, Afande Mlage Kabange pamoja na timu yake akina Masinde tunawapongeza sana wote. Wapo pia Makamishina wa Kanda; Msaidizi Mwandamizi Mark Chuwa pamoja na akina Masinde ninawapongeza wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Meneja wangu wa *Maswa Game Reserve*, ndugu yangu Reuben pamoja na timu yote pale *Maswa Game Reserve*. Wanafanya kazi nzuri, muda wote wanatusikiliza, iwe ni usiku, iwe ni mchana. Kwa hiyo akina Reuben Joseph ninawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na timu yote pale Makao Makuu ya wale maafisa wanaoshughulika na kudhibiti wanyama wakali pamoja na waharibifu, akina Isack, Yohana Chamba pamoja na timu yote. Ninawashukuru pamoja na kuwapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti hii nijielekeze kwenye mambo machache. Nianze na yale mambo ambayo Wizara imefanya vizuri sana Kisesa: yapo mambo ambayo Wizara imefanya vizuri nitayataja kwa uchache. Wizara hii imetujengea vituo viwili vya doria pale Kisesa. Ninawashukuru na ninawapongeza sana, lakini Wizara wamekuwa ni wasikivu, tuliwaomba gari kwa ajili ya doria na ninakiri kwamba

tumeshapokea gari kwa ajili ya Kituo cha Malwilo. Kwa hiyo, ninaishukuru Wizara sana sana

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia imeanzisha utaratibu wa *SWICA* na huu utaratibu umesaidia sana wananchi kunufaika na uwekezaji ambao unafanyika *Maswa Game Reserve*. Ninawashukuru kwa ajili ya miradi mbalimbali ambayo imetekelezwa jimboni kwangu takribani shilingi 973,000,000 nimezipata kupitia Mradi huu wa *SWICA*. Matale peke yake nimepata shilingi 390,000,000 ambapo tumejenga zahanati, nyumba za watumishi, wodi ya wazazi. Nanga peke yake tumepata shilingi 181,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya watumishi; Bulyandulu tumepata shilingi 181,000,000; na Mbugayabanghya tumepata shilingi 216,000,000. Ni lazima kushukuru, kwa hiyo tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nina kila sababu ya kuishukuru na kuipongeza Wizara hii ni nia yake ya dhati ya kujenga uzio wa umeme kwenye hifadhi ya *Maswa Game Reserve*. Zipo kilomita 20 ambazo tayari Serikali imeshaonesha nia, lakini bado ukiangalia kwenye bajeti zinaonekana kuna kilomita nyingine 84. Kwa hiyo kufanya idadi kuwa kilomita 104, kwa nia peke yake ninapongeza sana maana inaonesha ule utayari wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niwaombe Wizara, mwaka jana pia waliweka *commitment* ya kilomita 53 za uzio, lakini utekelezaji wake haukufanyika. Niwaombe mwaka huu tunapokwenda kuwapitishia hii bajeti, hizi kilomita 20 ambazo wamesema wanakwenda kujenga pamoja na zile 84, jumla 104 niwaombe sana waweke mkakati madhubuti wa kuhakikisha wanatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ambayo Wizara haijafanya vizuri. Nitaje kwa uchache na nishauri: la kwanza, yapo malipo ya wafugaji ambao ng'ombe wao walikamatwa kwa kisingizio kwamba wameingia kwenye hifadhi. Wamehangaika kila sehemu mara wanaambiwa Wizara ya Mifugo, mara Wizara ya Katiba, wamezungushwa kwa muda mrefu. Niwaombe Wizara waje na majibu ya kueleweka na ikiwa sitaridhika na majibu hapa

nitashikilia shilingi Mheshimiwa Waziri, nitaondoka na mshahara wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini hata Mheshimiwa Dkt. Bashiru ataniunga mkono. Maana hawa ni wafugaji wake: maana hii ni mifugo yake na hata yeye amelipigia kelele sana akiwa Katibu Mkuu na limepata maelekezo na miongozo ya viongozi wakubwa wengi sana, lakini haijatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwenye kifuta machozi hakiendani na uhalisia, lakini kuna sheria kandamizi. Kwa mfano, unaambiwa ili ulipwe fidia ni lazima uwe zaidi ya mita 500 na hata kama shamba lako limeathiriwa hata kama ni eka 100 wanakuja kukulipa eka tano tu. Hizi ni sheria kandamizi, niwaombe Wizara, waje na mkakati, walete maboresho ya sheria humu Bungeni ili tuweze kufanya marekebisho ya hizi sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano yupo ndugu yangu, Godfrey Mwigulu Nyaligwa kutoka Kijiji cha Mwamashimba, shamba lake la ekari 24 lote limeliwa. Sasa mwananchi kama huyu unapokwenda kumwambia analipwa heka tano atakuelewaje na ameshakuwa maskini. Kwa hiyo, niombe hii sheria ya kifuta machozi na kifuta jasho iletwe tuirekebishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoelekea mwisho…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MUSA G. MBUGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Wizara ya Maliasili na Utalii, iboreshe vitendea kazi na iongeze vitendea kazi, lakini iboreshe pia hata maslahi kwa watumishi wake. Wanafanya kazi ngumu, hasa watumishi wa *TAWA* ni taasisi changa, kwa hiyo waboreshewe maslahi yao ili waweze kujitoa kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Musa.

**MHE. MUSA G. MBUGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Nilimwita Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, atafuatiwa na Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao; Mheshimiwa Yannick Ikayo Ndoinyo na Mheshimiwa Emmanuel John Khambay wajiandae.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Nilikuwa ninaangalia kumbukumbu za watalii ambao wamekuja Tanzania na idadi kubwa ya watalii ilikuwa mwaka 2019 ambapo tulikuwa na watalii milioni 1,527,000 na hata ukiangalia hesabu za chini kuanzia 2017, 2016, na 2018. Hii ya mwaka 2019 ndiyo *peak*, ndiyo tumefikia sehemu ya juu kabisa. Bahati mbaya ikaingia *COVID*. *COVID* ikatufanya watalii wapungue na kufikia karibu 600,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, palihitajika uongozi madhubuti katika kipindi kama kile hasa ukitilia maanani kwamba utalii ni namba mbili kwa uletaji wa mchango wa pato la Taifa kwa asilimia hizo ambazo Mheshimiwa Waziri amezitaja. Palihitaji kiongozi madhubuti sana kuweza kufikiria *turnaround* anafanya nini na katika kipindi hiki ukomavu wa Rais wetu ukajitokeza akafanya kitu kinachoitwa *Royal Tour* ambapo yeye mwenyewe kuanzia Novemba, 2021 hadi Februari, 2022 alishiriki kufanya filamu hii. Nini matokeo yake? Matokeo yake filamu hii ilitazamwa na watu bilioni 1.2 duniani, ni kitu ambacho kina rekodi kubwa sana na tunaweza tukasema haijawahi kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa matokeo haya, hata ukiangalia takwimu yalisababisha kupanda kwa utalii kwa zaidi ya 132% kati ya mwaka 2021 hadi mwaka 2024. Kumetokea juhudi nyingine zimefanyika kwa mfano kama kutengeneza filamu ile ya *Amazing Tanzania* ambayo nayo ilileta msaada mkubwa katika kuhuuisha na kuongeza idadi ya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye Bunge lako hili nilitaka niseme maneno ambayo yupo mtaalamu mmoja alizungumzia aina ya kiuongozi ya mtu kama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, anasema nini yeye? Huyu bwana huyu, alikuwa anamzungumzia Rais wetu, sikiliza, nitatumia lugha ya Kingereza.

Anasema: "*Seeing that Tanzania could market itself global through a presidential documentary when no African Leader had done before. No African Leader has done before* na akaiita *big idea*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote mazuri ambayo tunayaona, leo tumefikisha watalii 5,000,000 na ushee na tukielekea 8,000,000. Sisi tulikuwa tunahitaji *someone with big ideas, that is* Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumpigie makofi Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tuna ushindani, tupo katikati ya ushindani: Kenya majirani zetu, Uganda, Rwanda wanazo mbuga za wanyama, wengine wana fukwe vilevile, Mombasa wana fukwe nzuri sana. Tuna *migration* ya wanyama, *more or less,* Kenya na sisi tunaangalia vitu kama hivyo. Sasa katika kushindana katika hali ya kibiashara lazima tuangalie tuna maliasili gani ambazo hatujazitumia: fukwe za bahari upande wa *Tanzania mainland* (upande wa bara) hatujazitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti ningependa sana na ninajua hawezi Mheshimiwa Waziri kufanya chochote sasa hivi katika bajeti yake hii, aweke kumbukumbu kwamba tunahitaji pafanyike *feasibility study*: ifanyike *feasibility study* ni jinsi gani bora ya fukwe za Tanzania zinaweza kutumika. Pangani kule wametumia kidogo, Mafia kidogo sana, Bagamoyo kidogo sana, hata Dar es Salaam pale kwetu tunaona pale sehemu ya Oysterbay ni mapori tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa tuone, waje na mpango iwe kama Mombasa. Mombasa wameitumia vizuri sana pwani yao. Watanzania hapa watu wa bara hasa *TTB* waende Zanzibar wakajifunze ni vipi Zanzibar wamefanikiwa sana katika utalii wa fukwe. Tunataka tuone hiyo inafanyika huku bara vilevile, maana yake sasa hivi Zanzibar kupo *crowded*, wanafanya kazi nzuri sana. Wizara watusaidie, ninajua kwa kuwa tuna kiongozi mahiri na dada yetu yupo mahiri, watusaidie kutuletea *new ideas*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu gani kingine hatuna wale ambao majirani zetu hawana: hawana Mlima Kilimanjaro. Mlima Kilimanjaro hatuutumii ipasavyo, eti sikilizeni watu wa nje

wanatuambia mkiutumia kwa kuweka *cable car* mnakwenda kuharibu mazingira, ebo! Mbona South Africa ule mlima unaitwa, *Table Mountain* wanatumia *cable car*. Kwa nini Alps wanatumia *cable car*, ukienda Canada wanatumia *cable car*, sisi tu wanatuonea gere. Sasa wanisikilize, tusikubali hata siku moja kuambiwa na watu wengine eti akili za kuambiwa changanya na za kwako: siyo kila siku tunaambiwa sisi tu kwamba oooh! Hapa ni mazingira, mazingira hapana, hebu sasa tuje na wazo hili la kuifanya Kilimanjaro ipate *cable car*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua watu wa *tours* wanalalamika wanasema, biashara itachukuliwa, itapungua, wanaopandisha wale wapagazi watapunguza, hawatapata ajira. Hebu tufanye hivi na sisi tuna akili, Mungu ametujalia Watanzania tuna akili, kwani lazima *cable car* ifike mpaka kilimani? Inaweza ikafika pale mita 3,000 huko kwingine wanaotaka kutembea watembee, lakini hebu niambie tajiri gani ambaye ana muda wa siku chache, atumie siku nane kupanda na kushuka: tunakosa watu wengi kufanya biashara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hivi watu wanajipanga foleni kupanda *Eiffel Tower* pale Ufaransa. Wanatumia dola karibu 50 au *euro* 50, kwa nini sisi tusiwe na utaratibu wa kuitisha watu wakatutengenezea *cable car* ili matajiri wengi na sisi wengine ambao tungependa kufika karibu na kufanya ule utalii kidogo Kilimanjaro tuweze kuusikia. Ningependa kumsikiliza kwa sababu kuna wakati mwaka 2019, Naibu Waziri wa Maliasili, Mheshimiwa Kanyasu aliwahi kulizungumza suala hili Bungeni, lakini limekufakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *LATRA* wametengeneza mpaka kanuni za *cable car*. Kwa nini sasa hivi tusilifikirie wazo lile kama wazo jipya na tuchukue maneno yale aliyosifiwa Rais wetu, "*big ideas*": hebu tufanye hayo mambo, yanawezekana kabisa. Mheshimiwa Waziri, wakati akimalizia hotuba yake, atuambie mtazamo wake juu ya *cable car* huko baadaye siyo lazima kesho...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** … huko baadaye Mheshimiwa Waziri, atuambie Tanzania tungependa iwe *modernized,* siyo mambo yale ya kizamani kila siku. Kuna maarifa mengine yameshachoka, waje na maarifa mapya, *cable car* ni maarifa mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tarimba Abbas, kwa mchango wako. Ninamwita sasa Mheshimiwa Yannick Ikayo Ndoinyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel John Khambay na Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela ajiandae.

**MHE. YANNICK I. NDOINYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi ili niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Nikiri kabisa kwamba, hii sekta ya uhifadhi na utalii pamoja na ufugaji zote mbili ni za kwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli niwapongeze kwanza watumishi wale wa Wizara, Waziri Mheshimiwa Dkt. Ashatu; Naibu Waziri, Mheshimiwa Chande; Katibu Mkuu, Ndugu Abbas; na Naibu wake, Ndugu Mkuba kwa kazi nzuri wanazofanya pamoja na zile taasisi zote ambazo zipo chini ya Wizara hii. Hii Wizara ni ngumu, lakini wanafanya kazi nzuri sana kwa sababu wanapita malengo ambayo wanajiwekea, kwa kweli niwashukuru na niwapongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia kwa sababu amekuwa kinara na ameleta mageuzi makubwa sana kwenye sekta hii ya uhifadhi na utalii. Kwa vile mimi ninatokea Wilaya ya Ngorongoro ninaomba pia niseme kwamba sababu nyingine ambayo kwa kweli inanifanya ninamshukuru Mama Samia ni kwa sababu ametuletea utulivu mkubwa sana ndani ya wilaya yetu. Huko nyuma tulikuwa na migongano mingi, lakini ninashukuru sana utulivu aliouleta na sasa tunaongea vizuri: Mheshimiwa Waziri Mkuu naye ametupokea vizuri, Mheshimiwa Waziri ni watu wasikivu sana kwa kweli tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Wizara ni nyeti sana na nianze kwa kuipongeza tena kwa kuweza kuhifadhi karibu nusu ya nchi. 32.5% kufanya uhifadhi siyo kazi ndogo ni kazi kubwa sana, lakini uhifadhi siyo tu kwamba tumepewa na Mungu kufanya huo uhifadhi, lakini pia uhifadhi ni biashara. Niungane na wenzangu waliosema ni muhimu sasa tu-*translate* kwa vitendo uhifadhi tunaoufanya kuboresha maisha yetu kama Watanzania. Utalii hatuufanyi kulingana na uhifadhi tuliofanya na kwa bahati nzuri Chama Cha Mapinduzi kwa ilani yake imetoa malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kushauri, utalii tunafanya unakuwa mgumu sana kunufaisha wananchi wa kawaida kwa sababu, mara nyingi sana unafanywa ndani ya maeneo yaliyohifadhiwa. Hoteli nyingi za kitalii zenye hadhi ya nyota tatu mpaka tano, nyingi sana zipo ndani ya maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Wizara, waanze sasa kutengeneza mikakati na sera ya kurudisha miundombinu ya utalii vijijini kwa wananchi, ili waweze kunufaika moja kwa moja na utalii. Watalii waje walale *guest* zetu, wanywe chai zetu, wale maandazi yetu kwa sababu, hapo ndipo mtu wa kawaida anaweza kuona manufaa ya utalii moja kwa moja na utaingia kwenye uchumi wa nchi na kaya na lile daraja la kati linaweza kunufaika na utalii. Kwa hiyo, ninataka niwaombe, wasichukulie idadi ya watalii 8,000,000 kama ni lengo kubwa, hilo ni lengo dogo sana kulifikia kwa sababu, uwezo na nia yao, kama Wizara, ninajua watafikia haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile muda unakwenda, ninaomba nigusie suala la wanyama wakali na waharibifu na niongeze pia na mahusiano yaliyopo kati ya wahifadhi na wananchi. Ninataka kushauri kwa sababu, leo ndiyo tunaanza kuchangia hii bajeti kwa mara ya kwanza, Wizara hii itoke iende vijijini ikazungumze na wananchi, wakajue ni changamoto gani zipo kati yao na wananchi, ili kuleta urafiki wa karibu sana kati yao na wananchi, kwa sababu, ni muhimu wananchi wathamini kazi hizi ambazo wanazifanya. Ni muhimu sana pia, wizara hii isikilize na kuchukua maoni ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wasione kama wanyama wakali ni adui na hata wahifadhi nao wasione shughuli za kibinadamu kama ni adui wa uhifadhi kwa sababu, siyo mara chache tumeona wanyamapori wanafuata wanavijiji na ng'ombe wao vijijini na hakuna bugudha, lakini ng'ombe wakiwafuata wanyamapori kule hifadhini mara moja inakuwa kama dhambi! Ni kitu ambacho hatukielewi kisayansi na pia, hatukielewi kijamii. Kwa hiyo, ni vizuri hili suala la kutengeneza mahusiano mema kati ya uhifadhi na wananchi likafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo tumesema huko nyuma, wanyama wakali hawa, hasa tembo, ni vizuri pia, tufanye utafiti ni nini wanafuata vijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana ukiona kitu wanachofuata vijijini ni mahindi au chakula chochote kinacholimwa na binadamu, sasa tuwashauri hifadhi waanze kulima mahindi huko hifadhini, ili kuwazuia tembo wasije vijijini. Watatuambia haikubaliki kwa sababu ni hifadhi, lakini sisi tunachotaka ni kutafuta urafiki wa wanyamapori na wananchi na ikiwezekana kuwamilikisha kabisa wananchi wanyamapori wanaokuja vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, tunajua nyumbu wanapovuka Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kwenda Kenya wanakuwa mali ya Wakenya, wanapokuja Serengeti wanakuwa mali yetu Watanzania. Ni kwa nini inakuwa ngumu kuwa mali ya wanakijiji wanapokwenda maeneo yao vijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Ninamwita sasa, Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela. Kabla ya Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela ni Mheshimiwa Emmanuel John Khambay, atafuatia Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela. Mheshimiwa Isack Joseph Copriano, ajiandae.

**MHE. EMMANUEL J. KHAMBAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi niungane na wachangiaji wengine katika kuchangia Wizara yetu hii ya Maliasili. Awali ya yote

namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuweza kusimama hapa kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Babati Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia nafasi hii kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji; Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Omary Chande; Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu yangu Dkt. Hassan Abbasi; na Naibu Katibu Mkuu, Ndugu yangu Nkoba, kwa jitihada za dhati na taasisi nyingine zote zilizopo chini ya Wizara kwa jitihada ambazo wameendelea kuzionesha katika kuhakikisha Wizara hii inaendelea kusonga mbele. Kutokana na muda nitajikita katika maeneo machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninatumia nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jitihada zake za dhati kabisa katika kuitangaza nchi yetu Kitaifa na Kimataifa katika suala zima la utalii kwa kupitia *Royal Tour,* ambayo imeleta matokeo chanya. Sisi sote, hususani watu tuliotoka Kanda ya Kaskazini, tumeendelea kujionea hayo kwa ustawi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijikite moja kwa moja katika eneo la uhifadhi wa misitu nchini, hususani *TFS*. Ninatumia nafasi hii kumpongeza Mkurugenzi Dkt. Daniel, ambaye ni Mkurugenzi wa Misitu na Nyuki; Kamishna Mhifadhi Mkuu wa Misitu, Ndugu yangu Prof. Dos Santos Silayo; kwa jitihada ambazo wameendelea kuzifanya katika kuhakikisha tasnia hii ya misitu nchini, hususan misitu na nyuki, kuendelea kukua kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameendelea kuwa na utaratibu mzuri wa uoteshaji miti katika mashamba yetu ya Serikali na kuwa na utaratibu mzuri katika suala zima la uvunaji, ambapo ninachukulia tasnia hii kama ni dhahabu ya kijani. Ninasema ni dhahabu ya kijani kwa sababu, tunapanda miti na tunakata miti, kwa hiyo, ni dhahiri ninachukulia kama ni dhahabu ya kijani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona mpango mzuri wa Wizara, kupitia *TFS,* ifikapo mwaka 2031 kwamba, tutakwenda kwenye *engineering wood product* kwamba, tunakwenda kwenye mitambo ya uhandisi wa mbao. Hiyo itatusaidia kukuza uchumi

wa nchi yetu na kuendelea kuongeza ajira nchini, lakini ili tuweze kufikia humo ni lazima tuangalie mnyororo wa thamani katika tasnia yetu hii ya misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongezeka kwa tozo nyingi kwenye misitu hakuwezi kuchangia kukuza tasnia hii, tunaendelea kuidumaza kwa sababu, tasnia hii inahitaji ushirikiano wa kina, ili kuwawezesha wajasiriamali na makundi mengine, ambayo yapo humo ili yaweze kuchangia pato la Taifa na pia, yaweze kutoa ajira. Tunapozungumzia *engineering wood product* ni tunakwenda kuzalisha, badala ya kuuza magogo yetu kama malighafi, basi tuweze kuuza ile *finished product;* tuweze kutengeneza *MDF*, tuweze kutengeneza *plywood*, tuweze kutengeneza *marine boards,* tuweze kutengeneza *particle boards* na zile *waste* zote ambazo zinatokana na malighafi ya misitu tuweze kuziongezea thamani kwa kuzalisha hata mkaa mbadala, ili kuendelea kutunza mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kufika huku ni lazima Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Uwekezaji, pamoja na Wizara ya Fedha ziweze kuisaidia *TFS,* ili kuondoa *exemption* katika *importation* ya mitambo, ili tuweze kukuza tasnia hii iweze kuwa na mchango mkubwa katika pato la Taifa, kuliko sasa ambapo inachangia *GDP 3.5*. Kwa kweli, hairidhishi kwa sababu, ukifananisha nchi ya kwetu na Nchi kama Vietnam; Nchi ya Vietnam misitu yake ni michache, lakini Nchi ya Tanzania tumejaliwa kuwa na misitu mingi, hivyo basi tukiwekeza vizuri tu-*deal* moja kwa moja na *finished products* zitaweza kukuza uchumi na kuongeza mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia ninagusia suala zima la upandaji wa miti. Kuna jamii ya miti, ambayo inaitwa *sandalwood* au *lim*, ni miti ambayo inatumika kuzalisha *perfume* na vipodozi, miti hii tuiangalie. Tume-*prohibit* kwamba, hatuivuni, lakini turudi nyuma kwenye sera zetu tuangalie nchi nyingine zinalima miti hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa *TAFORI* washirikiane na *TFS* kuanzisha upandaji wa miti hii, ili iweze kuchangia pato la Taifa kwa sababu, ni miti ambayo ina gharama, ina thamani kubwa na

inakubali katika maeneo mengi ya nchi hii, hususan kama Dodoma hapa, miti hii inakubali katika maeneo ya Chemba. Kule kwangu Babati inakubali, maeneo ya Singida inakubali na maeneo mengi nchini inakubali kwa sababu ya asili ya udongo huu. Ni wakati sasa wa kuona namna ya kuachia miti hiyo itumike, lakini tuweke utaratibu tusi-*export* kama malighafi, tu-*export finished product,* ambayo inatokana na viwanda vidogo vitakavyowekezwa nchini, ambavyo vitachochea ukuaji wa ajira kwa watu wetu, lakini itachochea pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kumalizia ninamwomba dada yangu, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, kwa kupitia Wakala wetu wa Huduma za Misitu Tanzania aweze kusimamia hilo, ili tuweze kukuza uchumi kuliko kuendelea kui-*prohibit* wakati tuna uwezo wa kuitumia ika-*generate* fedha nyingi na ajira kwa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Ninamwita sasa Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mheshimiwa Isack Joseph Copriano atafuatia. Mheshimiwa Kangi Lugola ajiandae, Mheshimiwa Hawa Mwaifunga ajiandae.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninakushukuru kwa nafasi. Ninaomba pia, niishukuru familia yangu kwa uvumilivu wa muda mrefu nikiwa hapa na wenyewe wako huko mbali na mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaanza kwa kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono bora kabisa katika taasisi au sekta hii ya utalii. Ni kweli, tumepiga hatua kubwa sana, ni jambo ambalo halipingiki tumefanya kazi kubwa kufika tulipofika ukilinganisha na tulikotoka. Miaka ya nyuma ya 2018 tulikuwa na pato la utalii, takriban Dola za Kimarekani bilioni 2.43, lakini kwa miaka hii ya karibuni, kwa maana ya mpaka kufikia mwaka 2026, tayari tumepata kiasi cha dola takriban bilioni 4.2. Kiasi hiki siyo kidogo, hususan, katika masuala haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ni mengi ambayo hata katika hotuba tumesikia kwa kadri Mheshimiwa Dkt. Kijaji alivyojaribu kuyaelezea. Ni kwamba, tumepata mafanikio, tuzo nyingi sana tumepata zinazoonesha kwamba, tuna-*improve* kutoka tulipokuwa. lakini kuzungumzia tu utalii pasipo kuangalia mawanda yake, bado tutaishia kujisifia na kuona kwamba, tumefanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumefanya vizuri, hilo halipingiki, lakini inabidi tuangalie mawanda mapana ya utalii. Tumefanya vizuri sisi wenyewe tukipima hatua zetu kutoka pale tulipo, lakini kwa uhalisia wa *resources* tulizonazo sisi, bado hatujafanya vizuri. Tunahitaji kufanya kazi kubwa sana angalau tufike tunapostahili kuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli hii imeleta kazi fulani yenye muonekano mzuri, lakini ukiangalia, kama nilivyosema, sekta nzima ya utalii duniani kwenye biashara yake inaleta mchango wa fedha takriban shilingi 11,000,000,000,000, lakini pia, ukienda katika biashara yenyewe ile ya utalii, kwa maana ya kitu ambacho watu wanaweza wakapata, kuna pesa takriban shilingi trilioni 1.9 ambazo zenyewe tunaweza kusema ni *market share* ya biashara ya utalii. Kwenye hili, kama unavyoona kutoka kwenye shilingi trilioni 1.9 na sisi kuambulia shilingi bilioni 4.2, hakika tuna kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashangaa baadhi yetu kusema kwa nini tunataka kujilinganisha na watu ambao wamefanikiwa kupata pesa nyingi! Kwa mfano, Marekani wenyewe wamekuwa na uwezo wa kupata takriban dola 100,000,000,000, Ufaransa dola takriban 90,000,000,000 na wengineo, lakini hata Morocco pia, dola takriban 11,000,000,000. Sasa sisi kwa nini tujilinganishe nao? Baadhi ya watu wanafikiri wanaweza wakauliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu ni rahisi tu kwamba, sisi tuna vivutio bora kabisa duniani ikiwezekana kuliko nchi hizo zote ambazo nimezitaja hapa. Kama siyo kuwa ni mtu wa kwanza au nchi ya kwanza duniani kwa vivutio vilivyokuwa bora, hususani vile vya asili. Sasa, lakini kwa nini mpaka sasa hivi tuko hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu, bado hatujawekeza vya kutosha katika eneo hili la utalii. Bado hatujaweka pesa nyingi kutangaza utalii, bado hatujaweka pesa nyingi kutengeneza miundombinu na halikadhalika. Hata suala la elimu ya utalii, bado hatujawekeza pesa za kutosha kiasi cha kuweza kushawishi watu waweze kutupa pesa ambazo sisi tunatamani kuzipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajaribu pia, kuzungumzia hili jambo la utangazaji wa utalii. Jambo hili kwa mujibu wa sheria limekabidhiwa kwa *TTB*, kwa maana ya Bodi ya Utalii, lakini kutokana na ushawishi wa asili wa biashara hii eneo la matangazo ni ambalo linatoa kazi sana, linatumia pesa nyingi, kwa matumizi ya utalii. Hivyo, pameleta kivutio kwa baadhi ya watendaji wengi na taasisi nyingi kujishughulisha na shughuli hii ya utalii, kwa maana ya kutangaza kiasi cha kwamba, kupora Mamlaka ya *TTB* na sasa taasisi nyingi zimekuwa zikiamua kufanya utangazaji wenyewe na hivyo kuzorotesha *TTB* na kukosa nguvu ya kuonekana kwamba, ina uwezo wa kufanya chochote.

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha, Mheshimiwa Mchungahela.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ninamwita Isack Joseph Copriano, Mheshimiwa Kangi Lugola atafuatia; Mheshimiwa Hawa Mwaifunga na Mheshimiwa Yahya Mhata, wajiandae.

**MHE. ISACK J. COPRIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Wizara yetu hii nyeti ya Maliasili. Kwanza ninasema, ninaunga mkono hoja, ili kama huko mwisho nitakuwa nimesahau, niwe tayari nimeshaunga tangu mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninachukua nafasi hii kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Kuna watu wanaweza wakafikiri tunapongeza tu kwa sababu, tunapongeza; la hasha,

tunapongeza kwa sababu, Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa na ya kutukuka, ambayo vizazi vyote vitakuja kujifunza na kuona kazi iliyofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya *Royal Tour*. Hakuna mtu atakayekuwa na ubishi kwenye hilo, itaingia kwenye historia. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais na Mungu ampe maisha marefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri naye kwa kuendelea kupambana kwa sababu, unapotengenezewa chakula ukishindwa kula, utakuwa wewe ndio mzembe. Sasa ninamwona Mheshimiwa Waziri na timu yake wanapambana kuhakikisha kwamba, yale matunda mazuri ambayo Mheshimiwa Rais ameyatengeneza wanaendelea kuyasimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninaendelea kumpongeza Katibu Mkuu, Ndugu Abbas, amekuwa ni mtu ambaye ni msikivu. Unapompigia, kama Mbunge, ukimwambia matatizo ya kwenye jimbo, anasikiliza. Ninamwomba aendelee na moyo huo huo na ninadhani wakienda hivi na Mheshimiwa Waziri, basi maswali yatakuwa machache sana siku za usoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja ambalo ninapenda kulijua na ninatamani sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kwenye hotuba yake, atuambie. Katika Sheria ambayo ninaiona kama kandamizi, ni hii ya faini ya mifugo wanapoingia kwenye hifadhi zetu, ya shilingi 100,000 kwa kichwa cha ng'ombe. Jamani, 100,000! Mimi kuna wananchi wangu wa Monduli wanaotoka Kata ya Esilalei, Makuyuni na Mswakini majuzi walikamatwa kwenye eneo la Tarangire wakalipa zaidi ya shilingi 38,000,000! Sasa hayo si tunawafilisi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa, faini imewekwa, kwa ajili ya kuzuia kusiwe na uharibifu, lakini huyu ng'ombe bahati mbaya ameingia pale, hajavunja mti, amekula majani, amefanya nini, unam-*charge* kichwa cha ng'ombe. Ninaomba kabisa, sheria sijui ilitungwa mwaka gani, lakini ni sheria ambayo ni kandamizi na inaumiza Watanzania, hususani wananchi wangu wa Monduli, pale walipokuwa wamekamatwa. Kweli, jambo hilo ninakumbuka

nilihangaika nalo nikashindwa, lakini ni sheria ambayo kwa kweli, tunaomba iangaliwe upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kwamba ukisema kwamba sheria ikiwa ngumu ndiyo watu hawataendelea labda kuingiza au kujisahau na kwenda kwenye hifadhi, la hasha! Kama ingekuwa hivyo basi wananchi wangekuwa wanauza ng'ombe wote kipindi unapotokea ukame kwa sababu ng'ombe wengi wanakufa, hivyo Serikali ikiendelea kuweka sheria hii haiwatendei haki wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kabisa sheria hii iangaliwe kwa sababu ni sheria ambayo inawaumiza Watanzania. Ardhi hii ni yetu, hifadhi ni zetu na hao ng'ombe. Kwa nini wasimkamate hata huyo mtu wakati yeye ameingiza ng'ombe wakabaki naye hawa ng'ombe wakatoka? Wanawafungia mpaka wengine wanakufa huko na bado wanawa-*charge* hata wale waliokufa. Hivyo, nilisema nilitangulize hili suala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, pamoja na kazi kubwa iliyofanywa na Mheshimiwa Rais kwenye sekta hii ya utalii, kuna *issue* ya barabara kule Ngorongoro. Wapeleke fedha, Wizara ipeleke fedha ili barabara itengenezwe. Tunaona jinsi watu wanavyokwama kule Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaangalia ile sehemu ambayo magari yanakwama, ni maeneo ambayo wakijenga *vent drift* ndefu za mita 10, 15 wakaweka *vent drift* zitawasaidia watalii ili waendelee kufurahia matunda ya mbuga zetu. Wapeleke fedha za miradi zikatengeneze barabara hizo ili watalii waendelee kufurahia matunda haya mazuri ambayo Mheshimiwa Rais wetu ametengeneza kwenye *Royal Tour.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ni wanyamapori. Ndugu zangu wanyamapori wanatusumbua kwenye maeneo ya Makuyuni, Mswakini, Sepeko, Lepurko, Nalarami, Moita na Lepromoti. Wanyama wamekuwa wakitoka kwenye maeneo ya Serengeti hususan tembo kuja kuvamia maeneo yetu. Wote wanajua kuwa Makuyuni huko nyuma

hakukuwa na hifadhi, lakini hifadhi imekuja sasa. Sasa ile hifadhi imeingia karibu na wananchi, halafu wakisema zile mita wanazosema, sasa na hawa ambao hifadhi imewakuta wanawahesabu vipi? Tuangalie vizuri maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mahali kweli hifadhi ilikuwepo, na je, Makuyuni hifadhi ni mpya! Ukienda pale Naiti na Mbuyuni wale wanyama ni mita 300 wameingia kwenye mashamba ya watu na hiyo hifadhi imewakuta. Kwa hiyo, ninatamani sana sheria hiyo iangalie na upande huo tuone tunakwendaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fidia; nilizungumza hapa juzi ninaomba nisirudie, ninaamini Mheshimiwa Waziri ni msikivu na namkubali sana na anajua namkubali, hata leo nimevaa kama na mimi ni mhifadhi ili nimuunge mkono kwenye Wizara yake. Anaona leo nimevaa kaunda suti inayofanana na watumishi wake ninamuunga, lakini ninatamani warudi waangalie hifadhi hizi je, zina faida? Fidia hii ni sawa wamesema wakilipa fidia hailingani na utu wa binadamu, lakini basi lipa tu angalau hata kama hailingani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema nilizungumze hilo ili angalau, *TAWA* nawaomba wafanye doria kwenye maeneo ya Makuyuni, Mswakini ili kuwasaidia wananchi wetu wale wasiendelee kuuawa na wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarudia kusema ninaunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana kwa mchango wako. Nimwite sasa Mheshimiwa Kangi Lugola, atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga.

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Kwa sababu ninachangia dakika saba nitakuwa *very brief*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ninampongeza Mheshimiwa Waziri na Serikali ya Mama Samia kwamba wanafanya kazi vizuri, lakini nimtahadharishe jambo moja, kuna kitu kinaitwa

kubweteka. Unajua kati ya Wizara au sekta ambayo ina bahati ni hii ya Maliasili na Utalii, kwa sababu uwekezaji mkubwa tayari Mungu alishawekeza. Alishawaweka wanyama, alishaweka kila kitu, fukwe, maziwa, milima, misitu. Kwa hiyo, uwekezaji mkubwa umeshafanyiwa kazi na Mwenyezi Mungu, kwa hiyo wanaweza wakabweteka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nishauri tu kwamba, sekta ya utalii inachangia takriban 17% kwenye *GDP* lakini kwenye fedha za kigeni sekta ya utalii, inachangia zaidi ya 24%. Sasa kama haya ninayoenda kuyashauri hawatayafanyia kazi, tunaweza tukarudi nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuwekeza kwenye matangazo. Pili, ni kuwekeza kwenye huduma zilizo bora za utalii. Nianze na matangazo. Wenzetu wa *South Africa* wamenufaika sana, wamepiga hatua kwa sababu wameweka takriban dola 100,000,000 kuwekeza kwenye matangazo peke yake. Rwanda na Kenya kadhalika. Matangazo ambayo mimi ninataka nianze kushauri ni kwanza kwenye hizi *football clubs* ambazo ziko kwenye ligi ya Uingereza, ligi ya Ufaransa, ligi ya Ujerumani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa *South Africa* wamefikia hatua ya kuingia *partnership* na *Tottenham Hotspur,* kwa hiyo unakuta zile jezi wanazivaa zikionyesha utalii wa Nchi ya *South Africa*. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, ajitanue ahakikishe kwamba na sisi utalii wetu wanatumia timu za mpira katika kutangaza utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni hili la *influencers* limeongelewa sana. Tunamshukuru Mheshimiwa Samia ni mwanzilishi wa *influencers* alipoandaa *Royal Tour.* Imesaidia sana, tumeongeza namba ya watalii katika nchi yetu. Sasa, kama Mkuu wa nchi ameweza kuingia kwenye filamu ya *Royal Tour,* sasa Wizara inasubiri nini kupata *influencers* ambao ni maarufu pia ili waweze kuendeleza matangazo haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwatahadharishe kwenye baadhi ya *influencers*, wapo wengine ambao wana *followers fake* kwenye mitandao, kwa hiyo, lazima wafanye *due diligence* ya

kutosha. *Influencers* wengine hawana mvuto, wanaweza wakawapata pia lakini wasilete matokeo mazuri. Kwa hiyo, ninawatahadharisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wajaribu pia kuingia *partnerships*. Ninajua pengine wanaingia lakini hawajaingia kwa nguvu, kuhakikisha kwamba wanaingia *partnerships* kwenye mashirika makubwa ya ndege, wanaingia *partnerships* kwenye *tour operators* pamoja na *hotel operators* hasa wale wakubwa ili kuweza kutangaza vizuri utalii wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kuwekeza hapo hapo ni kwenye suala la kuhamasisha utalii wa ndani kwa bei nafuu. Kwa sababu inawezekana wale watalii ambao tumepewa *figures* hapa 8,000,000 utalii wa ndani unaweza ukawa ni mdogo sana kuliko wale wanaotoka nje. Kwa hiyo, wekezeni kabisa ili Watanzania wenyewe ndiyo tuwe watalii namba moja badala ya kusubiri wa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhakikisha kwamba wanatoa elimu na mafunzo ya kutosha ya hali ya juu kwa wafanyakazi wao. Sekta ya utalii inahitaji teknolojia na maarifa ya kisasa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende katika jambo la mwisho maana naona nimepigiwa kengele, nalo ni kuhusu wanyama wakali. Mheshimiwa Kijaji, hawa wanyama wakali, juzi nimeuliza swali Bungeni, wamenijibu watajenga vizimba, sawa vizimba vingine vipo vimejengwa lakini wanyama wakali hawa ambao wako Ziwa Victoria wamekuwa ni wengi sana, tunachoomba na sijui kwa nini wanasita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona waliweza kuhamisha wanyama kutoka Serengeti wakapeleka Burigi-Chato? Mbona waliweza kuhamisha wanyama kutoka Mikumi wakapeleka Burigi-Chato? Waliwatoa wengine Ngorongoro wakapeleka Burigi-Chato, wanashindwa nini kutuhamishia wanyama hawa wakali ambao wanatumaliza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona kuwahamisha ni rahisi maana hatusemi kwamba wawaue! Wanakuja wanawavuna, wanakusanya na mayai, wanakusanya na vifaranga visivyozidi sentimita 50, wanaviondoa pale sisi hatuwahitaji hawa mamba pale, wawapeleke kwenye maeneo ya uhitaji. Sasa anashindwa nini Mheshimiwa Waziri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashindwa kusema nimshikie shilingi kwa sababu ninajua yeye ni msikivu, waondoe wanyama hawa, hatuwahitaji Mwibara, hatuwahitaji ni maadui zetu, wawaondoe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende la mwisho, uwanja wa ndege wa Serengeti, Wizara imejiandaaje? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kangi ahsante sana kwa mchango wako na Serengeti imezungumziwa sana.

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, Mheshimiwa Yahya Mhata ajiandae, Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao ajiandae.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na uzima. Nimesimama hapa jioni ya leo kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wangu, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya kwenye hii Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kweli ni mfano wa kuigwa. Ametufanya wengi tuendelee kuupenda utalii wetu pamoja na maliasili tulizonazo, kuhakikisha kwenye maeneo yetu tunafanya kazi kweli kweli, kuhakikisha yale

ambayo ni maono yake tunaweza na sisi kuyafanya kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ninapenda nitoe pongezi kubwa pia kwa Wizara. Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, kaka yangu Dkt. Abbas kwa kazi kubwa wanayoifanya, lakini nimwambie tu Mheshimiwa Naibu Waziri ninamshukuru sana kwa kazi ambayo ameifanya kwenye maeneo yangu, kuni-*please* kwa ajili ya watu wangu ambao walipata changamoto ya viboko pamoja na mamba kama alivyosema kaka yangu Kangi Lugola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hata sisi hatuwahitaji kwa sababu kale kabwawa ka Igombe tulikonako ni kadogo, lakini wale majamaa wapo pale wanaumiza na kuua wananchi wangu. Kwa kweli hata mimi nitaungana na Mheshimiwa Kangi ili tuweze kuona tunafanyaje. Mheshimiwa Chande, ile kazi tuliyosema tutaifanya, tuifanye ili tuweze kuwasaidia wananchi wangu wa Jimbo la Tabora Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa kwangu mimi niwapongeze sana watu wa *TAWA*. *TAWA* imekuwa ikifanya kazi kubwa katika Jimbo la Tabora Mjini, kwa sababu wametuwekea pale bustani nzuri sana na hili nimekuwa nikilisema mara kwa mara, pale tunayo bustani nzuri sana ambayo ni Tabora *Zoo*, tumekuwa tukiitangaza kwa kweli kwa hali na mali kuhakikisha kwamba, bustani hii watu wengi wakifika Tabora wanafika kuitembelea na kuiona bustani hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipoanza na sasa tulipofikia kwa kweli watu wameanza kuizoea na wameanza kuiona na sasa tunaongeza mapato. Ninawashukuru pia *TAWA* kwa kuwa wasikivu wamesikia kilio chetu ya kwamba tunahitaji tujengewe uzio kwenye ile bustani nzuri. Ilivyo sasa hivi ni hatari kwa maisha ya binadamu kwa sababu iko maeneo ya mjini inaweza kuleta madhara. *TAWA* tuendelee kufanya kazi, mimi Mbunge wao wa Tabora niko pamoja na wao kuwa-*support* na kuweza kufanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na *TAWA*, lakini niseme watu wa Mkoa wa Tabora, kwanza ndiyo mkoa mkubwa, lakini pili ndiyo tumezungukwa na mapori mengi nadhani kuliko mkoa mwingine wowote. Kwa hiyo, sisi ni walinzi wazuri sana wa rasilimali hii ya misitu katika Mkoa wa Tabora na hususan kwenye Jimbo la Tabora Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa ninaomba nizungumze leo na Waziri na hili jambo ninaomba Mheshimiwa Waziri anisikilize, *I'm very serious* kwa kweli kwenye jambo hili, inapofika wakati unamwona askari anakwenda nyumbani kwa mwananchi eti amesikia mwananchi huyu amebeba gunia la mkaa, wanampiga mwananchi huyu mbele ya watoto na mke wake, kwa kweli Mheshimiwa Waziri jambo hili halipendezi hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya askari wasiokuwa waadilifu, hawafanyi kazi kisheria, wanachofanya kazi wanatumia nguvu zaidi kuliko akili. Mama amesema kazi na utu, hajasema kazi na unyanyasaji. Hii Wizara haipaswi, kunyanyasa wananchi eti kwa sababu amebeba gunia moja la mkaa, amevuna gunia moja la mkaa, tena wanamfuata mpaka nyumbani kwake wanakwenda kumfanyia vitendo vya ajabu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefika mahali mwananchi huyu ananyweshwa asali. Jamani, asali inalambwa polepole, asali inaliwa taratibu, asali hainywewi. Ukimnywesha mtu asali, wewe huyu unataka kumuua? Mheshimiwa Dkt. Ashatu, hali ndivyo ilivyo kwangu Tabora. Waziri akimaliza bajeti yake tujipange ndugu yangu twende Tabora na anipe *lift* kwa sababu nitakuwa sina mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo naomba nichangie hoja hii na nikubaliane na Kamati. Nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati hii ya Maliasili. Nilizungumza mwaka 2023, 2024 na 2025 kuhusiana na suala zima la hii *AFCON*. Tuliijua muda mrefu, lakini nikisema nimepitia bajeti ya Wizara hii, yaani unaona kabisa kama vile kale kakipengele wamefanya kukachomeka tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *AFCON* ni suala kubwa katika nchi hii, lakini mpaka leo ninavyokwambia mimi binafsi ukweni kwangu ni Arusha, nenda Arusha pale muulize mtu wa Arusha unajua *AFCON* ni nini na ina faida gani kwa wananchi wa Arusha na Tanzania kwa ujumla na fursa zipi zipo? Hakuna watu wanaojua. Sasa hii *AFCON* inakuja Tanzania kufanya nini kama hata wale ambao wanapelekewa hiyo *AFCON* hapo nyumbani kwao hawajui chochote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiambie Wizara na hili ninalirudia hii siyo mara moja, niliwaambia hata mwanzo, Wizara ya Maliasili hili siyo jambo la Wizara ya Michezo peke yake! Ni lazima sasa wajitokeze kwa sababu tuna vivutio vya kutosha, tena Arusha imekithiri kwa vivutio vya kutosha, wamejiandaaje? Wamejipangaje? Wananchi wa Tanzania wana fursa gani? Hatuoni hata mabango yaani hamna hata amshaamsha pale Arusha kwamba kuna *AFCON*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani *AFCON* ni jambo kubwa na ni lazima liheshimike, ama tunamsubiri Mheshimiwa Rais atoke tena aanze kutangaza *AFCON* ndiyo na sisi wengine tujitokeze? Haiwezekani! Tumpunguzie kazi Mheshimiwa Rais, tutekeleze majukumu yetu, tufanye kazi zetu. Rais aone tulichokifanya kina tija katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hawa. Nilimwita Mheshimiwa Yahya Mhata, Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao ajiandae, atafuatiwa na Mheshimiwa Dickson Nathan Lutevele, ajiandae pia Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninaomba nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ameniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Ninaomba nimshukuru sana Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya katika jamii zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia niwashukuru wahifadhi wetu wa Mkoani Mtwara, Wilaya ya Nanyumbu kule, dada yangu Khadija, ninathamini sana mchango wake na usikivu wake alionao kwa wananchi wangu hasa wanaposhambuliwa na wanyama wakali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijielekeze kwenye changamoto zilizopo ndani ya Jimbo la Nanyumbu. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri anisikilize kwa makini sana. Mheshimiwa Rais alipokuja ndani ya Jimbo letu wakati wa kampeni, alitambua changamoto zilizopo za wanyama waharibifu na wanyama wakali wanaolikabili Jimbo la Nanyumbu. Mheshimiwa Rais alitoa agizo, maelekezo, kwangu mimi maelekezo ya Rais ni maagizo. Ni matarajio yangu kwamba bajeti hii imeyazingatia maelekezo ya Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais alielekeza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, alitambua uwepo wa wanyama waharibifu hasa tembo na aliagiza yafuatayo. Kwamba, katika mwaka huu wa fedha atahakikisha tunapatiwa watumishi wapya ili kuweza kuungana na wale waliopo wachache kukabiliana na wanyama waharibifu. Ninasikia Wizara imeajiri watumishi, ninataka Mheshimiwa Waziri atakapokuja Jumatatu ku-*wind up*, anieleze ni watumishi wangapi amewapeleka Nanyumbu? Kwa sababu tuna hali ngumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais pia aliahidi kutupatia ndege nyuki. Mheshimiwa Waziri, sisi pale tuna mapori mawili, tuna pori la Lukwika Lumesule na tunalo pori la Mfinjasi, mapori yote haya yana wanyama waharibifu hasa tembo. Ninamwambia Waziri kwamba, kila mwezi, pale tunazika watu kwa sababu ya hawa tembo. Ninamwomba sana atuletee ndege nyuki, mara baada ya kupitisha bajeti yake, tunahitaji tupatiwe ndege nyuki zisizopungua tatu ndani ya jimbo letu, jimbo lile ni kubwa na tunayo mapori makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kuna suala la ulipaji fidia. Ni kweli kwamba Bunge hili lilipitisha viwango, lakini viwango vile si msahafu kwamba havibadilishwi, viwango vile vimepitwa na wakati. Leo ninavyozungumza, haiwezekani mtu

ambaye shamba lake la mikorosho limeliwa hekari 10 akalipwa hekari tano, hela zenyewe asipate. Ninao wananchi 600 mpaka leo hawajalipwa fedha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Jumatatu hapa mimi sitakubali. Ninataka maelezo ya kina, kwamba ni lini wananchi hawa watalipwa fedha zao. Haiwezekani mwananchi ameharibikiwa, ameliwa shamba lake, anakaa mwaka mzima hajalipwa fidia. Hili jambo hatulikubali; tunaomba Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi sana jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao wanyama wengine wakali. Ndugu yangu Mheshimiwa Lugola amesema, hata sisi tunao. Ukija jimboni kwangu tuna walemavu wengi wanaosababishwa na hawa wanyama wakali, mamba. Sasa ninawauliza hata hawa nao haturuhusiwi kuwaua? Nenda Mto Ruvuma, wamejaa mamba. Ukienda pale Masuguru kuna walemavu kibao wameliwa mikono, miguu kwa sababu ya mamba hawa. Nenda pale Kata ya Likokona, kuna kabwawa pale kuna mamba sijui wanne, watano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoa taarifa kwa ndugu zangu wa Maliasili wanakuja wanapigapiga bunduki tu ili wakimbie ndani ya maji, lakini baadaye wanakuja kuleta uharibifu. Sasa ninataka maelezo hawa mamba tutakaa nao hadi lini. Waziri alete vizimba ili wananchi hawa waweze kuepukana na wanyama hawa waharibifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu fursa zilizopo ndani ya jimbo. Sisi tumepakana na Msumbiji, vijana wangu wanavuka wanakwenda Msumbiji kutafuta maisha, wanakuja na mbao *TFS* wanawakamata. Sasa hata mbao za Msumbiji wanazikamata kweli jamani? Mbona kwa upande wa madini wamefungua kituo pale na madini yanayochimbwa Msumbiji wanakuja kuuza pale mbona hawaulizwi madini hayo wameyapata wapi? Inakuwaje leo mbao za Msumbiji watu wakamatwe? Hebu vijana hawa waachiwe ili wafanye kazi za kujitafutia riziki. Sasa watafanya kazi gani ikiwa kila kitu wanachokifanya wanasumbuliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili ninaomba sana na hili ni takribani kwa kanda nzima ya kusini. Ninaomba vijana waachiwe ili watumie fursa zilizopo. Watumie fursa ya mpaka ili waweze kujipatia riziki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua muda si rafiki. Baada ya kusema hayo ninategemea haya niliyoyasema Mheshimiwa Waziri atayatekeleza na Jumatatu tutapata majibu sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yahya Mhata. Nimwite Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao atafuatiwa na Mheshimiwa Dickson Nathan Lutevele, Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga ajiandae.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninauchunga muda hapa, maana inakuwa tabu, nyakati nyingine ninaongea dakika mbili tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninawaombea dua sana hawa viongozi wetu ambao ni Mawaziri, Wabunge wenzetu ambao wametishwa zigo hili la Maliasili na Utalii. Jamani hii Wizara ni ya hatari, kwa sababu mimi nimekuwa Bungeni kwa miaka mitano, Waheshimiwa Wabunge wenzangu; wameshabadilishwa Mawaziri wanne, sasa hivi hawa ni Mawaziri wanaenda kuwa Mawaziri watano na wanakaa mwaka mmoja tu wameondoka, siyo mchezo. Hii Wizara watu wakiingia hapo; hawa ni wakuombewa dua; waombewe dua sana, hawalali. Kabisa, ndicho ninachotaka kuwaambia. Unafikiri ni Wizara ya mchezo? Pamoja na shida tulizonazo tunatakiwa tuwaombee kwa Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba wanyamapori ni tatizo. Hakuna mtu yeyote ambaye anaona kabisa kwamba kwake watu wanashambuliwa akakaa kimya. Bahati nzuri hawa wenzetu walioko hapa, hawa Mawaziri wote wamekuwa ni Manaibu Waziri wa Fedha, wanajua shida ya fedha tuliyonayo katika nchi hii, hasa dola. Tumekuwa na mamba wengi wa kutosha. Sasa imefikia mahali mamba hawa wavunwe. Nyama ya mamba

ndiyo nyama bora duniani, inatafutwa. Tani moja ya nyama ya mamba ni dola 1,400; hii nchi isingekosa dola. Kwanza Wachina wanatushangaa wakisikia tunalalamikia sana chakula. Mamba hawa wavunwe; kiwekwe kitengo cha biashara ili nyama ya mamba itangazwe, kwamba iko Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi mamba tunao hapa hatuna mahali pa kuwapeleka. Niambiwe tu, kwamba kuna *game reserve* gani katika nchi hii ambayo tunaenda kuwaweka mamba, kwamba ndiko wanapokaa, ndiko kwao? Sasa hivi mamba wanatembea tu, wanaingia, hata kisima kidogo tu mamba anakwenda kule. Sasa hali ya mamba imekuwa si nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Sengerema, mwenzangu umemsikia, kule Buchosa wananchi 32, mimi wa kwangu walioliwa na mamba ni 17; jumla ya wananchi takribani 50 katika hii miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vijiji 53 vyote vinazungukwa na ziwa. Tumejengewa vizimba saba, Sengerema sijapata kizimba hata kimoja. Sasa tunaomba waone, sisi maeneo yetu watu wanakwenda kuchota maji, wanakwenda kufanyaje; tujengewe vizimba sasa. Kama wao wanaona si rahisi kuwavuna mamba hawa watujengee vizimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na tatizo la fisi. Ninawashukuru sana watu wa *TAWA,* wamejitahidi sana, tunawapigia kwa wepesi wanakuja, lakini kuna watu wanaitwa Wagalu, hawa wako Mbalika, ni wawindaji wazuri sana. Hata kama fisi watakuwa ni wale fisi wa miujiza wale jamaa huwa wanawatoa. Sasa wapewe leseni nao, waache kuwakamata wale watu wanaotusaidia kuwavuna hawa fisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote hawa wanajua, kuna viboko na mamba. Yaani leo mamba anaweza akakamata watu, lakini baada ya siku tatu mamba wale, wakitumwa wale watu wa *TFS,* hawa watu wa *TAWA,* wanawakosa wale mamba, lakini hawa watu wakija wale Wagalu wananchi wanajikusanya, sasa na wenyewe tena

wanakamatwa. Hebu liangaliwe jambo hilo, hawa Wagalu wapewe *certificates* ili wasaidie wananchi kule katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ninataka kulizungumzia hapa ni suala la nguvu kazi. Hawa binadamu tulio nao, ndugu zetu hebu kwanza pia wafundishwe namna ya kuishi na Watanzania. Unafahamu wakishakuwa watu wako kule kwenye *game reserve* akili zao nazo huwa zinakuwa tayari za hatari kweli kweli; kwa sababu na wao huwa si kwamba eti hawaliwi na wale wanyama, wanaliwa ila kwa sababu hawatangazi tu kwamba askari wawili wameliwa na simba. Kwa hiyo na wao tunatakiwa tuwaombee Mungu, wako wachache. Hawana nguvu kazi, hawana magari, hawafiki kwa wakati. Sasa hili ni tatizo kubwa; hivyo liangaliwe sana. *Manpower* kule katika wenzetu hawa wa *TAWA* wasaidiwe, wawape magari na kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hakuna fedha, hizi *TANAPA* ni mamlaka, *TFS* ni mamlaka; kama tunachukua fedha zao; tulikuwa tuna matatizo wakati ule wa *COVID;* zirudishwe ili waweze kujitegemea. Wapunguze na wao wafanye kazi zao kwa sababu yameshakuwa malalamiko hapa. Kila Mheshimiwa Mbunge anayesimama malalamiko ni hayo hayo. Hebu warudishiwe fedha zao watu wa *TAWA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana ndugu yetu Profesa Dos Santos, sisi anatusaidia. Tuna msitu kule Sengerema hekta 21,280, sisi watu wa Buchosa na Sengerema hatupati *CSR* yake. Wazazi wetu wamepanda ule msitu kuanzia mwaka 1969, sisi wenyewe tumepanda ule msitu; na ndugu yangu hapa Mheshimiwa Eric Shigongo tulikuwa tunafanya kazi kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo tuna wanafunzi wanakaa chini. Tuna msitu halafu wanafunzi wanakaa chini? Mwaka jana nimepewa madawati 160, sijui mwenzangu amepewa mangapi. Ninamshukuru hata hayo madawati machache aliyonipa ndugu yangu Dos Santos. Mungu amjalie sana, lakini watuongezee watu wa Sengerema wenye huo msitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungukwa na msitu halafu watoto wanakaa chini kweli? Hii ni aibu. Tunamwomba Mheshimiwa Chande baada ya Bunge hili twende akayaone haya matatizo ya watu wa mchangani na akaone matatizo yetu kule Mesome; tuna matatizo makubwa kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ninataka nilizungumze hapa, la muhimu sana ni suala la ofisi hizi za hawa watu wa *TAWA*. Sisi kitengo chetu kwa Mwanza kiko Bunda. Hawa watu kuja Bunda pamekuwa ni mbali. Watuwekee sisi Sengerema, na Buchosa. Sisi watu wenye matatizo ya viboko na mamba, tufunguliwe hizi ofisi zikae kule. Hawa maafisa tulionao Sengerema pale hawana hata bunduki. Yaani tatizo likipatikana hadi aombe tena kutoka Bunda. Tuwekewe tu ofisi sisi katika Wilaya ya Sengerema ili nasi tuweze kunufaika na uwepo wa watu wa *TAWA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya, ninawaombea sana kwa Mwenyezi Mungu. Sijui na wao kama tena wataendelea kuwepo mpaka mwaka kesho, maana sasa tunaanza nao na wenyewe tena waje wabadilishwe tena. Hawa wamesikia matatizo, wanakuja tena, wengine wanasikia tena matatizo. Tunaomba atuombee kwenye mamlaka wakaekae kidogo ili watumalizie haya matatizo tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Tabasam. Nilimwita Mheshimiwa Dickson Nathan Lutevele, atafuatia Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga na Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe, ajiandae.

**MHE. DICKSON N. LUTEVELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie kwenye Wizara hii muhimu sana ya Maliasili na Utalii. Kwanza ninaomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana na kumshukuru Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea Waziri anayechapa kazi pamoja na sekta zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoka Jimbo la Mafinga Mjini sehemu ambako ardhi kubwa ya msitu wa *Sao Hill* ndiko uliko. Ninaomba niishukuru sana Serikali, lakini ninaishukuru sana *TFS* kwa kufanya kazi kubwa, kwa kufanya juhudi nyingi sana za kuwagawia miche wananchi wanaozunguka maeneo ya msitu; na wao sasa wamepanda msitu na eneo lile sasa ni msitu mkubwa mno, ambapo wananchi wa Jimbo la Mafinga pamoja na kata za jirani wanaweza kujipatia kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza sana wizara kwa kutoa ajira za muda mfupi na za muda mrefu za wananchi wangu wa Jimbo la Mafinga. Katika jambo hili ninampongeza Mheshimiwa Waziri. Ninawapongeza *TFS* na pia ninampongeza sana Meneja wa Shamba la Miti *Sao Hill,* dada yangu Tedy Yoram; ni mtu bingwa sana. Ni mtu ambaye tunampenda na anafanya kazi kwa kushirikiana sana na wananchi pamoja na jamii inayomzunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, baada ya shukrani hizo ninaomba nijielekeze kwenye kuishauri Serikali. Kama nilivyosema Jimbo langu la Mafinga ni sehemu ambako tunazalisha sana mbao kutoka kwenye Msitu wa *Sao Hill,* lakini mbao zile zote tunazisafirisha kama malighafi. Sasa ninaomba niishauri Serikali kupitia wizara kwamba, wizara ifanye mchakato tuanzishe kongani za viwanda pale vya kuongeza thamani ili zile mbao zisiwe zinatoka pale kwenda maeneo mengine, ikiwemo nje ya nchi. Tutengeneze *furniture* pale pale Mafinga. Tukifanya haya tutakuwa tumewapatia ajira vijana, lakini pia tutakuwa tumeongeza pato la Serikali kuanzia kwenye sehemu ambako mbao zinatoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana kwenye jambo hili, pamoja na mipango mingine mizuri; leo nimesimama kuishauri Wizara kwa ajili ya kuongeza ajira. Tumepata ajira za vibarua, lakini tunao mafundi seremala kwenye Mji wa Mafinga pamoja na Wilaya nzima ya Mufindi ambao wangeweza kuajiriwa kwa kongani hizi za viwanda kwa kutengeneza *furniture* kwenye maeneo yale. Ninaomba sana wizara itenge bajeti maalum kwa ajili ya kuweka miundombinu hiyo ya kongani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ushauri huo pia ninaomba kuitaka Maliasili ikae meza moja na Wizara ya Fedha pamoja na TAMISEMI ili kuwa na mfumo wa pamoja wa malipo. Ukiwatazama wafanyabiashara ambao wanazalisha mbao kwenye Msitu wa *Sao Hill* malalamiko yao makubwa ni tozo za *Cess*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka kwamba Wilaya ya Mufindi inazo halmashauri mbili. Ndani ya halmashauri moja mvunaji anatozwa *Cess* kwenye vituo viwili hadi vinne. Kwa hiyo unaona kwamba wananchi wanaofanya kazi za uzalishaji wa mbao hawanufaiki sana na biashara hii kwa sababu ya tozo nyingi ambazo Serikali pamoja na halmashauri zinachukua. Kwa hiyo hizi wizara nilizozitaja ningeshauri wakae pamoja waone ni namna gani wanaweza kuwapunguzia tozo wananchi ili mitaji yao iendelee kuwa bora na waendelee kufurahia hii kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo hayo niliyoyasema, mimi ni muumini wa misitu ninawaitisha na ninawahamasisha sana Wanamafinga waendelee kupanda misitu kuuzunguka msitu wa *Sao Hill* kwa pamoja tuweze kuendelea kulinda moto. Sasa basi, ninaiomba wizara kupitia *TFS* yale maeneo ambayo vijiji vinazunguka kwenye msitu huu wa *Sao Hill* waangalie namna ya kuendelea kuwapa motisha vijiji hivi ili waendelee kuwa walinzi wazuri wa moto, kwa sababu adui mkubwa wa misitu ni moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzo walikuwa wanatoa motisha za namna hii, lakini sasa hivi ni kama waliacha. Ninaomba niikumbushe wizara kupitia *TFS*, bado msitu wa *Sao Hill* utaendelea kuwa na manufaa makubwa kwa vizazi vijavyo. Mahusiano baina ya Serikali na wanaozunguka msitu ni muhimu sana kwa ajili ya ulinzi wa msitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu kwamba wizara hii ina wachangiaji wengi na mimi sitaki kuchukua muda mrefu. Ninaomba hayo niliyoyaomba kwa Mheshimiwa Waziri yazingatiwe, Serikali ianzishe kongani kwenye Halmashauri ya Mji wa Mafinga ili tusisafirishe mbao zikiwa ghafi; wananchi wapate ajira pale pale Mafinga. Wazalishe *furniture* pale pale Mafinga.

Kwanza tutaongeza pato la Serikali, lakini pia tutaweza kuongeza ajira. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Vila kwa mchango wako mzuri. Nilimwita Thomas Kampala Maganga.

**MHE. THOMAS K. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwanza kabisa ninataka nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa moyo wake wa upendo na kwa kukubali kujenga Uwanja wa Kimataifa wa Serengeti. Kwa kweli mama huyu ana maono makubwa hasa kwenye nyanja za utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa leo sijui nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri; yaani sijui hata anafanya nini. Watu wote hapa wamenyanyuka kila mtu anaongelea utalii hiki na hiki na hiki ni kwa sababu wana raha. Mimi nina matatizo makubwa sana kwenye jimbo langu. Dada yangu ninamwamini sana, anachapa kazi. Hii wizara waliyompa dada yangu ina changamoto nyingi, ina watu wana vichwa vigumu utafikiri samaki wale gogogo wa Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo langu la Katavi ziko changamoto nyingi; na nimesikiliza bajeti yake yote Mheshimiwa Waziri sijaona mkakati wa makusudi wa namna atakavyotatua changamoto za wananchi na misitu ya hifadhi. Kwenye Jimbo la Katavi, mipaka ya Jimbo la Katavi ilipimwa mwaka 1954, ikafanyiwa *review* mwaka 1978 kwenye *operation* ya vijiji. Kipindi chote hicho Jimbo la Katavi lilikuwa linaitwa kijiji. Kulikuwa na watu wasiozidi 1,000 hadi 800. Hivi leo tunavyoongea Jimbo la Katavi lina watu zaidi ya 200,000. Maeneo ni yale yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Waziri anataka kumaliza migogoro hii ni lazima aje na mpango mahususi wa ku-*review* mipaka. Kwenye Jimbo la Katavi kila sehemu ukizunguka *GN*, *GN* huku *GN* tumezungukwa na misitu. *GN* kwenye Jimbo la Katavi zimekuwa kama *combat* ya jeshi, kila sehemu *GN*. Watu hawana raha, mambo hayaeleweki kila siku ni migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameongea Mheshimiwa Tabasam hapa, kila Waziri akija hapa anaondoka; siyo kwa sababu ya nini, ni malalamiko ya wananchi. Mimi ninamwamini, ni lazima aandae mpango wa makusudi wa kuja kuondoa hii changamoto. *Otherwise* sijui dada yangu atafanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la pili, alikuja Waziri Mkuu alifanya ziara kwenye Jimbo la Katavi akatoa maelekezo. Changamoto aliyokutana nayo ni hii hii, maeneo na ma-*GN*. Akasema, wapo wananchi pale waliondoka wengine wamekwenda kulima maeneo ambayo yanaonekana ni ya hifadhi, lakini hakuna mwananchi aliyevamia hifadhi, hifadhi ndizo zilizotuvamia sisi. Wamekuja wanachukua maeneo yetu, wanaweka ma-*GN* yao; sijui *TFS* sijui na kitu gani hapo. Tunakubali, sawa wakati huo tulikuwa wachache tumewaachia, sasa tumekuwa wengi ku-*review* mipaka hawataki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani ni sawa na treni ya *SGR* inakuja wanalazimisha watu walioshuka kwenye *SGR* wakapande kwenye *Hiace* waondoke, haiwezekani, hawatatoka. Ninaomba sana; kwenye hili dada yangu ninampenda na yeye anajua, kwa jinsi anavyochapa kazi, lakini leo nitakuwa kama mamba. Mamba akiwa na njaa huwa anamla mtoto wake huku analia. Nitaondoka na shilingi yake. Asipokuja na mpango mahususi wa kuniambia ni taratibu gani na nini atakifanya kwenye Jimbo langu la Katavi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimwambie dada yangu, watu wengine hapa, kaka yangu Tarimba na wengine, wameongelea utalii kwa sababu wana raha. Mimi kule kwangu *people are suffering*, watu wanachomewa mazao yao kunatokea vifo. Ng'ombe wanashikwa, mbuzi wanashikwa, pia kuku. Yaani hawa *TFS* na *TAWA* ninashangaa. kuna wengine wanasifia *TFS* na *TAWA* hapa. Yaani wao polisi, Mahakama sijui kitu gani, wana jela, wana *lock up,* wana kila kitu; wao ni Usalama wa Taifa. Haiwezekani, hakuna nchi ya namna hii. Wamsaidie huyu mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alipokuja kwenye Jimbo la Katavi aliniita, Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga njoo, nikaenda nikaongea. Nikamwambia Mheshimiwa Rais

mgombea wewe ni Rais na Jimbo la Katavi tutakupigia kura kama tumechanganyikiwa na watu walitoka kupiga kura. Ninataka nimwambie dada, mimi sikuwahi kuwa mtumishi wa Serikali. Nimekuwa kwenye chama nimekuwa Mwenyekiti wa Vijana nimeanza na machipukizi huko, Mjumbe wa *NEC*, Mkuu wa Operesheni ya Umoja wa Vijana Tanzania, kazi yangu ya kwanza yenye mshahara ni hii, wasiweke mshahara wangu rehani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu; ninaomba dada yangu leo aniambie hapa. Watu wangu wanachomewa mazao na Waziri Mkuu alitoa maelekezo, wale wote walioingia wakalima, askari wa *TAWA* na *TFS,* wanawaacha watu wanakwenda kulima, halafu mazao yamekomaa na kila kitu kimekamilika, wanakwenda wanachoma mabani ya tumbaku, wanakata mazao ya watu na kuwazuia wasivune.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinga ni bora kuliko tiba. Ninataka nimwambie dada yangu asipotoa maelekezo leo hapa, wale watu waachwe kuvuna yale mazao, shilingi mimi ninakwenda nayo. Wajomba zangu watajua wenyewe huko kama watalala na njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nimeona Wahadzabe hapa wamekuja. Wahadzabe ni kabila ambalo linaendeleza utamaduni wetu. Leo wanawaleta wamewavalisha suti, wanaharibu utamaduni. Wanakwenda kuwanywesha *whisky,* halafu kesho tutakwenda kuwatafuta wale wapi, tuwakose. Atatoka mtu kule, kuna watu wanatoka Ulaya kwenda kuwatazama Wahadzabe, kuna watu wanatoka Marekani wanakuja kutazama Wahadzabe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wanawaleta hapa mjini wamewavalisha suti; nini hiki, ndiyo kuendeleza utalii? Niwaombe sana na nimwombe dada yangu kupanga ni kuchagua. Akitaka shilingi yake ibaki, ninaomba majibu wananchi wangu waruhusiwe kwenda kuvuna mazao yao. Waziri akitaka niondoke na shilingi yake akae kimya na Wabunge wenye changamoto kama zangu ninaomba waniunge mkono. Ninajua wako wengi wamekaa kimya, wataniunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, sitaki kuongea mengi, ninataka nikuachie nafasi uendelee na wengine. Ninamwomba dada yangu akisimama, anipe maelezo ya kutosha kuhusu Jimbo la Katavi. Ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe, atafuatiwa na Mheshimiwa Mbwilo Kapunda.

**MHE. EXAUD S. KIGAHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia, kwenye wizara hii muhimu sana. Kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, aliyetujalia uhai kukutana siku hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mwanautalii namba moja katika nchi yetu, Rais wetu mpendwa, kwa kazi kubwa ambayo amefanya katika wizara hii na hasa kwenye sekta ya utalii. Hakika nimekuwa nikisema na leo ninarudia, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweka historia katika kila nyanja na katika kila sekta katika nchi hii ndani ya Awamu hii ya Sita katika uongozi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika maendeleo na hasa mimi kutoka Jimbo la Mufindi Kaskazini, ninamshukuru sana. Nimpongeze kupitia Waziri wangu, Dkt. Kijaji pamoja na Naibu Waziri *Comrade* Chande na uongozi mzima wa Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na taasisi zake wamefanya kazi kubwa kwenye Sekta ya Misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kwenda kwenye sekta ya misitu, sisi wana Iringa, tunamshukuru Mheshimiwa Rais, tunashukuru Wizara na Waziri wetu, kwa kuanza sasa kufungua Sekta ya Utalii Nyanda za Juu Kusini. Moja, kwa kuboresha Uwanja wa Ndege wa pale Iringa wa Nduli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuhakikisha Kituo cha Utalii pale Kihesa kinaanza kuimarishwa na kuwekewa miundombinu. Zaidi ni ujenzi wa Barabara ya kwenda katika Mbuga - Hifadhi ya Wanyama ya Ruaha na zaidi kule kwenyewe Mbugani kuimarisha miundombinu, ili kuhakikisha sasa na sisi Wanairinga tutaanza

kushindana na hifadhi nyingine kama Serengeti, Mikumi na kadhalika. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Waziri pamoja na timu nzima ya wizara hii, kwa kazi kubwa kwa ajili ya sisi Wanairinga na Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wana Jimbo la Mufindi Kaskazini, misitu ni uchumi na misitu ni uhai. Ndiyo maana leo lazima niseme ukweli kwamba, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, baada ya kuanzisha ile kampeni ya tarehe 27 ya kijani na kusema kwamba misitu ni uchumi endelevu, lazima tuendelee kuulinda kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wanamufindi, Jimbo la Mufindi Kaskazini tumeendelea kufanya hivyo. Ninamshukuru Mheshimiwa Vila amesema, sisi kule misitu ni uchumi. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, Mwalimu Nyerere ambaye, ndiye aliona sisi Jimbo la Mufindi Kaskazini, eneo kubwa ilikuwa ni Mbuga, *savana*, ambayo ilikuwa haifai kwa kilimo chochote. Kwa kuleta miti ile, misindano na milingoti, leo hii uchumi wa Wanamufindi unategemea misitu, viwanda vyote vingi viko pale kwa ajili ya kuvuna mazao ya misitu na maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika Profesa Silayo na timu yake wamefanya kazi kubwa kuhakikisha uchumi wetu, sisi wana Jimbo la Mufindi Kaskazini na Mufindi nzima tunaendelea na misitu ile zaidi ya 60% iko Jimbo la Mufindi Kaskazini. Sasa hii maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maendeleo haya tuna mambo ya kushauri katika kuhakikisha maendeleo haya na uchumi wa nchi hii unaendelea. Moja, sisi ndiyo sehemu ambako mito mingi inayozalisha umeme kuelekea Kihansi, lakini pia na kampuni binafsi kama Mwenga *Hydro*, lakini pia hata maji yanayoenda kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere, yametoka katika milima ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lazima tuhakikishe tunawasaidia wananchi hawa, ambao na sisi tumenufaika kupata miche ya kupanda kupitia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika siku hii ya tarehe 27 ya kijani ambayo hata mimi, yule Mkuu

wa Misitu Tarafa ya Ihalimba, nimepata miche 10,000 nimepanda mimi mwenyewe, lakini na wananchi wangu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kupanda na ndiyo maana tarehe mbili, wakati Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri Mkuu alikuja jimboni kwangu, akasema kweli hii ndiyo Mufindi. Maana yake amekuta mwezi huu Mei mvua inanyesha na wananchi tunaendelea kufanya kazi. Ili haya yaweze kuendelea, sisi kama nilivyosema katika hifadhi ile ya zaidi ya hekta 135,000, hekta zilizopandwa si zaidi ya hekta 60. Maana yake ni nini? Maeneo mengi bado wenzetu *TFS* hawajaendeleza zao hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, kama ambavyo Mheshimiwa Maganga amesema na sisi kule miaka ile ya 1970 wananchi walikuwa wachache siyo zaidi hata ya 10,000. Sasa hivi Jimbo la Mufindi Kaskazini tuko na wananchi zaidi ya 100,000. Sasa wananchi hawa, maeneo yale ambayo hayakuendelezwa wananchi wakasogea kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile Kamati ya Wizara Nane, ilipita kule kuhusiana na migogoro ya mipaka. Moja ya pendekezo lilikuwa kuwafidia wale wananchi wachache walioingia maeneo haya ya *Sao Hill*. Maeneo walioingia wananchi hawa haizidi hata ekari 200, sio hekta; ekari 200. Katika maeneo hayo wananchi hawa, kuna shule na makanisa, lakini pia hata watoto wetu na ndugu zetu wamezikwa hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, hao wenzetu walikuwa wametenga zaidi ya shilingi 6,000,000,000 kwa ajili ya kufidia wananchi wale waondoke. Ekari 200 na kwa sababu maeneo yale yalikuwa hayajaendelezwa na maeneo mengine makubwa, ambayo wananchi wengine na wawekezaji walikuwa wameyachukua na kupanda miti, tulikubaliana kwamba wakishavuna miti ile, yarudi *Sao Hill*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali yangu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Waziri wangu Mheshimiwa Dkt. Kijaji tuone namna ya kuwaachia ekari hizi 200 ambazo hazizidi hata 200, wananchi wa Mapanda, Igeleke,

Kibengu, Usokami, Wamimbarwe, Ihalimba na Ugesa ili kuendeleza upendo wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukilipa fidia hiyo ya shilingi 6,000,000,000 wananchi wale wakapata 20,000,000 au 30,000,000, hawaoni tija kwa sababu pale ndipo kuna makazi na wazazi wao wamezikwa pale. Kama nilivyosema maeneo haya, Mwalimu Nyerere alivyochukua yalikuwa ni maeneo ya hawa wazawa. Hivi kuna hoja gani ya kuachia ekari 100 au 200, badala ya kulipa fidia shilingi 6,000,000,000 ambazo hazitakuwa na tija kwa wananchi hawa, ambao kwa kweli ndiyo wanaolinda misitu ile kwenye moto na kuhakikisha wanalinda ili kupata vyanzo vya maji, kama nilivyosema ambavyo ndiyo wanaendeleza na mabwawa ya kuzalisha umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, ushauri wangu. Sisi maendeleo yetu kama nilivyosema ni misitu. Sasa barabara nyingi jimbo langu liko vijijini, tumehangaika sana na *TARURA*. Hapa ninarudia tena, nimeona wamefanya kazi nzuri katika maeneo mengine wamejenga barabara, wanasaidia kama, Kilombero, Rungwe na maeneo mengine. Pia, hata sisi kule tuna utalii sasa wa magari, ile *rally*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati wa magari yale yanapita, wenzetu hawa *Sao Hill* huwa wanatengeneza barabara zile. Niombe kupitia Mfuko wao wa Misitu Tanzania *(TaFF)*, watusaidie angalau kutengeneza barabara hizi, ambazo sehemu kubwa zinatumika kusafirisha magogo, mbao na miti inayotokana na mashamba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *TARURA* wakitengeneza si zaidi ya miezi mitatu imeshaharibika kwa sababu magogo yale mazito mbao na kadhalika yanapita kwenye barabara hizi ambazo ni za udongo. Kabla ya hapo walikuwa na magreda yalikuwa yanasaidia wakati fulani. Mheshimiwa Waziri awasaidie, Profesa Dos Santos, lakini pia na dada yangu Tabu Yoram, wakati mwingine magreda yale hayana hata *spare*. Wawekewe bajeti kidogo angalau watusaidie na sisi kutengeneza barabara zile, ili tuweze kusafirisha magogo na mbao na uchumi uendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, sisi uchumi kwetu ni miti. Miti ile tunatunza zaidi ya miaka 10 ili uvune. Hapo kabla tulikuwa tunauza gogo moja au mti mmoja karibu shilingi 8,000 au 10,000. Sasa hivi kutokana na hali mbaya ya barabara wananchi wale hata kuuza kwa 2,000, ambalo gogo umetunza miaka 10 haliuziki. Kwa sababu, wale wafanyabiashara wanasema kusafirisha kutoka kule porini ni gharama, ni ghali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana watusaidie kwenye sekta ya barabara. Nimalizie kuunga mkono hoja kwamba, moja ya mambo makubwa ambayo wamefanya ni kuhakikisha tunaendelea kuchakata, maliasili ya misitu, kuongeza thamani ili tuhakikishe tunauza bidhaa za mwisho. Kuna viwanda vingi vinavyozalisha *veneer*, *plywood* na *ceiling board*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba, Serikali ilifanya kazi kubwa sana kupiga marufuku kuuza *veneer* nje ya nchi. Ninaomba Mheshimiwa Waziri, kale kanafasi kadogo walikokuwa wamekaacha, sasa tukaze tufike mwisho. Bidhaa zote zizalishwe Mafinga Mufindi, Tanzania tuuze nje bidhaa zilizoisha *(finished products)* badala ya kuuza *intermediate goods* ambazo wanaenda kuzalisha kule, halafu tena watuletee sisi samani ambapo sisi ndiyo wazalishaji wa maliasili na *raw materials* hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Mbwilo Kapunda atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara na Mheshimiwa Daniel Awack ajiandae.

**MHE. BAZILIO K. MBWILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa ili nichangie. Kwanza nianze kwa kuwapongeza sana wafanyakazi wa *TAWA,* Jimbo la Nkasi Kaskazini, ikiwa ni pamoja vilevile na wafanyakazi wa wanyamapori katika Wilaya ya Nkasi; wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana, huko kwangu tembo ndiyo balaa kweli kweli. Kwa taarifa niliyoipata kutoka *TAWA* - Wilaya, miaka miwili iliyopita idadi ya tembo ilikuwa ni 19,000, lakini mwaka huu wamefikia tembo 21,000 na kwamba kila tembo wanatembea sita, watano majike kila mmoja ana mtoto. Hao watoto hawajahesabiwa bado. Kwa hiyo, hili ni tatizo kubwa kweli kweli na eneo ni kubwa watumishi waliopo hawatoshi hata kidogo. Kwa wanaolifahamu Jimbo hilo kuanzia Kalila mpaka Masolo ni karibu kilomita 40. Sasa hata wangekuwa wafanyakazi 100, wanaweza kweli na ni msituni huko porini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi imetokea tembo siyo usiku tu kwenye jimbo langu, hata mchana tembo wapo barabarani wanaingia hadi vijijini. Kuna Barabara sasa hazipitiki, kwa mfano ile ya Mongamkulu kwenda Korongwe haipitiki tena, kwa sababu hata ukipita saa nane mchana utakutana na tembo, tena wakorofi kweli kweli hawataki kupisha barabara. Hata ukiwa na gari ukipiga honi hawataki kutoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba katika hili basi tuwawezeshe hawa vijana wetu wazuri sana, hawapati usingizi walau tuwaongeze vyombo vya usafiri, lakini vilevile tuwaongezee na vifaa vya kufukuzia tembo. Mimi huku jimboni kwangu nimewezesha kuwepo na vikundi vya jamii, ambavyo vinasaidiana na hawa *TAWA* pamoja na halmashauri kufukuza hawa tembo. Sasa tungeomba waongezewe vifaa *gumboot*, makoti yale ya mvua, tochi ili mradi wasaidiane. Safari hii uzalishaji utashuka sana kutokana na uvamizi wa hawa wanyama tembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachopendekeza ambacho ninadhani inaweza ikatusaidia sana, ni kujenga hizi fensi. Tujenge kutoka Kalila kwa Jimbo la Nkansi tuje mpaka Masolo wala tusione kwamba ni gharama kubwa kwa sababu madhara tunayoyapata ni makubwa kuliko hiyo gharama ya fensi. Uzuri tukishajenga fensi mara moja hatutajenga tena itachukua miaka mingi. Hii itatusaidia sana kuwaokoa hawa vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia na wenzangu wamechangia, lakini kwa kuwa wao hawatoki kwangu na mimi nichangie. Mpaka leo hii kuna

mvurugano sijui ni kiswahili au cha Kifipa hicho. Kuna mvurugano mkubwa, hatujui mipaka, wapi hifadhi zinaishia na wapi kijiji kinaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tukifahamu mipaka inakopita, lakini sasa hivi tayari alama zimesogea karibu kabisa na na vijiji. Kwa hiyo, ningeomba sana tufanye kila linalowezekana, mwaka huu ikiwezekana, twende tukaonyeshe upya mipaka ili tujue. Maana sasa tunaambiwa kwamba tunavamia misitu, lakini sisi tunasema misitu imetuvamia. Kwa hiyo, ningeomba sana hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo ombi lingine. Kama tulivyosema, binadamu tunaongezeka ardhi haiongezeki. Sijui tutafanya *reclamation* gani ili kuona kwamba ardhi imeongezeka. Niombe tupitie tena upya, tuongeze maeneo haya tunayoyaita ya hifadhi yasogee kwa wananchi. Tukiongeza walau kilomita kadhaa huko ndani itatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vijiji sasa hivi, kwa mfano, Kijiji cha Masolo hakina tena eneo la kilimo. Hakina kwa sababu walikokuwa wanategemea mwisho mtoni, sasa tumeambiwa kule kote ni hifadhi, *beacon* zimekuja kama mita 100 kutoka kijijini. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri, atuone katika hilo tauongezee eneo ili tuweze kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninajua kuna wachangiaji wengi. Ninaomba sana haya niliyoyaomba, yazingatiwe. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Nimwite sasa Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai na Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa ajiandae.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia. Hii Wizara ya Maliasili ni maarufu sana na inaongeza pato la Taifa katika nchi yetu, lakini kwa Wabunge na watu ambao tunaishi karibu na hifadhi mbalimbali, mtazamo wao ni tofauti sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafuatilia tangu tumeanza kuchangia *session* ya asubuhi mpaka sasa hivi, kila Mbunge akisimama hapa analalamika. Hii inatuonyesha kwamba Mawaziri wa wizara hii, waje na mawazo tofauti. Tumekaa hapa hiki mimi ni kipindi cha tatu, nitakayoyazungumza hapa nimezungumza tangu Bunge la mwaka 2015, majibu hayajawahi kupatikana. Sasa maana yake ni kwamba, tunazungumza mapato ya nchi, lakini tunazungumza maisha ya watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anavyokwambia kwamba, tembo ameua, huyu ni mtu ameuawa. Yaani huyo angeweza kuwa kama Waitara hivi, angeweza kuwa Mbunge, angeweza kuwa Waziri, huyu aliyekanyagwa na tembo au huyu ambaye ameliwa na mamba. Kwa hiyo, tunapozungumza Waheshimiwa Wabunge, mambo ya watu wetu kupotea, mambo ya watu kuuliwa, siyo mambo ya kucheka kwamba halikuhusu, tunazungumza uhai wa watu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri na wenzake, lazima waone kwamba, hapa tunazungumza habari ya pesa ya utalii na maisha ya watu, kipi ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko changamoto, kwa mfano pale Tarime Vijijini, mimi nimepakana na Hifadhi ya Serengeti. Habari ya *CSR*, ukienda pale Kwihancha hawana maji, hawana barabara, hakuna vifaa shuleni na kwenye hospitali, lakini kuna Hifadhi ya Serengeti pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda Kata ya Gorong'a, hamna kituo cha afya, hakuna madarasa, mchango wao ni nini pale? Nenda Kata ya Nyanungu, ile *CSR* ya pale haieleweki, haina *formula*. Yaani anaweza akaamua ajenge darasa moja au asijenge. Tunaomba tupate utaratibu, namna tunaweza kupata *CSR* ya kuwanufaisha watu wetu ambao wapo karibu na Hifadhi ya Serengeti, pale Tarime Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi wizara; Wizara ya Ardhi, Wizara ya Maliasili, Wizara ya Mifugo, Wizara ya Kilimo, TAMISEMI hawa Rais ameshawapa nafasi wanatakiwa wakae pamoja. Wewe angalia mchezo uliopo hapa unazungumza habari ya watu walime, wakishalima mwenye ng'ombe anaenda kulisha mazao ya mwenzake. Unazungumza habari ya kwamba watu walime

wakilima karibu na Hifadhi ya Serengeti wanaenda kufyeka mazao, hii ni *mark time*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ina maana hizi wizara wakae pamoja watafuta suluhisho, changamoto ni nini? Kuna maeneo mengine tupo karibu na hifadhi wakati wa kiangazi, hakuna maji wameshindwa kuchimba marambo pale. Kwa hiyo, mfugaji analazimika kuchukua mifugo akanyweshe maji karibu na mto. Akikamatwa, anataifishiwa ng'ombe zake; akikamatwa anapigwa; akikamatwa wakati mwingine anapotea. Migogoro iliyopo hapa ni mingi kila jimbo maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba Wabunge ambao tupo karibu na hifadhi hizi na misitu tupate muda tuzungumze tuiambie Serikali ifanye nini ili watu wetu wasiendelee kuumia. Kila Bunge watu wanalalamika humu Hifadhi ya Serengeti, kila Bunge watu wanasema migogoro. Unazungumza hapa mamba, tembo yaani ni vurumai haiwezi kuwa hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapenda watalii, tunapenda fedha tupate maendeleo, lakini lazima tuangalie pia ustawi wa watu wetu. Kuna mgogoro wa ardhi, mwaka 2021 Mawaziri Nane walizunguka walienda Tarime Vijijini. walipofika pale Tarime katika Vijiji saba kwa maana ya Kuihanja, Gorong'a, Nyanungu kuna *GN* ya mwaka 1968 mimi nilikuwepo, kilichofanyika eti Mawaziri wamekwenda pale badala ya kuwasikiza wananchi ambao wanaishi lile eneo unajua hifadhi ndiyo inaonyesha *beacon* walikuwa wanapindisha ile migogoro mpaka leo wameacha pale kiporo. Tunataka suluhu ya migogoro hii, hizi *GN* wananchi wanazijua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamekaa pale miaka zaidi ya 100. Leo sasa mtu anaishi kwa kuelewa; Yaani haelewi kwamba atahama, ataishi, yupo yupo tu. Hawezi kuendeleza eneo lao. Ninaomba mgogoro wa Tarime Vijijini wa Hifadhi ya Serengeti vijiji saba, twende, wapo wazee wana miaka 70, miaka 80 wamezika pale wamezaliwa pale, twende tupitie *beacon* moja baada ya nyingine. *GN* hii hapa wanaikubali. Isiwe ile ya kutengeneza ya kwao. *Huwezi kwenda kutatua mgogoro wa wananchi, huwasilikizi wananchi, mhifadhi ndiyo anakupa*

*mipaka, Waziri anapiga makofi halafu anaondoka yamekwisha? Hapana, twende tukafanye shirikishi.* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli nchi hii hivi tutatumia akili gani? Katika hali ya kawaida watu wako hawana sehemu ya kulima, watu wako hawana sehemu ya kuishi. Wewe unazungumza habari ya wanyama ndiyo ni muhimu? Kipi muhimu kati ya binadamu na wanyama? Hayo manufaa ya maliasili ni wananchi hawa hawa, si Serikali ifunguke tu Mawaziri wafunguke. Twende, Wabunge wana migogoro mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri atuite kikao siyo kwenye bajeti hii, tuzungumze naye. Twende kwenye majimbo tutafute suluhu, lazima tukubali, tupanue maeneo watu waendelee kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitaomba Bunge la Kumi na Mbili, nilikuja hapa nikawaambia watu wamepotea Kuihancha, watu wamepotea Karakatonga, Nyanungu nikaandika ripoti sina majibu, ninaileta tena. Nilisema watu wangu wamepotea maelfu pale Tarime Vijijini nikaambiwa nithibitishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikaleta *document* hapa sina majibu ninataka majibu ya taarifa ile kama mimi ni muongo, anitangaze mimi ni mwongo, kama nimedanganya watu nishtakiwe. Nina picha za makovu, nina picha za risasi, nina picha za makaburi. Wale ni ndugu zetu na wananchi wananihoji. Nitampa *document* hii Mheshimiwa Waziri, ninataka nipate taarifa ya kwenu, hii hapa nilidanganya au nilisema ukweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaunga mkono hoja Jumatatu, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe, ninaomba usimame Mheshimiwa Mwita. Kuna maneno umeyatumia hapa ambayo ninadhani hayaendani na kanuni zetu. Tungetaka uyaondoe kwamba Waziri anampigia makofi mtendaji wa taasisi, ninadhani tuondoe hayo maneno kwamba Waziri anampigia makofi. Uyaondoe hayo maneno.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Sijaelewa.

**MWENYEKITI:** Umeongea kwamba.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Naam.

**MWENYEKITI:** …Waziri ndiyo anapiga makofi kwa mkuu wa taasisi.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Aah kumbe ni hilo?

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo nadhani katika kuongea...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Yaani iko hivi Mwenyekiti, tumeenda *site* mimi Mbunge nimelalamika…

**MWENYEKITI:** Wala kiti hakitaki kuhojiana na wewe.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Sikuhoji Mheshimiwa ninakuheshimu tu.

**MWENYEKITI:** Ninasema uondoe hayo maneno.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Basi kwa heshima ya Kiti, nimeondoa.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Walikubaliana tu, ahsante. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninashukuru. Waheshimiwa tunaendelea nimwite sasa Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai, atafuatiwa na Mheshimiwa *Eng.* Ezra John Chiwelesa.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Kwanza nimshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nimshukuru Waziri, Naibu Waziri na wote walioko katika Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninamshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan? Ninamshukuru kwa kazi kubwa aliyofanya ya *Royal Tour* ambayo katika Jimbo la Karatu imeleta maendeleo makubwa kwa kutokana na jiografia ambayo tuko nayo katika Jimbo la Karatu. Jimbo la Karatu limepakana na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na pia imeweza kupakana na *Manyara National Park*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Karatu tuna kata 14. Katika kata 14, kata tisa zimezungukwa na hifadhi. Kata tano tu ndiyo hazijazungukwa na Hifadhi hizo za Manyara na Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jimbo kama hilo kwanza hatuna gari, idara ile ya utalii pale halmashauri imekaa tu, lakini pia sisi kwa Jimbo la Karatu kupitia mapato yetu, pia hawana hata bunduki. Wanyama wakiingia katika maeneo hayo bado ni changamoto. Katika Jimbo letu la Karatu tumejitahidi kupitia halmashauri tukanunua bunduki karibu miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile kupatikana tu kwa bunduki imekuwa changamoto na sisi tumetoa fedha na bunduki tumenunua, lakini kusajiliwa tu kwa bunduki imechukua muda mrefu, ili watumishi walioko katika eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Karatu wawasaidie wananchi wetu katika ukanda huu wenye kata tisa ambao wanapata changamoto kubwa ya tembo na wanyama wengine wakali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizara hii ina changamoto kubwa kama mchangiaji aliyemaliza kuongea na sisi hatulaumu kwa nini tunapakana na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na hatulaumu kwa nini tunapakana na *Manyara National Park*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uzembe mkubwa unaotokana na changamoto inayotokea katika maeneo yetu. Kwa mfano, sheria zile za uhifadhi inasema mnyama akitoka katika *Fireline* akiingia katika eneo ya kijiji wanaotakiwa kumtoa pale ni wale ambao wako ndani ya halmashauri husika. Sasa kwa sasa tuna changamoto kubwa kwa sababu hamna gari na watu wetu wanauliwa kila leo na katika mbuga hizo zote mbili nilizotaja

zina wanyama wakali ambazo zimepakana na Jimbo letu la Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto kubwa hii ya wanyama kuingia katika maeneo ya wananchi wetu. Kwa leo hii unaambiwa fidia ekari moja inafidia shilingi 25,000. Juzi wamedai kwamba wamepandisha kutoka shilingi 25,000 kwenda shilingi 37,000, leo kulima tu ekari moja kwa trekta, hizo fedha shilingi 37,000 hazitoshi ambapo wizara wanadai kwamba wameongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na fidia hiyo ya shilingi 25,000 kwa sasa sisi Jimbo la Karatu tunadai zaidi ya shilingi 100,000,000 na hebu fikiria shilingi 25,000 mpaka upate shilingi 100,000,000 na wananchi wetu ni wangapi ambao wanasubiri fidia hiyo yenyewe ya shilingi 25,000 ambayo wizara wamesema kwamba ndiyo fidia halali kutoka mita 500 kwenda mita, 1,000 kilomita moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto kubwa kama inavyoelezwa sisi tuliokutana na hifadhi na tunakutana na changamoto hiyo kwa mfano Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro chanzo cha maji katika jimbo langu maeneo makubwa yanatoka katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kuingia tu ndani ya ile hifadhi unatakiwa upate kibali, lakini vilevile pamoja na kupata kibali lakini pia Serikali ilitoa fedha na kwamba sasa maji inatakiwa tuchukue katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, mamlaka yenyewe watumishi wa mamlaka wanahitaji kwamba yule mtu wao atakayekuwa analinda kule msituni Serikali imlipe na wakati wa fedha zinatoka Serikalini haina malipo hayo ya mtu ambaye atakwenda kusaidia ambayo yanatokana na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni changamoto kubwa, kuna miradi mingine ilikwama karibu miaka miwili ambayo Serikali imetoa fedha kutokana na changamoto hii ambayo ipo katika upande wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ng'ombe akiingia katika hifadhi hizi anachajiwa shilingi 100,000 lakini tembo akija kwenye shamba lako anakula shamba lako na bei unakadiriwa. Kwa nini tusihesabu tembo wakiingia watano, kama ng'ombe analipa shilingi 100,000 kwa nini tembo watano wakiingia kwenye maeneo yetu tusihesabu shilingi 100,000 kwa kila mmoja ili tupate shilingi 500,000 kwa tembo ambao wameingia katika mashamba yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafikiri ifike muda tusiangalie ekari tuangalie tembo wanaokuja kwenye maeneo yetu tuhesabu tembo. Kwa sababu wanyama hao wakiingia kwenye maeneo yetu wanakadiriwa kwa ekari, lakini tembo akiingia kwenye mashamba yetu ekari inalipwa shilingi 25,000, utaona hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hivi kwenye utaifishaji wa mali za umma, ng'ombe za watu hivi mpaka saa hii umeona faida wanayopata wananchi wetu, Serikali inapata faida gani kwenye upande wa kutaifisha? Hapa nitampa Waziri ushahidi katika jimbo langu, ng'ombe walitaifishwa, mimi mwenyewe nilipambana, nilitaka nimlipe yule mwananchi faini ya laki moja moja, wale ng'ombe wote niwalipie, mwananchi abaki na wale ng'ombe, lakini walikataa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanachotumia hawa watumishi wanasema mwenye ng'ombe hayupo. Wanakwenda mahakamani, wanafanya kesi wenyewe kwa upande mmoja, Ng’ombe wakati huo wamezuiliwa msituni na wanahukumu, wanaondoka na yule ambaye anayekwenda kwenye mnada kutoka kwenye mahakama hiyo ya wilaya na wanatengeneza ng'ombe ambao ni shilingi milioni mbili wanakwenda kuuzwa kwa shilingi laki tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni unyanyasaji kwa sisi tuliokutana na hifadhi hizi nami ninafikiri, sipingani sana na faini ya shilingi 100,000 japo ni kubwa, lakini eneo hili la utaifishaji lina unyanyasaji mkubwa sana katika maeneo yetu na watu wetu wanateseka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejitahidi kuona, kukaa karibu na maeneo yale kuna changamoto, kwa mfano Kata ya Buger. Kata ya Buger mwaka 2009 waliweka mipaka, lakini mwaka 2014 walienda kuweka mipaka, lakini mwaka na 2017 Maliasili ni hawa hawa, mwaka wa 2017 walisema hapo tumekosea, wameingia kwa wananchi wetu na wamekata maeneo ya wananchi wangu katika Kata ya Buger katika Kijiji cha Buger na Kijiji kinaitwa Analiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo lingine la Kanzai unyweshaji wa ng'ombe ni katika eneo ina maana bila kuwa na eneo hilo wananchi hawawezi kupata maji. Wamekataza tusinyweshe ng'ombe katika eneo hilo ili wananchi wetu waweze kupata tabu, kwa sababu hilo eneo lilikuwa ni eneo la hifadhi limepakana na wananchi wetu, lakini ukienda kunywesha hapo wanazuiliwa wananchi wetu na ng'ombe wetu wananyang’anya na imekuwa unyanyasaji wa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyomaliza kuongea huyu mchangiaji wa mbele yangu sisi tuliokutana na hifadhi tuna changamoto kubwa, kuna unyanyasaji mkubwa sana wa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano katika Jimbo la Karatu katika eneo la ukanda wa Buger wamewanyang'anya wananchi maeneo makubwa halafu baadaye wanasema watatupa fidia. Sisi hatuna shida na fidia. Eneo lilikuwa letu na nimekwishawahi kusema wananchi wale hawana shida na fidia kama maliasili wanaona lile eneo ni lao wachukue, lakini wananchi wangu hawana shida na fidia kwa sababu sisi hatuna mahali pa kupeleka fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna shida eneo letu na ardhi yetu ambayo wamenyang'anya mwaka wa 2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maliasili hiyo 2009 wameweka mipaka hao hao ambao wako *Manyara National Park*. 2014 wameenda kuweka mpaka hao hao Maliasili, 2017 wanatunyang’anya eneo letu. Haiwezekani! Wizara iangalie na

waende Buger na warudishe maeneo ya wananchi wetu wa Kata ya Buger. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Awack ahsante sana. Nimwite mchangiaji wetu wa mwisho, Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba ya bajeti hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii, lakini kipekee kwa nafasi nyingine kwa niaba ya watu wa Biharamulo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizidi kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa maelekezo aliyoyatoa akiwa katika ziara ya Mkoa wa Kagera, Wilayani Biharamulo tarehe 8 Juni, 2022, lakini pia tarehe 16 Oktoba, 2022. Tulipata bahati ya kutembelewa na Mheshimiwa Rais mara mbili kwa mwaka, mwaka 2022, kwetu sisi ni heshima kubwa na kilio chetu kikubwa labda nikitaka kurudia ni suala la ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Biharamuro kijiografia na ukubwa wake ina ukubwa wa hekta 5,627. Eneo linalokaliwa na watu tukimaanisha mito, milima, mashamba na vitu vingine vyote ni hekta 183,000 sawa na 32.67%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine yote ni Hifadhi ya Burigi-Chato ambayo ina hekta 213,000 sawa na 37.9% na maeneo yaliyohifadhiwa chini ya *TFS* tukiwa na hekta 166,100 sawa na 29.5%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nimeamua nianze na hii? Nimeanza na hii kwa sababu Wilaya ya Biharamulo idadi yetu imekuwa inaongezeka lakini maeneo yetu ya kufanyia kazi bado ni yale yale. Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2002, Wilaya ya Biharamulo ilikuwa na watu 159,000 lakini eneo ni 183,000 hekta lile lile. Mwaka 2012 tukawa na watu 323,466 eneo ni lile lile 183,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sensa watu na makazi ya mwaka 2022, Wilaya ya Biharamulo tuna watu 457,114 eneo letu la kufanyia kazi na makazi ya wananchi bado ni lile lile. Huku tukiwa tumezungukwa na misitu na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nimeanza na hii, ninaomba tu Mungu anipe busara na hekima tuongee vizuri hapa tuweze kuelewana. Niko hapa kwa ajili ya wananchi 457,114 wa Biharamulo. Bila wao kunileta hapa nisingekuwepo, lakini *sufferings* wananchi wanazopata ni kubwa. *We have to say the truth*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tukijifungia humu ndani tusiseme ukweli wa shida wananchi wanazopata hatu-*represent* wananchi. Asubuhi huwa tunaanza na sala hapa. Mungu atupe hekima ya kufanya maamuzi kwa mujibu wa walio wengi. Walio wengi tumewacha huko nje, sisi tuko 400 tu hapa, kwa hiyo, tufanye maamuzi sahihi kwa ajili ya Watanzania walio wengi huko nje, wananchi wananyasika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeomba maeneo haya Mheshimiwa Rais akatoa maelekezo. Mwaka jana kwenye kampeni Makamu wa Rais alipokuja Biharamulo, Nyakanazi pale alitoa maelekezo, TAMISEMI, Maliasili na Ardhi wakutane, lakini mpaka sasa sijaona kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais amekuja Kagera akatoa maelekezo *specific* tarehe 9 Agosti, 2022 akiwa katika Uwanja wa Kaitaba kwamba anataka aione Kagera ile aliyokuwa anaisikia zamani. Kagera maisha yetu ni kilimo na akatoa maelekezo zitafutwe ardhi. Huwezi kutafuta ardhi kwa wananchi kwa sababu hazipo. Ardhi zinatafutwa kwa Serikali, tumeandika barua tangu 2022 hatujibiwi wakati ni maelekezo ya Rais alipokuwa Kitaba pale, sasa *what do want us to do*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanaongezeka, hatuna viwanda, sisi Biharamulo maisha yetu ni kilimo na mifugo, lakini wananchi wananyasika usiku kucha, hawa wananchi walio wengi haya mapori si kusema yako hewani. Yanapakana na wananchi

hawa ambao tunawakilisha sisi waliotuchagua tuje hapa. Sasa huwezi kuniambia mwananchi hata kuokota kuni tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaongelea umeme, vitongojini, si tumeanza kupeleka umeme leo? Hivi kweli tunasahau labda ninyi mliozaliwa mijini watoto wa kishua, lakini huko kuna watu wanaishi kwa nyumba za nyasi. Yule mtu hata ukimwambia kuhusu mkaa anakushangaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu kwenye maisha yake hajawahi kushika 20,000, unaiona 20,000 ni ndogo, lakini kuna mtu hajawahi kuishika, akiamka asubuhi amepeleka ndizi sokoni, akiuza ndizi anapata shilingi 10,000 na hiyo shilingi 10,000 ananunua vyakula vya mahitaji ya nyumbani harudi hata na shilingi. Hao watu wapo ndiyo hao tumekuja kuwawakilisha humu, tusifike humu tukasahau tulipotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu hawana umeme hata huko ndiyo Serikali inapeleka umeme leo. Tunalia maji kila siku hapa, kwa nini tukija humu tunajisahau? Hao watu ambao wananyanyasa wananchi, kumnyang’anya kuni tu mwananchi kaokota akiwa ametoka shamba, anaenda kupika, alishe watoto wake wanaotembea kilomita tisa mpaka 10 kutafuta shule kwa sababu hata shule shikizi kijijini hazipo. Anamshika mama ana baiskeli anamnyang'anya, anamshika mtu ana mzigo wa kuni anamnyanganya, *where are we going*? Hawa watu wametoka wapi kutunyanyasa namna hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika mtu aliyezaliwa kijijini anayajua haya mateso hawezi kufanya hivi kwa Watanzania wenzake. Tunateseka, tunaomba Wizara hii Mheshimiwa Dkt. Ashatu ni shemeji yangu. Msimu uliopita ametoka nje na ni shemeji yangu, nimeyasema yote haya, lakini masuala ya familia tunaweka huko, leo tusimame kwa ajili ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *our people are suffering*. Tuko hapa kwa ajili ya kuwakilisha wananchi. *TFS* hizi sheria wamezitungia wapi? Nami niko hapa Bungeni, ninajua wakati wa kutunga sheria huwa wanahusisha hata hizo jamii, ndiyo maana tunaita wadau hapa wakati wa kutunga sheria, waje watoe maoni. Hizi sheria

zao wanazotunga ndugu zangu, barabara za lami zimepita kwenye Hifadhi ya Mikumi; barabara za lami zinapita Serengeti na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwananchi anayeishi kijiji hiki anataka kuvuka kwenda kijiji hiki kupita tu kwenye hifadhi hapa akikamatwa baiskeli hana, huyo mtu kashikwa, kapigwa viboko, kanyanyaswa. Mwananchi wa kijijini kuna mtu hajawahi kupanda gari mwaka mzima, hana sababu ya kumfanya apande gari kwa sababu hana usafiri, lakini anapoishi huku kuna msitu, huku kuna msitu, anataka kwenda kijiji cha pili katikati anaweza akakatiza akawahi kufika, wanamkamata ndani ya pori wanamfanyia *hammering* kama hizo, wanamnyanyasa, huelewi hawa watu wanataka nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2023 Biharamulo pale, kwenye mapori haya ya *TFS*, Mkuu wetu wa Wilaya wakati huo Mheshimiwa Kemilembe Lwota na Kamati ya Ulinzi na Usalama waliongoza kikosi cha ulinzi na usalama kuvuna bangi ekari 200 za bangi ninadhani. Sasa unajiuliza ekari 200 za bangi unajiuliza hiyo bangi imeoteshwa katikati ya Hifadhi ya *TFS* hawa jamaa hawaioni ile bangi, lakini mwananchi anayepita na baiskeli wanamwona, wanamnyanyasa, wanamkamata namna hiyo. *Let's be fair*. Hiki tunakisema kwa sababu kimefanywa na Serikali na kilikuwa wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sina ugomvi na Waziri wala Naibu Waziri kwa sababu huyu ni Mbunge mwenzetu na yeye anawakilisha wananchi. Tuna shida sana na watendaji wa chini. Tumewatungia sheria za kuwafanya kwanza wao wawe matajiri, *they are making a lot of money* huko vijijini, *they are making a lot of money*. Tumewapa utajiri bila sababu, tumewafanya wananyanyasa wananchi bila sababu. Bahati mbaya hata akija Profesa Silayo De Santos tutamtesa, hii nchi ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nimesema Biharamulo misitu aliyonayo ni 166,000 hekta. Huyu Profesa anaijua hiyo misitu? Akija watampa maelezo haya, wakimaliza watampa maelezo haya. Yeye ataona wamefanya sawa, lakini *let's go back*, ningeomba hata kama wametunga sheria; hata kama hawa *TFS* ni jeshi, ifikie

*stage* wawajibike kwa wakuu wa wilaya kama viongozi wa Kamati za Ulinzi na Usalama, wao ndiyo wanaosikiliza wananchi. *TFS* wamekuwa na viburi kupita kiasi, hawezi kusikiliza mtu zaidi ya Waziri wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri wanatusaidia wananchi wakikamatwa Mbunge ukimbilie kwa Waziri. Waziri apige simu wao ndiyo wasikilize, lakini hawezi kumsikiliza Mkuu wa Wilaya, hawezi kumsikiliza Mbunge, hawezi kusikiliza mtu mwingine yeyote yule. Sasa yaani hawa wanaishi na sisi kufanya nini kule vijijini? Kama hawawezi kusikiliza mtu mwingine yeyote yule isipokuwa viongozi hawa ambao wako kwenye *line* yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachoomba kwa niaba ya Watanzania wengi ambao *wana-suffer* kwenye maeneo haya. Wameletwa kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania kuhifadhi haya maeneo, hatukatai lazima maeneo yahifadhiwe, lakini twende mbele turudi nyuma. Mateso ni makubwa, haturuhusu watu kuingia kwenye hifadhi, sawa, lakini busara zitumike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaumia ndiyo maana leo nimeongea kwa uchungu namna hii kwa sababu *it's hurting us*. Unakwenda kijijini, mtu anakupigia simu Mbunge uanze kubembelezana na yule mtu, unahangaika na vitu vingapi hapa? Unapokuja kuomba miradi ya barabara na maji na vitu vingine na yeye unamwombea, *yet* hakuheshimu, anafanya nini kwenye jimbo lako sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaomba haya mambo yaangaliwe. Serikali ni moja, watu wawe na heshima. Sisi ni viongozi tuko hapa, Wabunge wanalalamika, tunajua tunavyowafuata Mawaziri kila wakati ukabembeleze *chain saw* imechukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *last time* mimi Kanisa wamekata miti pale, si kila mtu anajua hizi sheria. Kanisa limekata miti kwenye eneo lao pale, wakafika wamekata mbao, wanaezeka kanisa la Wasabato pale Kata ya Kaniha. Wakawabeba wachungaji na wakabeba hivyo, hivi kesho hawa watu kweli unakuja kuliambia lile kanisa kwamba Serikali ipo watakuelewa? Yaani wanatutesa

kwa vitu ambavyo havina maana. Kwa hiyo tulikuwa tunaomba tusaidiwe kwenye haya mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye masuala ya kijimbo kwa kumalizia, yote haya yalikuwa ni ya kijimbo lakini kwenye masuala ya kijimbo kwa kumalizia. Niliomba geti pale Biharamulo. Mheshimiwa Rais akiwa Biharamulo tarehe 8 Juni, 2022 lipite Ruziba, Katerera kuingia kwenye Hifadhi ya Taifa, Mwenyekiti akasema amesikia kuingia kwenye Hifadhi ya Burigi tunaomba hayo mambo yatekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili kwa kumalizia, unajua sisi tunaotoka mikoa ile kule tuna mchanganyiko mwingi sana. Mimi nikikuangalia usoni tu hata bila kuniambia nitajua unatoka nchi gani au nitajua unatoka sehemu gani. Wananchi wangu ng'ombe wao wanamalizika kwa sababu wanakamatwa kwenye hifadhi, wengine ndiyo hao kwenye *TFS* au Burigi penyewe, lakini *reality* ni kwamba hatuna haja ya kusema, lakini ng'ombe wako wengi sana kwenye hifadhi ya Burigi-Chato wanaotoka nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ng'ombe wanavyokamatwa, wananchi wanakuja wanakwambia Mheshimiwa Mbunge tunanyanyasika kwenye nchi yetu, wa kwetu wanakamatwa lakini wako waliotoka jirani wako humo. Sasa tunasababisha wananchi wanaingiza ng'ombe kwenye hifadhi kwa sababu wanaona ng'ombe wa sehemu nyingine wanaingia mle. Tunavyojijua Watanzania hata wale ng'ombe ukiwapanga hivi sisi tunawajua. Nikishajua huyu ni *Nyankole,* huyu ni *Nyabugesera,* ninajua huyu ni wapi anatoka. Sasa tunaiomba Wizara ya Maliasili itusaidie kwenye haya mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani ng'ombe wakaja wakakaa kwenye Hifadhi ya Burigi-Chato, Watanzania wa kwao wakiingia wanakamatwa, halafu hao wengine wako mle na tunawaona kwa sababu wananchi wanasema na tunawajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukienda pale kwenye mnada wa Rusahunga na maeneo mengine ng'ombe waliotoka hifadhi wanajulikana na ng'ombe ambao siyo wa kwetu wanajulikana. Yaani ni sawa na kuleta ng'ombe wa Biharamulo unaleta

Dodoma hapa. Akishafika atajua kabisa huyu siyo wa hapa huyu ni wa sehemu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaomba hilo tusaidiwe. Hifadhi ile ni kwa ajili ya wanyama, tumepeleka simba, tumepeleka wanyama wengine, tunataka tuone watalii lakini siyo ng'ombe wanaotoka sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina haja ya kutaja, lakini...

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Taarifa.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia ninadhani muda wangu umekwisha…

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Suala hili la ng'ombe kutoka nchi jirani kuingizwa kwenye mbuga zetu linasemwasemwa sana inaonekana kuna watendaji ambao wanafanya *deal.* Ninaomba hili jambo Serikali ifuatilie kwa ukali kabisa na ifahamu kinachoendelea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chiwelesa amekupa taarifa, lakini ninaona kama alikuwa anachangia kinamna huyu, unaipokea? *(Kicheko)*

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, amechangia kinamna na taarifa hiyo ninaipokea kwa sababu inaumiza. Inaumiza, tunajua mengi sasa tusingependa twende huko. Nilikwishasema kwenye kikao cha ndani *last time* tukiwa na Waziri wa Maliasili aliyepita, kwa sababu kipindi hicho walikuwa wanafanya *plan* ya kuhamisha tembo zaidi ya 200, wawatoe Kimisi wawalete Burigi-Chato, Biharamulo, nikapinga. Hata hivyo nikasema tembo wananitesa mimi Kata ya Nyakahura Kijiji cha

Mgombe wananchi wamehama kabisa halafu unabeba tena tembo 200 unatoa Kimisi unawaleta pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado ng'ombe wako mle ndani. kwa hiyo, tunaomba tusaidiwe. Hifadhi tunazitaka lakini kama hifadhi zipo haziwezi kutumika vizuri kusaidia wananchi, wananchi wenyewe Watanzania ambao ni za kwao wanateseka halafu kuna watu wamehifadhi mle ng'ombe, si sawa. Sisi tunajuana leo mtu anaamka na ng'ombe 300, baada ya muda unasikia jamaa ana 3,000 si tunaambiana, 3,000 aliwatoa wapi? Wamezaliana lini? Maana yake limeletwa kundi kutoka sehemu fulani, limevushwa mpaka limeingizwa kwenye hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba watusaidie, hifadhi zilindwe zilete maendeleo, lakini Watanzania wakae sehemu ambayo na wao wajione kwamba ni Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Ezra J. Chiwelesa, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge tumefikia mwisho kwa kipindi hiki cha uchangiaji kwa majina yaliyoletwa mbele ya meza leo hii.

Nina tangazo moja la kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba au mnatangaziwa kwamba, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *NHIF* umeandaa programu maalum ya kutoa huduma ya upimaji wa afya katika viwanja vya Bunge kwa Wabunge na watumishi.

Huduma hiyo kimsingi imeshaanza toka tarehe 13 Mei na itaendelea hadi tarehe 26 Mei, 2026 katika Kituo cha Afya cha Bunge. Aidha, huduma zinazotolewa ni uchunguzi na ushauri wa kitaalamu kuhusu magonjwa ya moyo, mifupa, magonjwa ya akina mama na huduma ya lishe.

Hivyo Waheshimiwa mnaombwa kufika Kituo cha Afya cha Bunge ili kupata huduma hizo muhimu. Waheshimiwa tusisitize

sana suala hili; kwa shughuli za hapa Bungeni wote tunajua mambo ni mengi na mara nyingi hatuna muda. Kwa hiyo, huduma kama hii ya kitaalamu ya mabingwa inapokuja karibu na wewe, tuitumie. Kwa hiyo, niwaombe sana.

Baada ya kusema hilo, ninaahirisha kikao hiki cha Bunge mpaka siku ya Jumatatu tarehe 18 Mei, 2026 saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.06 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 18 Mei, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA